# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Thelathini na Tatu – Tarehe 27 Julai, 2007**

(*Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi*)

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma* Dua

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko kwa mwaka wa Fedha 2007/2008.

**MHE. ABDALLAH S. SUMRY (K.n.y. MHE. WILIAM H. SHELLUKINDO - MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA)**:

Taarifa ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2007/2008.

**MHE. LUCY F. OWENYA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI**:

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2007/2008

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 302

**Hati yenye Shaka ya TACAIDS**

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2006 ilionyesha kuwa, *TACAIDS* ilipata Hati yenye shaka kutokana na matumizi ya fedha za Maendeleo Tshs.24,063,871,428:-

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya matumizi hayo yanayotia shaka?

(b) Je, Serikali inaweza kutoa maelezo kamili Bungeni ya jinsi fedha hizo zilivyotumika na kwa malengo gani?

(c) Je, ni kazi zipi za Maendeleo zilikusudiwa kutekelezwa, kwa kipindi gani na ni mafanikio gani yalipatikana na utekelezaji ulikumbana na matatizo gani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni, 30, 2006 *TACAIDS* ilipata Hati yenye shaka katika matumizi ya fedha kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge. Sababu kuwa ni kwamba utekelezaji wa shughuli za *UKIMWI* unahusisha Wizara mbalimbali, Mamlaka zote za Serikali za Mitaa, Asasi za Kiraia na baadhi ya Sekta binafsi. Wote hawa wanapata fedha za utekelezaji kutoka T*ACAIDS*. Zaidi ya asilimia 80 ya fedha zilizoko kwenye Bajeti ya *TACAIDS* hupelekwa kwa watekelezaji mbalimbali nchini. Watekelezaji hawa wanahitaji muda wa utekelezaji kabla ya kutoa taarifa ya matumizi ya fedha hizo. Kwa utaratibu uliokuwepo siku zilizopita Taarifa ya matumizi ya fedha ndiyo ilikuwa ikitumiwa na Wakaguzi kuhakiki na kuthibitisha matumizi hayo.

Kutokana na hali hiyo Mkaguzi wa Hesabu za Serikali alipofika kukagua *TACAIDS* alikuta kuna fedha ambazo zilikuwa zimetolewa kwa watekelezaji mbalimbali lakini taarifa ya matumizi yake ilikuwa haijarejeshwa, na hivyo kusababisha kutolewa kwa hati hiyo yenye shaka. Hata hivyo, kutokana na maelekezo mapya ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ni kwamba watekelezaji wanaohusika wanatakiwa wawasilishe kwa *TACAIDS* stakabadhi ya kukiri mapokezi ya fedha hizo wanazopewa ili kuanzia hapo Vyombo ama Taasisi hizo ndizo ziwe na jukumu la kutunza nyaraka zote zinazotakiwa kumwezesha Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi.

(b) Mheshimiwa Spika, maelezo ya matumizi ya fedha za Maendeleo jumla ya Tshs.24,063,871,428/= kwa miradi mitano iliyopata fedha ili kutekeleza malengo yaliyopangwa katika kipindi hicho ni kama ifuatavyo:-

(i) Ushirikishwaji wa Sekta mbalimbali katika Udhibiti wa *UKIMWI*- Shs.10,402,173,532/= kwa ajili ya kutekeleza lengo la kuongeza kasi ya udhibiti wa *UKIMWI* kwenye jamii ya Watanzania kwa kushirikisha Sekta mbalimbali.

(ii) Kuufanya *UKIMWI* moja ya shughuli za kila siku za Sekta ya Umma Shs.383,655,617/= kwa ajili ya kujenga uwezo wa Sekta ya Umma na Asasi za Kiraia katika kuufanya UKIMWI moja ya shughuli zao za kila siku.

(iii) *Global Fund* – Shs. 9,206,166,991/= kwa ajili ya kuboresha Huduma za Ushauri Nasaha na Upimaji wa hiari ili kuweza kuanzisha tiba na huduma za wagonjwa wa Kifua Kikuu na *UKIMWI* kwa kushirikisha Asasi mbalimbali. Kwa upande wa Asasi za Kiraia na za Dini, fedha zao hupitia kwenye Tume kutokea Hazina, lakini pia Wizara ya Afya na Ulinzi hupata fedha hizi kupitia Hazina. Fedha hizi walilipwa *Christian Social Services Commission* kwa ajili ya uratibu wa Asasi za Kidini na *AMREF* kwa ajili ya Uratibu wa Asasi za Kiraia.

(iv) *Rapid Fund Envelope (DFID*) Shs.2,082,596,939/= kutekeleza mradi wa Kusaidia Asasi za Kiraia zenye miradi ya muda mfupi ambayo haizidi mwaka mmoja. Mradi huu unaratibiwa na Sekta Binafsi – *Delloitte and Touche*.

(v) *Rapid Funding Envelope* kutoka Serikali ya *Ireland* Shs. 1,989,278,349/= Mradi wa kusaidia Asasi za Kiraia zenye miradi ya muda mfupi ambayo haizidi mwaka mmoja nao unaratibiwa na Sekta Binafsi *Delloitte and Touche*.

(c) Mheshimiwa Spika, kazi za Maendeleo zilizokuwa zimetarajiwa kutekelezwa ili kudhibiti *UKIMWI* ni nyingi na Taasisi/Mamlaka mbalimbali zinashirikishwa katika utekelezaji huo. Haitakuwa rahisi kwa muda wa maswali uliowekwa kuniwezesha kutaja shughuli hizo, matatizo yanayotukabili na mafanikio yake. Hata hivyo, orodha ya kazi hizo ipo na inaonyesha kipindi cha utekelezaji wake, matatizo yaliyopo na mafanikio. Nitamkabidhi Mheshimiwa Dr. Slaa na Waheshimiwa Wabunge wengine wote watakaozihitaji.

**MHE. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, kwa kuwa, malalamiko mengi tunayoyapata ni kutoka kwa walengwa kwamba fedha hizi ambazo ni nyingi haziwafikii na zinaishia katika ngazi ya uratibu, ushirikishwaji na semina kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Waziri anatoa kauli gani kwamba sasa kunatakiwa mkakati

maalum ambao utatolewa taarifa rasmi kwamba walengwa wenyewe waweze kufikiwa na fedha hizo nyingi ambazo zinatoka kwa wafadhili hasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, ni kweli kwamba wakati wa ukaguzi inawezekana taarifa hazikupatikana. Lakini Waheshimiwa Wabunge tulio wengi na tunaokuwepo kwenye Halmashauri tunafahamu kwamba tumeunda Kamati za UKIMWI mpaka vijijini na ngazi ya Vitongoji, na fedha kidogo zinazoenda kule hata taarifa pia hazipatikani. Je, utawekwa utaratibu gani wa uhakika wa ukaguzi ili taarifa ziweze kupatikana tokea kule chini kabisa ambapo fedha hizi zitapelekwa ili kuwe na uhakika wa matumizi mazuri ya fedha hizo ambazo kwa kweli ni uhaki wa watanzania? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI:** Mheshimiwa Spika, napenda nikubaliane naye kabisa kwamba tunahitaji mkakati wa kuhakikisha tunawashirikisha walengwa kuanzia ngazi ya chini, na hilo ndilo lengo la Serikali la kufanya kwamba baada ya Mkoa yaani zile *Regional RFA* zile kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya wananchi vijijini washirikishwe moja kwa moja katika kuhakikisha kwamba hiyo miradi inayowafikia. Ndiyo sababu kunakuwa na uhakika wa ile miradi inayoibuliwa na wananchi wenyewe kule kuhakikiwa na Halmashauri za Wilaya na kisha kuzi-*forward* kwa *RFA* ambao ndiyo ulete *TACAIDS.*

Pili, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa amesema kwamba wakati wa ukaguzi wameshuhudia kwamba fedha hizo hawaziwafiki wananchi, na hivyo angependa kuwe na utaratibu wa uhakika wa kuhakikisha kwamba hizo fedha zinafika. Kwa utaratibu huo mpya wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali baada ya *TACAIDS* kuwa imefikisha fedha kwa walengwa, na walengwa wale wakishakiri kupokea hizo fedha, basi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atahakikisha ukaguzi wake unafika mpaka kwenye ngazi ya chini.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tena nikumbushe utaratibu kuhusu wageni. Kuna Waheshimiwa Wabunge wanaendelea na huu utaratibu wa kuandika hivi sasa kwamba wana wageni wao. Sasa tulikwishakubaliana kwamba wageni wanaokusudiwa kutambulishwa ni wale tu ambao saa 2.30 asubuhi Katibu atakuwa amekwishapata majina yao. Kwa hiyo, naomba mniwie radhi leo hao mnaoendelea kuleta majina ya wageni wenu sitawatambulisha. Kwa hiyo, ndiyo hali yenyewe halisi. Ninawaomba *Presiding Officers* wenzangu kama walilegeza kidogo wakati sipo, basi wajue kwamba huo ndiyo utaratibu sasa. Hakuna ruksa yoyote baada ya kusoma Dua unaleta karatasi unasema una mgeni hatatambulishwa.

Na. 303

**Hitaji la Umeme – Peramiho**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Bajeti ya mwaka 2006/2007 Serikali iliahidi kupeleka umeme katika Mji Mdogo wa Peramiho kutokea Kijiji cha Lilambo Wilayani Songea na kwa kuwa, Serikali iliahidi pia kuwa, umeme huo wa *TANESCO* ungepita katika maeneo ya vijiji jirani vya Likuyufusi, Lilambo, Perahamiho A na B, Lundusi na Maposeni:-

Je, Serikali itatimiza lini ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI YA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2006/2007 *TANESCO* ilikuwa imepanga kutekeleza mradi wa kupeleka umeme katika Mji mdogo wa Peramiho. Katika kutekeleza mradi huo, vijiji vya Likuyufusi, Lilambo, Peramiho A na B, Lundusi na Maposeni vingeweza kunufaika na kupatiwa umeme pia. Gharama za mradi huo ni shilingi milioni 480.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa kuupatia umeme Mji mdogo wa Peramiho na vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge haukuweza kutekelezwa kutokana na hali mbaya ya kifedha ya *TANESCO.* Mipango iliyopo ni kutekeleza mradi huu kupitia Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini utakaotekelezwa kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (*Rural Energy Agency*) unaotarajiwa kuanza katika mwaka huu wa fedha 2007/2008 kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kutamka sasa kwamba Mradi huo utatekelezwa katika Awamu hii kupitia Mpango wa Umeme Vijijini.

Mheshimiwa Spika, wakati pia Waziri wa Nishati na Madini alipokuwa akijibu hoja yangu hiyo hiyo wakati wa Bajeti yake aliahidi pia kwamba Mradi huo pia ungeweza kutekelezwa kwa kupitia Mradi wa Umeme wa Makambako-Songea. Sasa kwa kuwa, *alternative* zote mbili zipo katika Mpango huo. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari sasa kutoa jina rasmi la mradi wa Makambako-Songea akaongeza Makambako-Songea-Peramiho ili nguvu hizo zote ziweze kuwekwa pamoja kwa ajili ya kuhakikisha kwamba azma hiyo sasa inatekelezeka? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI YA MADINI**: Mheshimiwa Spika, cha msingi na lengo ambalo Serikali inalo ni kuhakikisha kwamba Mradi huu unatekelezwa kwa mipango iliyopo. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kama hiyo itampendeza kwa kubadilisha jina la Mradi. Sisi nadhani hatuna matatizo na Mradi huu

tuuite jina gani, lakini cha msingi ni kwamba upo katika Mipango yetu ya utekelezaji na tunarudia kumwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutatekeleza mradi huo. *(Makofi)*

Na. 304

**Milipuko wakati wa Uchimbaji Madini - Geita**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (k.n.y MHE. ERNEST G. MABINA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika uchimbaji madini hasa katika Mgodi wa Geita ambao uko wazi, hutokea milipuko ambayo husababisha wananchi walio karibu na mradi huo kupata adha ya kupasuliwa nyumba zao na mavumbi yanayosababishwa na milipuko hiyo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi wa Nyamalembo, Katumaini, Magema, Nyakabale, Katoma na Mji wa Geita kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina, Mbunge wa Geita, naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mgodi wa Geita ni wa wazi (*open cast*) na dhahabu yake iko katika miamba. Kutokana na ugumu wa miamba iliyopo inalazimu mgodi kutumia baruti kuipasua miamba hiyo kabla ya kuitoa toka chini ardhini na kisha kuisaga ili kutenganisha dhahabu.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya baruti katika uchimbaji wa madini yana athari mbalimbali. Baadhi ya athari ambazo zinaweza kuathiri binadamu ni pamoja na matetemeko au mawimbi ya ardhi *(ground vibrations*); shinikizo la mawimbi ya sauti (*air or sound pressure*); na miamba kuruka hewani *(fly-rocks*). Hata hivyo teknolojia ya ulipuaji imeendelea sana kuweza kupunguza athari hizo. Aidha, matumizi salama ya baruti yanayozingatia Sheria ya Baruti ya mwaka 1963 na kanuni zake za mwaka 1964 yakizingatiwa yanaondoa athari kwa binadamu wakati wa matumizi ya baruti.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina, Mbunge wa Geita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, umbali yalipo makazi ya wananchi kutoka sehemu inayochimbwa madini ni zaidi ya kilomita 2. Umbali huu ni salama kwa uchimbaji unaofanyika mgodi kutegemea na kiasi cha juu cha baruti ambacho hutumika kwa wakati mmoja katika mgodi huo.

Mheshimiwa Spika, mgodi wa Geita una kipimo cha *Seismograph* cha kufuatilia nguvu ya mawimbi ya baruti ardhini (*Ground Vibration Intensity*) na nguvu ya sauti (*Noise Level)* katika eneo la kiwanda cha kuchambuliwa pamba na *COPCOT* kilichopo jirani na mgodi huo.

Mheshimiwa Spika, wakaguzi kutoka Wizara yangu hufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika migodi yote hapa nchini ukiwemo mgodi wa Geita ili kuhakikisha kuwa uchimbaji na ulipuaji wa baruti unazingatia Kanuni za usalama chini ya Sheria ya Madini na Sheria ya Baruti na hivyo kutosababisha madhara kwa binadamu na mali zao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuitumia fursa hii kuwahakikisha wananchi wa vijiji au maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge na wananchi wanaoishi karibu na migodi kwa ujumla kwamba Serikali inawajali na iko tayari na imara kulinda maisha yao na mali zao kwa mujibu wa sheria za nchi yetu.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri kabisa kwamba hao Ndugu zetu wawekezaji wanatumia baruti kuhakikisha kwamba wanatafuta hizo dhahabu katika maeneo hayo ambayo yametajwa hapo kwenye swali la msingi.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, naomba Mheshimiwa NaibuWaziri anisaidie kunieleza katika Mkataba na wawekezaji kuna masharti yoyote ya kuhakikisha kwamba athari zinazotokea kwa wananchi wanaopata madhara hayo wanapimwa na mwekezaji huyo?

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa kuwa athari wanazozipata hao wananchi, na kilomita 2 ni kiasi kidogo sana kutoka kwenye lile eneo alilolieleza Mheshimiwa Naibu Waziri. Je, fidia kwa wale wanaothirika na baruti hizo ni nani analipa, mwekezaji au Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza, tumesema ulipuaji wa baruti wa mgodi kama wa Geita ambao ni mgodi wa wazi unaongozwa na Sheria ya Madini lakini pia Sheria ya Baruti. Sheria hizo zimeweka masharti ambayo yanawaongoza wachimbaji au mwekezaji yeyote atakayekwenda kinyume masharti na kanuni zilizomo kwenye Sheria hizo au Kanuni hizo, basi anakuwa amevunja sheria na hatua inachukuliwa mara moja kwa mujibu wa sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwa ujumla kupitia Bunge lako Tukufu kwamba hiyo ndiyo miongozo ambayo inazingatiwa na Serikali iko karibu sana kuhakikisha kwamba haiwaathiri wananchi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kilomita 2 zinaweza kuonekana ni ndogo au ni fupi sana kutoka kwenye eneo la mgodi, lakini hayo ni mambo ya kitaalam. Sheria na

miongozo vimezingatiwa, na kimsingi kilomita 2 ndizo ambazo zimethibitika kwamba haziwezi kumwaathiri mwananchi au mali zake kwa vyovyote ambaye atakuwa karibu na maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kwamba kilomita 2 zinazingatia kanuni, sheria na taratibu zilizopo. Lakini endapo litajitokeza lolote na likawa kinyume na sheria na taratibu zilizopo, basi fidia italipwa na huyo aliyevunja sheria. Kimsingi katika hilo atakuwa ni mwekezaji na wala siyo Serikali.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa matumizi ya baruti katika migodi inaleta ufanisi katika shughuli nzima za uchimbaji wa madini; na kwa kuwa wachimbaji wadogo wadogo ili kuleta ufanisi hawana budi watumie baruti katika migodi yao. Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwapa mafunzo wachimbaji wadogo wadogo ili waweze kutumia baruti hizo na kuwapa *Blasting Certificate*?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, sheria ambayo tumeisema hapa ni Sheria ya Madini na Sheria ya Baruti zinawahusu wote wanaojihusisha na shughuli za uchimbaji madini. Kwa hiyo, hazibagui mchimbaji mdogo wala mkubwa.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu utaratibu uliopo kuwasaidia wachimbaji wadogo nirudie kusema ambayo tumekuwa tukisema kupitia Wizara yetu kwamba Serikali inaendelea na utaratibu wa kuwashirikisha wachimbaji wadogo, na mojawapo ya mpango tulionao ni kuwawezesha kupata maarifa mapya. Maarifa mapya ikiwa ni pamoja na kuwa na vitendea kazi vya kisasa zaidi na utaratibu tunauandaa. Utaratibu tunaofanya sasa hivi na kwa kweli tumeishaanza tunakuwa tunashirikiana na wadau wote, wachimbaji wawe wakubwa au wadogo na wadau wengine.

Lakini kwa hili kuhusu wachimbaji wadogo ili wapate maarifa mapya na teknolojia ya kisasa tumekuwa tukijitahidi kushirikiana na wadau wengine wakiwemo wawekezaji wakubwa ambao teknolojia yao ni kubwa kuwawezesha wachimbaji wadogo wapate hayo maarifa.

Mheshimiwa kuhusu kupata *Blasting Certificate* hili ni suala la kikanuni na miongozo iliyopo. Kwa hiyo, ni mambo ambayo Wizara yetu inayashughulikia na tunamshauri Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwa ujumla kwamba wazidi kuwasiliana na Ofisi zetu za Madini za Kanda ambazo zipo karibu kila kona ya nchi ili kuhakikisha kwamba wanapata miongozo sahihi kwa ajili ya utekelezaji na kupata vitu ambavyo vinahitajika katika shughuli hizo.

Na. 305

**Suala la Mgombea Binafsi katika Ngazi Mbalimbali za Uchaguzi**

**MHE. KABWE Z. ZITTO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mahakama Kuu ya Tanzania imetoa hukumu ambayo inaitaka Serikali kuleta Muswada wa Sheria ya kufanya mabadiliko katika Katiba ya Nchi ili kuruhusu wagombea binafsi katika uchaguzi kwenye ngazi mbalimbali nchini:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya hukumu hiyo na inadhani kutakuwa na madhara gani katika ujenzi wa demokrasia?

(b) Je, Serikali haioni kuwa, sasa ni wakati muafaka wa kuanzisha mjadala wa Mabadiliko ya Katiba ya Nchi ili pamoja na mambo mengine kuboresha mfumo wa uchaguzi na hatimaye kuwa na mifumo mchanganyiko wa Wengi wape na ule wa uwakilishi wa uwiano yaani *first-past-the post* na *proportional representation system*?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika kesi namba *Misc. C.C. N. 10/2005* Mhakama Kuu ya Tanzania imetoa hukumu ambayo inaitaka Serikali kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya kufanya mabadiliko katika Katiba ya nchi ili kuruhusu dhana ya ugombea binafsi katika uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Serikali haikuridhika na uamuzi huo na hivyo imekata rufaa katika Mahakama ya Rufani ya Tanzania. Kwa sasa Serikali haiwezi kujadili suala hilo kwa kuwa bado lipo Mahakamani.

(b) Kuhusu suala la Serikali kuanzisha mjadala wa mabadiliko ya Katiba ya nchi napenda kueleza kwamba kwa sasa Serikali haina mpango huo. Kupitia Waraka wa Serikali Namba 1 wa mwaka 1998 ambao Serikali iliutumia kukusanya maoni ya wananchi kuhusu mabadiliko ya Katiba, mambo mengi yalipendekezwa na Serikali imekuwa ikirekebisha Katiba kwa kuzingatia mapendekezo hayo kwa awamu. Suala la *Proportional Representation* kuboresha mfumo wa uchaguzi ni miongoni mwa masuala ambayo Serikali iliyakubali na itaendelea kuboresha Sheria kwa kadri hali itakavyoruhusu. Hivi sasa Wabunge wa Viti Maalum wanaingia Bungeni kupitia mfumo huo wa *Proportional Representation*.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo napenda kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba yeye kama raia wa nchi hii anayo haki ya kufikisha maoni au mapendekezo yake kwenye vyombo vinavyohusika ikiwemo Wizara yangu ili yaweze kufanyiwa kazi wakati muafaka utakapowadia.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Suala la mfumo wa uwakilishi wa uwiano si suala la jipya katika mijadala ya Kikatiba. Mtakumbuka kwamba

aliyekuwa Waziri wa Sheria na Katiba Mwaka 1999 ambaye sasa ni Spika wa Bunge hili aliwasilisha katika Bunge hoja hii ya kuwa na Viti Maalum kwa ajili ya *Proportional Representation* kwa Vyama ambavyo vimepata zaidi ya asilimia 5 ya kura. Hata Bunge hili Tukufu lina jumla ya viti 350 kwa sababu katika mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2005 katika Muswada ilikuwa imependekezwa kwamba kuwe na viti 28 kutokana na *Proportional Representation*. Lakini katika mazingira ambayo hayaeleweki viti hivyo vikawa vimeondolewa. Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka wa kuhakikisha kwamba hakuna kura inayopotea kwa kuweka mfumo huu kuhakikisha kwamba vyama ambavyo vinapata zaidi ya asilimia 5 ya kura vinapata viti kutokana na kura za uwiano?

**NAIBU WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, nchi yetu tuliamua kutumia mifumo yetu yote miwili. Ile *first past post* na *proportional representation.* Na watu wengi humu ndani wamo kwa kutumia mfumo huo wa *proportional representation.* Lakini hata hivyo kama bado kuna viwango vya zaidi vinatakiwa nimeshasema katika jibu langu la awali kwamba Wizara yangu itaratibu maoni yote yatakayotolewa na wananchi kwa sababu Katiba yetu ni Hati hai ambayo inabadilika kila mara ambapo tunahitaji kufanya hivyo kwa mahitaji ya nchi yetu.

Na. 306

**Utaratibu wa Ushahidi Mahakamani**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mahakimu wa Mahakama zote pamoja na Majaji wakati wanachukua maelezo ya shahidi, shahidi hapati nafasi ya kujua kama Hakimu au Jaji ameandika kama alivyosema au la, tofauti na inavyofanyika katika Jeshi la Polisi ambapo Polisi baada ya kuandika maelezo ya shahidi humsomea na shahidi anapoyakubali huweka saini yake:-

(a) Je, kwa nini utaratibu huo unaotumiwa na Askari Polisi usitumiwe pia katika Mahakama zetu ili kuondoa dhana mbaya iliyopo kwamba, Polisi ndio wanaoharibu kesi;

(b) Je, ni uhuru mkubwa waliopewa Mahakimu na Majaji ndio unasababisha kuharibika kwa kesi nyingi na hivyo wanyonge kukosa haki zao na kuwatupia lawama Askari wanaopeleleza kesi?

**NAIBU WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mahakama zimewekewa utaratibu wa kuchukua ushahidi chini ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, 1985, Sura ya 20 na Sheria ya Mahakimu ya 1984 Sura ya 11 kama ifuatavyo:-

(b) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuchukua ushahidi katika Mahakama za Mwanzo umewekwa katika Jedwali la tatu, Kifungu cha 35(6) cha Sheria ya Mahakimu ambayo inaipa Mahakama jukumu la kuchukua ushahidi wa mlalamikaji, mshtakiwa

pamoja na mashahidi katika kesi zote. Mahakama pia inalo jukumu la kusoma ushahidi uliotolewa Mahakamani hapo kwa waliotoa ushahidi kwa lugha wanayoielewa na kama yapo mabadiliko au masahihisho, kuyaandika na kuthibitishwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mahakama za Wilaya na za Hakimu Mkazi, utaratibu wa Mahakama hizi kuchukua ushahidi unatolewa na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, 1985, Sura ya 20.

Kifungu cha 210(3) cha sheria hiyo kinamtaka Hakimu kumfahamisha shahidi kuwa anayo haki ya kusomewa maelezo yake. Iwapo shahidi huyo atapendelea kusomewa maelezo yake, basi Mahakama itamsomea na kuandika mabadiliko yoyote yatakayokuwa yamefanywa na shahidi huyo baada ya yeye kusomewa maelezo yake.

Aidha, kifungu cha 211 kinampa Hakimu wajibu wa kumfahamisha mshtakiwa ushahidi wote utakaokuwa umenakiliwa kwa lugha ambayo yeye (mshtakiwa) au Wakili wake (iwapo atakuwa amewakilishwa) haielewi, na Mahakama hiyo itautafsiri ushahidi huo kwa lugha inayoeleweka kwa mshtakiwa au katika lugha ya Mahakama kwa Wakili wake.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuchukua ushahidi wa Mahakama Kuu haujafafanuliwa na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, kama ilivyo kwa Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi. Isipokuwa, Sheria hiyo katika kifungu cha 215, imeipa Mahakama Kuu uwezo wa kutengeneza kanuni zitakazoiongoza Mahakama hiyo katika utaratibu mzima wa kuchukua ushahidi Kanuni hizo za Mahakama Kuu zinapatikana katika *Criminal Procedure (Record of Evidence) High Court Rules (G.Ss. 28 of 1953 and 286 of 19560.* Taratibu hizo zimeainishwa katika kanuni ya 3 hadi 5.

( c)Mheshimiwa Spika, sheria iko wazi katika kuangalia utaratibu mzima wa uchukuliwaji wa ushahidi Mahakamani. Hivyo, iwapo kuna kesi ambazo zimeharibika kufuatia ukiukwaji wa sheria zilizopo, basi kuharibika kwa kesi hizo kutakuwa kumesababishwa na udhaifu wa watendaji na sio wa sheria.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza suala la nyongeza.

Kwa kuwa mara nyingi kwenye Mahakama mshtakiwa anapoeleza maelezo yake na Hakimu hamhakikishii mshitakiwa kile ambacho amekiandika. Kutokana na hali hii Hakimu anaweza kuandika kinyume na alivyoeleza mshtakiwa na ikathibiti kwamba ndivyo ukweli ulivyo. Huoni sasa kwamba ni wakati muafaka kuweka taratibu maalum kwamba lazima Hakimu ahakikishe kwamba yule anayehukumiwa lile aliloandika ndilo sahihi? Kutokufanya hivyo huoni kwamba ukweli unaweza kupotea na usawa wa haki za binadamu vilevile?

**NAIBU WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, sheria yetu iko wazi kama nilivyoeleza mwanzo kwamba mshtakiwa, shahidi na mlalamikaji katika kesi za madai wanayo haki ya kusomewa maelezo waliyoyatoa na

kama hawaelewi lugha hiyo basi wataelezwa katika lugha wanayoielewa ili wakishakubali basi Hakimu atahakikisha kama ndio sawa. Wakiona kama kuna mabadiliko wataleta mabadiliko yao. Hakimu atayachukua mabadiliko hayo atayaweka. Hivyo ndivyo sheria ilivyo, sasa kama kuna matatizo katika utendaji kama nilivyosema awali siyo tatizo la sheria ni tatizo la utekelezaji tu.

Sasa kama Mheshimiwa Mbunge anataka labda tuwakumbushe Mahakimu wetu, Mahakimu wanajua. Mwisho wa kuchukua maelezo yote ya mshtakiwa ama shahidi Hakimu huwa anaandika na kuthibitisha kwamba haya ndiyo yaliyosemwa. Sasa kama mshtakiwa ana wasi wasi basi anamwambia Hakimu naomba unisomee maelezo yangu na Hakimu atamsomea na kama kuna mabadiliko Hakimu atayaingiza.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa taarifa ya Mheshimiwa Jaji Mark Bomani iliyohusu *Legal Sector Reform* ilipendekeza kwamba kuwe na wapelelezi na waendesha mashtaka tofauti. Mmoja afanye kazi ya upelelezi na mwingine afanye kazi ya kuendesha mashtaka.

Je, Serikali imefikia wapi juu ya taarifa hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA**: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mapendekezo ya Tume ya Jaji Bomani yalipendekeza kwamba kuwepo na mgawanyo kati ya upelelezi na uendeshaji wa mashtaka. Sasa hivi Serikali iko katika hatua za kwanza za mradi huu. Tumechagua mikoa sita ambapo tutatenganisha shughuli hizi kuanzia mwaka huu wa fedha tunaita *Civilinasation Project.* Katika mikoa hii sita tutaanza kuondoa Polisi katika masuala mazima ya uendeshaji wa kesi. Polisi watashughulika na masuala tu ya upelelezi halafu Mawakili wa Serikali ndio watakaokuwa wanaendesha kesi Mahakamani. Kwa hiyo mradi huo umeanza na katika mwaka huo wa fedha kama nilivyosema tutaanza na mikoa sita na tunatarajia hivyo hivyo baadaye tuusambaze mradi huu nchi nzima.

**SPIKA:** Kabla hatujahamia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii naendelea kuikumbusha Serikali kwamba jina la Wizara hii bado linaendelea kuwa la utata na hakuna sababu. *GN* iliyotangaza Serikali kuonyesha majina ya Wizara inaita ni Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba. Wao wanapokuja hapa wanang'ang'ania ni Wizara ya Katiba na Sheria. Hili sio jambo dogo lazima tujue jina la Wizara hatuwezi kwa kuendelea kuwa jina la Wizara halieleweki. *(Makofi)*

Na. 307

**Ongezeko la Watoto Yatima**

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE** aliuliza:-

Kwa kuwa, tatizo la watoto yatima limekuwa ni tatizo kubwa linaloongezeka siku baada ya siku hasa baada ya kuingia kwa ugonjwa wa UKIMWI:-

(a) Je, kuna watoto yatima wangapi walio chini ya umri wa miaka 15 katika Wilaya ya Kahama; na kuna vituo vingapi vya kulelea watoto hao Wilayani Kahama?

(b) Je, kuna Mashirika mangapi yasiyo ya Ki-Serikali yanayotoa huduma kwa watoto yatima Kahama na ni huduma gani zinazotolewa na ni watoto wangapi wanaonufaika na huduma hizo?

(c) Je, Serikali kwa upande wake ina mpango gani wa kuwasaidia watoto hao ili wapate haki zao za msingi kama vile elimu na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mbunge wa Msalala, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu na Sensa ya Kitaifa iliyofanyika mwaka 2002 Wilaya ya Kahama ilikuwa na watoto 316,599 wenye umri chini ya miaka 17 wavulana ni 158,972 na wasichana 157,627. Kati ya watoto hao watoto yatima walikuwa 2,469 wavulana wakiwa 1,239 na wasichana 1,229.

(b) Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kahama ina kituo kimoja tu cha kulelea watoto yatima kinajulikana kwa jina la Tusiwaache *Orphans Centre*. Kituo hiki kinamilikiwa na Taasisi isiyo ya Kiserikali inayoitwa MVUMA yaani Muungano wa Vikundi vya Uzalishaji mali na kina jumla ya watoto yatima 18 wavulana 10 na wasichana 8.

Mheshimiwa Spika, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayotoa huduma kwa watoto yatima Wilayani Kahama ni:- SHIDEPHA, *Good Samaritan,* Wawape, Mvuma, *ZOFADA, KADINWOF, KACODA, CADETO,* na *CITIZEN CARE PROJECT.* Huduma zinazotolewa na idadi ya watoto wanaonufaika na huduma hizo ni kama ifuatavyo:-

| **Na.** | **Aina ya Huduma** | **Idadi ya Watoto** |
|---|---|---|
| 1. | Chakula | 187 |
| 2. | Vifaa vya shule | 622 |
| 3. | Ada za Shule | 175 |
| 4. | Sare za Shule | 722 |
| 5. | Matibabu | 1,870 |
| 6. | Magododo, Shuka na Mablanketi | 375 |

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kahama na Shirika Lisilo la Kiserikali *(PACT* Tanzania kwa kutumia fedha za Mfuko wa Dunia (*Global Fund Rounds*) tunatakeleza mpango shirikishi jamii wa utambuzi na huduma kwa yatima na watoto walio katika mazingira hatarishi. Utekelezaji wa mpango huu umeanza mwaka huu 2007 na tayari watoto 2,822 kutoka Kata 7 wamepewa huduma zifuatazo:-

Huduma za matibabu (Kadi za Mfuko wa Afya ya Jamii ( *CHF)*

Vifaa vya shule

Sare za shule kwa wanafunzi wa Shule ya msingi

Mafunzo ya ufundi (wasichana 32)

Ada za shule na michango (wanafunzi 42)

Chakula watoto 169 (mahindi kilo 650, maharage kilo 20, sukari kilo 5 na lishe kwa watoto chini ya miaka 5).

Watoto wanaolelewa na walezi wazee sana). Hawa wamepatiwa vitanda, magodoro, mashuke, mablanketi, neti, nguo na sweta

Mabati na misumari kwa ajili ya kujengea nyumba za watoto hao ambao wanaishi kwenye nyumba mbovu sana.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nilitaka kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Mashirika mengi Yasiyo ya Kiserikali yamekuwa yakifanya shughuli zake kwa kufuata miongozi ya wafadhili wao ikiwemo ile inayosema ni wapi wafanye kazi na shughuli zipi wazifanye kitu ambacho tumekiwa tukizifanya *NGO's* nyingi ziwe kwenye maeneo fulani tu badala ya kufika kwenye maeneo yote ya nchi hasa maeneo ya mijini. Je Serikali kwa nini isishiriki moja kwa moja katika kuratibu shughuli za *NGO's* na kuwapangia kwamba Shirika fulani lifanye kazi sehemu fulani kwa kuzingatia matatizo yaliyoko kwenye eneo husika.

Swali la pili, kwa kuwa *NGO's* zimekuwa zikifanya kazi zake zenyewe kuangalia tatizo gani zi-*address* na matatizo yaliyo mengi ambayo yanasibu jamii zetu yamekuwa hayaangaliwi moja ya tatizo kubwa tulilonalo ni tatizo la chakula hasa mashuleni kwa watoto ambao hawana wazazi wao. Je, Serikali inaonaje ikitafuta au ikiwasiliana na Mashirika yanayohusika na miradi hii ili walau kuwepo mpango wa kusaidia chakula kwa watoto wa shule za msingi ambao hawana wazazi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza Mashirika mengi yanayokwenda kufanya kazi katika maeneo husika ni Mashirika ambayo hayasajiliwi na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hatuna wajibu wa kujua kwamba hili Shiriki lipi linakwenda na hayo Mashirika ya Yasiyo ya Kisekali yanasajiliwa katiika Wizara ya Mambo ya Ndani.Hali kadhalika ninachotaka kusema hapa ni kwamba hata kama watakuwa wanakwenda kule wanachagua napenda kusema kwamba tumekuwa tukishirikiana nao kwa mfano kama hao niliowataja katika jibu la msingi tumekuwa na ushirikiano wa karibu baina yao na Wizara ya Afya na hivyo tutaendelea kuwahamasisha ili waweze kwenda katika yale maeneo ambayo yanaona kwamba yana tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, suala la pili alilozungumzia Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa nini sisi kama Wizara tusiangalie tatizo la *NGO's* ku-*address* katika yale maeneo hasa utoaji wa chakula mashuleni. Tumekuwa tukizungumza hapa kama Serikali kwamba sisi kama jamii suala la watoto ambao ni yatima tusione kama ni suala la *NGO's* peke yake au ni suala la Serikali. Nilikuwa nimesema hapa kwamba suala hili ni suala la kwetu sisi kama wana jamii kwqa hiyo sisi Waheshimiwa wabunge badala ya kutegemea *NGOs* ndio watoe chakula ni lazima tuangalie kama ni jinsi gani katika maeneo yetu tukaweza kuhamasisha sisi jamii ili waweze kuwapatia chakula watoto wanapokuwa mashuleni.

Hali kadhalika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kama mlikuwa mmemsikia hapa Mheshimiwa waziri alikuwa amezungumzia pia mpango wa kuanzisha chakula, kuwahamasisha na kutoa ufafanuzi wa chakula mashuleni. Kwa hiyo naomba tushirikiane na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jmii ili tuone watoto wetu sisi wenyewe kama wazazi tunawapa watoto wetu chakula mashuleni badala ya kutegemea Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Na. 308

**Tatizo la Nyumba za Walimu**

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imeongeza idadi ya walimu ili kukidhi matakwa ya kuboresha ufundishaji; na kwa kuwa, ongezeko la shule na wanafunzi wa Shule za Sekondari limeonyesha matumaini katika bajeti iliyokuwepo:_

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kumaliza tatizo sugu la walimu kuchelewa kujengewa nyumba na kuboresha mazingira ya kazi zao?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kimeongezeka katika matumizi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mbunge Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, kutokana na Serikali kuongeza idadi ya walimu, mkakati wa Serikali wa kupunguza tatizo la uhaba wa nyumba za walimu ni kuendelea kujenga nyumba za walimu kwa kushirikiana na wananchi. Mwaka 2006/2007 Serikali ilichangia ujenzi wa nyumba 1,000 kwa kutoa Ruzuku ya shilingi 9,000,000,000/=.

Mwaka huu inatarajia kuchangia ujenzi wa nyumba 1,500 kwa kutoa Ruzuku ya shilingi 13,500,000,000/=. Aidha, Serikali itaendelea kutoa mafunzo kazini na kununua vifaa vya kufundishia na kujifunza kama sehemu ya kuboresha mazingira ya kazi za walimu

(b)Mheshimiwa Spika, kiasi cha fedha za Ruzuku ya ujenzi wa nyumba za walimu kilichoongezeka ni shilingi 4,500,000,000/=.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa ujenzi wa shule na nyumba za walimu umekuwa ukisimamiwa na Walimu Wakuu au Wakuu wa Shule. Na kwamba hali hiyo imewasababishia kashfa, kero na lawama kubwa wasimamizi hawa hadi kuitwa wabatilifu ambao sio kweli. Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kutafuta Wakala Mjenzi ambaye atasimamia masuala yote ya ujenzi wa nyumba za walimu na shule ili walimu hao waendelee na majukumu yao waliyosomea.Pili, kwa kuwa Jeshi la Kujenga Taifa limekuwa likifanya kazi nzuri ya kujenga nyumba za makazi ya viongozi na mfano mzuri za Mawaziri. Je, ni kitu gani kinasababisha kwamba Wizara isiingie mkataba na asasi hii ili kuondoa kero hiyo na kujengwa nyumba hizi kwa wakati?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)**: Mheshimiwa Spika, usimamizi wa ujenzi wa nyumba za walimu pamoja na vyumba vya madarasa ya Shule za Sekondari umekuwa chini ya usimamizi wa walimu wa shule hizo kwa sababu hawa ndio wasimamizi wa karibu wa fedha zile ambazo tumekuwa tukizipeleka katika shule zetu za sekondari. Tatizo hili tumeliona ni kweli limekuwa likijitokeza walimu wengi wakishindwa kuzidhibitiana wao wenyewe wameshaanza kueleza kwamba tunaomba tusaidiwe ili tuweze kuepukana na matumizi mabaya ya fedha wanayoambiwa. Wizara imeshalitambua na tutalishughulikia ili kuhakikisha kwamba suala hili walimu wanapunguziwa mzigo huu. Moja ni pamoja na kutafuta Wahasibu wazuri watakaokwenda katika Shule za Sekondari zote. Kama hali itaruhusu ili Wahasibu hao wawepo karibu kuweza kuwasaidia katika usimamizi wa fedha hizi.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, kuhusu JKT katika ujenzi. Suala hili Wizara imeshalitumia. Mfano Mkuu wa Mkoa wa Kigoma katika kipindi kilichopita ametumia JKT kujenga madarasa pamoja na nyumba za walimu. Amefanikiwa vizuri sana. Wizara inafanya mazungumzo na JKT, Magereza na vyombo vingine vya Serikali ambavyo

vinafanya kazi nzuri katika Serikali hii. Tuna uhakika kabisa tukishakubaliana Wizara ya Elimu itaingia katika Mkataba na makubaliano katika vyombo hivi vya Serikali ili tuweze kujenga nyumba nzuri, nyingi bila kuwa na matatizo yale ya nyongeza ukichukua mkandarasi wa kawaida unakuta wengine wanaongeza hata gharama ya ujenzi baada ya kuwekeana mkataba. Kumbe hili tunalizingatia na tumeshaanza kulifanyia kazi.

Na. 309

**Ujenzi wa barabara ya Igawa – Rujewa – Ubaruku**

**MHE. ESTHERINA J. KILASI** aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara ya Igawa-Rujewa-Ubaruku ni barabara inayounganisha Makao Makuu ya Wilaya ya Mbarali na Miji Midogo ya Rujewa na Ubaruku. Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga barabara hiyo inayounganisha Makao Makuu ya Wilaya na barabara kuu kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Estherina Julio Kilasi, Mbunge wa Mbarali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Igawa – Rujewa – Ubaruku yenye jumla ya kilometa 18.7 ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Mkoa wa Mbeya. Barabara hii inaunganisha Makao Makuu ya Wilaya ya Mbarali na miji midogo ya Rujewa na Ubaruku pia inaunganisha Makao Makuu ya Wilaya na Barabara Kuu ya Makambako kwenda Mbeya (*Tanzania Highway).*Kutokana na umuhimu wa barabara hiyo, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara imekuwa ikiifanyia matengenezo ya aina mbalimbali barabara hiyo ili iendelee kupitika wakati wote. Kuanzia mwaka wa fedha wa 2004/2005 hadi 2006/2007, matengenezo ya kawaida ya barabara yote na ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa jumla ya kilometa 5 yamefanyika. Kiasi cha shilingi 97.966 milioni kimetumika kugharamia kazi hiyo. Ili kutimiza ahadi ya Serikali ya kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami, Wizara yangu itaanza kutenga fedha kwa awamu kwa miaka ijayo kadri uwezo wa kibajeti utakavyoruhusu.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Ninashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu nina swali moja la nyongeza.Kwa kuwa hii barabara kama alivyokiri mwenyewe imeshagharimu shilingi 97.966 na mwaka huu kwenye Bajeti yake Wizara imetenga shilingi milioni 20. Sasa ni gharama kubwa sana na akizungumzia ni zaidi ya kilomitai 18. Ninachokizungumzia hapa kuunganisha Makao Makuu ya Wilaya ambayo ni kilomita 4 tu. Sasa ninachomwomba Waziri aniahidi kuanzia Bajeti hii ataongezea kiasi gani ingawa imeshapita kuna milioni 20 lakini ili hizo kilomita 4 tu kutoka pale barabara kuu kwenda pale kwenye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Naomba anipe hiyo ahadi kama atatekeleza.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Wizara imeshapita na fedha zilizotengwa kwa ajili ya barabara zimeshaelezwa. Siwezi nikaahidi kwamba ndani ya Bajeti ya mwaka huu kunaweza kuwepo na hela yoyote. Lakini kama ikitokea basi tunaweza tukaangalia. Lakini kitu ambacho naweza kuwa na hakika nacho ni fedha kuanzia Bajeti inayofuata.

Na. 310

**JKT Kuwajenga Vijana Kiuzalendo**

**MHE. AME PANDU AME** aliuliza:-

Kwa kuwa, Jeshi la Kujenga Taifa limeanzishwa kwa lengo la kuwajenga vijana kiuzalendo na Kiutaifa pamoja na kuwafunza vijana mafunzo ya awali:-

(a) Je, Serikali inaelewa kuwa, vijana hao hufunzwa pia matumizi ya silaha, na wakati huo huo si vijana wote hupata ajira katika vyombo vya Ulinzi na Usalama, hali inayoweza kuchangia ongezeko la uhalifu?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha hali hiyo?

(c) Je, Serikali haioni kuwa, sasa umefika wakati wa kuchukua vijana wachache watakaoweza kuajiriwa katika Vyombo vya Ulinzi na Usalama?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mbunge wa Jimbo la Nungwi, lenye sehemu (a), (b), na (c) napenda kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 1963, Serikali ilianzisha Jeshi la Kujenga Taifa kwa lengo la kuwapatia vijana mafunzo na malezi bora. Mafunzo ambayo hujenga moyo wa uzalendo, uvumilivu na mapenzi ya kulitumikia Taifa. Aidha, vijana waliojiunga na JKT, pia hupatiwa mafunzo ya uzalishaji mali ambayo yanalenga katika kuwawezesha vijana kujitegemea, kwa kujiajiri wenyewe na hatimaye kumudu vyema maisha yao.Baada ya maelezo hayo, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Ame Pandu Ame, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inaelewa kuwa vijana wanaopata mafunzo kupitia JKT pia hufunzwa matumizi ya silaha na ni kweli kwamba siyo wote wanaopata ajira katika vyombo vya ulinzi na usalama. Aidha, vijana wa JKT wanapokuwa mafunzoni pia hupewa mafunzo ya ufundi wa fani mbalimbali, jambo ambalo huwapa vijana hao nafasi ya kujiajiri na kuwawezesha kuishi kwa kujitegemea. Napenda kulifahamisha Bunge lako

Tukufu kuwa, vijana hawa ni kikosi cha akiba, kwa maana hiyo, mafunzo ya matumizi ya silaha yana umuhimu mkubwa kwa nchi yetu. Kwa upande wa ajira, vijana wengi waliopitia JKT wamepata ajira katika taasisi mbalimbali, ndani ya nchi na nje ya nchi, na wengine hawana ajira za kudumu, lakini ni raia wema na wanaheshimu sheria za nchi. Uhalifu unaofanywa na baadhi ya vijana ni hulka ya mtu binafsi na wala haitokani na kupitia mafunzo ya JKT. Kijana aliyefuzu vyema mafunzo ya JKT, hatarajiwi kujishughulisha na vitendo vya uhalifu.

(b) Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuimarisha zaidi Jeshi la Kujenga Taifa, ili liwe na uwezo mzuri wa kuwaandaa vijana katika kuipenda nchi yao. Pia kuweza kuanzisha vikundi vidogo vidogo vya uzalishaji mali ili viwe chachu ya kujitegemea. Kufanya hivyo kutapunguza pia idadi ya vijana wasio na ajira.

(c) Mheshimiwa Spika, lengo kuu la kuanzishwa JKT sio kuwaandaa vijana kwa ajili ya kupata ajira katika vyombo vya ulinzi na usalama, bali ni kuwafanya wawe na moyo wa kulitumikia Taifa lao na kuwawezesha ili waweze kujitegemea zaidi. Ajira katika vyombo vya ulinzi na usalama itapatikana pale tu itakapotokea nafasi na ni kwa wale wenye sifa zinazohitajika na vyombo hivyo.

**MHE. AME PANDU AME**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba sasa umefika wakati wa vyombo vyote vya ulinzi na usalama pamoj na makampuni ya ulinzi binafsi kuajiri vijana kutoka JKT? Swali la pili ili kuwafanya vijana wetu wawe wazalendo zaidi wale wanaotaka kujiunga na vyuo vikuu. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba vijana hao wapitie JKT kwanza ndipo wajiunge na vyuo vikuu.

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA**: Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira kama nilivyoeleza katika Jibu langu la msingi Serikali tayari imeshatoa mwongozo kwa vyombo vya ulinzi na usalama kwamba wanapopata nafasi za ajira waajiri kupitia JKT. Lakini kama nilivyoeleza, waajiri kwa mujibu wa sifa zinazohitajika na vyombo hivyo. Kuhusu makampuni binafsi ya ulinzi tutashauriana na Wizara husika yanayosimamia makampuni binafsi ili na wao walione hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la vijana wanaojiunga na Chuo Kikuu wapitie JKT kabla ya kujiunga na vyuo vikuu. Sheria iko wazi, Sheria yetu inawataka vijana wafanye hivyo lakini kutokana na ufinyu wa Bajeti na upungufu wa miundombinu na kwa uwezo alipewa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa tumeghairisha lakini tunatarajia kwamba kuongeza makambi ya JKT hadi itakapofika mwaka 2010 vijana wote watapita JKT kabla ya kujiunga na Chuo Kikuu. (*Makofi*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa hivi sasa kumekuwa na vijana wengi sana wanaojiunga na siasa na wengine wameweza kuwa viongozi kama Wabunge na kadhalika na wengi hatukupata nafasi ya kupita JKT kwa hiyo unakosekana uzalendo na ujasiri ambao unahitajika kwa mtu kuwa kiongozi. Je, Wizara haioni kwamba ni wakati

mwafaka kuanzisha porogramu maalum kwa Wabunge wote ambao hawakupita JKT wapite JKT? *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA**: Mheshimiwa Spika, tunao utaratibu wa kujitolea. Kama ombi hili ni la makini kabisa kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge tunalipokea na tunalifanyia kazi na tunaandaa *programme* ambayo inaweza ikawafaa Wabunge ambao wapo tayari kwenda kujitolea.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umekwisha. Matangazo machache, kwanza ni wageni.

Waheshimiwa Wabunge ninafurahi sana asubuhi hii katika *Speaker's Gallery* kumtambulisha kwenu mmoja wa Watanzania mashuhuri sana, ambaye amehusika katika mambo mengi ya Maendeleo na siasa katika nchi yetu na si mwingine ni Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba. (*Makofi*)

Hahitaji utambulisho mrefu na maneno mengi zaidi wengi wetu ambao tumefanya naye kazi tunapenda kutamka kwamba tunaendelea kumshukuru kwa mchango wake kwa taifa na tunamwomba Mwenyezi Mungu aendelee kumpa maisha marefu kwa sababu mchango wake unahitajika sana. Karibu sana Mheshimiwa Joseph. (*Makofi*)

Mheshimiwa Ponsiano Nyami Mbunge wa Nkasi anaye mgeni wake Bwana Nimrod Kaishozi, ambaye ni Mjumbe wa TUGHE Taifa na ni Katibu Tarafa wa Tarafa ya Namanyere. Naomba asimame yule pale. Karibu sana na pole na safari ndefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya anao wageni ambao ni wanae Yohana Fidelis Owenya na Lucia Owenya naomba wasimame. Yupo mmoja tu. Ahsante karibu sana.

Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni ameniomba nimtambulishe mgeni wake Bwana Alexander Bosmask kutoka G*eorge Town University* Marekani. *I'm not sure Sir if you can follow swahili language but you are warmly welcome to Dodoma and Tanzania in general. We are very happy to see you and obviously you love Tanzania and send good news to all your fellow Americans. Thank you*. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Muhonga Said Ruhwanya, ni mdogo wake anaitwa Zena Ruhwanya. Karibu sana sijui na wewe unafuata nyayo hizo hizo au wewe unafanya mambo mengine. Kama unafanya mambo mengine, lakini dada hapa anafanya kazi nzuri ya siasa.

Wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba au Katiba na Sheria chochote ilivyo ni Mheshimiwa Marry Nagu ni wajumbe wa Umoja wa Wanawake Tanzania kutoka Mkoa wa Manyara. Naona wamewahi kwenye mkutano, hata hivyo tunawakabisha.

Wageni wa Mheshimiwa John Paul Lwanji ni Bwana Michael Mnyabai, Katibu Kata wa Kata ya Sanjaranda. Nilidhani Saranda kumbe kuna Sanjaranda pia. Sisi tumezoea Saranda pale kwa tunaotumia reli na huwa tunapata wali pale lakini kuna uvumi Mheshimiwa Mbunge kwamba kile kinachoonekana kuwa ni kuku wa kukaanga mara nyingine ni kunguru na vitu vingine kwa hiyo sijui, naomba utusaidie tusije tuka…(*Kicheko*)

Mheshimiwa Charles Keenja, wageni wake kama ifuatavyo, Mwalimu Juma Nchimbi naona hawa wanatoka Jimboni kwake hawa wanapita Ikamba naomba wasimame tafadhali. Mwenyekiti, wa Tamasha la Michezo Bwana Emmanuel Itatiro, Katibu wa CCM Tawi la Kikuyu na Bwana William Manyama, Katibu wa CCM Tawi la Madale. Karibuni sana. *(Makofi)*

Hawa pia ni wageni kutoka *Kikuyu Development Association* ambayo Mheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa ni mlezi wake. Kumbe mzee wetu ndiyo mlezi wa asasi hiyo. ahsante sana mkamsalimiea sana Mzee Kawawa na tunaendelea kumtakia Afya njema.

Pia tunao wanafunzi kutoka shule ya msingi ya Jenerali Msuguli Dodoma, naomba wasimame na walimu wao. Karibuni sana Walimu na wanafunzi wa shule ya Jenerali Msuguri. Nina hakika kwa jina hili shule hii itakuwa inaongoza hapa Dodoma kwa nidhamu kwa sababu Jenerali Msuguli ni hodari sana katika nidhamu. Karibuni sana. (*Makofi*)

Pia tunao wanafunzi kutoka shule ya Kiwandani sijui ni shule ya sekondari au, wamesema tu shule ya Kiwandani Morogoro, wale pale. *Smart* kabisa naona hii ji shule ya msingi. Karibuni sana kutoka Morogoro, tunaomba mtakaporejea muwasalimu Wazazi. *(Makofi)*

Tunataka vijana wa Kitanzania msome kwa bidii kweli kweli. Nchi yetu inahitaji Maendeleo na Maendeleo yanapatikana na watu waliosoma vizuri. Basi tunawatakia kazi njema na safari njema kurudi Morogoro. *(Makofi)*

Matangazo mengine, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mwenyekiti, wa *APNARC* ameniomba nitangaze kwamba Jumapili tarehe 29 saa tano asubuhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa kutakuwa na uzinduzi wa Ripoti ya Utawala Bora Rasilimali watu katika Maendeleo ya Taifa. Kwa hiyo, Wabunge wote waliomo katika Mtandao wa *APNAC* wanaombwa kuhudhuria ili washuhudie uzinduzi wa taarifa hiyo muhimu.

Waheshimiwa Wabunge, kesho tarehe 28 saa tatu asubuhi katika ukumbi huo huo wa Pius Msekwa, itaendeshwa Semina inayohusu masuala mbalimbali ya watu wenye ulemavu. Taasisi inayohusika inaitwa *The Disabled Organization for Legal Affairs and Social Economic Development.* Sasa kulingana na hali yenyewe ya Taasisi hii utaratibu wetu ule wa kawaida hautakuwepo. Kwa hiyo, ni muhimu tukawasikilize wenzetu katika jamii ambao ni walemavu twende tukawasikilize yale ambayo watatuambia. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nimerejea kutoka Cape Town, Afrika Kusini ni salama na nimewaacha wenzetu huko Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Omar Sheha na Mheshimiwa Susan Lyimo wanaendelea vizuri sana wanachangia vizuri katika mada zilizoko huko na kama kawaida tumeendelea kuonyesha kwamba Tanzania tuna Wabunge Makini na wengi wa Wajumbe kutoka Nchi mbalimbali hizo za *CPA* walikuwa na hamu sana ya kuongea na sisi na tumefanya nao hafla na kadhalika.

Tumewawakilisha vizuri, tuwaombee wenzetu waliobaki huko warudi salama siku ya Jumapili.(*Makofi*)

Kutokana na kutokuwepo kwangu Ofisini nalazimika nikaangalie kidogo mambo yalivyo. Kwa hiyo, namwomba sasa Naibu Spika, aweze kuja ili aweze kuendeleza shughuli za asubuhi hii.

*Hapa Naibu Spika, (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti.*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, habari ya asubuhi tunaendelea na kazi. Katibu endelea na *Order Paper.*

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2007/2008**
**Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko.**

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maandalizi ya hotuba hii, Wizara yangu imefuatilia kwa karibu changamoto na masuala ya msingi yanayoihusu Wizara yangu yaliyoainishwa katika Hotuba za Bajeti za Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, pia Bajeti ya Waziri wa Fedha, hotuba za Bajeti za Mawaziri Mipango, Uchumi na Uwezeshaji; Kilimo, Chakula na Ushirika, Miundombinu, Mifugo, Maji Nishati na Madini na Maliasili na Utalii. Wakati wakiwasilisha hotuba zao za bajeti katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nawapongeza kwa hotuba zao nzuri zilizoweka mwelekeo na dira ya Bajeti ya Serikali katika mwaka wa fedha wa 2007/2008. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa masuala na changamoto hizo zimezingatiwa katika hotuba hii ya bajeti ya Wizara yangu ninayoiwasilisha leo katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi ya pekee kumpongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake iliyofafanua majukumu na mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Nne katika kusukuma mbele maendeleo ya wananchi wa Tanzania. Aidha, nawashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote waliotangulia kutoa hotuba zao ambazo zimefafanua mafanikio, shabaha na malengo ya sekta zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa William Shellukindo, ambao wamechambua kwa kina mapendekezo ya Bajeti ya Wizara hii na kutoa ushauri na maelekezo muhimu. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba hoja na michango ya Kamati imezingatiwa katika bajeti ninayowasilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, ambaye alikuwa Waziri wa Wizara hii kabla ya kuhamishiwa Wizara ya Nishati na Madini; Mheshimiwa Dr. David M. David, ambaye alikuwa Naibu Waziri wa Wizara hii kabla kuhamishiwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; na Ndugu Wilfred L. Nyachia ambaye alikuwa Katibu Mkuu wake kabla ya kuhamishiwa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa kuweka misingi mizuri walipoanzisha Wizara hii mpya. Aidha, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Rombo kwa kuendelea kunichagua na kunipa ushirikiano mkubwa kama Mbunge wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha napenda kuwashukuru wafanyakazi wenzangu wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko nikianzia na Mheshimiwa Hezekiah N. Chibulunje, Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko; Dr. Stergomena L. Tax, Katibu Mkuu; Dr. Florens M. Turuka, Naibu Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko; Wakuu wa Idara na watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake. Pia napenda kuzishukuru jumuiya mbalimbali za viwanda na wafanyabiashara, na taasisi nyingine zisizo za kiserikali kwa michango yao katika kuendeleza Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko. Vile vile, napenda kumshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuwezesha kuchapisha hotuba hii kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuungana na Waheshimiwa Mawaziri wenzangu katika kumpongeza Mtanzania mwenzetu Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, kwa kuteuliwa kushika wadhifa mkubwa wa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Kutokana na uwezo wake mkubwa, nina imani kuwa atatekeleza kikamilifu wajibu wake huo mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kipindi cha bajeti cha mwaka jana, tumeshuhudia matukio mbalimbali hapa Bungeni. Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Wabunge wapya ambao ni Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba (Mbunge wa Kuteuliwa); Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya Viti Maalum) na Mheshimiwa

Mtutura Abdallah Mtutura (Mbunge wa Tunduru). Aidha, napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wapya ambao ni Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Burian, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Bunge; Mheshimiwa Bernard K. Membe, kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa; Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, kuwa Naibu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji; na Mheshimiwa William Ngeleja, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

Aidha, nawapongeza waheshimiwa wabunge waliochaguliwa na Bunge lako kuiwakilisha nchi yetu katika Bunge la Afrika ya Mashariki, ambao ni Mheshimiwa Dr. Didas John Masaburi, Dr. Aman Walid Kabourou, Mheshimiwa Dr. George Francis Nangale, Mheshimiwa Sylvia Kate Kamba, Mheshimiwa Isaack Sepetu Nassoro, Mheshimiwa Abdallah Ali Hassan Mwinyi, Mheshimiwa Dr. Said Gharib Bilal, Mheshimiwa Janet Deo Mmari na Mheshimiwa Dr. Fortunatus Rwanyatika Masha. Ninawatakia mafanikio katika majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa majonzi makubwa, naungana na wenzangu katika kuwaombea marehemu Juma Jamaldin Akukweti aliyekuwa Mbunge wa CCM, Jimbo la Tunduru, na marehemu Amina Chifupa Mpakanjia, aliyekuwa Mbunge wa CCM (Viti Maalum). Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko katika Mwaka 2006/2007. Malengo ya Bajeti ya mwaka 2006/2007, yalizingatia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005 na utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini (MKUKUTA) ambapo Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko zinatakiwa kuwa miongoni mwa mihimili mikuu katika kukuza uchumi na kuondoa umaskini kwa kuifanya Tanzania ifikie kiwango cha kati cha maendeleo ya uchumi wa viwanda *(semi industrialised economy*) kama ilivyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025. Ili kuweza kufikia lengo hilo, Sekta ya Viwanda inatakiwa kukua kwa asilimia 15 ifikapo mwaka 2010, na Sekta za Biashara na Masoko zinatakiwa ziiwezeshe nchi kunufaika na fursa za masoko na mifumo ya biashara za kikanda, kimataifa na utandawazi. Aidha, Sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko inatakiwa kuboresha miundombinu ya masoko na mifumo ya upatikanaji na utoaji taarifa za biashara na masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza malengo ya Wizara yangu katika mwaka 2006/2007, Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda; Sera ya Taifa ya Biashara; na Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo zimezingatiwa kama miongozo mikuu ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu ililenga kuweka mkazo katika kuanzisha viwanda mama, kwa kutafuta wabia wa kuwekeza katika mradi wa makaa ya mawe ya Mchuchuma, mradi wa chuma wa Liganga na tafiti za miradi mingine iliyo katika Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara. Aidha, Wizara yangu ililenga katika kuimarisha usindikaji, kuhamasisha uanzishaji wa Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (*EPZ*), na kuendelea kuwezesha ubunifu na uenezaji wa

teknolojia zinazofaa vijijini ili kurahisisha kazi ya uanzishaji wa viwanda vidogo, hususan vya usindikaji ili kuongeza thamani ya mazao na bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ililenga vile vile katika kufanya utafiti wa maendeleo ya Viwanda, kuandaa taarifa kuhusu fursa za uwekezaji katika miradi ya maendeleo ya viwanda, kutekeleza Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta ya Ngozi, kuimarisha taasisi za utafiti na maendeleo, kuandaa Mkakati wa Kukuza Mauzo Nje, kuandaa Sera ya Kuendeleza Masoko ya Kilimo, na kushirikiana na Sekta Binafsi katika kubuni mikakati ya kuendeleza sekta ya viwanda, biashara na masoko kwa lengo la kukuza mchango wa sekta hizi katika maendeleo ya uchumi wa Taifa. Aidha, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara yangu ililenga kukamilisha maandalizi ya Sheria ya Uandikishaji wa Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara iliendeleza na kuboresha mfumo wa ukusanyaji; uchambuzi na usambazaji wa taarifa za masoko; kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa masoko ya kimataifa ya mazao na bidhaa za kilimo ya Segera na Makambako; kufanya tathmini ya uboreshaji wa miundombinu ya masoko; na kuwaelimisha wadau kuhusu maendeleo na fursa za masoko zilizopo ndani ya nchi na nje. Aidha, Wizara iliendelea kuimarisha uwezo wa Halmashauri na Manispaa wa kukusanya na kusambaza taarifa za masoko; kuendeleza utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani; na kuendeleza jitihada za kukuza soko la ndani kwa kukuza matumizi ya mazao na bidhaa mbalimbali zinazozalishwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo kwa mwaka 2006/2007, Wizara iliweka msukumo katika kuhamasisha uanzishaji na uimarishaji wa viwanda vidogo na biashara ndogo; na utoaji wa huduma zinazolenga katika kuchochea kuanzishwa na kuimarisha viwanda vidogo na biashara ndogo hususan katika nyanja za ufundi, mafunzo, ushauri; kuboresha ubora wa bidhaa na kupanua wigo wa masoko. Aidha, Wizara iliendelea kuimarisha upatikanaji wa mitaji; usambazaji wa teknolojia zinazofaa kwa lengo la kuongeza tija na kuongeza nafasi za ajira na kipato, hususan kwa wanawake na vijana. Vile vile, kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa, Wizara kwa kupitia *SIDO* ililenga kuanzisha vituo vya biashara katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya wajasiriamali wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapitio ya Utekelezaji ya Mwaka 2006/2007 na Mipango ya Mwaka 2007/2008 Katika Sekta za Viwanda, Biashara Na Masoko. Sekta ya Viwanda mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa umeongezeka kutoka shilingi bilioni 200.8 mwaka 2005, hadi shilingi bilioni 218.1 mwaka 2006 kwa kigezo cha bei za mwaka 1992. Mchango huo umeongezeka kutoka asilimia 9.0 mwaka 2005 hadi asilimia 9.2 mwaka 2006. Ongezeko hilo limetokana na kukua kwa uzalishaji wa baadhi ya bidhaa viwandani zikiwemo unga wa ngano, nguo, mabati, chuma, saruji, bia, sigara na rangi za ujenzi kama ilivyoonyeshwa katika. Hata hivyo, ukuaji wa Sekta ya viwanda uliathiriwa na tatizo kubwa la uhaba wa umeme lililolikabili Taifa katika mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu kwa kushirikiana na Taasisi ya Takwimu ya Taifa *(National Bureau of Statistics)* imefanya utafiti katika sekta ya viwanda kwa mikoa yote 21 ya Tanzania Bara kwa lengo la kukusanya takwimu, kujua hali halisi ya maendeleo ya viwanda na kubainisha changamoto zinazokabili sekta ya viwanda. Utafiti huo umebainisha kwamba katika kipindi cha utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda (*SIDP*) tangu mwaka 1996 hadi sasa, kumekuwa na ongezeko la uanzishwaji wa viwanda vipya na ufufuaji wa viwanda vingi vya zamani vya umma ambavyo vimebinafsishwa. Aidha, kwa sasa asilimia 97.6 ya viwanda vipo mikononi mwa sekta binafsi. Vile vile, utumiaji wa uwezo *(Capacity Utilization)* katika sekta ya viwanda umekua kutoka wastani wa asilimia 37 mwaka 2005, hadi wastani wa asilimia 43 mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mwelekeo wa uzalishaji katika sekta umeonyesha mabadiliko katika uongezaji wa thamani ya mazao. Asilimia 53 ya viwanda vilivyotembelewa vinatengeneza bidhaa *(manufacturing)* badala ya kufanya usindikaji wa awali tu. Hali kadhalika, imebainika kwamba uzalishaji katika viwanda vingi ni kwa ajili ya soko la ndani. Hii ni changamoto kwa Wizara na Sekta binafsi kuweka mikakati ya kubadilisha hali hiyo ili kuwa na viwanda ambavyo vitakuza mauzo nje. Masuala mengine yaliyothibitishwa na utafiti huo ni pamoja na ongezeko la ajira katika sekta ya viwanda kutoka watu 88,713 mwaka 2005 hadi watu 93,426 mwaka 2006 sawa na ongezeko la asilimia 5.3, na ongezeko la mauzo ya bidhaa za viwanda, hususan katika soko la ndani. Hata hivyo, suala la tija katika sekta ya viwanda limeonekana kuwa changamoto kubwa kwa sekta hiyo. Tija bado ni ndogo katika viwanda vingi na inatofautiana kati ya sekta na sekta. Hata hivyo, tija ni ya kiwango cha juu katika viwanda vipya ikilinganishwa na viwanda vya zamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti huo pia umethibitisha kuwepo kwa rasilimali nyingi ambazo ni hazina kubwa ya malighafi ya kuvutia wawekezaji kwa viwanda mbalimbali vinavyoweza kuanzishwa hapa nchini. Hii ikiwa ni pamoja na mazao ya kilimo, madini, misitu, mifugo na maliasili. Hata hivyo, pia zipo changamoto nyingi zilizobainishwa ambazo zinakwamisha maendeleo ya viwanda katika mikoa mingi ya Tanzania, jambo ambalo linadhihirishwa na viwanda vingi kuanzishwa katika mikoa michache pamoja na kwamba malighafi za viwanda hivyo zinapatikana katika mikoa yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hizo ni pamoja na uhaba wa umeme; miundombinu duni; gharama kubwa za kufanya biashara; uhaba wa huduma za maji; teknolojia na utaalam hafifu; matatizo ya upatikanaji wa mitaji na kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania. Changamoto hizo zimethibitishwa na utafiti uliofanyika. Ripoti ya utafiti huo imechapishwa na itasambazwa kwa wadau mbalimbali. Zoezi hilo ni endelevu na litafanyika kila mwaka kwa kutegemea hali ya Bajeti.

Takwimu na taarifa katika ripoti hiyo zitatumika katika kuboresha *industrial database.* Ili kupambana na changamoto hizo, Wizara itaandaa mkakati kabambe na unganishi wa kuendeleza sekta ya viwanda nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto hizo, nafurahi kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, kutokana na juhudi za uhamasishaji wa kuanzisha viwanda zinazofanywa na Serikali kwa kushirikiana na wadau mbali mbali, miradi 66 ilipewa leseni za kuanzisha viwanda vipya na kufanya upanuzi kati ya mwaka 2005 hadi Machi, 2007. Kati ya hivyo, viwanda 48 tayari vimekamilika na kuanza uzalishaji ambapo vimeajiri watu 4,337. Aidha, viwanda vilivyobaki viko katika hatua mbalimbali za ujenzi. Kati ya viwanda 66 vilivyopewa leseni, viwanda 41 ni vya usindikaji wa mazao ya kilimo, maliasili na misitu. Viwanda vingine ni katika sekta ndogo za chuma, rangi na karatasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine itaandaa mkakati unganishi na mpango kabambe wa kuendeleza viwanda nchini. Katika maandalizi ya mkakati na mpango huo, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itarejea na kuendeleza utekelezaji wa *Basic Industry Strategy (BIS),* ikiainishwa na Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda. Utekelezaji wa mkakati na mpango huo utashirikisha wadau mbalimbali, hususan Serikali na sekta binafsi. Serikali itakuwa chachu ya kuhamasisha wawekezaji wa nje na ndani kuwekeza katika viwanda, na vilevile kuendelea kuweka mazingira bora ya kuendeleza viwanda. Aidha, katika kutekeleza mkakati na mpango huo, zitabuniwa mbinu madhubuti za kuwawezesha wananchi. Wizara itaendelea pia kukusanya taarifa na kuboresha takwimu kuhusiana na maendeleo ya viwanda na kufanya uperembaji wa maendeleo ya viwanda, hususan viwanda vilivyobinafsishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Wizara kupitia Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje *(Export Processing Zones Authority - EPZA)*, iliendelea kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha viwanda na kuwekeza katika Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (*EPZ*), ambapo katika kipindi hicho viwanda vitano vilianzishwa chini ya mpango huo. Viwanda hivyo ni kiwanda cha kutengeneza madini ya risasi cha *Metrec International Ltd* (Dar es Salaam); kiwanda cha kutengeneza nyuzi maalum za katani cha *21st Century Holdings Ltd (Dar es Salaam);* kiwanda cha kutengeneza maji mazito ya matunda *(juice concentrates)* cha *Unnat Fruits Processing Ltd* (Morogoro) na viwanda vya kutengeneza mavazi vya *CAMI Apparels Ltd na Kibotrade Textile Ltd (Dar es Salaam).* Aidha, makampuni matatu yamepewa leseni ya kujenga miundombinu ya *EPZ* ambayo ni *Unnat Fruit Processing Ltd (Morogoro), 21st Century Holdings Ltd (Dar es Salaam*) na *Kibotrade Textile Ltd (Dar es Salaam).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutenga maeneo kwa ajili ya kuendeleza viwanda na biashara ni muhimu sana katika kuvutia wawekezaji. Aidha, wawekezaji wengi hupenda kuwekeza katika maeneo ambayo tayari yana miundombinu muhimu kama barabara, umeme, maji, na mawasiliano. Wizara, kupitia Mamlaka ya *EPZ*, kwa kushirikiana na Mikoa mbali mbali, imeweza kubainisha maeneo makubwa kwa ajili ya *EPZ* katika mikoa ya Mara, Pwani, Morogoro, Arusha na Kilimanjaro. Katika mwaka 2007/2008, moja ya vipaumbele vya Wizara itakuwa ni kuendelea kushirikiana na Wizara nyingine, Mikoa, wadau na taasisi ili kupata maeneo kwa ajili ya kuendeleza viwanda na biashara na masoko. Aidha, Wizara itaweka mkazo katika kuhamasisha uwekezaji kwenye

miundombinu muhimu katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kuendeleza viwanda na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia uamuzi wa Serikali, na kwa kuzingatia umuhimu na uharaka wa kufanikisha uwekezaji katika viwanda mama, Wizara hii, kupitia Shirika la Maendeleo la Taifa *(National Development Corporation-NDC)*, inaendelea na mchakato wa kiushindani wa kutafuta wawekezaji watakaowekeza katika mradi wa makaa ya mawe ya Mchuchuma na wawekezaji watakaoshirikiana na Serikali kufanya utafiti zaidi katika mradi wa chuma cha Liganga ili kubainisha aina, kiasi na thamani ya madini yaliyopo ya Chuma, Vanadium, Titanium n.k.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia, watateuliwa wawekezaji kuanza uchimbaji wa chuma na makaa ya mawe katika vilima vidogo vilivyopo kwa utengenezaji wa sponge iron na hatimaye bidhaa za chuma. Utengenezaji wa chuma kwa kutumia chuma cha mlima wa Liganga utafanyika baada ya kukamilisha uchambuzi wa chuma cha Liganga ambao umekuwa ukiendelea. Uwekezaji katika maeneo haya unasimamiwa na Kamati ya Kitaasisi ambayo imekwishaundwa kufuatia uamuzi wa Baraza la Mawaziri. Kamati hiyo inajumuisha wataalam kutoka Wizara ya Fedha; Mipango, Uchumi na Uwezeshaji; Viwanda, Biashara na Masoko; Nishati na Madini; Miundombinu; Ardhi na Maendeleo ya Makazi; Katiba na Sheria na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (*TIC*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia ubia kati ya *NDC* na Kampuni ya *TATA Chemicals* ya India, utafiti unaendelea kufanywa juu ya ubora na upatikanaji wa magadi chini ya mradi wa magadi *(Soda Ash)* katika Ziwa *Natron*. Aidha, inakadiriwa kuwa kiasi cha dola za kimarekani milioni 300 zitawekezwa na kiwanda kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani milioni moja za magadi kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara itaweka msukumo zaidi katika utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri kuhusu miradi ya makaa ya mawe ya Mchuchuma na chuma cha Liganga, hususan Mpango wa Kasi Mpya ili kuhakikisha kwamba wawekezaji wanapatikana na utekelezaji wa miradi hiyo unaanza. Miradi ya makaa ya mawe, chuma na magadi itaendelea kupewa kipaumbele kwani ni kichocheo kikubwa katika maendeleo ya viwanda nchini. Miradi hiyo itahamasisha uwekezaji katika viwanda vya kutengeneza mashine, mitambo, vipuri na bidhaa za kemikali ambazo zitachangia katika kuendeleza viwanda na sekta nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, *NDC* kwa kushirikiana na wadau wengine ndani ya Serikali na kutoka sekta binafsi, itaendeleza kazi za kuibua na kuendeleza viwanda mama na miradi mikubwa ya kiuchumi, ikiwa ni pamoja na usindikaji wa mazao na ufufuaji wa viwanda mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia, iliendelea na juhudi za kutekeleza mkakati wa kufufua na kuendeleza Sekta na viwanda vya Ngozi. Kufuatia uamuzi wa Serikali, umeanzishwa mfuko ambao utatumika kutekeleza mpango mkakati wa kufufua na kuendeleza sekta na viwanda vya ngozi. Mfuko huo unasimamiwa na Wizara ya

Maendeleo ya Mifugo na unaitwa *Livestock Development Fund* badala ya *Leather Development Fund.* Mpango-Kazi umekwisha andaliwa na utekelezaji utaanza katika mwaka wa fedha 2007/2008. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili 2007, mfuko huo umekusanya jumla ya shilingi bilioni 4.045.

Kazi zitakazotekelezwa na Wizara yangu kwa kutumia mfuko huo ni pamoja na kufufua vituo vya mafunzo ya utengenezaji wa bidhaa za ngozi vya Dar es Salaam na Morogoro; kuimarisha Chuo cha Taaluma ya Ngozi cha Mwanza (*TILT*); kufanya tathmini ya bidhaa za ngozi na viwanda vya ngozi vilivyobinafsishwa; kufuatilia upatikanaji wa ngozi; na kuimarisha Chama cha Wadau wa Ngozi (*LAT*) ili kiweze kusimamia kikamilifu maendeleo ya sekta ya ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nyingine za Mfuko huo ambazo zitatekelezwa na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo ni kuboresha ubora wa ngozi kwa kutoa elimu kwa wafugaji, wachinjaji, wachunaji na wakaushaji wa ngozi; kuimarisha makusanyo ya ngozi; kuweka viwango vya ubora wa ngozi; kufanya marekebisho ya sheria ya ngozi na kufuatilia utekelezaji wake. Lengo ni kuhakikisha viwanda vya kusindika ngozi vinapata ngozi za kutosha na bora ili kuuza ngozi zilizosindikwa nje badala ya ngozi ghafi na hivyo kuwaongezea wafugaji kipato, kukuza mauzo nje na hivyo kuliingizia taifa fedha za kigeni.Viwanda Vidogo Na Biashara Ndogo

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuchochea uanzishaji na uimarishaji wa jasiriamali ndogo, katika mwaka 2006/2007, Wizara iliendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo. Hii ikiwa ni pamoja na kuimarisha utoaji wa huduma katika nyanja za uendelezaji wa teknolojia, utoaji wa mafunzo na upatikanaji wa masoko, habari na mitaji. Kwa kutambua umuhimu wa kupeleka huduma kwa wananchi mahali walipo, na huduma za kuwawezesha wajasiriamali kuanzisha miradi yao vijijini; *SIDO* ilitoa mafunzo ya uhunzi kwa vikundi 841, na mafunzo ya useketaji *(handloom weaving)* kwa wajasiriamali 100 katika mikoa ya Mwanza, Tabora, Dar es Salaam, Arusha na Morogoro. Aidha, mafunzo ya kusindika ngozi yalifanyika kwa vikundi 12 katika mikoa ya Manyara, Singida na Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika, mafunzo ya ujasiriamali yaliyolenga kutoa ujuzi maalum katika uzalishaji mali kama vile usindikaji wa ngozi; utengenezaji wa chaki; ubanguaji korosho; utengenezaji vyakula vya mifugo; utengenezaji wa bidhaa za mianzi; ufinyanzi; kuhifadhi na kusindika vyakula vya aina mbalimbali yalitolewa kwa wajasiriamali 3,397. Vilevile, Halmashauri ya Biashara ya Nje (*BET*) ilitoa mafunzo kwa wavuvi na wafanyabiashara wadogo wa mkoani Kigoma kuhusu njia bora za ukaushaji, ufungashaji na uhifadhi wa dagaa kwa ajili ya soko la ndani na la nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya kwanza, Wizara iliandaa maadhimisho ya "Mwezi wa Mwanamke Mjasiriamali" katika harakati za kukuza maendeleo ya ujasiriamali kwa wanawake, wakiwemo wenye ulemavu na wanaoishi na Virusi vya UKIMWI. Maadhimisho hayo yalifanyika mwezi Novemba 2006, katika mikoa ya Pwani, Mbeya, Morogoro, Tanga na Dar es Salaam. Katika maadhimisho hayo,

wanawake wajasiriamali walipata fursa ya kuonesha bidhaa, na kushiriki katika warsha zilizowapatia mafunzo ya ubora wa bidhaa, ujasiriamali, umuhimu wa kutumia vyombo vya habari katika biashara, uongozi na kubadilishana uzoefu. Zaidi ya wajasiriamali 1,000 walifaidika. Aidha, kwa njia ya maadhimisho kama haya, walengwa wameendelea kuboresha bidhaa zao, kugundua na kuzitumia fursa zilizopo, na hivyo kukuza masoko ya bidhaa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (*TIRDO*) ilitoa mafunzo kwa mafundi na vikundi vya wajasiriamali kwa lengo la kueneza teknolojia mbalimbali zilizobuniwa na kuthibitika.

Mafunzo yaliyotolewa ni pamoja na kusindika matunda; utengenezaji wa wanga kutokana na zao la muhogo kwa matumzi ya viwanda na matumizi mengine; urejelezaji wa taka za plastiki; kutengeneza chaki; kukausha dagaa kwa vikausho vinavyotumia mwanga wa jua na utengenezaji wa chumvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji na usambazaji wa teknolojia ni muhimu kwa maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo. Wizara imeendelea kujenga uwezo wa taasisi za utafiti wa kubuni na kutengeneza teknolojia muafaka. Teknolojia zilizobuniwa na kutengenezwa na taasisi hizo, hususan Kituo cha Maendeleo ya Teknolojia Vijijini *(Centre for Agricultural Mechanisation and Rural Technology - CAMARTEC)* na Shirika la Huduma za Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania *(Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organization - TEMDO)*, zimesambazwa ili ziweze kuzalishwa na kutumika kibiashara. Pamoja na wadau wengine, *SIDO* imesambaza teknolojia mpya, zikiwemo za ubanguaji wa korosho; usindikaji wa muhogo; ukamuaji wa mafuta; usindikaji wa matunda na mboga; utengenezaji wa matofali ya bei nafuu na umeme wa mionzi ya jua.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ili kuendeleza ubunifu katika ujasiriamali, Serikali imeanzisha utaratibu wa kulea na kukuza wabunifu kwa kupitia utaratibu wa viatamizi *(Technology and business incubators).* Utaratibu huo kwa sasa unatekelezwa na *SIDO, TEMDO, TIRDO* na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Asasi zisizo za Kiserikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Serikali ikishirikiana na taasisi za utafiti na *SIDO* itaendelea kuhamasisha na kuendeleza ubunifu na kusambaza teknolojia muafaka. Teknolojia hizo ni pamoja na mitambo ya uchimbaji mdogo; vifaa vya ujenzi; ukamuaji mafuta ya mbegu; zana za kusindikia mazao ya kilimo; asali na bidhaa zake; teknolojia ya kupunguza matumizi ya kuni na mkaa. Aidha, Programu ya viatamizi itaendelezwa ili kuwezesha wananchi kushiriki katika kuibua mawazo ya bidhaa mpya. Vilevile, Serikali itaendelea kujenga vituo vya biashara kwa ajili ya wajasiriamali wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia nyingine ya kuwaendeleza wajasiriamali wadogo ni pamoja na kuwawezesha kushiriki katika maonesho. Katika mwaka 2006/2007, jumla ya maonesho 13 ya bidhaa za wajasiriamali wadogo yalifanyika kikanda na kuwashirikisha wajasiriamali 1,030. Maonesho hayo yameleta mafanikio makubwa

kwani yamewawezesha wajasiriamali kutambua matakwa ya soko, kuboresha viwango na pia yaliwapa fursa ya kutangaza na kupata masoko ya bidhaa zao. Katika mwaka wa 2007/2008, *SIDO* watafanya maonesho katika kanda 8. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007, *SIDO* imetayarisha toleo la pili la katalogi ya bidhaa za viwanda vidogo na biashara ndogo. Aidha, Wizara imewezesha wajasiriamali wadogo wanaozalisha bidhaa za sanaa za mikono kuanzisha Chama cha Kitaifa kiitwacho *TANCRAFT*, ambacho kwa mara ya kwanza mwaka 2006/2007 kilifanya maonesho ya bidhaa zao. Chama hicho kitawawezesha wanasanaa hao kuunganisha nguvu katika uzalishaji na utafutaji wa masoko. Vile vile, mfuko wa kusaidia wajasiriamali wadogo kuhimili ushindani ujulikanao kama *SME Competitiveness Facility (SCF)* umehudumia vikundi 45 katika nyanja mbali mbali, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa teknolojia na ushiriki katika maonesho ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na *SIDO* imekamilisha ujenzi wa vituo vya biashara vya Songea, Moshi na Babati na wajasiriamali 42 wamepata mahali pa kuoneshea na kuuzia bidhaa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutoa mikopo kwa wajasiriamali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wajasiriamali Wadogo (*National Enterpreneurship Development Fund (NEDF).* Tangu mfuko huo ulipoanzishwa mwaka 1994, hadi mwezi Machi 2007, ulikuwa umetoa jumla ya mikopo 28,847 yenye thamani ya shilingi bilioni 10.7. Aidha, mfuko huo uliwezesha kupatikana kwa takriban ajira 48,000 na kiwango cha marejesho katika mwaka 2006/07 kilikuwa wastani wa asilimia 86.8. Pamoja na utendaji unaoridhisha wa Mfuko wa *NEDF*, bado mahitaji ya mikopo ni makubwa sana ikilinganishwa na uwezo wa mfuko ambao kwa sasa unakidhi asilimia 8 tu ya maombi yanayopokelewa. Aidha, miradi 22 imenufaika kupitia Mfuko wa Dhamana ulioanzishwa mwaka 2003/2004, kwa ajili ya kuwadhamini wajasiriamali wadogo ili waweze kukopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2007/2008, huduma ya mitaji kwa ajili ya wajasiriamali itaendelea kuimarishwa, hii ikiwa ni pamoja na kuuongezea mfuko wa *NEDF* mtaji wa shilingi milioni 500. Aidha, kiwango cha juu cha mkopo kitaongezwa kutoka shilingi 500,000 kinachotolewa kwa mwombaji hadi kufikia shilingi milioni 2.5 kwa miradi ya uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa maeneo maalumu kwa wajasiriamali wadogo ni tatizo kubwa kwa maendeleo ya sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo hapa nchini. Ili kuondokana na tatizo hilo, mikoa inahimizwa kutenga maeneo maalum yanayokidhi mahitaji na kuzingatia ukuaji wa sekta kwa mujibu wa bajeti zao na kwa kuwashirikisha wananchi katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, teknolojia zinazofaa ni muhimu katika kuongeza tija na ubora wa bidhaa zinazozalishwa na wafanyabiashara wadogo. Wizara yangu kupitia taasisi zake za utafiti imekwishabuni teknolojia nyingi zinazofaa kwa wajasiriamali wadogo na wakubwa. Hata hivyo, teknolojia hizo hazijasambaa na kuwafikia walengwa.

Natoa wito kwa Halmashauri kushirikiana na taasisi hizo ikiwemo *SIDO*, ili kusambaza teknolojia hizo muhimu ambazo zitawasaidia sana wajasiriamali katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, masoko endelevu kwa ajili ya wajasiriamali wa Kitanzania yanaweza kupatikana ikiwa tutathamini na kuendeleza dhana ya: "Nunua Bidhaa za Tanzania Jenga Tanzania". Aidha, katika kuwaendeleza wajasiriamali wadogo, ni vyema wakapewa kipaumbele katika zabuni zinazotolewa na Serikali na Taasisi mbalimbali kulingana na Sera na Kanuni tulizojiwekea kama njia mojawapo ya kuwapatia masoko ya bidhaa wanazozalisha na huduma wanazotoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wajasiriamali wadogo wanashindwa kuendeleza miradi na kuanzisha miradi mipya kwa sababu ya ukosefu wa mitaji. Taasisi za fedha zimekuwa zikitoa mikopo yenye masharti magumu na hazitoi mikopo ya muda mrefu kwa maelezo kuwa walengwa hawakopesheki. Hata hivyo, hali halisi na tafiti mbalimbali zimeonyesha kwamba wajasirimali wadogo ni warejeshaji wazuri wa mikopo. Kwa misingi hii, ninavihimiza vyombo vya fedha vikubali kutoa mikopo kwa sekta hii ambayo ndiyo tegemeo la wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefikia makubaliano na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya *Kilimo (International Fund for Agricultural Development (IFAD)* kuhusu kuanzishwa kwa programu ya kuendeleza viwanda vidogo na biashara ndogo vijijini ijulikanayo kama "Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini (MUVI)." Programu hiyo ambayo itagharimu shilingi bilioni 25 itaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2007/2008, na kuendelea kwa kipindi cha miaka saba. Mikoa itakayohusika ni Tanga, Pwani, Manyara, Mwanza, Ruvuma na Iringa. Programu hiyo inalenga kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na ufanisi wa viwanda vidogo vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Biashara. Sekta ya Biashara ya Ndani katika mwaka 2006 ilichangia kwa kiasi kidogo katika Pato la Taifa ikilinganishwa na mwaka 2005. Hali kadhalika ukuaji wa sekta hiyo ulikuwa na badiliko dogo ikilinganishwa mwaka 2005 na 2006. Hata hivyo, badiliko hili dogo kwa sekta limetokana na juhudi zilizofanywa na Serikali za kuboresha mazingira ya kufanya biashara ikiwa ni pamoja na kupitia Programu ya Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara (MKUMBITA). Hata hivyo, ukuaji wa Sekta hiyo bado ni mdogo. Hii inatokana na changamoto mbali mbali zinazoikabili sekta hiyo ikiwa ni pamoja na uchanga wa sekta binafsi, uhaba na masharti magumu ya upatikanaji wa mitaji, miundombinu duni hususan inayounganisha miji na vijiji na inayowezesha usindikaji (barabara, reli, maji, umeme na miundombinu ya kimasoko), uzalishaji mdogo usiokidhi mahitaji ya soko na viwango vya ubora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeandaa programu na mipango mbali mbali kupitia sekta mbali mbali na inaendelea na jitihada za makusudi za kupambana na changamoto hizo. Aidha, nawahimiza wananchi wachangamke kutumia fursa mbalimbali zilizopo na zinazojitokeza kama zile za *SIDO*, Mabaraza ya Wafanyabiashara na Mashirika yasiyo ya Kiserikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu biashara ya nje, katika mwaka 2006, mapato kutokana na mauzo ya bidhaa asilia yameshuka kwa asilimia 24.6 ukilinganisha na mwaka 2005, ambapo yameliingizia Taifa dola za kimarekani milioni 267.1 katika mwaka 2006 tu ukilinganisha na dola milioni 354.4 mwaka 2005. Kwa upande wa bidhaa zisizo asilia, mapato yaliongezeka kwa asilimia 7.4 kutoka Dola za kimarekani milioni 1,321.0 mwaka 2005 hadi Dola za kimarekani milioni 1,419.5 mwaka 2006. Ongezeko hilo limechangiwa sana na madini hasa mauzo ya dhahabu na bidhaa za viwandani. Kwa upande wa dhahabu, ongezeko la mapato lilitokana na kupanda kwa bei kwani kiasi kilichouzwa nje kilipungua. Kadhalika, mauzo ya nje ya bidhaa za viwandani yamekuwa yakiongezeka kwa wastani wa asilimia 36 kila mwaka kwa muda wa miaka miwili iliyopita isipokuwa kwa mwaka 2006 ambapo mauzo yameongezeka kwa asilimia 25.4 kutokana na upungufu wa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa manunuzi, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje mwaka 2006 zilikuwa dola za kimarekani milioni 3,864.1 ikilinganishwa na dola za kimarekani milioni 2,997.6 mwaka 2005. Hilo ni ongezeko la asilimia 28.9. Ongezeko hilo limechangiwa sana na kupanda kwa bei ya mafuta ya petroli; ongezeko la thamani ya uagizaji wa mashine na mitambo; malighafi za viwanda na bidhaa za matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Serikali iliendelea kushiriki kikamilifu katika majadiliano ya kibiashara yanayolenga kupanua fursa za masoko ya upendeleo maalum kupitia taratibu mbalimbali.

Serikali pia, iliendelea kuhamasisha sekta binafsi kutumia fursa hizo ikiwa ni pamoja na zile za kikanda *(EAC* na *SADC),* masoko ya upendeleo maalum unayotolewa na nchi za China, Japani, Kanada, Korea Kusini, Jumuiya ya Ulaya, na fursa zitokanazo na mikataba ya nchi na nchi. Juhudi hizo zimejumuisha pia matumizi ya fursa za masoko zitokanazo na matokeo ya majadiliano ya kimataifa yanayoratibiwa na Shirika la Biashara la Dunia (*WTO*).

Mheshimiwa Naibu Spika, ushiriki wetu katika Jumiya ya Afrika Mashariki umeendelea kuimarika mwaka hadi mwaka hasa baada ya kusainiwa kwa Itifaki ya Umoja wa Forodha. Katika kutekeleza Itifaki hiyo, tumeendelea kuondoleana ushuru wa forodha hasa kwa bidhaa kutoka Kenya, ikizingatiwa kwamba bidhaa za nchi nyingine wanachama ikiwemo Tanzania hazitozwi ushuru katika soko la Afrika Mashariki; kurazinisha taratibu na nyaraka za kiforodha; na kuondoleana vikwazo visivyo vya ushuru *(Non-Tariff Barriers),* hali ambayo imeiwezesha Tanzania kuongeza mauzo zaidi katika soko la Jumuiya. Kwa mfano mwaka 2006, Tanzania imeuza bidhaa zenye thamani ya dola za kimarekani milioni 117.7 ikilinganishwa na dola za kimarekani milioni 96.4 mwaka 2005, ikiwa ni ongezeko la asilimia 22.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*), nchi wanachama zimeendelea kupunguziana vikwazo vya kiushuru vyenye lengo la kufikia eneo huru la biashara ifikapo Januari 2008. Mchakato huo umeanza tangu mwaka 2000 na Tanzania imekuwa ikipata fursa zaidi kwa utaratibu huo.

Mauzo ya bidhaa zetu kwenye soko hilo yameongezeka kufikia dola za kimarekani milioni 341.1 mwaka 2006 ikilinganishwa na dola za kimarekani milioni 322.3 mwaka 2005, ikiwa ni ongezeko la asilimia 6.0. Ni mategemeo ya Wizara yangu kuwa mauzo yataongezeka zaidi tutakapofikia hatua ya kuwa eneo huru la biashara. Mchakato wa kufunguliana biashara za huduma *(Trade in Services)* unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania, chini ya kundi la *SADC-EPA*, imeendelea kushiriki katika majadiliano ya ubia wa kiuchumi (*EPAs*) na *EU* yanayolenga kuingia mkataba wa kuanzisha eneo huru la biashara kati ya nchi za Afrika, Karibiani na Pasifiki (*ACP*), na Jumuiya ya Ulaya. Majadiliano hayo yanategemewa kukamilika ifikapo tarehe 31 Desemba 2007. Mkataba wa makubaliano kutokana na majadiliano hayo utaanza kutekelezwa Januari 2008, ambapo nchi za Jumuiya ya Ulaya zitaanza mara moja kufungua masoko yake kwa bidhaa za nchi za *ACP* bila ushuru wala ukomo *(Duty free, Quota free -DFQF).* Nchi wanachama wa *SADC-EPA* na EU wamekubaliana maeneo ambayo wataingia mkataba; majadiliano yanaendelea kwa maeneo mengine kwa lengo la kufikia makubaliano kwa muda uliopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya China kupitia mpango wake wa *Special Preferential Tariff Treatment* imeipatia Tanzania pamoja na nchi nyingine za Afrika fursa ya kuuza aina 440 za bidhaa nchini mwao bila ushuru wala ukomo kuanzia Januari, 2006. Mwaka 2006, makampuni 20 ya Tanzania yaliuzia China bidhaa 187 zenye thamani ya dola za kimarekani milioni 12.1. Aidha, mwezi Juni, 2007 ujumbe wa wafanyabiashara na wawekezaji 405 kutoka jimbo la Guangdong – China ulitembelea Tanzania. Ujumbe huo na wafanyabiashara wa Tanzania walikutana na kujulishana fursa zilizopo katika pande zote mbili na kufanya makubaliano mbalimbali ya kibiashara ya awali yenye thamani ya Dola za kimarekani milioni 54.8. Tanzania itaendelea kutoa umuhimu mkubwa sana kwenye uhusiano wake wa kibiashara na uwekezaji na China na nchi nyingine za Asia na Mashariki ya Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2006/2007, Wizara ilishiriki katika kikao cha Kamati ya Pamoja ya Biashara baina ya Tanzania na India ambapo India, pamoja na mambo mengine, ilikubali kutoa wawekezaji wa viwanda na bishara na pia utaalam kwa Tanzania katika uzalishaji wa chuma *(sponge iron)* kwa kutumia makaa ya mawe na udongo wa chuma Wilayani Ludewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Tanzania ilitiliana saini mikataba ya kibiashara na nchi za Comoro, Burundi, Rwanda na Uturuki kwa nia ya kukuza biashara. Aidha, katika juhudi za kupanua wigo wa soko na kuepuka kuendelea kutegemea masoko asilia ya nchi za Ulaya Magharibi, Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano wa kibiashara na nchi ambazo ni masoko ya kutegemewa, hususan nchi za Mashariki ya Mbali na Mashariki ya Kati. Katika juhudi hizo mwaka 2006/2007, Japani na Korea Kusini ziliipatia Tanzania fursa za kuuza bidhaa 128 na 87 mtawalia katika masoko ya nchi hizo bila kutozwa ushuru. Kwa mfano, katika mwaka 2006, Tanzania iliuza bidhaa zenye thamani ya dola za kimarekani milioni 82.0 katika nchi ya Japan ukilinganisha na mauzo ya dola milioni 68.7 mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi za Serikali za kuboresha mazingira ya biashara, na kuongezeka kwa mauzo katika masoko haya, takwimu hizi zinaonyesha kuwa bado Watanzania hatujatumia ipasavyo fursa za masoko, ikiwa ni pamoja na fursa za upendeleo. Mfano hai ni ule wa soko la *AGOA* ambapo katika mwaka 2006 Tanzania iliuza bidhaa zenye thamani ya dola za kimarekani milion 4.2 ukilinganisha na dola za kimarekani milion 4.0 mwaka 2005. Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai kwa Watanzania tuzitumie fursa hizo ili kuboresha maisha yetu, na wakati huo huo kuendeleza uchumi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imeendelea kushiriki kikamilifu katika majadiliano ya duru la Doha yanayoendelea chini ya Shirika la Biashara la Dunia (*WTO*). Majadiliano katika duru la Doha yalisitishwa mwezi Julai mwaka 2006 kutokana na tofauti zilizojitokeza kati ya nchi zilizoendelea na zinazoendelea, hususan katika ufunguaji wa masoko kwa mazao ya kilimo kutoka nchi zinazoendelea na suala la uondoshwaji wa ruzuku kwa wakulima wa nchi zilizoendelea. Kutokana na juhudi za kidiplomasia, nchi wanachama wa *WTO* zilikubaliana kufufua tena majadiliano mwezi Februari mwaka huu. Kwa ratiba iliyopo, majadiliano hayo yanatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba 2007. Kama tunavyofahamu, majadiliano katika duru la Doha yanagusa maeneo nyeti kwani yanagusa maisha ya kila siku ya mwanadamu duniani, hususan maisha ya mwananchi kutoka nchi maskini ambaye anaathirika sana na mbinu za kulinda masoko. Hivyo ni muhimu kuchambua kwa makini na kutoa mwanya wa kujadili zaidi ili kufikia makubaliano yenye manufaa kwa makundi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Oktoba 2006, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ziliwasilisha na kutetea sera zao za biashara katika Bodi ya Shirika la *WTO* kwa ajili ya kuangalia ni kwa kiwango gani zimerazinishwa. Katika mkutano huo ilibainika kuwa, nchi hizo zina zina sera zenye mwelekeo mzuri wa biashara na kupongezwa. Hii ni moja ya matakwa ya *WTO* kwa nchi zinazounda Umoja wa Forodha kuwezesha nchi hizo kushiriki majadiliano ya *WTO* kama kundi moja badala ya nchi moja moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2006/2007, kituo cha Biashara cha Tanzania kilichopo London, Uingereza, kiliendelea kubainisha na kutoa taarifa za fursa za masoko na uwekezaji kwa wafanyabiashara wa Uingereza na Ulaya ikiwa ni pamoja na kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo Tanzania. Katika juhudi hizo, Tanzania imeanzisha kituo kingine cha biashara na uwekezaji huko Dubai kwa ajili ya kutafuta masoko muhimu ya kutegemewa *(potential and emerging markets*) na kupata wawekezaji kutoka katika nchi za Uarabuni na Mashariki ya Kati kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za kupanua wigo na kukuza mauzo nje kwa madhumuni ya kupunguza urari hasi, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo na wadau wengine imeidhinisha uchambuzi wa kina wa Mchango wa Sekta za Kiuchumi katika Kukuza Mauzo (*Diagnostic Trade Integration Study (DTIS)* ambao unabainisha maeneo ya kipaumbele katika kuchangia ukuaji wa uchumi wetu. Uchambuzi huo umetoa mapendekezo yanayolenga kukuza uzalishaji na mauzo nje kwa kujenga uwezo wa ushindani kwa kuanzia na sekta ndogo sita zilizopewa kipaumbele

ambazo ni madini, samaki na mazao yatokanayo na samaki, kazi za mikono, mazao ya mboga, matunda na maua, utalii pamoja na mazao asilia. Utekelezaji utaanza katika mwaka 2007/2008.Ili kuleta matokeo ya haraka katika kupanua wigo na kukuza mauzo nje na urari hasi wa biashara, Wizara yangu kwa kushirikiana na wizara nyingine ambazo ni wadau wa sekta zilizoainishwa inaendelea na maandalizi ya utekelezaji wa Mpango-Mkakati wa kuongeza uzalishaji na kukuza mauzo nje katika mwaka wa fedha 2007/2008. Mkakati huo utabainisha maeneo yatakayoleta matokeo ya haraka *(quick wins),* na mikakati ya muda wa kati na ya muda mrefu *(targeted strategic interventions).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkazo umewekwa kwenye usindikaji wa mazao kwa kutatua matatizo ya msingi na kuleta matokeo ya haraka. Katika hatua za mwanzo zitakazoleta matokeo ya haraka katika kukuza mauzo nje na kupunguza urari hasi, mazao, bidhaa na huduma zitakazolengwa ni pamoja na zao la korosho, kahawa, pamba, matunda, maua na mboga mboga, asali, nyama, ngozi, utalii, na vito vya thamani. Mkakati huo pia utalenga zaidi kuingia kwenye masoko mapya na yanayokua kwa haraka, ikiwa ni pamoja na masoko katika nchi jirani, Ghuba ya Uarabuni, Mashariki ya Kati, na Mashariki ya Mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika karne hii, taarifa ni muhimu sana na ni msingi katika kusukuma maendeleo ya kiuchumi. Kama ilivyo kwa nchi nyingine duniani, uchumi wa Tanzania unaongozwa na mfumo wa kimataifa wa uzalishaji na biashara ambao ni wa ushindani mkubwa na unaozingatia uchumi-elimu *(knowledge economy)* badala ya uchumi bidhaa *(commodity economy).* Mfumo huo unahitaji wazalishaji na wafanyabiashara kwenda na wakati ili kuweza kuwaridhisha wateja kwa kubuni mawazo mapya na uzalishaji wa bidhaa mpya za kulingana na mabadiliko na mahitaji ya soko. Ili kukabiliana na matakwa hayo, nchi haina budi kutumia mtandao wa taarifa wa kisasa ili kutabiri mabadiliko, mwenendo katika masoko, viwango vya ubora, mahitaji na matakwa ya bidhaa na huduma, mwenendo wa gharama za uzalishaji, na mwenendo wa bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Wizara yangu itajenga mfumo wa mawasiliano wa ukusanyaji, uchambuzi, na usambazaji wa taarifa na takwimu, utakaounganisha wadau mbali mbali ndani na nje *(Global Electronic Data Interchange Network)*. Wizara itatoa pia kipaumbele katika kuvutia wawekezaji ili kuanzisha miji/vitovu vya kibiashara *(trade hubs).*

Aidha, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu inatarajia kukamilisha mazungumzo na wawekezaji kwa lengo la kuanzisha kituo cha kwanza cha kibiashara cha kimataifa *(satellite town and trade hub).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itaendelea kujihusisha na utekelezaji wa Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kuingia katika Soko la Pamoja. Vile vile, Wizara itaendelea na ukamilishaji wa taratibu za kuingia eneo huru la kibiashara katika Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*). Kadhalika, tutaendelea na ukamilishaji wa majadiliano ya Ubia wa Uchumi na Jumuiya ya nchi za Ulaya *(Economic Partnership Agreement (EPA)* ili kufikia makubaliano ifikapo Desemba 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara itaendelea kuhamasisha wafanyabiashara kutumia kikamilifu fursa za masoko nafuu zilizotolewa. Vilevile, Wizara itakamilisha mikataba ya biashara na nchi za Algeria, Malawi, Mauritius, Zambia na Zimbabwe. Aidha, Serikali itatilia mkazo zaidi masoko ya nchi za Mashariki ya Mbali na Kati kwa kupeleka ujumbe wa wafanyabiashara na wawekezaji na kuhudhuria maonesho ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Masoko. Katika mwaka 2006/2007, Wizara iliandaa Rasimu ya Sera ya Masoko ya Mazao na Bidhaa za Kilimo inayolenga kutoa mwongozo wa kuboresha mfumo wa masoko ya mazao na bidhaa za kilimo. Wizara itakamilisha Sera hiyo katika mwaka 2007/2008 na kuandaa Mkakati wa Utekelezaji, kuhamasisha umma pamoja na kuisambaza Sera hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine katika Sekta ya Kilimo kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Programme (ASDP)* na Programu ya Kuendeleza Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo *(Aagricultural Marketing Systems Development Programme (AMSDP)* imeendelea kuboresha mfumo wa masoko yenye ushindani; ushirikishaji wa sekta binafsi katika kukuza masoko; kuhamasisha masoko ya vyama vya wazalishaji wadogo wadogo; kuunganisha wazalishaji na masoko ya ndani na nje ya nchi; kuimarisha uwezo wa wadau katika shughuli za masoko na kuongeza ubora wa bidhaa wanazozalisha nchini. Katika kutekeleza hayo, mfumo wa kutoa taarifa umepanuliwa kutoka masoko 75 mwaka 2005/2006 hadi 96 mwaka 2006/2007, utangazaji wa bei za mazao sasa unafanywa mara tatu kwa juma katika vyombo vya habari ikiwa ni pamoja na redio na magazeti na matumizi ya ujumbe mfupi wa maneno kupitia simu za kiganjani. Aidha, mfumo wa ufuatiliaji na tathmini unaandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na athari za kushuka kwa bei ya mazao, Wizara imekamilisha Kanuni za kutekeleza Sheria ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala. Katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itaendelea na mchakato wa kuunda Bodi ya kusimamia mfumo huo *(Tanzania Warehouse Licensing Board).* Mfumo huo umeshaanza kutumika katika mazao ya pamba, kahawa, mpunga na mahindi. Maandalizi ya kutumia mfumo huo katika zao la korosho yanaendelea. Matumizi ya mfumo huo kwenye zao la korosho yataimarisha ushindani katika soko; upangaji wa madaraja ya korosho; na yatawezesha viwanda vya korosho kupata malighafi katika kipindi chote cha mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Biashara ya Nje *(BET)* ilichukua hatua za makusudi kuitangaza kahawa ya Tanzania katika maonesho ya *World Trade Week* yaliyofanyika New York, Marekani mwezi Mei, 2007. Maonesho hayo yalikuwa na mafanikio makubwa ambapo kahawa ya Tanzania ilipokelewa vizuri sana. Jitihada hizo zitawezesha kuongezeka kwa mauzo ya kahawa yetu katika soko la Marekani siku zijazo. Ni makusudio yetu kufanya maonesho mengine kama haya kwa zao hili na mengineyo ili kupata masoko katika nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ukusanyaji wa taarifa za mifugo uliongezwa kutoka kwenye minada mitano mwaka 2005/2006 hadi minada 14 mwaka 2006/2007. Vile vile, Wizara ilitoa mafunzo kwa wakusanyaji wa taarifa hizo na kuwapatia vitendea kazi. Lengo ni kuimarisha uwezo wa Halmashauri wa kukusanya taarifa ili tuweze kukusanya taarifa kutoka katika Wilaya zote nchini. Hali kadhalika, wigo wa usambazaji wa taarifa za bei za mazao umepanuliwa kwa kutumia njia mbalimbali. Katika mwaka 2007/2008, Serikali itaendelea kupanua wigo wa taarifa kwa kuongeza aina ya taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia imehamasisha jamii ya wafanyabiashara na wazalishaji kuhusu fursa na mahitaji ya masoko kupitia warsha, mafunzo, vipeperushi mbalimbali na Maonesho ya Kimataifa ya Saba Saba na Nane Nane. Wizara itaendelea na uhamasishaji na uelimishaji umma juu ya fursa za masoko zilizopo ndani na nje ya nchi. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha na kuhamasisha soko la ndani kwa ajili ya kukuza matumizi ya mazao na bidhaa mbalimbali zinazozalishwa nchini.

Natoa wito kwa Watanzania wenzangu kuongeza kasi na uzalendo wetu wa kuthamini zaidi mazao na bidhaa zetu zinazozalishwa nchini ambazo zinaendelea kuboreshwa na wazalishaji wetu wa ndani ili kupambana na changamoto za utandawazi unaoleta ushindani mkubwa. Kauli mbiu ni "Nunua bidhaa za Tanzania jenga Tanzania".(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kuwa miundombinu ya masoko ya mazao nchini inaendelezwa, Wizara katika mwaka 2006/2007 imeanza kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa masoko ya kimataifa *(Integrated International Markets)* ya mazao ya kilimo katika miji midogo ya Makambako na Segera. Kazi hiyo inaendelea na inatarajiwa kukamilika katika robo ya kwanza ya mwaka 2007/2008.

Baada ya hapo, Wizara kwa kutumia ushauri utakaotokana na upembuzi yakinifu itawahamasisha wawekezaji pamoja na wadau wa maendeleo kushiriki katika kuendeleza masoko hayo. Aidha, katika mwaka 2007/08, Wizara itaendelea kufanya tathmini ya mahitaji ya uboreshaji wa miundombinu ya masoko ya mazao na kuzishauri Halmashauri kuendeleza miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2006/2007, ununuzi wa mazao asilia ikiwa ni pamoja na kahawa, chai, korosho, tumbaku ya mvuke, pareto na mkonge uliongezeka kwa ujumla ikilinganishwa na ununuzi katika msimu wa 2005/2006.

Katika msimu wa mwaka 2006/2007, ununuzi wa kahawa safi uliongezeka kwa asilimia 60.2, korosho asilimia 10.6, chai asilimia 13.6, tumbaku asilimia 2.6 na mkonge asilimia 7.9. Aidha, ununuzi wa pamba ulishuka kwa asilimia 65.3 na pareto kwa asilimia 42.8. Kushuka kwa ununuzi wa mazao hayo kulisababishwa na kushuka kwa uzalishaji uliotokana na baadhi ya maeneo kukumbwa na upungufu wa mvua na kuchelewa kupata pembejeo hasa mbolea na madawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu wa mwaka 2006/2007, kiasi cha mauzo nje kwa mazao ya korosho, kahawa na chai kiliongezeka, lakini kiasi kilipungua kwa mazao ya tumbaku na pamba ikilinganishwa na msimu wa 2005/2006. Hata hivyo, thamani ya mauzo nje kwa zao la tumbaku na pamba imeongezeka kutokana na kuimarika kwa bei za mazao asilia nje ya nchi.

Katika msimu wa 2006/2007, ununuzi wa ngozi za ng'ombe uliongezeka kwa asilimia 19 kufikia vipande milioni 1.9 na kondoo asilimia 7 kufikia vipande milioni 1.2, wakati ununuzi wa ngozi za mbuzi ulipungua kwa asilimia 13 kufikia vipande milioni 1.6 ikilinganishwa na msimu wa 2005/2006. Thamani ya manunuzi hayo imeongezeka kwa asilimia 40.3 toka shilingi bilioni 6.2 hadi shilingi bilioni 8.7 mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mauzo ya ngozi nje ya nchi, kumekuwa na ongezeko isipokuwa mauzo ya ngozi za mbuzi ambayo yalishuka kutoka vipande milioni 1.2 mwaka 2005 hadi vipande milioni 1.1 mwaka 2006. Kushuka huko kumetokana na ongezeko la mahitaji ya matumizi ya ngozi za mbuzi ndani ya nchi. Mauzo ya ngozi nje yameliingizia taifa jumla ya shilingi bilioni 16.1 ikilinganishwa na shilingi bilioni 7.5 mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, mauzo ya mifugo nje katika nchi za Comoro, Kenya, Burundi na Rwanda yalifikia jumla ya ng'ombe 12,118 na mbuzi 3,636 ikilinganishwa na ng'ombe 8,124 na mbuzi 308 mwaka 2005. Mauzo haya yalilipatia taifa shilingi bilioni 3.20 mwaka 2006 na shilingi bilioni 3.10 mwaka 2005, ikiwa ni ongezeko la mapato kwa asilimia 3.2.

Aidha, kuanzia mwaka 2006, Tanzania imekuwa ikiuza nyama ya ng'ombe na mbuzi katika nchi za Ghuba hasa Falme za Kiarabu na Kuwait ambapo hadi kufikia mwezi Aprili 2007, taifa limejiingizia takriban shilingi bilioni 181.0 Lengo ni kukuza mauzo ya nyama badala ya mifugo hai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Usajili wa Shughuli za Biashara. Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara *(Business Activities Registration Act),* kwa biashara zisizohitaji udhibiti ilipitishwa na Bunge lako Tukufu mwezi Februari 2007 badala ya Sheria Leseni za Biashara Na. 25 ya mwaka 1972.

Wizara inaandaa Kanuni za utekelezaji ambazo zitakamilika mwaka huu. Hata hivyo, sheria na kanuni nyingine zilizopo za leseni za biashara kwenye maeneo yanayohitaji udhibiti zitaendelea kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Usajili wa Biashara ya 2007 inaeleza kuwa vitafunguliwa vituo vya usajili wa shughuli za biashara katika kila Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji. Vituo hivyo vitasajili biashara zote ambazo zipo chini ya Mamlaka za Halmashauri ikiwa ni pamoja na biashara za mpakani, za kupeleka bidhaa nje na za kuingiza bidhaa toka nje ya nchi.

Kwa mantiki hiyo, wafanyabiashara wadogo, hususan wale wa mipakani, hawatalazimika tena kwenda Wizarani kupata leseni hizo na hivyo wataondokana na adha ya kugharamia safari kufuata leseni hizo Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara imetoa leseni 1,025 za biashara. Kati ya hizo, leseni 604 (asilimia 59) zilihusu uingizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi. Jumla ya leseni 78 (asilimia 7.6) zilitolewa kwa ajili ya uuzaji wa bidhaa nje ya nchi. Leseni zilizotolewa kwa ajili ya utengenezaji na uuzaji wa *bidhaa (manufacturing)* zilikuwa 35 ikiwa ni sawa na asilimia 3.4.

Aidha, Halmashauri zimeendelea kutoa leseni katika maeneo mbalimbali ambayo kwa utaratibu uliopo hayashughulikiwi na makao makuu ya Wizara. Wizara pia imeanzisha utaratibu wa kuweka kumbukumbu za leseni za biashara katika kompyuta ili kurahisisha utoaji wa leseni na upatikanaji wa taarifa za leseni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni *(Business Registration and Licensing Authority (BRELA)* imeendelea kusajili makampuni, majina ya biashara na alama za biashara na huduma na utoaji wa leseni za viwanda. Katika kipindi cha mwaka uliopita, *BRELA* imesajili makampuni 3,850, majina ya biashara 7,273, alama za biashara na huduma *(Trade and Services Marks)* 1,140, hataza *(patents)* 26 na leseni za viwanda 56. Aidha, katika kipindi hicho, Wakala imefuta makampuni 19 na majina ya biashara 168. Mchakato wa kuweka takwimu na taarifa za *BRELA* katika mtandao unaendelea chini ya Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia *BRELA* na kwa kushirikiana na Shirika la Miliki Ubunifu la Dunia *(WIPO)* pamoja na Tume ya Sayansi na Teknolojia wameanzisha kituo cha kutoa taarifa zilizomo katika hataza *(patent documents)* kwa watafiti wa teknolojia hapa nchini ili kulinda matokeo ya tafiti zao. Kituo hicho kilichozinduliwa mwezi Machi, 2007 ni cha kwanza na cha aina yake katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, ukiacha Afrika Kusini. Vile vile, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kuboresha masijala za kisheria za Wakala ambao unafadhiliwa na MKUMBITA kwa kuweka kumbukumbu kwenye mfumo wa kompyuta *(digitising paper records)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa ushindani, ubora wa bidhaa na huduma: Katika mwaka 2006/2007, Wizara kwa kupitia Shirika la Viwango Tanzania *(Tanzania Bureau of Standards (TBS)* imetayarisha viwango vya kitaifa vya ubora wa bidhaa 987 katika sekta za kilimo na chakula, nguo, kemikali, uhandisi na mazingira. Aidha, TBS imetoa leseni 774 za ubora wa bidhaa mbalimbali katika viwanda 447 vya humu nchini. Katika mkakati wa kudhibiti bidhaa duni kutoka nje ya nchi, leseni 9,457 za ubora wa bidhaa zilizoingizwa kutoka nje zilitolewa. Vile vile, *TBS* imechangia katika harakati za kuboresha mazingira kwa kuhakiki viwango vya majokofu ili kuhakikisha kuwa majokofu yanayoingizwa nchini hayatumii viini vya kemikali ambazo zinaleta madhara katika ukanda wa ozoni *(Ozone Layer Depleting Substances)*. Hadi kufikia mwezi Machi 2007, viwango vya Afrika Mashariki 757 viliandaliwa kwa kushirikiana na mashirika ya

viwango ya Kenya na Uganda. Pia mafunzo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati kuhusu ubora yalitolewa na jumla ya viwanda vidogo 35 vilipatiwa leseni za ubora baada ya kuthibitishwa kuwa vinazalisha kulingana na viwango vya Kitaifa. Katika mwaka 2007/2008, Kituo cha Ufungashaji kitakamilishwa. Kituo hicho kitatoa huduma za mafunzo ya kupima sampuli za viwanda vya ufungashaji kwa lengo la kuongeza ubora wa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini na kuhakiki vifungashio vya bidhaa zinazotoka nje ya nchi. Aidha, Serikali kupitia TBS inakusudia kuanzisha vituo na kuweka wakaguzi sehemu za mipakani ikiwa ni pamoja na Holili, Namanga, Tunduma na Bandari ya Tanga ili kudhibiti ubora wa bidhaa kutoka nje. Aidha, *TBS* itaendelea na juhudi za kuboresha miundombinu yake, hususan maabara, ili kukidhi mahitaji na matakwa ya soko, viwanda na biashara ya ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kupitia Tume ya Ushindani *(Fair Competition Commission (FCC),* imeanza kutoa huduma kwa Baraza la Kushauri Mlaji ili hatimaye kuwe na asasi au umoja wa kitaifa unaojitegemea wa kutetea maslahi ya mlaji nchini. Aidha, Tume kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Dola imeanza kudhibiti bidhaa bandia zinazoingizwa nchini kwa kuzikamata na kuziharibu kila zinapopatikana.

Vile vile, katika kudhibiti ushindani, Serikali imeanzisha Baraza la Ushindani *(Fair Competition Tribunal (FCT)* ambalo kazi yake kubwa ni kusikiliza rufaa zote zinazotoka Tume ya Ushindani wa Biashara *(FCC),* Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji *(EWURA),* Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini *(SUMATRA),* Mamlaka ya Udhibiti wa Safari za Anga *(TCAA)* na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Mawasiliano *(TCRA)*. Baraza limeanza kazi hivi majuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Tume itaendelea kutangaza shughuli zake kwa Umma, kukamilisha tafsiri ya Sheria ya Ushindani katika lugha ya Kiswahili, na kurekebisha kanuni za sheria ili kurahisisha utekelezaji wa sheria ya Alama za Bidhaa na hivyo kuwezesha kupambana na bidhaa bandia kwa kasi zaidi kuliko ilivyo hivi sasa. Vile vile, Tume itashiriki katika utekelezaji wa Sheria ya Ushindani ya Afrika Mashariki, na Serikali itaboresha zaidi mfumo wa ukaguzi wa bidhaa zinazoingia nchini kwa kushirikisha sekta binafsi na kwa kushirikiana na taasisi za viwango katika nchi mbalimbali kukagua bidhaa kabla hazijaingia nchini *(Pre-Verification of Conformity to Standards).* Serikali kupitia Wakala wa Vipimo *(Weights and Measures Authority)* imeendelea kuhakikisha kuwa walaji wananufaika na vipimo sahihi vya biashara. Katika mwaka uliopita, wananchi waliendelea kuhamasishwa kuhusu matumizi ya vipimo sahihi vya shughuli za kibiashara hasa katika Mikoa ya Iringa, Mara, Mbeya na katika Wilaya za Arumeru na Monduli mkoani Arusha. Uhamasishaji huo ulifanywa na Wakala wa Vipimo kwa kushirikiana na Wakuu wa Mikoa, Wilaya na wadau wa pamba na samaki chini ya Programu ya Kuendeleza wa Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo *(AMSDP).*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tahadhari zimetolewa na Wakala kuhusu madhara ya kutumia vipimo visivyo sahihi kama vile lumbesa na kosovo katika biashara. Hatua hizo zimehamasisha wafanyabiashara kujitokeza kwa wingi katika kukagua vipimo wanavyovitumia. Vipimo vilivyokaguliwa kwa mwaka uliopita ni 426,556 ukilinganisha

na vipimo 321,742 katika mwaka 2005/2006, hilo likiwa ni ongezeko la asilimia 32.6. Ili kubaini vituo vya mafuta vinavyowauzia wateja mafuta ya petroli na dizeli kwa ujazo pungufu, Wakala imeendelea kuendesha operesheni za ukaguzi wa kushtukiza mikoani, na hasa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, usahihi wa vipimo ni suala muhimu katika uchumi wa nchi na maisha ya kila siku ya kila mwananchi. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Wakala wa Vipimo inatarajia kupima malori ya mchanga na kokoto ili wateja wafahamu ujazo halisi wa malori hayo. Maandalizi rasmi yamefanyika kwa ajili ya upimaji huo, ambayo ni pamoja na kununua vifaa na kuendesha warsha kwa wadau katika kuwaelimisha kuhusu huduma hii mpya. Upimaji wa malori ya mchanga utasaidia kupata vipimo sahihi katika sekta ya ujenzi na hivyo kupunguza athari za kufanya ujenzi hafifu unaotokana na ukadiriaji wa vipimo kama mchanga na kokoto. Katika hatua nyingine ya kuendelea kumlinda mlaji, Wakala wa Vipimo pia imeanza rasmi kutoa huduma ya upimaji wa matenki makubwa ya mafuta. Upimaji huo utaiwezesha Serikali kufahamu kwa usahihi zaidi kiasi cha mafuta yanayoingizwa nchini ili yalipiwe kodi inayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la matumizi ya vipimo batili kama lumbesa limekuwa likichangia kuongeza umaskini kwa wakulima na pia kuchangia katika uharibifu wa miundombinu na vyombo vya usafiri. Serikali inaandaa marekebisho ya kanuni husika ili kuweza kusimamia kwa ufanisi zaidi matumizi ya vipimo sahihi ikiwa ni pamoja na kukomesha vipimo batili.Wizara imeendelea kukuza na kulinda maslahi ya wasanii kupitia Chama cha Hakimiliki cha Tanzania *(Copyright Society of Tanzania (COSOTA).* Mambo muhimu yaliyofanywa na Taasisi hiyo kwa mwaka uliopita ni pamoja na kusajili jumla ya wanachama wapya 103 na kazi 1,242. Kati ya wanachama hao, wanamuziki ni 68 na waandishi wa vitabu na maigizo ni 35. Kazi za muziki zilizosajiliwa ni 1,138 na zile za vitabu na maandishi ni 104. Aidha, semina za uelimishaji kuhusu masuala ya Hakimiliki zilifanyika katika miji mbalimbali. Kutokana na juhudi hizo, *COSOTA* imegawa mirahaba ya shilingi milioni 78 kwa wanachama wake na iliendelea kusuluhisha migogoro mbalimbali baina ya wadau. Jumla ya migogoro 41 ilisuluhishwa na kumalizwa nje ya Mahakama. *COSOTA* itaendelea kusajili wanachama na kusuluhisha migogoro mbalimbali baina ya wadau wake. Aidha, kwa kuwa bado kuna uelewa mdogo wa sheria na kanuni za hakimiliki na hakishirikishi, na masuala ya Intellectual Property Rights Serikali itaendelea kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi kuhusiana na masuala hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utafiti na Maendeleo ya Teknolojia: Katika mwaka 2006/2007, shughuli za ubunifu na maendeleo ya teknolojia mbalimbali ziliendelea kutekelezwa na Kituo cha Maendeleo ya Teknolojia Vijijini *(CAMARTEC),* Shirika la Huduma za Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania *(TEMDO)* na Taasisi ya Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania *(TIRDO).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, *CAMARTEC* iliendelea kubuni na kuunda teknolojia ya trekta ndogo ya kutumika mashambani; mashine ya kukatia malisho ya wanyama *(forage chopper)* yenye kuendeshwa kwa injini ndogo; mashine ya kutengeneza siagi ya karanga; plau ya pande mbili *(reversible plough)* na teknolojia mbalimbali zinazotumia nishati jadidifu (renewable energy). Teknolojia zote

hizo zimelenga kumpunguzia mkulima harubu za kilimo na kuongeza ajira. Kituo hiki pia, kimeendesha mafunzo ya ujenzi wa mitambo ya biogas kwa wajasiriamali wajenzi kutoka wilaya za Songea, Monduli, Kibaha, Bagamoyo na Kinondoni, kupitia mpango wa uatamizi (incubation). Katika mwaka 2007/2008, *CAMARTEC* itaendelea kufanya shughuli zake za kubuni na kueneza zana bora za kilimo na teknolojia sahihi na rahisi kwa jamii inayoishi vijijini.

Katika mwaka 2007/2008, *TEMDO* itaendelea kutoa ushauri wa kihandisi kwa viwanda na kusanifu vipuri na mitambo. Aidha, Shirika pia litasambaza na kuhamasisha matumizi ya mashine na teknolojia mbalimbali za kusindika matunda, asali na maziwa, na litatoa huduma za viwandani zenye lengo la kuongeza uzalishaji wa bidhaa bora bila kuchafua mazingira na pia zinazolenga matumizi bora ya nishati. *TIRDO* itaendelea kuimarisha maabara zake ili ziweze kukubalika kimataifa *(accreditation). TIRDO* pia itaendelea kutoa elimu kuhusu mfumo wa ufuatiliaji *(traceability)* katika sekta nyingine zaidi ili kupanua wigo wa Tanzania kuelewa mfumo huo na athari zake katika masoko ya kimataifa hususan katika sekta za nyama na asali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushiriki wa Sekta Binafsi na Ubinafsishaji: Wizara iliendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kubuni mikakati ya kuendeleza sekta ya viwanda, biashara na masoko kwa lengo la kukuza mchango wa sekta hii katika maendeleo ya uchumi wa Taifa. Vikao vya pamoja vimefanywa kwa lengo la kujadili na kupata ufumbuzi wa matatizo yanayokwamisha maendeleo ya sekta na kutoa mapendekezo Serikalini. Wizara pia imekuwa ikitoa nafasi kwa sekta binafsi kushiriki katika mikutano nje ya nchi ili kubadilishana uzoefu kwa nia ya kufahamu jinsi ya kuendesha shughuli za kiuchumi katika sekta za viwanda, biashara na masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine itafanya tathmini ya viwanda vyote vilivyobinafsishwa vilivyoko chini ya sekta ya viwanda, biashara na masoko ili kupata hali halisi na kupendekeza hatua muafaka za kuchukuliwa. Katika kipindi cha 2007/2008, msisitizo utawekwa katika kukamilisha ubinafsishaji wa mashirika ambayo bado hayajabinafsishwa. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika sekta za viwanda, biashara na masoko. Msukumo mkubwa utawekwa katika kuwavutia wawekezaji toka Afrika, nchi za Ghuba na Asia kwa mujibu wa sera, sheria na taratibu zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Masuala Mtambuka, Uendeshaji na Uimarishaji wa Uwezo wa Wizara na Taasisi: Katika zoezi la kukamilisha muundo mpya wa Wizara, mwaka 2006/2007 tulijaza nafasi nne za ngazi za juu na nafasi 19 za maafisa wengine. Aidha, Wizara ilisomesha jumla ya watumishi 50 katika taaluma mbalimbali. Katika mwaka 2007/2008, tutaendelea kujaza nafasi kwa mujibu wa ikama na kusomesha watumishi katika taaluma mbalimbali kulingana na mahitaji. Aidha, Wizara itaendelea kurekebisha Sheria zilizoanzisha taasisi zilizo chini yake ili ziweze kukidhi matakwa mapya. Wizara ina jumla ya watumishi 188, kati yao wanaume ni 99 na wanawake ni 89. Katika mwaka 2007/2008, Wizara inatarajia kuajiri watumishi 54 wa fani mbalimbali. Pamoja na changamoto ya upungufu wa wataalam kiidadi, changamoto kubwa zaidi ni

ukosefu wa ujuzi na utaalamu wa kutosha kulingana na matakwa ya karne ya 21 na uchumi wa sasa ambao ni uchumi elimu *(knowledge economy).*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kati ya wanataaluma waliopo Wizarani, asilimia 60.7 wana umri zaidi ya miaka 45 na asilimia 39.3 wana uzoefu usiozidi miaka mitano. Takwimu hizi zinaonyesha wazi kuwa kuna pengo kubwa la wataalamu wa kada ya kati ambao ni muhimu kitaaluma ambao hutegemewa sana, hususan katika shughuli zinazohitaji kujituma, kufikiri na kufanya uchambuzi wa kinawa masuala mbalimbali. Wataalam hao ni kiungo kati ya uongozi na wataalamu vijana pia ni chachu ya kuendeleza wataalamu vijana ili waweze kufikia upeo wa juu. Wizara itaendelea kujenga uwezo wa wafanyakazi wake kwa njia mbali mbali. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara imetenga kiasi cha shilingi milioni 240.2 kwa ajili ya mafunzo mbalimbali. Wizara itaendelea kutoa mafunzo kadiri bajeti itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za kupambana na rushwa, Wizara na taasisi zilizo chini yake iliendelea kutoa elimu kuhusu utawala bora na huduma kwa mteja kwa watumishi na viongozi ili kuboresha huduma na kuondoa mianya ya rushwa. *(Makofi)*

Katika juhudi za kupambana na janga la UKIMWI, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Kuthibiti UKIMWI *(TACAIDS)* imekuwa ikitoa mafunzo na uhamasishaji wa njia sahihi za kujikinga na maambukizi na kupima Virusi vya UKIMWI kwa hiari. Katika mwaka 2007/2008, Wizara imepanga kutekeleza Mfumo wa ukusanyaji Takwimu za UKIMWI zisizohusiana na tiba *(Tanzania Output Monitoring System for Non Medical HIV and AIDS Interventions (TOMSHA)* ikiwa ni moja ya utekelezaji wa mwongozo wa Serikali unaohusu kusaidia watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Vile vile, Wizara itaandaa mpango wa kutekeleza utoaji huduma za lishe bora na dawa kwa waathirika kwa kuzingatia mwongozo wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara ilitoa mafunzo ya masuala ya jinsia ambapo katika mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara itaendelea kuzingatia masuala ya jinsia katika utekelezaji wa majukumu yake.Wizara ina wajibu wa kuhakikisha kuwa kuna uzalishaji bora viwandani unaotunza mazingira na kulinda afya za wafanyakazi. Wataalamu wa Wizara, kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Baraza la Mazingira *(NEMC)* na *TIRDO,* wamekuwa wakifuatilia viwanda ili kubaini matatizo ya mazingira, kutoa mafunzo ya utunzaji wa mazingira na kuchunguza mitambo kwa kuifanyia ukaguzi. Katika mwaka 2006/2007, wataalam wa Wizara kwa kushirikiana na wataalam kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Baraza la Mazingira la Taifa *(NEMC)* na *TIRDO* wamefanya ukaguzi wa mazingira katika viwanda vya *Mutex (Musoma), Karibu Textile (Dar es Salaam), Nyakato Steel (Mwanza)* na *Metro Steel (Dar es Salaam).* Aidha, Wizara imekuwa ikifanya semina kwa viongozi wa viwanda na kuwapa mbinu za uzalishaji usiotoa taka *(zero waste production strategy). (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara ilifanya semina mbili za kutoa elimu ya hifadhi ya mazingira katika uzalishaji na uzingatiaji wa Sheria ya mazingira na kanuni zake. Semina hizo zililenga kuhamasisha watumiaji wakubwa wa

kuni kuwa na mashamba ya miti na matumizi ya nishati mbadala; na kuhamasisha utumiaji wa mabomba ya chuma badala ya mirunda ya miti. Hii ilikuwa moja ya hatua ya kutekeleza mkakati wa kisekta wa kutunza ardhi na vyanzo vya maji. Aidha, baadhi ya viwanda vimeanza kutumia makaa ya mawe, mabaki ya mbao na makapi ya nafaka na mazao ya kilimo katika kuzalisha mvuke wa kuendesha mitambo badala ya kuni. Vile vile, Wizara kwa kushirikiana na *CAMARTEC* itaendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya *bio-latrine* kama nishati mbadala hasa katika taasisi zinazohudumia watu wengi kama vile shule, vyuo, magereza na hospitali. Katika mwaka 2007/2008, Wizara kwa kushirikiana na taasisi zilizo chini yake na wadau wengine itaeneza teknolojia zinazosaidia uhifadhi wa mazingira kama vile nishati jadidifu na mbadala zikiwemo biogas, bio-latrine; nishati ya mionzi ya jua na teknolojia ya kutengeneza mkaa unaotokana na vumbi la mbao pamoja na mabaki ya mimea. Uenezi utafanyika kwa kuhusisha pia vikundi vya wajasiriamali wadogo. Aidha, Wizara itatoa huduma kwa wenye viwanda zenye lengo la kuongeza uzalishaji wa bidhaa bora bila kuchafua mazingira na zinazolenga matumizi bora ya nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Changamoto Kuu za Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko: Ilani ya uchaguzi imeitaka sekta ya viwanda kuwa sekta kiongozi wa uchumi yenye jukumu la kubadilisha uchumi kuwa wa kisasa, unaojitegemea, unaoeneza teknolojia ya kisasa katika sekta zote muhimu kama vile kilimo, mifugo, maliasili n.k. Aidha, sekta ya viwanda na biashara ndizo zenye uwezekano mkubwa wa kutoa ajira nyingi, kulipa kodi kubwa kubwa Serikalini na kuondoa umaskini kwa kasi. Ili kufanikisha ukuaji wa dhati wa uchumi wetu ni lazima tuongeze zaidi uzalishaji wenye tija kubwa katika sekta zote za uzalishaji na huduma na vile vile tuongeze sana mauzo ya bidhaa na huduma hizo nje. Hali halisi kwa sasa haitoshelezi matakwa ya Ilani kutokana na changamoto nyingi zinazoukabili uchumi wetu. Changamoto hizo ambazo ni vikwazo vikubwa kwa ukuaji wa uchumi na upunguzaji wa umaskini ni:-

Uduni na ukosefu wa miundombinu inayounganisha wazalishaji na masoko ya ndani na nje. Hii ni pamoja na barabara kuu na za vijijini, umeme, reli, viwanja vya ndege, bandari, maji, mawasiliano ya simu na maeneo ya viwanda yaliyopimwa.Ukosefu wa ujuzi wa shughuli nyingi za viwanda na biashara na uwezo mdogo wa kupambana katika uchumi wa kileo wa kimataifa unaosababishwa na utandawazi.Ukosefu wa mitaji, masharti magumu ya kuweka amana na kupata mitaji kwenye mabenki na hivyo kuiweka nchi yetu kwenye hali ya kutegemea utaalamu na mitaji kutoka nje, tena kwa kubembeleza sana. Kutegemea mno wawekezaji wa nje hatimaye kuna athari zake, hasa kama uondoshaji wa fedha za kigeni utazidi ukomo unaokubalika au wawekezaji wakiamua kuondosha mitaji yao.

Uchanga wa sekta binafsi ya ndani na pia udhaifu na udogo wa soko la ndani lenyewe ambalo lazima lisaidiwe na masoko ya nje, hasa ya kikanda, ili kuvutia wawekezaji wakubwa mfano katika viwanda mama. Hali hii haina budi kufuatiliwa vizuri hasa kwa Serikali kuchukua hatua za makusudi za kuchochea na kuwezesha wawekezaji wengi zaidi wa ndani wakiwemo wajasiriamali wadogo na wakubwa katika sekta za viwanda, kilimo, mifugo, utalii, madini, maliasili, huduma na biashara. Uzoefu duniani unaonyesha kuwa kuimarisha wawekezaji wa ndani kimkakati ni mbinu muhimu ya kukuza uchumi endelevu na kuondoa umaskini.Serikali imeanza kuchukua hatua za

kukabiliana na changamoto hizi. Kwa mfano bajeti ya mwaka 2007/08 imetilia mkazo sekta za miundombinu, maji, na elimu. Hatua zilizoanza kuchukuliwa mwaka jana na kabla kukabiliana na matatizo ya umeme, kudhamini baadhi ya wakulima, vyama vya ushirika na wanaviwanda kwa njia ya credit guarantee schemes, kuleta mageuzi katika sekta ya fedha, uwekezaji viwandani kwenye maeneo ya uuzaji nje *(EPZ),* kuongeza idadi ya wanafunzi wa shule, vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu yaani rasilimali watu, ni hatua muhimu zitakazoendeleza viwanda na biashara zitakapofanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika hali hii, na ili kutekeleza matakwa ya Ilani, itabidi uwekezaji katika sekta ya viwanda na biashara na pia Wizara na taasisi za kuendeleza viwanda, uwe mkubwa kuliko ilivyokuwa miaka iliyopita. Mashirika ya *NDC, BET* na *SIDO* yatahitaji mitaji zaidi ili yaweze kuchochea na kuhamasisha ukuaji wa viwanda na mauzo ya bidhaa nje, na hivyo kuiweka sekta hii katika nafasi stahili ya kukuza na kuleta modenaizesheni ya uchumi, kuboresha maisha ya wananchi na kuifikisha Tanzania kwenye kundi la nchi zenye uchumi unaoibukia *(middle income, emerging market economy)* ifikapo mwaka 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hizi ni kubwa; zinahitaji rasilimali nyingi ikilinganishwa na zilizopo hivi sasa. Hata hivyo, Serikali itaendelea kutenga rasilimali za kutosha ili kupambana na changamoto hizo kulingana na uwezo unavyoongezeka kama mwelekeo wa sasa unavyoonyesha. Sekta binafsi inategemewa sana katika kukabiliana na changamoto hizi; Serikali itaendelea kuweka mazingira muafaka ya kisheria na kiuwezeshaji na washiriki wetu wa maendeleo, nao wana nafasi kubwa, hasa ya kuhamasisha na kuwezesha wawekezaji toka makwao, na kufungulia milango bidhaa toka Tanzania. Tunataka tufanye biashara zaidi kuliko kusaidiwa zaidi. *(Makofi)*

Namalizia kwa kuzishukuru nchi rafiki na Mashirika ya Kimataifa ambayo yamekuwa yakitoa misaada iliyoiongezea Wizara uwezo wa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na tija zaidi. Nchi hizo ni Afrika Kusini, Austria, Canada, China, Denmark, Finland, Ireland, Uswisi, India, Japan, Marekani, Sweden, Uholanzi, Uingereza na Ujerumani. Aidha, napenda kuyashukuru Mashirika ya Sida, *UNIDO, DANIDA, DFID, GTZ, ILO, IFAD, NORAD, WTO, UNCTAD, OECD, USAID, UNDP, OPEC Fund, JICA, WIPO, ARIPO, SECO, IMF* na *ITC.* Pia napenda kuzishukuru Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika na *Common Fund for Commodities* kwa misaada na michango yao ya fedha na ya kitaalamu katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara.Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2007/2008; Matumizi ya Kawaida: Wizara na taasisi zilizo chini yake inaomba kutengewa jumla ya Shilingi bilioni kumi na saba, milioni mia mbili thelathini na nne, mia tano na arobaini na saba elfu (17,234,547,000) kwa ajili ya matumizi ya kawaida ili iweze kutekeleza majukumu niliyoelezea ya kuendeleza Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko kwa mwaka wa fedha ujao wa 2007/2008. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni nne, milioni mia tano sabini na sita, mia moja hamsini na tisa elfu na mia saba (4,576,159,700) ni kwa ajili ya Wizara na Shilingi bilioni kumi na mbili, milioni mia sita hamsini na nane, mia tatu themanini na saba elfu na mia tatu (12,658,387,300) ni ruzuku kwa taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matumizi ya Maendeleo: Kiasi cha Shilingi bilioni saba, milioni mia tatu tisini na tano, mia tatu sabini na sita elfu (7,395,376,000/=)

kinaombwa kwa ajili ya shughuli za miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni moja, milioni mia mbili sitini na nne (1,264,000,000/=) ni fedha za ndani, na Shilingi bilioni sita, milioni mia moja thelathini na moja, mia tatu sabini na sita elfu (6,131,376,000/=) ni fedha za nje zitakazotolewa na Wadau wa Maendeleo. Kuhusu fedha za ndani, jumla ya Shilingi milioni mia mbili sitini na nne (264,000,000/=) zitatumika katika kugharamia shughuli za maendeleo katika taasisi zilizo chini ya Wizara, na Shilingi bilioni moja (1,000,000,000/=) zitatumika katika utekelezaji wa uanzishwaji wa maeneo maalum ya kuzalisha bidhaa za kuuza nje *(Export Processing Zones).* Fedha za nje zitatumika kwa ajili ya kutekeleza Agricultural Sector Development Programme *(ASDP);* Tanzania *Multi-sectoral HIV/AIDS Project* na Muunganisho Ujasiriamali Vijijini (MUVI). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hotuba hii, nimeambatisha majedwali mbalimbali ambayo yanatoa takwimu zitakazowawezesha Waheshimiwa Wabunge kutafakari vizuri maendeleo katika Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko. Naomba takwimu hizo zichukuliwe kama vielelezo zaidi vya hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. ABDALLAH S. SUMRY- (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA):** Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2007/2008. Naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunipatia nafasi hii adhimu ya kusimama mbele ya Bunge letu Tukufu ili niweze kutoa Taarifa, kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2007/2008 kwa Mujibu wa Kanuni Na.81 (1) ya Kanuni za Bunge – Toleo la Mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo kawaida wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara, Kamati ilizingatia vipengele vifuatavyo kuhusu Fungu 44 - Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko.

§ Dira/Mwelekeo wa Wizara kuhusu kushughulikia masuala ya Viwanda, Biashara na Masoko nchini.

§ Majukumu ya Wizara.

§ Taarifa kuhusu utekelezaji wa malengo ya Wizara katika Mwaka 2006/2007.

§ Taarifa ya Utekelezaji wa ushauri wa Kamati wakati wa kuchambua Bajeti ya Mwaka 2006/2007.

§ Maelezo kuhusu Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2006/2007.

§ Maelezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kupitia Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara na Ushauri Uliotolewa Wakati wa Mchakato wa Bajeti 2006/2007: Katika Mwaka wa Fedha wa 2006/2007 Kamati yangu ilitoa maoni na ushauri katika maeneo kadhaa. Tunapenda kuipongeza Wizara kwa hatua mbalimbali ilizofikia katika kutekeleza maoni na ushauri wa Kamati. Hata hivyo, katika maeneo ambayo yameonekana kuhitaji juhudi za uboreshaji, Kamati inaendelea kutoa ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mafanikio ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2006/2007: Kamati ilifahamishwa baadhi ya mafanikio ambayo ni pamoja na haya yafuatayo:-Mradi wa Kuendeleza Masoko ya Mazao ya Kahawa na Pamba *(Cotton and Coffee Marketing Development Project).* Shughuli zilizofanyika kupita Mradi huu ni pamoja na:-Kujenga na kuimarisha uwezo katika kusimamia matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Mazao katika Maghala. Kuwezesha maendeleo ya usindikaji na mazao chini ya mfumo wa Stakabadhi za mazao katika Maghala.Kupembua na kutathmini matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao katika maghala. Programu ya Kuendeleza

Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Programme).*Mheshimiwa Naibu Spika, Programu iliwezesha kufanikisha yafuatayo:-

Kukusanya, kuchambua na kusambaza Taarifa za Masoko ya Mazao ndani na nje ya nchi.Kuhamasisha usindikaji na ufungashaji wa mazao ya Kilimo, kufanya utekelezaji na mapitio ya makubaliano ya kimataifa kuhusu mazao ya kilimo;Kuwaunganisha wa kulima na masoko;Kuimarisha na kuhamasisha ujenzi wa miundombinu ya masoko; Kutoa mafunzo ya kitaalamu kwa Watendaji wanaoshughulikia masoko ya mazao; na Kurahisisha mfumo wa kufanya biashara ya mazao nchini (leseni za biashara).Mheshimiwa Naibu Spika Mpango Maalum wa kuendeleza Viwanda Awamu ya Pili *(Integrated Programme Phase II):* Mpango huu umesaidia kufanikisha yafuatayo:-

Kuboresha bidhaa zetu ili ziweze kupata masoko ya nje; Kuboresha maabara ya Shirika la Viwango Tanzania kufikia kiwango cha kimataifa,Kuanzisha kituo cha kusindika vyakula huko Kigoma, Kuwawezesha wajasiriamali wa Zanzibar kupata vifaa vya kusindika vyakula.Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa kuendeleza Sekta ya Biashara *(Business Sector Programme Support (BSPS II):* Mradi umewezesha kujenga uwezo wa Watanzania kama ifuatavyo:-Kutoa mafunzo ya Shahada ya Uzamili ya Biashara ya Kimataifa *(Master Programmme in International Trade)* katika Chuo Kikuu Dar es Salaam. Kusaidia juhudi za kutengeneza maabara ya Shirika la Viwango Tanzania ili ziendane na matakwa ya Kimataifa *(Accreditation).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa kupambana na Janga la UKIMWI *(Tanzania Multi-Sectoral HIV/AIDS):* Mradi huu unasaidia kuelimisha watumishi wa Wizara na Mashirika yaliyo chini ya Wizara juu ya masuala ya UKIMWI mahala pa kazi. Katika kutekeleza mradi huu kwa kipindi cha mwaka 2006/2007, Kamati imefahamishwa kuwa Wizara imeweza kufanya tathmini ya hali halisi ya ugonjwa wa UKIMWI Wizarani na kwenye Taasisi za Wizara ili kuiwezesha Wizara kupanga mikakati yake vizuri katika mapambano dhidi ya janga hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kujenga uwezo wa Watumishi: Wizara imekuwa ikiendelea na juhudi za kuendeleza Watumishi wake kitaaluma katika kuwawezesha kufanya kazi zenye ubora na kuleta tija kwa Taifa kwa kupitia Bajeti ya Wizara na Fedha za Washirika wa Maendeleo kwa kozi za muda mrefu na mfupi. Kwa mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara ilisomesha watumishi hamsini (50) katika taaluma mbalimbali kwenye vyuo vya ndani na nje ya nchi.Mheshimiwa Naibu Spika, Matatizo ya Sekta za Viwanda, Biashara na masoko: Kamati ilifahamishwa na kubaini changamoto zifuatazo kwa Wizara kama ifuatavyo:-Mheshimiwa Naibu Spika, Miundombinu duni ya masoko: Hali duni ya miundombinu ya masoko (barabara za vijijini, reli, magulio/masoko ya mazao, maghala) husababisha kuongezeka kwa gharama za kusafirisha, kuhifadhi mazao na uharibifu wa mazao baada ya mavuno. Aidha, uduni wa vifaa vya mawasiliano unachangia sana katika kudhoofisha usambazaji wa taarifa za masoko kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miundombinu duni katika maeneo ya viwanda: Kamati ilibaini kuwepo kwa miundombinu hafifu. Katika maeneo mengi ya viwanda

tuliyoyatembela, na Kamati ilishuhudia barabara mbovu ambazo zinakwamisha uchukuzi wa kuingiza malighafi Viwandani na kutoa bidhaa zinazozalishwa. Aidha, upatikanaji wa umeme na maji katika baadhi ya Viwanda nao pia haukidhi mahitaji halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kushuka kwa bei za mazao ya kilimo katika soko la dunia: Kushuka kwa bei ya mazao katika soko la dunia husababisha kuporomoka kwa bei za mazao ya wakulima na hivyo kupunguza kipato chao na ari ya uzalishaji zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ubora wa mazao: Uzalishaji wa mazao na bidhaa zenye viwango duni hukosa sifa za kuuzwa kwa bei nzuri katika masoko ya ndani na nje. Aidha, kuwepo kwa magonjwa ya mifugo kama vile ugonjwa wa bonde la ufa *(RV*F) ni kikwazo kwa biashara ya mifugo na bidhaa zake ndani na nje ya nchi. Uwezo mdogo wa kusindika mazao: Uwezo mdogo wa usindikaji wa mazao hapa nchini husababisha mazao mengi kuuzwa nje ya nchi bila kusindikwa na hivyo kulipunguzia Taifa mapato ya fedha za kigeni na ajira, mfano – Matunda yanayopatikana Tanga, Morogoro, na mikoa mingineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ufinyu wa mitaji: Pamoja na mifuko mbalimbali ambayo imeanzishwa, upatikanaji wa mitaji kwa wajasiriamali wadogo na wa kati bado ni tatizo. Pia ukosefu wa mikopo ya muda mrefu unazorotesha sana maendeleo za sekta za uzalishaji. Kuongezeka kwa Ushindani wa Biashara: Wajasiriamali wadogo wanakabiliwa na changamoto kubwa ya ushindani wa bidhaa katika soko huria hasa kutokana na viwango hafifu vya bidhaa na gharama za juu za uzalishaji wake.Mfumo wa majadiliano ya kibiashara ya Kimataifa: Mfumo, mbinu duni na uwezo mdogo katika majadiliano ya biashara ya Kimataifa husababisha nchi kukosa fursa ya kukuza biashara na Mataifa ya nje.

Uelewa mdogo wa Sheria na taratibu za biashara ya Kimataifa: Soko la Biashara ya Kimataifa linatawaliwa na Mitakaba, protokali na taratibu ambazo kwa bahati mbaya wengi wa wazalishaji na wafanyabiashara wa Tanzania hawazielewi kikamilifu. Mheshimiwa Naibu Spika, Gharama za uzalishaji Viwandani: Gharama za uzalishaji nchini ni za juu ikilinganishwa na Nchi nyingine kutokana na sababu zifuatazo:-§ Miundombinu duni inayosababisha kupanda kwa gharama za uchukuzi wa malighafi na usambazaji wa bidhaa. Gharama kubwa za huduma za kiuchumi (umeme, maji, mawasiliano) na kadhalika.Gharama kubwa za kufanya biashara ikiwa ni pamoja na mifumo ya kodi, kwa mfano *VAT* ya Tanzania ni kbwa ukilinganisha na nchi jirani za Kenya na Uganda.Ucheleweshwaji katika utoaji na uingizaji wa mizigo bandarini. Upungufu wa malighafi kama vile chuma kwa viwanda vya kuyeyusha chuma na ngozi kwa Viwanda vya kusindika ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati: Sekta a Viwanda: Wakati wa kuwasilisha Makadirio yake kwa Kamati, Wizara iliarifu kuwa, imefanya utafiti katika Mikoa yote 21 ya Tanzania bara kwa lengo la kujua hali halisi ya maendeleo ya Viwanda. Katika utafiti huo Viwanda 550 vilitembelewa. Viwanda hivyo vimeajiri Wafanyakazi wapatao 115,000. Kamati inashauri kuwa pamoja na nia njema ya Wizara katika utafiti huo ni vema Wizara ikabainisha ni viwanda gani vinaendelea vizuri na ni vipi vinasuasua. Aidha, ni vema pia Wizara ikafuatilia viwanda vilivyo binafsishwa

lakini vimetelekezwa tu bila kujali mahitaji ya Mikataba ya Makubaliano *(MOU)* kuhusu kubinafsishwa huko, kama vile viwanda vya Ngozi, viatu vya (Morogoro) pamoja na Kiwanda cha Mbao *(Mkata Saw Mill)* n.k. Inaelekea baadhi ya Viwanda vinanunuliwa tu bila ya dhamira ya kuviendeleza. Katika miaka ya Sabini (1970), Tanzania ilikuwa na Sera nzuri ya Viwanda, kama vile Viwanda Mama *(Basic Industrial Strategy),* Viwanda vya Kati. n.k. Sera hii ilitoa muelekeo rasmi katika masuala ya uendelezaji Viwanda nchini. Muelekeo wetu hivi sasa hauko wazi sana katika hili. Kwa kuwa ni ukweli usiofichika kuwa Viwanda Mama ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa, Kamati inashauri kwamba Wizara itoe kipaumbele kwenye Viwanda vya aina hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Mpira *(General Tyre East Africa):* Serikali imewekeza asilimia 74 katika Kiwanda hiki lakini uendeshaji wake unakwama kutokana na upungufu wa mali ghafi na mtaji. Kiwanda hiki kinaweza kuchangia kwa kiwango kikubwa kwenye uchumi wa nchi hii kama hatua madhubuti zikichukuliwa kutatuwa matatizo yanayo kikabili. Kamati inashauri kwamba Serikali isaidie kiwanda hiki kwa kukiongezea mtaji au kwa utaratibu wa kukidhamini kiwanda hiki ili kiweze kukopa kwenye Mabenki na Tasisi nyinginezo za fedha. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuboresha upatikanaji wa malighafi kutoka mashamba ya mpira ya Kihuhwi, Zanzibar na Kilombero ili malighafi hiyo iweze kutumika kwenye Kiwanda hiki. Kamati iliapata nafasi ya kulitembelea shamba la mpira la Kihuhwi na kupatiwa maelezo kuwa muda wa ubora wake ni mfupi na hivyo panahitajika kupanda mpira mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ina mashaka na wale wanaotaka kununua shamba hilo kwani nia yao ni kupata Ardhi tu na kuvuna mpira uliobaki na si kuendeleza mpira kama ilivyo katika mashamba ya mkonge. Vilevile Kamati inaishauri serikali kubuni njia ya kukifanya kiwanda hiki kiweze kujitegemea kwa kuzalisha mpira wake hapo baadaye.Kiwanda cha Kutengeneza Vifaa mbalimbali *(Kilimanjaro Machine Tools):* Kiwanda hiki ni muhimu kwani kinazalisha bidhaa/mashine za aina mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya viwanda vingine. Kwa muda mrefu sasa, Kiwanda hiki hakifanyi kazi zilizokusudiwa kwani kimekuwa ni Kiwanda mfu. Kamati inashauri kwamba Serikali ikifufue Kiwanda hiki kwani ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa hasa kwa sababu ni miongoni mwa Viwanda mama hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nafasi za Taasisi za Utafiti na Maendeleo: Sisi kama taifa ni vizuri tuelewe kuwa hakuna Mfadhili yeyote atakayefadhili Taasisi zetu za utafiti kwa lengo la kujinasua kutoka kwenye mfumo wa nchi yetu wa kuagiza bidhaa kutoka nje au Mataifa yanayoendelea, kwa vile kufanya hivyo kutakuwa na maana ya kujitia kitanzi kiuchumi. Kwa hiyo, Kamati inashauri kuwa Taasisi zetu zitumike kikamilifu kwa mujibu wa majukumu ya kuzianzisha ili ziwe msingi thabiti wa maendeleo ya taifa hili na hatimaye kujitosheleza kwa chakula, bidhaa muhimu, teknolojia.na kadhalika.

Kutokana na umuhimu huo Kamati inaishauri Wizara iendelee kuziwezesha taasisi za utafiti na maendeleo *(Ressearch and Development (R & D) hususani CAMARTEC, TEMDO,TIRDO,*na .kadhalika ili kutekeleza majukumu yao ya kubuni na kuhamishia nchini teknolojia sahihi na rahisi kwa maendeleo ya viwanda na sekta nyingine za uchumi kwa kuzitengea fedha za kutosha kwa matumizi ya kawaida na za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madini ya Chuma Liganga na Mkaa wa Mawe, Mchuchuma: Wakati Kamati inapitia na kujadili makisio ya Bajeti ya Fungu 44; Wizara ya Viwanda na Biashara, ilifahamishwa kwamba Wizara iliwasilisha kwenye Baraza la Mawaziri taarifa ya utekelezaji kuhusiana na miradi ya Madini ya Chuma Liganga na Baraza lilikubali ushauri wa Wizara kuanza kutekeleza miradi hiyo. Aidha, Waziri aliifahamisha Kamati kwamba Kamati ya wataalamu itakayosimamia utekelezaji wa maamuzi hayo ya Baraza la Mawaziri imekwisha undwa. Baada ya kutafakari taarifa hiyo, Kamati inashauri ifuatavyo:-

(a) Kuwepo na uwazi katika kuitisha na kuteua Wawekezaji katika mradi huo.

(b) Uwepo wa utaalamu wa kuchimba na kuchenjua madini ya aina mbalimbali yaliyotajwa kuwepo katika eneo hilo.

(c) Kuhakiki uwezo wa wawekezaji wa kifedha na uzoefu wa muda mrefu katika shughuli hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ingependa ieleweke wazi kwamba Madini yaliyopo Linganga si chuma pekee, bali pia Madini mengine kama Venadium na Titanium ambayo thamani yake ni kubwa duniani kuliko hata chuma chenyewe.Kamati inasisitiza kwamba vigezo vilivyotajwa punde vizingatiwe ili Taifa liepuke hasara kama ilivyowahi kutokea katika Miradi mingine nchini kama ule wa uzalishaji umeme kwa kutumia gesi asilia kupitia Kampuni ya *Richmond Development Corporation* ya Marekani. Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeshauri kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa ni muhimu ikashirikishwa katika miradi hiyo ya Chuma na Makaa ya Mawe na hisa zao za kushiriki zingehesabiwa kuwa ni ile thamani ya rasilimali ya ardhi iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matumizi ya Raslimali za hapa nchini: Mojawapo ya faida inayoweza kupatikana kutokana na Uwekezaji katika Viwanda hapa nchini, ni matumizi ya malighafi inayopatikana nchini. Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipotembelea Kiwanda cha Twiga *Cement* jijini Dar es Salaam ilifahamishwa kuwa katika uzalishaji wa Saruji wanatumia malighafi *(Gypsum)* kutoka Japan lakini ilifahamishwa pia kuwa *Gypsum* inayopatikana Wilayani Kilwa ina thamani, na ni bora zaidi kuliko inayoagizwa kutoka nje ya nchi. Kamati inashauri kuwa Serikali iliangalie suala hili ili raslimali yetu iweze kutumika na hivyo kutoa ajira hapa nchini na kuongeza pato la Taifa. Viwanda kuwa Chini ya Wizara ya Viwanda: Kumekuwa na mtawanyiko wa Viwanda katika Wizara mbalimbali hali inayosababisha kuzorota kwa ufanisi wa Viwanda kwa jumla. Kamati inaona kwamba ni vema Viwanda vyote vikawa chini ya Wizara ya Viwanda, na Biashara na Masoko ili uratibu wa shughuli zote za viwanda uwe rahisi na wenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Shirika la Maendeleo la Viwanda Vidogo (*SIDO*) kama vile kutoa mafunzo maalumu katika uzalishaji mali, mfano wa usindikaji wa ngozi, utengenezaji wa chaki, ubanguzi wa korosho na kadhalika lakini bado Shirika linakabiliwa na uhaba wa fedha. Kamati inaishauri Serikali ilisaidie kifedha ili liweze kutekeleza kazi zake kwa ufanisi. Aidha,

Kamati inashauri kuwa shirika liandae mkakati wa kuendelea kutoka viwanda vidogo *(small scale)* na kwenda viwanda vya kati *(medium scale)* ili kuendana na mabadiliko ya kiuchumi na teknolojia hivi sasa duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maeneo huru ya uwekezaji (*EPZ*), Kamati ilifahamishwa kuwa Wizara kupitia mamlaka ya maeneo ya uzalishaji kwa ajili ya mauzo nje *(Export Processing Zones Authority) EPZ* inaendelea kuvutia sekta binafsi kuanzisha viwanda na kuwekeza kwenye miundombinu ya *EPZ*. Aidha, Kamati imefurahishwa na namna *EPZ* inavyojitanua nchini kama tulivyoshauri hapo awali. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa *EPZ* bado inaonekana kama ni kwa ajili ya wageni kuja kuwekeza Tanzania. Hivyo, Kamati inashauri kwamba ni vema Wizara ikabuni njia na mbinu za kuwashawishi na kuwawezesha Watanzania kuchangamkia maeneo haya huru ya uzalishaji bidhaa za kuuza nje. Vile vile Kamati inashauri kwamba utengaji na ujenzi katika maeneo ya *EPZ* uhusishe taasisi nyingine kama *TANESCO, TTCL* na Wizara za Miundombinu, Maji, Mazingira na kadhalika ili kurahisisha uwekezaji katika maeneo hayo ya biashara. Aidha, Kamati inapenda kuipongeza mikoa ambayo imekwishatenga maeneo ya uanzishaji wa *EPZ* na pia kuishauri mikoa ambayo bado haijatenga maeneo haya kufanya hivyo mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na fursa zilizopo kibiashara na masoko zitokanazo na uhusiano wa Tanzania na nchi mbalimbali kama vile za soko la upendeleo la China, Japan, Korea Kusini, Jumuiya ya Ulaya (*EBA*), Marekani chini ya mpango wa *AGOA*, na kadhalika, bado fursa hizi zote hazijatumika ipasavyo. Kwa hiyo, Kamati inaishauri Wizara kwamba ni vema utafutwe utaratibu wa kuwasaidia wawekezaji/wafanyabiashara nchini ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha na kuwapa mbinu za kuuza bidhaa nje. Adha, msaada huu uwafikie wakulima walioko sehemu za vijijini ili nao waweze kushiriki katika ukuzaji wa biashara kati ya Tanzania na masoko ya nje. Chini ya mpango wa *AGOA*, bidhaa za nguo kama vile mashuka hivi sasa zimeruhusiwa. Wakati Kamati ilipotembelea mabanda ya Marekani katika maeneo ya Saba Saba, Dar es Salaam, tarehe 5 Julai, 2007 ilifahamishwa na Maafisa wa Ubalozi wa Marekani, kuruhusiwa kwa mashuka katika mpango wa *AGOA*. Kiwanda cha *NIDA* hapana nchini kinatengeneza mashuka mazuri sana na yenye ubora unaotakiwa ndani ya *AGOA*. Kamati imeshindwa kupata maelezo sahihi ya kuhusu kiwanda cha *NIDA* kutouza bidhaa hii katika soko la *AGOA*. Kamati inashauri kuwa Wizara kutazama suala hili la *NIDA* kutumia fursa hii adhimu ya *AGOA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (*EAC*) na pia ni mwanachama wa Jumuiya ya Nchi zilizo Kusini mwa Afrika (*SADC*), wakati nchi za Uganda na Kenya ambazo ni wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki pia ni wanachama wa *Common Market for Eastern and Southern Africa. (COMESA).*

Katika kushiriki kikamilifu kuendeleza majadiliano ya kibiashara yenye lengo la kukuza na kuongeza fursa za masoko ya kikanda na kimataifa *(Economic Partnership Agreements)* (*EPA*), kumekuwa na tatizo la wapi Tanzania ijikite katika majadiliano hayo muhimu kiuchumi. Kinachohitajika katika mijadala hiyo ni Tanzania kufanya

majadiliano hayo ya *Economic Partnership Agreements* (*EPA*) chini ya Jumuiya moja yenye wanachama wengi *(One Big Custom Union).* Kamati inashauri kuwa Serikali iharakishe maamuzi katika suala hili kabla ya mwisho wa mwaka huu 2007/2008 ili faida inayopatikana kupitia makubaliano hayo Tanzania inufaike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Kamati inapenda kuipongeza Halmashauri ya Biashara ya Nje *(BET),* kwa kufanikisha kwa kiwango kizuri maonyesho ya Saba Saba, 2007. Kamati iliona kuwa mpangilio wa bidhaa, ubora wa bidhaa na upangaji wa mabanda ulikuwa mzuri mno. Kwa upande wa bidhaa za wajasiriamali wa hapa nchini ambao wadogo wadogo bado wanalo tatizo la kiwango cha ufungashaji (*packaging*) wa bidhaa. Ni matarajio ya Kamati kwamba baada ya Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) kukamilisha ujenzi wa Kituo cha kufungasha (*packaging*) tatizo hili litakuwa limepatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini kuwa *BET* haina fedha za kutosha kutekeleza shughuli zake muhimu za kitaifa. Kamati inashauri kwamba *BET* ipatiwe fedha za kutosha na wafanyakazi wenye uzoefu wa kiwango cha juu katika masuala ya kibiashara ili hatimaye Tanzania iweze kukuza biashara ya nje kwa kasi kubwa. Aidha, Kamati inashauri kuwa Sheria Na. 5 ya kuanzishwa kwa *BET* iletwe Bungeni ili ifanyiwe marekebisho na hatimaye Shirika lipate fedha za kujiendesha lenyewe. . Pia Kamati inaishauri *BET* kujitanua mikoani ili iwe karibu na wananchi ambao wanahusika moja kwa moja na uzalishaji wa bidhaa mbalimbali za kuuza nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni ushauri wa Kamati kuwa Uwanja wa Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa wa Mwalimu J. K. Nyerere ufanyiwe marekebisho ili ulingane na hadhi ya kimataifa na pia uwe mahali panapoweza kutumika kwa shughuli za kijamii na uchumi kwa mwaka mzima na si wakati wa maonyesho tu. Yakifanyika marekebisho hayo yatasaidia kuongeza mapato ya *BET.* Mkakati huu mpya unaweza kutekelezwa katika muda wa kati na muda mrefu. Kamati inazipongeza juhudi za Halmashauri ya Biashara ya Nje kwa kuwaondoa wavamizi katika eneo la maonyesho. Na jitihada hizo ziendelezwe na kuhakikisha kuwa waliovamia uwanja huo wote wameondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la Viwango (*TBS*) na Ukaguzi wa Magari yanayoingizwa nchini, kumekuwa na ukaguzi wa magari nje ya nchi yanayoingia Tanzania. Wakaguzi hao wamepewa tenda ya ukaguzi huo ambao Kamati inaona ni usumbufu kwa Watanzania na ni aina fulani ya watu kujipatia kipato bure tena cha fedha za kigeni kisichofaidisha nchi. Hii ni kwa sababu tayari tunayo sheria ya kudhibiti uingizwaji wa magari chakavu ambapo *TRA* hufanya ukaguzi huo na mwenye gari hulazimika kulipa ushuru zaidi kama gari lake litakuwa ni la zaidi ya miaka kumi. Kamati inashauri kwamba ukaguzi huu usiendelee ili kutowabebesha mzigo Watanzania wanaoagiza magari kutoka nje, ila sheria tuliyoipitisha hapa Bungeni ifanye kazi yake kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifahamishwa na Wizara kwamba rasimu ya mwisho ya kitabu cha orodha ya wafanyabiashara wa mazao ya kilimo na bidhaa zake *(Tanzania Agri Business Directory)* imekamilika. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuandaa Kitabu cha takwimu hizo ambazo zitasaidia kujua idadi ya wafanyabiashara na hata kuwafikia walipo. Aidha, Kamati inaishauri Wizara kuharakisha mikakati ya kuendeleza mifugo ya masoko ya mazao ya kilimo na kukarabati miundombinu ya masoko katika Mikoa mbalimbali ambayo ni pamoja na masoko, maghala na barabara za vijiji. Aidha, Kamati inashauri vilevile ujenzi wa masoko katika maeneo ya Segera (Tanga) na Makambako (Iringa) uanze haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baaada ya mawasiliano ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ya Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka 2007/2008, kwa niaba ya Bunge lako Tukufu, Kamati ilipitia na kujadili kwa kina taarifa hizo na sasa inaliomba Bunge lako tukufu lijadili na kukubali kupitisha kiasi kinachoombwa cha shilingi 24,629,923,000/=, kati ya fedha hizo shilingi 17,234,547,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 7,395,376,000/= ni kwa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii muhimu kuwasilisha taarifa ya Kamati. Pili, napenda kumshukuru Mheshimiwa Basil Mramba, (Mb.), Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Mb., Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Katibu Mkuu na Watalaamu wote wa Wizara na Taasisi zote chini ya Wizara hiyo kwa maelezo yao ya kina na ushirikiano wa hali ya juu waliotoa kwa Kamati na hivyo kuiwezesha kutoa maoni na kushauri ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa kazi nzuri ya uchambuzi wa Makadirio ya Wizara kwa umakini mkubwa. Naomba kuwatambua kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Mohammed Amour Chomboh, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Asha M. Jecha, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Mohammed H. Mnyaa, Luhanga Mpina, Mheshimiwa Mbaruku Mwandoro, Mheshimiwa Saverina Mwijage, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Christopher Ole- Sendeka, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mheshimiwa Haji J. Sereweji, Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Mohamed S. Sinani, na mimi Mheshimiwa Abdallah S. Sumry. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka, pamoja na Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Abdallah Hancha na Ndugu Lina Kitosi, kwa kuihudumia Kamati hii kwa ufanisi mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda,

Biashara na Masoko kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. LUCY F. OWENYA – MSEMAJI WA UPINZANI WA WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba upokee shukrani zetu za dhati kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Hotuba ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2007/2008 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 43(5)(b)(c) na 81(1), Toleo la Mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nachukua fursa hii kutoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu Amina Chifupa. Natambua kuwa mimi na marehemu tulikuwa tukisimamia itikadi tofauti lakini tuliunganishwa na Utanzania wetu kwa kuweka mbele maslahi ya Taifa letu na wananchi kwa ujumla. Kwa vile Mwenyezi Mungu ameamua kuvuna kwenye shamba lake, tunamwomba ampe raha ya milele. Amina!

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwa nafasi ya kipekee kabisa kuwashukuru wanachama na wote wenye mapenzi mema na Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kwa kuendelea kutuunga mkono katika mapambano ya kumwendeleza Mtanzania. Kura zao ndizo zilizoniwezesha kuteuliwa kuwa Mbunge. Nawaahidi kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu nitaendelea kuwatumikia kwa umahiri na uadilifu mkubwa ili tufikie azma yetu ya kuleta mabadiliko ya kweli na uhuru wa kweli, uhuru unaokwenda zaidi ya uhuru wa bendera ikiwa ni pamoja na uhuru wa kujieleza bila woga. Uhuru ambao haukupatii maradhi, umaskini, ujinga na rushwa. *Inshallah* tutafika! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawajibika kwa moyo wa dhati kuwashukuru viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamadi Rashid, (Mb.) na Dr Wilbrod Slaa, (Mb.) ikiwa ni pamoja na Wabunge wengine, na wananchi, kwa ushirikiano wao mkubwa walionipa hadi kuniwezesha kusimama mbele yenu kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2007/08. Pia napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Basil Mramba, Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara, kwa kuandaa hotuba hii. (*Makofi*)

Nitakuwa sina fadhila kama sitamtaja msaidizi wangu, Mheshimiwa Khadija Al-Qassmy, (Mb.), ambaye angesaidia katika kuandaa hotuba hii lakini kwa bahati mbaya aliondoka ghafla kutokana na ajali mbaya iliyotokea Zanzibar ambapo watoto watatu walikufa na mwanae kujeruliwa vibaya. Mungu amjalie mwanae apate kupona haraka. Bila kumsahau mume wangu mpenzi, Dr. Fidelis John Owenya kwa kuniunga mkono wakati wote nikiwa ndani na nje ya Bunge hili. (*Makofi*)

Vilevile napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza kwa dhati Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri mpya ya Wilaya Tarime kwa kupata ushindi wa kishindo dhidi ya wagombea wa CCM. Matokeo yanayoifanya CHADEMA kutawala Halmashauri ya Wilaya ya Tarime. Naamini kabisa watatumia fursa hii adhimu

kuwaletea maendelea wananchi wa Tarime kama tulivyofanikiwa katika Halmashauri tunazoziongoza! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza wewe binafsi kwa jinsi unavyofanya kazi zako kwa ujasiri na umakini, na kujaribu kujenga na kuleta mabadiliko ya demokrasia ndani ya Bunge hili. Naomba salamu hizi unifikishie kwa Mheshimiwa Spika, pamoja na Wenyeviti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi lengo letu sisi wabunge ni kuhakikisha kuwa uongozi wa Serikali unakwenda vyema. Sisi kama wawakilishi wa wananchi kwa pamoja tunatoa uwezekano kwa watu wa Tanzania kutumia rasilimali za Tanzania katika kujiletea maendeleo yao binafsi na Taifa kwa ujumla. Kwa miaka takriban 46 tumeshuhudia mazuri na mapungufu makubwa katika uendeshaji wa Serikali ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa adui rushwa akiunganishwa na maadui wetu wakuu: ujinga, maradhi na umasikini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa nipitie japo kwa muhtasari tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya 2006/2007 kabla ya kutoa mapendekezo ya Kambi ya Upinzani kwa bajeti ya 2007/2008. Katika bajeti ya mwaka 2006/2007, Wizara ya Viwanda na Biashara, iliomba fedha kwa ajili ya kuendeleza miradi mbalimbali ikiwemo miradi ya Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga, *EPZ, SIDO, TIRDO,NDC, CARMATEC,TBS* na kadhalika. Hata hivyo, Wizara ya Viwanda na Biashara ilishauriwa kushirikiana na wadau wengine katika kutatua matatizo ya viwanda vilivyobinafsishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mashirika yaliyotajwa hapo juu ni yenye umuhimu mkubwa katika maendeleo ya Taifa letu katika kazi zao za utafiti na uendelezaji wa kilimo na viwanda. Lakini yamekuwa katika bajeti ya miaka yote iliyopita pamoja na mwaka huu yamekuwa yakitengewa fedha ndogo sana kuliko walichoomba. Kwa mfano *SIDO* mwaka 2006/2007 waliomba shilingi bilioni 3.99, fedha zilizotolowa na Serikali ni shilingi bilioni 1.46 tofauti ya shilingi bilioni 2.53 na mwaka huu wa 2007/2008 *SIDO* wameomba shilingi bilioni 3.99 lakini wamepewa 0.99 tofauti ya shilingi bilioni 3. Kwa mfano huu tu, Kambi ya Upinzani inahoji kama kweli maendeleo ya viwanda na kilimo yatapatikana katika Taifa letu ikiwa Serikali haiyatilii *(priority)* umuhimu mashirika haya. (*Makofi*)

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iachane na kauli zake za kawaida kuwa haina pesa. Kwa mujibu wa Hotuba ya Kambi ya Upinzani kama ilivyowasilishwa na Waziri wetu Kivuli wa Wizara ya Fedha, ilionyesha wapi fedha zilipo. Na mimi nitawaonyesha pia wapi fedha zilipo katika utendaji mzima wa sekta ya viwanda na Biashara nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *National Development Cooperation (NDC),* Wizara imeomba shilingi 1,025,000,000 kwa ajili ya *National Development Cooperation* (*NDC*). Kwa vile fedha hizi ni kidogo ukilinganisha na shughuli za *NDC*, Kambi ya Upinzani inataka maelezo ya kina kuhusu matumizi ya fedha hizi. Aidha, kulingana na maombi ya

Wizara, mradi wa Mchuchuma tu umeombewa jumla ya shilingi bilioni 1.023 kwa ajili ya mshauri kutoka India ambaye ataharakisha utekelezaji wa mpango kwa kasi mpya. Kulingana na ufuatiliaji wa mradi huo, makubaliano ya kupata mwekezaji yalikwisha kuwa katika hatua nzuri, kwa mujibu wa Kamati zilizoundwa na vilevile kwa mujibu wa taarifa ya Waziri aliyekuwepo Mheshimiwa Nazir Karamagi. Kambi ya Upinzani, inadhani kwa sasa Serikali imekosa mwelekeo katika suala hili, kwani tunaamini kabisa kuwa wataalamu waliopo chini ya usimamizi wa *NDC* walikwishatoa ushauri na mapendekezo mengi kwa maslahi ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga ina manufaa makubwa katika kuchangia ukuaji wa uchumi wa Taifa letu. Hii ni pamoja na kuzalisha umeme wa uhakika na wa kutosha kutokana na makaa ya mawe ya Mchuchuma na uanzishwaji wa viwanda mama kutokana na chuma cha Liganga. Tusisahau kuwa tafiti zilizofanywa na *NDC* zinaonyesha kuwa rasilimali tulizonazo Mchuchuma na Liganga ni adimu duniani. Makaa ya mawe ya Mchuchuma, kwa mfano, ni ya ubora wa hali ya juu unaoweza kutupatia makaa maalumu kwa matumizi ya viwandani *(industrial coal),* makaa ya kuzalisha umeme na mabaki ya makaa yaliyopunguzwa nguvu kwa matumizi ya nyumbani. *Industrial Coal* ambayo ni *high calorific value* itatumika katika viwanda vyetu vya chuma, sementi, karatasi, mbolea na kadhalika pamoja na kuuza nje ya nchi ambako kwa bei za soko la dunia za mwaka jana, tani moja ilikuwa inauzwa kwa US$ 64.72. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti zimeonyesha kuwa rasilimali iliyopo Liganga ina madini matatu kwa pamoja: (*sponge iron)* chuma cha kawaida ambacho matumizi yake wote tunayajua, (*titanium*) madini yanayotumika kwenye viwanda vya kutengenezea rangi, plastiki, magari, karatasi, nguo, *powder coating* na kadhalika, (*vanadium)* madini inayotumika katika kuzalisha chuma, na *(titanium alloys)* kwa ajili ya kutengeneza injini na fremu za ndege, mitambo ya nyuklia, roketi, vifaa vya kijeshi na kadhalika. Kwa bei za mwaka jana katika soko la dunia tani moja ya *sponge iron* ilikuwa inauzwa kwa *US$* 250 kwa tani moja, *titanium* iliuzwa kwa karibu *US$*3000 na tani moja ya *vanadium* ilikuwa kiasi cha *US$*30,000. Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwepo kwa uwazi katika kuwatafuta wawekezaji katika eneo hili ili Taifa linufaike. Wawekezaji wenye mtaji wa kutosha na utaalamu stahili wapewe kipaumbele na *NDC* wawezeshwe kushikilia hisa za asilimia 30 kwa niaba ya wananchi katika miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, ilifarijika sana mwaka jana kusikia kuwa Wizara imeteua jopo la wataalamu kupitia maombi yote ya wawekezaji na kuwapendekeza wenye uwezo huo kifedha na kiteknolojia. Wasiwasi unaanza kutupata hasa wanasiasa wanapoanza kubadilisha kauli na kuwataja wawekezaji kutoka Bara la Asia, kama suluhisho la matatizo yote ya Watanzania. Tunamtaka Waziri atueleze katika maelezo yake ya mwisho mapendekezo ya hao wataalamu. Je, wataalamu waliwapendekeza wawekezaji wa wapi? Watanzania wamechoshwa na mikataba mibovu ya madini, wamechoshwa na mikataba kama ile ya *IPTL* na ile ya *Richmond*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia nzuri ya serikali ya kuanzisha maeneo maalum *Export Processing Zone (EPZ* ) ya biashara za kimataifa, bado haijaweka

bayana mipango kamili *(time framework)* ya maeneo haya ikiwa ni pamoja na changamoto wanazokabiliana nazo kwani kasi ya kazi hii inaonekana kusuasua. Kwa mwaka wa fedha 2006/07 Serikali ilitenga na kutoa kiasi cha shilingi milioni 50 kwa ajili ya kuendeleza mradi huu. Kambi ya Upinzani inadhani kulingana na umuhimu wa mradi huu bado kiasi hiki ni kidogo. Bado kuna fursa nyingi mno za bidhaa zinazoweza kuzalishwa Tanzania kwa ajili ya kuuzwa nchi za nje, na si bidhaa za nguo tu na fursa za viwanda hivyo haziko Dar es Salaam pekee. Aidha, tunadhani *CTI* na *TCCIA* wako katika nafasi nzuri kuelekeza wapi kunaweza kuwemo katika *EPZ* kulingana na upatikanaji wa malighafi, Serikali ikaangalia ni jinsi gani ya kulifanyia kazi suala la miundombinu katika eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika , suala la *Tanzania Bureau of Standards (TBS),* kuteua mawakala maalumu katika nchi kama vile *Dubai, Hong Kong, Thailand, Japan*, Uingereza na kadhalika kwa ajili ya i*nspection* za magari yanoingizwa Tanzania, mpango huo umeshapitwa na wakati kwa hivi sasa baada ya Wizara ya fedha kupitisha *by-law* ya kwamba magari yenye umri zaidi ya miaka 10 yanatozwa ushuru mkubwa mno. Kwa maana hiyo, hakuna mtu atakayeiingiza gari bovu kutokana na kipengele hicho. Kambi ya Upinzani inaona vitengo hivyo vilivyoko huko ni njia ya kuwatafutia ulaji baadhi ya watu kwa jasho la Watanzania wanaoleta magari nchini. Je, Serikali imepata kiasi gani tangu zoezi hili lianze? Kambi ya Upinzani inataka kitengo hicho kiondolewe mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa *TBS* kwa bidhaa mbalimbali zinazoingizwa nchini inaonekana ni hafifu mno kwa sababu bidhaa nyingi ambazo zipo chini ya viwango zimezagaa Tanzania. Kwa mfano, bati ambazo *gauge* zake hazikutimia, nyaya za umeme, *bulb* za umeme, *spare* za magari na kadhalika. Katika suala hili la viwango kero kubwa ipo katika suala zima la mafuta ya petroli na dizeli kuchanganywa na mafuta ya taa.

Kitendo ambacho wakati kinawapa faida nono na utajiri wa haraka wamiliki wa vituo vya mafuta lakini kwa upande mwingine ni uharibufu mkubwa wa mazingira pamoja na magari kutokana na *carbon dioxide emission* kubwa inayotokana na mchanganyo huo. Kambi ya Upinzani inapenda kupata maelezo katika ulimwengu huu unaojali mazingira; je, lini Serikali itakataza uingizaji wa petroli isiyokuwa na madini nchini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vilivyobinafisishwa, sera ya ubinafsishaji ilikuwa ni njia ya kuchochea ukuaji wa uchumi. Taarifa mbali mbali zinaonyesha kwamba ubinafsishaji ulioanza miaka ya 1990 unatarajiwa kukamilika Desemba, 2007. Kwa mujibu wa *PSRC* viwanda 322 tayari vimeshabinafsishwa na 35 vilivyosalia viko katika mchakato huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kasi hii ya ubinafsishaji kuna umuhimu wa kujiuliza kuna tija kiasi gani iliyopatikana? Ni muhimu Serikali ikatueleza katika viwanda vyote hivyo vilivyobinafsishwa ni viwanda vingapi vinavyoendelea na uzalishaji madhumuni yakiwa ni kujiandaa kimkakati kuhakikisha kwamba 35 vilivyosalia haviingii katika mkumbo huo huo. Usimamizi wa zoezi hili umekuwa na matatizo ya

hapa na pale kwani bado baadhi ya viwanda vimeshindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa. Kama kiwanda cha Ngozi, kiwanda cha magunia vyote viko Mkoa wa Kilimanjaro havifanyi kazi viko *hoi bin taaban!*

Viwanda vya kubangulia korosho navyo havijakidhi mantiki ya ubinafsishaji kwani korosho nyingi zimeendelea kuuzwa nje bila kubanguliwa. Mkata *Saw Mill*, na kiwanda cha chuma, vyote vya Tanga, kiwanda cha chumvi Uvinza, havifanyi kazi. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali ieleza nini hatima ya ufufuaji wa viwanda hivi na hatua zilizochukuliwa kwa ukiukwaji wa makubaliano ya awali pamoja na maslahi ya wafanyakazi wake yamefikia wapi? Ingawa Mheshimiwa Waziri katueleza kwamba wanajaribu kufufua, tunaomba atupe *time frame* vitafufuliwa lini? Hali hii ya viwanda ni kielelezo cha mikataba mibovu ambayo Serikali imekataa kuileta hapa Bungeni. Sielewi usiri huu wa mikataba unafuata sheria ipi na kifungu kipi. Kama sheria hiyo ipo basi inakinzana na sheria mama ya Katiba ambayo inaturuhusu kusimamia/kuihoji Serikali kupitia Ibara ya 63 ya Katiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zote duniani zinabinafsisha makampuni ili zifaidike na uwekezaji wa yule anayetaka kuja kuwekeza katika kiwanda hicho. Kufaidika huko hutokana na ajira, kodi, uuzaji wa nje, na mzunguko mzima wa fedha hiyo katika uchumi wa nchi. Na hii ndio sababu kubwa kwa makampuni kubinafsishwa kwa bei nafuu kutokana na Serikali kuamini kuwa itafaidika na yatokanayo na ubinafsishaji huo. Kiwanda cha Chumvi cha Uvinza *(*Nyanza *Mines)* kilikuwa kinazalisha chumvi kwa mtambo unaotumia Umeme kuzalisha (*Vacuum plant*). Mtambo huu ulijengwa na kampuni ya Kitaliano na kufunguliwa rasmi mwaka 1985, na unazalisha chumvi kwa kutumia umeme. Ulifanya kazi tangu mwaka 1985 mpaka 1992 ambapo uliharibika. Kutokana na Serikali kukosa fedha za kuukarabati, na uendeshaji mbovu wa yaliyokuwa mashirika ya umma, kiwanda hicho pamoja na mitambo yake yote ilibinafsishwa na hivyo hakikuzalisha tena. Sasa inastaajabisha kuona kuwa mwekezaji amekabidhiwa kiwanda cha Chumvi Uvinza tangu mwaka 1998 mpaka sasa ameshindwa kuufufua mtambo huo na kuamua kuuza nje tofauti na makubaliano ya ubinafsishwaji wa kiwanda hicho. Serikali ilitumia bilioni za shilingi kuutengeneza mtambo huo, wao wamenunua kiwanda hicho cha chumvi kilichokuwa na mitambo mitatu, ule wa *solar, thermal* na *Vacuum* kwa bilioni 0.9. Lakini kwa mujibu wa taarifa zilizopo ni kwamba mwekezaji huyo ameuza mtambo mmoja wa kutumia umeme huko Iran kwa shilingi bilioni 4.5. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali ilihakikishie Bunge hili ukweli wa kuuzwa kwa mtambo huo mmoja unaotumia umeme kwa bei hiyo iliyotajwa hapo juu na kama ni kweli ni kiasi gani Serikali imepata kutokana na kuuzwa huko kwa mtambo huo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani haitaki kuamini kama kweli tatizo lililopelekea hadi mtambo huo kuuzwa ni umeme kwani Serikali iliweza kuendesha kwa kutumia umeme wa mafuta mpaka pale ulipo haribika. Hata kama tatizo lingekuwa ni umeme, Mheshimiwa Rais Kikwete, alikwishaahidi kupeleka umeme wa uhakika Kigoma. Tunaiomba Serikali kupitia Wizara husika iangalie utendaji wa viwanda vilivyobinafsishwa kama vinatekeleza masharti ya ununuzi wa viwanda vyetu,vinginevyo

ni bora atafutwe mwekezaji mwenye uwezo na sio wale wanaotafuta na kupata mtaji wa uendeshaji kutokana na *assets* wanazozikuta kiwandani hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Viwanda na Biashara imetengewa jumla ya shilingi 17, 234, 547, 000 katika Bajeti yake kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 7, 395, 376, 000 kwa ajili ya shughuli za miradi ya maendeleo. Hii inafanya jumla ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Viwanda na Biashara na Masoko kuwa ni shilingi 24, 629, 923,000 ambayo ni asilimia 0.4 ya Bajeti nzima ya Serikali. Kiasi hiki ni kidogo mno na kwa mantiki hiyo ushauri wetu juu ya bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara, hauwezi kutimia bila kuunganisha na maoni tuliyotoa wakati wa hoja ya bajeti kuu iliyowasilishwa na Waziri na Fedha. Kambi ya Upinzani inafahamu kuwa bajeti kuu imekwisha kupita lakini bado maoni yetu mbadala yatabaki kwenye kumbukumbu na tunaitaka serikali iyatumie kwa ajili ya kuboresha bajeti ijayo ambayo ni muhimu kwa wananchi wote. Kama Serikali ingezingatia ushauri wa kiufundi uliotolewa katika hotuba ya Waziri Kivuli wa Fedha wa Upinzani, ingeweza kuwa na bajeti ya shilingi trilioni 7.9 badala ya trilioni 6 zinazofikiriwa kukusanywa na Serikali. Kwa trilioni 7.9 Serikali ingeweza kutenga bilioni 76.5 kwa ajili ya Wizara ya Viwanda na Biashara ambayo ingekuwa ni asilimia 1 ya bajeti nzima tofauti na fungu la Serikali ambalo ni asilimia 0.4 tu ya bajeti yake nzima. Kiasi hiki cha bilioni 76.5 kingezidi kile cha serikali kwa bilioni 51.9 na kuongeza ufanisi katika sekta ya viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imejaliwa rasilimali nyingi ambazo zinaweza kutumika kama malighafi katika sekta ya viwanda nchini. Ni vigumu kuongelea viwanda bila kugusa sekta ya kilimo ambayo inaajiri takribani 80% ya watanzania ambao ni wakulima na wanaishi vijijini. Huduma duni za maji, umeme na barabara katika sehemu kubwa nchini hasa vijijini zimekuwa ni kikwazo kikubwa katika kuanzisha/kuimarisha viwanda nchini. Hali kama hii ni mojawapo ya changamoto za kufikia malengo ya milenia, ajira milioni moja ambazo Watanzania wameahidiwa, ikiwa ni pamoja na kukuza biashara yetu katika soko la Jumuia ya Afrika ya Mashariki, *SADC, AGOA* na kadhalika. Aidha, matatizo ya umeme wa uhakika katika uzalishaji yamesababisha ughali wa bidhaa ambazo zinazalishwa na viwanda vyetu vya ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kupatikana kwa gesi asilia hapa kwetu na gesi hiyo kuanza kuingizwa moja kwa moja viwandani na kwa kiasi kikubwa viwanda kuacha kuzalisha kwa kutegemea umeme unaosambazwa na *TANESCO,* ni ukombozi mkubwa sana katika sekta ya viwanda. Na sio tu katika sekta ya viwanda bali ni kuokoa fedha za kigeni na kupunguza umaskini kwa Watanzania. Bila kusahau uimarishaji wa thamani ya shilingi yetu. Tunaamini kuwa mkombozi gesi asilia ambayo inachimbwa hapa kwetu na kutumika katika viwanda vyetu maana yake inapunguza ile hali iliyokuwa inatukabili kwa muda mrefu ya kuwa na uchumi ghali, jambo lililokuwa likisababisha bei ya bidhaa za ndani kuwa juu kulinganisha na bidhaa toka nje ya nchi. Kwa mujibu wa takwimu zilizopo ni kuwa takriban viwanda 18 vimekwisha badilisha mitambo yao ya umeme na kujiungana katika uzalishaji kwa kutumia gesi. Maana yake kuwa wamepunguza gharama zao za uzalishaji kwa zaidi ya asilimia 25. Vivyo hivyo, takwimu zinaonyesha

kuwa toka viwanda hivyo vianze kutumia gesi katika uzalishaji vimeokoa jumla ya *USD* 744,300,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukweli huu, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili ni kiasi gani Serikali imepata kutokana na viwanda kutumia gesi. Aidha, kwa mujibu wa taarifa ya *TPDC* inaonyesha kuwa viwanda vya Mabati *(ALAF),* sementi *(WAZO HILL CEMENT),* bia *(TBL, SERENGETI BREWERIES),* mafuta ya kupikia *(MURZHA OIL),* nguo (*NIDA, KARIBU, CHINESE TEXTILES)* na kadhalika, tayari vinatumia gesi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kushangaza ni kuwa bei za bidhaa zinazozalishwa na viwanda hivi bado ziko vilevile. Mfano mzuri ni bei ya sementi kwa wananchi inayozalishwa na *WAZO HILL CEMENT* haina tofauti na *cement* inayozalishwa na kiwanda cha Mbeya na Tanga *Cement*. Bei ya mafuta ya kupikia yanayozalishwa na *MURZHA OIL* haina tofauti na bei ya mafuta yanayoingizwa toka nje ya nchi. Hapa Watanzania kweli watafaidika vipi na gesi yetu au ni mambo yale yale kama ya madini ambayo wanaofaidika ni wageni zaidi kuliko wazawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inauliza, je, uzalendo tunaoambiwa uko wapi? Lile punguzo la asilimia 25 linalopatikana katika punguzo la utumiaji mafuta mazito *(heavy furnace oil)* linaonekana vipi katika bei ya bidhaa kama vile sementi*,* bia, mabati na kadhalika. Tuna wataalamu wengi sana na tunaamini kuwa wanaelewa sana haya tunayoyasema, ila kutokana na mambo yasiyoelezeka na kueleweka, kuna msemo unaosemwa, naomba ninukuu: *"if you can't fight them join them".* Wataalamu wanazidi kukosa maadili ya kiushauri au kutoa maamuzi kulingana na taaluma zao, jambo linalofuata ni kutumia mwavuli wa siasa kulinda na kuhalalisha ubadhirifu huo. Maslahi ya Taifa limekuwa si jambo tena linalopewa kipaumbele. Hili ndilo linalozidi kuididimiza nchi yetu na kundi fulani la watu wanazidi kufaidika na maliasili zetu. *(Makofi)*

Mheshiwa Naibu Spika, Mabenki mengi yaliyoko nchini sasa hayakidhi mahitaji ya kuwakopesha wajasiriamali jambo ambalo hailisaidii taifa letu. Ukiangalia faida ya mabenki mengi haitokani na shughuli za msingi za kibenki ambazo ni ukopeshaji, faida kubwa inatoka kwenye *non interest activities.* Kwa kuwa mabenki yetu yameonyesha uwezo mdogo katika kusaidia kuanzishwa kwa viwanda, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuweka nia ya dhati kwa kuipatia uwezo wa kifedha benki ya *TIB* ili iweze kutoa mikopo na mitaji mikubwa na ya muda mrefu (*long term financing*) kwa wafanyabiashara wanaotaka kuanzisha viwanda. Pia serikali iyabane mabenki yetu ili yaweze kutoa mitaji na mikopo mikubwa yenye kuweza kuchangia ukuaji wa viwanda na hatimaye uchumi kukua kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ulio dhahiri kuwa bajeti ya 2007/08 inapingana na dhana nzima ya maendeleo ya viwanda hasa kwa kuongeza kodi katika mafuta ambayo ni nyenzo kuu katika kuendeshea viwanda. Hali hii itaongeza gharama za uzalishaji na bidhaa zetu zitaendelea kuwa ghali na kushindwa katika ushindani wa soko la ndani na nje ya nchi na hatimaye kuathiri ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza, bado maendeleo ya viwanda nchini ni duni. Zaidi ya asilimia 80 ya bidhaa za viwandani tunaagiza kutoka nje ya nchi. Mwaka 2006 Tanzania ilisafirisha bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani bilioni 1.7 wakati bidhaa tulizoagiza kutoka nje ya nchi zilikuwa na thamani ya dola bilioni 3.8. Hii ni kwa mujibu wa takwimu za Benki Kuu ya Tanzania *(BoT).* Hali hii haitoi mwanga katika ukuaji wa viwanda vyetu.

Mheshimiwa NaibuSpika, kwa mfano India na China zinasifika kwa kuwa na kasi kubwa ya maendeleo ya viwanda katika uchumi kwa sababu kuu mbili: kwanza, ni kuongeza biashara za nje na pili ni kuleta maendeleo makubwa ya viwanda vyao. Yote haya yametokana na nchi hizi kuwa na sera nzuri za maendeleo na bajeti inayolenga maendeleo ya viwanda na kuongeza biashara za nje. Mathalani, India mwaka 1964 ilianzisha benki maalumu ya kutoa mikopo nafuu na ushauri juu ya kuendeleza viwanda *(Industrial Development Bank of India –IDBI)* na China mwaka 1998 ilianzisha benki nyingine ya maendeleo ya viwanda inayoitwa "*Fujian Industrial Bank"* yenye mtaji wa dola za Marekani karibu bilioni 1.514, haya ni mambo ambayo Tanzania inapaswa kuyaiga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwangu mimi wadau wengi wa sekta binafsi nchini ni wakulima ambao ni asilimia 80 ya Watanzania. Tukiwekeza kwao kwa njia ya viwanda, taifa litakuwa limepata mapinduzi ya uchumi katika viwanda. Wakati umefika kwa Serikali kuweka mikakati madhuti ya kumkomboa mkulima kwa kujenga mazingira mazuri ya uanzishwaji wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa vya kusindikia mazao yao ili kuongeza pato na kuondokana na maadui wetu wakuu watatu (ujinga,maradhi na umasikini). Kwa mfano, Tanzania inasindika chini ya asilimia moja ya matunda wakati Brazili ni asilimia 30 na Malaysia asilimia 82. Kama wao wameweza, Kambi ya Upinzani inahoji kulikoni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yangu mwaka 2006/2007 pamoja na hotuba ya Waziri Kivuli wa Uchumi na Mipango, tulizungumzia suala la majadiliano ya kibiashara na nchi za Jumuiya ya Ulaya *(EU).* Tumesikia kuwa Tanzania sasa imeamua kusaini mkataba huu kupitia *SADC-EPA.* Mkutano wa *SADC-EPA* uliofanyika huko *Walvis Bay*, Namibia pia umeruhusu nchi ya Afrika Kusini kuwa mjumbe wa *SADC-EPA* licha ya kwamba wao wana mkataba mwingine na Afrika Kusini *(Trade and Development Cooperation Agreement).* Tunaiomba Serikali ilipatie Bunge lako Tukufu maelezo ya kina kuhusiana na suala hili. Suala hili linahusu uhai wa wananchi *(it is a national security issues)* kwani linagusa masuala ya kodi na kupoteza mapato ya kodi. Pia linahusu kupoteza ajira kwa kuruhusu bidhaa kutoka Ulaya kuingia nchini bila ya kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matumaini ya Wizara, katika makadirio ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008, kuna kasma ambazo zimepanda sana na hivyo Kambi ya Upinzani inahitaji maelezo ya kina kuhusu sababu za kupanda huko. Mathalani gharama za kupanga ofisi katika jengo la *NSSF Water Front* kama inavyooneka katika maombi ya fedha ni makubwa mno imepanda kutoka shilingi

204,000,000 mwaka jana hadi shilingi 720,000,000 mwaka huu. Hapo hapo gharama za ukumbi nazo ni shilingi 18,530,000/= na kufanya jumla kuwa shilingi 738,530,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kupanga katika jengo la *NSSF Water Front* bado inabidi Wizara kukarabati kiyoyozi cha ofisi iliyopanga kwa jumla ya shilingi 88,500,000. Ukarabati katika ofisi za wizara ndani ya jengo hilo utagharimu shilingi 50,000,000. Jumla ya fedha ambazo wizara inaweka katika jengo la *NSSF Water Front* kwa kuwa tu imepanga hapo ni shilingi 877,030,000. Kambi ya Upinzani inahoji uhalali wa kupanda kwa gharama za upangaji wa ofisi kwa 429.9%. Je, si busara kwa wizara kujenga ofisi yake ya kisasa kabisa yenye ukumbi mzuri wa mikutano kwa fedha hizo hizo ili miaka ijayo tuondokane kabisa na gharama/ adha za upangaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtazamo na ushauri wetu kuhusu Wizara kwa ujumla, kila anayeitakia mema Tanzania na maendeleo yake kwa ujumla, hawezi kukataa mchango wa sekta ya viwanda katika kukuza uchumi wa nchi. Yote haya yataweza kufikiwa ikiwa tu kutakuwa na sera nzuri zenye kusimamiwa kwa hali ya juu ya uwajibikaji kwa kuheshimu michango ya wataalamu husika. Usimamiaji huu ni pamoja na Serikali kuhakikisha ushindani wenye usawa '*fair competition'* na mikataba madhubuti yenye kulinda maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuhitimisha, kama nilivyojieleza mwanzo, kimsingi lengo la hotuba hii ni kutoa mawazo mbadala kwa Serikali yetu tukufu ili kuweza kuchochea maendeleo ya viwanda kwa ujumla. Mapinduzi yanayokusudiwa ya kilimo *(green revolution)* ni lazima yaendane na mapinduzi ya viwanda *(industrial revolution)* nchini ili kuweza kumkomboa Mtanzania kutoka lindi la umaskini.

Ni matumaini yetu kuwa Serikali hii itajaribu kuwa sikivu kwa faida ya Watanzania wote. Serikali isitishe mara moja ununuzi wa samani *(furniture)* kutoka nje kama njia mojawapo ya kuchochoea ukuaji wa viwanda nchini, ikiwa ni pamoja na kudhibiti matumizi ya fedha za nje. Aidha, mkakati huu unaweza kuchangia ajira milioni moja walizoahidiwa Watanzania. Ni lazima tugawane keki hii na kuifurahia kwa maisha bora kwa kila Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru wote kwa kunisikiliza, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa kuwasilisha hotuba yako vizuri. Sasa Waheshimiwa Wabunge nikiangalia saa hii kama tutakuwa na wanaoweza kuchangia chini ya muda uliowekwa asubuhi tunaweza kupata watu 6. Lakini kama kila mtu atafika muda wake basi itakuwa watano tu. Kwa hiyo, nawaita Mheshimiwa Anna Komu, Mheshimiwa Mohamed Sinani, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo ajiandae, Mheshimiwa Ahamed Ali Salum ajiandae, Mheshimiwa Juma Njwayo ajiandae na Mheshimiwa Nimrodi Mkono. Na wengine watatajwa kwa ajili ya mchana.

**MHE. ANNA M. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote kwanza natanguliza shukrani zangu kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia kwenye Wizara

hii muhimu kwa maendeleo ya Watanzania wote na maendeleo ya nchi yetu. Maendeleo ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ni Wizara mama katika uchumi wa nchi yetu. Kama kweli tuna nia ya kutaka kukuza uchumi lazima tuhakikishe kwamba Wizara hii inafanya kazi yake kwa jinsi inavyotakikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na hotuba au mchango wangu, naanza kuzungumzia kuhusu viwanda. Tumeshuhudia Watanzania wote jinsi viwanda hivi vilivyokufa baada ya kufa kwa Azimio la Arusha na mengineyo. Kwani Mheshimiwa Baba wa Taifa, Mungu amrehemu alipolala alijitahidi sana kuwafanya Watanzania wawe na viwanda ili tuweze kuuza mali zetu, kilimo chetu na pia Watanzania waweze kupata ajira. Lakini kilichotokea hapo kati pia si kibaya kwamba Serikali isijihusishe na biashara, tukaweza kubinafsisha viwanda hivi na kuvitoa mikononi mwa wageni walio wengi na sisi wenyewe tukaja kushtuka kwa kuanzisha michango na kuanzisha kununua hisa katika kununua viwanda.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anna Komu, hatusomi hotuba sisi.

**MHE. ANNA M. KOMU:** Sisomi Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu naangalia chini? Siwezi kuangalia hivi. Samahani! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda hivi vimeanza kazi vizuri, baada ya wao wawekezaji kukubali kuja kushika viwanda vyetu. Lakini sasa mimi nina wasiwasi mkubwa na hali ilivyo katika nchi yetu. Nashukuru kabisa kwa sababu Mheshimiwa Waziri mwenyewe amekubali kabisa kwamba viwanda hivi vinakumbwa na matatizo yaliyo mengi. Na matatizo makubwa sana yanayoshika viwanda hivi ni umeme na maji. Sijui lini matatizo haya ya kukatika kwa umeme na kukosekana kwa maji yatakwisha. Sidhani kwamba safari zote ambazo Mheshimiwa Rais amezifanya nchi za nje na kutumia pesa za Watanzania kikubwa kilikuwa ni kukuza kwa uchumi wetu wa nchi yetu, kukaribisha wawekezaji ili waje wawekeze katika nchi yetu na viwanda vyetu viweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama kweli unamkaribisha mtu nyumbani kwako bila maji, bila ya kuona anakwenda wapi, chumba kiko wapi, ataishije hana maji, sidhani kwamba watakubali kuja kufanya kazi katika eneo letu. Kwa hiyo, mimi kitu kimoja muhimu ninachokiomba Serikali hii tufanye bidii kabisa kuhakikisha kwamba haya mazungumzo ya umeme yanafika mwisho. Mazungumzo ya maji yanafika mwisho. hapo Hapo tuna tatizo kubwa la upandaji wa mafuta kila mwaka; kila mwaka hakuna kitu kinachopanda katika nchi yetu ila mafuta, mafuta, mafuta. Nayo yamekuwa ni kikwazo kikubwa sana kwenye viwanda vyetu hivi. Kwa sababu huwezi ukamwambia aje awekeze kwenye kitu ambacho hatapata faida.

Kila mmoja anataka kuwekeza kwenye faida. Sasa kama pesa zote anazochuma ataishia kwenda kununua mafuta sidhani kwamba atakuja mtu kuja kuwekeza hapa kwetu. Kinachoendelea kingine nacho ni ughali wa vipuli. Vipuli hivi vinapoharibika nyingine huwa inabidi hata viagiziwe kutoka nchi za nje. Tumeshuhudia sisi wenyewe,

mimi katika Kamati yangu tulitembelea vyombo vya Habari tukakuta kuna mashine muhimu ambazo zimekufa, zina miaka, haziwezi kufanya kazi kwa sababu hakuna vipuli na hakuna pesa za kuweza kuagizia vipuli kwa sababu ni pesa nyingi sana. Sasa yote haya yanafanya kwamba viwanda vyetu havitaweza kuleta tija kama tunavyotegemea. Kwa hiyo, kinachofuata hapa inabidi lazima tuwe na uhakika wa kwamba tunawaita wawekezaji wanakuja kuwekeza kwenye eneo ambalo watapata tija nalo, tujitahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia sasa kuhusu biashara. Biashara ni kitu muhimu sana, na biashara hizo ndizo tunazozipigia kelele hapa kila siku. Biashara zinaweza zikaingiza tija katika nchi yetu na zikatupa pesa za kigeni na pia Watanzania wakaishi kwenye maisha mazuri, na biashara unapozungumza biashara, unakwenda mpaka kwa yule mkulima wa kule chini kabisa. Kama hatutakubali kabisa na kuhakikisha kwamba kilimo chetu kinakuwa chenye tija katika nchi yetu basi hata hizo biashara hazitakwenda popote na lazima tuhakikishe kwamba hizi biashara za wakulima wetu kwa mazao ambayo wanayalima na kuyakuza, wanasaidiwa katika pembejeo, wanasaidiwa mbolea ziwe zinawafikia. Pia wao wenyewe ndio wachague wanunuzi wa kununua biashara zao siyo kuwapelekea wanunuzi wa kununua mazao yao wakati wao ndio wakulima, wao ndio wanaojua taabu gani wameipata na gharama gani wameitumia kwenye biashara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama tutawapa nguvu tutawekeza kabisa kwenye kilimo basi tutahakikisha kwamba biashara zetu zitakwenda vizuri kwa sababu hata Watanzania watanufaika. Tunahangaika nini wakati tuna mimea ambayo inaweza ikaota kwenye hali yoyote ile kama mkonge. Mkonge una historia zaidi ya miaka 100 nchini kwetu. Mkonge unaweza ukaota mahali popote kwenye hali yoyote hata ukame, upate mvua ndogo tu ya milimita 600 kidogo tu 600 tu mkonge unaendelea. Na mkonge tayari ulishajiweka vizuri kwa sababu kwenye mashamba ya mkonge kuna nyumba ambazo tayari za wafanyakazi. Kwenye biashara ya mkonge tayari kuna mashine za kufanyia kazi kuweza kupambua mkonge huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkonge unaleta vitu vingi sana, mkonge huo huo kama tukiuangalia unaleta hata umeme. Mkonge huo huo unaweza kuleta pamoja na vitu vyote vinavyoletwa na mkonge basi *alcohol* tutaweza kuacha kupandisha bei ya pombe kila siku kwa sababu ya mkonge. Kwa nini basi tusiendeleze hili zao la mkonge? Kwa nini tunalitupa zao la mkonge? Tunaanza kuangalia mambo ambayo yatakuja kuwa faida ya baadaye wakati hiki kitu tayari kipo. Ninachoomba mimi tuangalie lile zao ambalo litaweza kuleta biashara nzuri katika nchi yetu na tayari lipo na halitatumia gharama kubwa katika uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea tena nakuja sasa kwenye masoko. Tunasema kila siku na vizuri *SACCOS* ziko chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, tunawalazimisha wajarisiamali kila siku, tunawapa moyo wajasiriamali kila siku lakini soko liko wapi? Juzi juzi hapa jana, kama sikosei kulikuwa na malalamiko makubwa sana ya *TISCAN* kwenye vyombo vya habari. Wanalalamikiwa hawa *TISCAN* Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara ya kwenda kutembelea pale bandarini. Baada

ya wiki moja tu kazi ilifanyika vizuri tu Waziri Mkuu alipopita pale, lakini baada ya wiki tu hakuna kitu kinachoendelea pale. *(Makofi)*

*TISCAN* imekufa kabisa, hata mashine zenyewe pia ziko nne, mbili zimekufa. Tunasema huyu mwekezaji kweli aendelee kuja hapa kwetu wakati hata akileta makontena yake ya biashara zake basi pale yataganda na yanapokaa pale zaidi ya siku kadhaa inabidi tena alipie. Tusiendelee kulea hawa watu ambao hawawezi kuwajibika, tusilete udugu, tusilete usisi, kama kweli tunataka kufanya kazi, basi kama mtu aliyeko kwenye *TISCAN* hawezi kuwajibika, anyang'anywe apewe mwingine ili kazi ziendelee. Tusiendelee kulelea lelea watu hawa tukisema, "usimwonde hapa Mheshimiwa Maulida!" Maana yake yeye hapa ni ndugu yetu, hatutafika! Tuhakikishe kama huyu ambaye tumempa hii biashara ya *TISCAN* pale hawezi apewe mtu mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tutafute masoko. Lazima maadhali Mheshimiwa Rais wetu amefungua njia ya kufanya ziara hizi kwenda kule na sisi tuyakuze. Biashara zipatikane na masoko yapatikane kwa sababu hata kama nitasema nitazalisha kama sipati masoko sasa vinavyozalishwa vina faida gani? Mheshimiwa mzungumzaji wa Kambi ya Upinzani hapa aliongea. Leo kweli Mtanzania unamwambia ajijenge au akae vizuri wakati ananunua sementi ya mfuko wa shilingi elfu zote zilizoko huku duniani. Unamwambia akanunue mabati kwa pesa zote, ataweza wapi? Wakati kuna viwanda kama cha Wazo kinachotumia gesi, kwa nini kiwanda hiki kisifanye biashara ya sementi kwa bei nafuu ili Mtanzania huyu akaweza kumudu. *(Makofi)*

Kwa nini hawa *ALAF* wasitengeneze kwa bei nafuu Mtanzania huyu akaweza kudumu bati. Kweli leo bati moja ununue kwa shilingi 10 na nani anaweza. Na huku tunasema tunataka maisha mazuri, tunataka kujenga maisha mazuri kwa Watanzania. Ninachoomba Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na hiyo hiyo ni Wizara ya Masoko vitu vyote vitatu vimekaliana pamoja, tujitahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikimalizia mambo ya kupanga panga haya sijui yatafufikisha wapi. Na ninashukuru Msemaji wa Upinzani amezungumza. Leo tuna chombo ambacho kinaandikisha hizi kampuni, kinaandikisha viwanda, kimekwenda kuwekwa kwenye eneo dogo, hawawezi kabisa kufanya kazi zao jinsi inavyotakiwa. Leo utawaambia wale watu waende tena wakakodishe kwa mabilioni kama leo Wizara inavyokodisha kwa mabilioni. Kwa nini tusiweke utaratibu wakati ardhi ipo ya kutosha, kama mwaka huu wamekodisha kwa mabilioni hayo, mabilioni hayo kwa mwaka ujao yakaanza kujenga nyumba ambayo Wizara itakuwa inakaa kwenye nyumba hiyo kuliko kuendelea kupoteza mabilioni ya Watanzania kwa ajili ya kulipia kodi.

Naomba yale ambayo tunayaona kwamba yamo ndani ya uwezo wetu basi tuyafanyie kazi kwa haraka zaidi , tuyaache yale ambayo hayamo ndani ya uwezo ya kwenda kukodisha mapango ya kutoa mapesa ya kulipa pango ya mabilioni kwa mabilioni ya pesa ya Mtanzania. Nashukuru kwa kunipa nafasi hii na naomba mchango wangu uchukuliwe, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa kunipa dakika 2. Sasa naendelea na Mheshimiwa Mohamed Sinani na wewe uniokolee muda.

**MHE. MOHAMED S. SINANI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja hii iliyopo mbele yetu. Kwanza kabisa kwa niaba ya wapiga kura wangu, ningependa kuishukuru Serikali kwa jitihada iliyofanya kuhakikisha kwamba kero ya umeme katika Mkoa wa Mtwara inamalizika. *(Makofi)*

La pili, tunaishukuru pia Serikali kwa kutambua kwamba Mkoa wa Mtwara nao umo katika mikoa iliyopo pembezoni na kwamba tunahitaji kipaumbele. Hilo nalo tunashukuru sana. Mtwara hivi sasa iko tayari kupokea viwanda. Miundombinu karibu imekamilika, kuna gesi ya kutosha, kuna umeme wa kutosha. Kwa hiyo tuko tayari kupokea viwanda kama vya semeniti ambavyo vinatumia *gypsum* ambayo pia ipo*, lime* chokaa ipo. Kwa hiyo, ningeshauri Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kufikiria kujenga au kushawishi wawekezaji kuja kujenga kiwanda cha sementi Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vidogo vidogo navyo tunavihitaji, sisi Mtwara ni maskini. Miongoni mwa mikoa maskini ni pamoja na Mtwara. Lakini tuna malighafi ya kutosha bali hatuna viwanda vidogo vidogo, tunahitaji msukumo. Tunahitaji Serikali itusaidie. Tukipata viwanda vidogo vidogo vya kubangua korosho, korosho tunazo, viwanda vya kutengeneza *starch* kutokana na muhogo, muhogo upo. Viwanda vidogo vidogo tunaagiza hata *top sticks* kutoka nchi za nje, sisi tunaweza kuchonga vinyago, kuchonga *top sticks* kama vinyago tunaweza kuchonga basi hata vijiti vya kujichokonyolea katika meno hatushindwi kuchonga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitarajia kwamba Wizara ya Madini na Nishati ingetaja katika hotuba yake viwanda vidogo vidogo vya chumvi lakini haikutaja kabisa. Chumvi inahitajika katika nchi hii. Ni aibu kwa nchi hii kuagiza chumvi kutoka nchi za nje wakati malighafi ya kutengeneza chumvi ni maji ya bahari. Najua mbinu inayotumika kukausha maji yale, haihitaji malighafi kutoka nje ili kutengeneza chumvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaagiza chumvi ya mezani *(table salt)* kutoka Kenya, wakati sisi tuna uwezo wa kutengeneza chumvi, ni aibu kabisa.! Tunahitaji chumvi katika kutengeneza ngozi, wenzetu wanasafirisha nchi za nje chumvi ya kutosha kabisa na kuiingizia nchi ya Kenya pesa za nje. Lakini sisi hapa tunashindwa hata ku-*export* chumvi. Naomba Mheshimiwa Waziri hili suala la viwanda vidogo vidogo vya chumvi ulitilie maanani. Vinatoa ajira kwa watu wengi kuanzia Mtwara hadi Tanga, wakazi wote wa pwani pwani wanashiriki katika uzalishaji wa chumvi lakini hawapati msaada wowote kutoka Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawapati msaada kutoka Wizara ya Madini na Nishati wala msaada kutoka Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Viwanda hivi vinaajiri watu wengi, vinaweza vikatoa ajira kubwa kabisa kwa wananchi wetu hususan wale wananchi ambao wanaishi kando kando ya bahari ya Hindi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naiomba Serikali itusaidie katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji viwanda vidogo vidogo vya kutengeneza mashua ili wananchi waende wakavue samaki. Wanashindwa kwenda kuvua samaki, hawana vifaa vya kuvulia. Tunaomba Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko tafadhali mlitazame hili. Sisi Mtwara hatuutaki umaskini. Tunauchukia, wala hatuupendi. Na wala watu wasiseme watu wa Mtwara ni wavivu, si kweli! Mtu anayelima korosho hawezi kuwa mvivu.

Adhabu ya korosho inatosha kabisa kusema mtu huyo ni hodari. Kwa sababu korosho unayoila leo imepitia katika mkono yaani inabanguliwa toka unaiokota shambani, unaivuna, unaigusa ile punje moja unaitia katika mashine ile punje moja, ukishaibangua uipeleke tena ukaimenye. Mpaka wewe kuitia mdomoni imeshapita katika mikono yote.

Ni kazi nzito sana. Kwa hiyo, kama Mkoa unaweza ukazalisha zaidi ya tani 100,000 za korosho hao si watu wavivu. Wananchi wanaweza wakafaidika sana ikiwa viwanda vidogo vidogo vitatiliwa maanani katika viwanda vidogo vya kubangua korosho vya kutengeneza *starch*, viwanda vidogo kwa ajili ya kutengeneza mashua kwa ajili ya kuvulia samaki. Tunahitaji viwanda hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika viwanda vikubwa Mtwara kuna kiwanda kikubwa sana cha kubangua korosho. Ningeomba Mheshimiwa Waziri au wawakilishi wake waende wakatembelee pale kiwandani waone wale akina mama jinsi wanavyotaabika. Adhabu ni kubwa sana. Afya zao zimo hatarini. Mikono yao inachubuka kwa mafuta ya korosho. Mafuta ya korosho ni sumu. Mikono yao ni kama msasa. Sijui huko akina baba majumbani mwao inakuwaje, kwa sababu mikono ya akina mama hawa inaumiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija Mtwara Mjini ukiondoka alfajiri kuelekea unakoelekea, ukiwaona akina mama wanatembea saa 8 ya usiku au saa 9 ya usiku usidhani kwamba hawa ni wachawi au wanga hapana! Wanakwenda katika kiwanda cha Korosho. Wanajihimu kwenda kule na kazi yenyewe wanafanya kazi ya kibarua, kama hukufika na lako halipo. Ukiumwa huna kitu.

Kwa hiyo, ile kazi ni nzito. Naomba akina mama hawa ambao wanapata zaidi ya 4,000 waangaliwe afya zao. Wanaathirika sana na kipato chenyewe wanacholipwa ni kidogo sana hakilingani na adhabu ambayo wanaipata. Kwa hiyo, naomba Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko nayo iangalie suala hili ili ikawatembelee wale akina mama waone wanafanye kazi ili kuangalia kwamba afya zao zinaboreshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo inaonyesha mwelekeo. Lakini pia tungeomba upande wa biashara, wafanya biashara wa Mikoa ya Kusini wakienda kukopa benki hawapati mikopo ambayo wanaihitaji. Wanaambiwa nyumba zao, mashamba yao hayana thamani ukilinganisha na mikoa mingine. Yaani ukiwa na nyumba wewe ina milioni 50, basi itathaminiwa utapata

mkopo wa milioni 10 au 5, wanasema kwamba nyumba za kule hazina thamani. Katika kujenga ni gharama kubwa sana.

Mfuko mmoja wa sementi shilingi 14,000 au 15,000 ukilinganisha na Dar es Salaam, shilingi 11,000/=. Kujenga ni gharama kubwa lakini ukija kutathmini kutaka mkopo hupati mkopo wa kutosha. Kwa hiyo, tunashindwa kufanya biashara. Wafanya biashara wa Mtwara na Lindi wanafanya biashara katika mazingira magumu, bila mikopo mfanyabiashara hawezi kufanya biashara. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wanapata tabu sana katika kupata mikopo. Nyumba zao hazina thamani, wanakuambia kwamba, "bwana aah!" Wanakutajia mikoa ambayo nyumba zao zina thamani. Sasa sisi tutabaki kuwa maskini mpaka lini ikiwa wafanyabiashara wanashindwa kufanya biashara? Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili nalo labda aongee na hao watu wa benki waangalie ni namna gani wanaweza kuwasaidia wafanyabiashara hawa. Biashara inakuwa nzito sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtwara na Lindi tunahitaji msaada wa Serikali, tuondokane na umaskini na viwanda vidogo vidogo vinaweza vikachangia kwa kiasi kikubwa. Eneo lingine ambalo ningelitilia maanani ni uvuvi, kwamba unahitaji maboti. Viwanda vya kutengeneza maboti vimekufa. Kilikuwepo kiwanda Mikindani, kimekufa, hakuna kiwanda kingine. Kwa hiyo, basi tutafute njia nyingine ya kuwasaidia wavuvi hawa nao wapate kuvua samaki waweze kukidhi mahitaji ya maisha yao. Umaskini ni mkubwa sana na ndiyo maana ukiangalia Dar es Salaam Wamachinga wengi asilimia kubwa sana inatoka Mikoa ya Kusini kwa sababu ya shida na kutokuwa na ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa kugongewa kengele, yangu yalikuwa ndiyo hayo na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PHILLEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Wizara ya Viwanda na Biashara. Kwanza, nimpe hongera sana kiongozi aliyesoma hotuba kwa niaba ya Upinzani, ilikuwa nzuri na amesema maneno na mengi niliyotaka kusema amekwisha yasema lakini nitasema mengine mbadala.

**NAIBU SPIKA:** Lazima u-*declare interest* hapo. (*Kicheko*)

**MHE. PHILLEMON NDESAMBURO:** Naomba na mimi niseme mimi ni mdau katika biashara....!

**NAIBU SPIKA:** Hapana sema huyu ni binti yangu basi, hiyo tunaelewa, Waheshimiwa huyu ni binti yake Mheshimiwa Ndesamburo. (*Kicheko*)

**MHE. PHILLEMON NDESAMBURO:** Naomba niseme ni mwanangu vilevile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukuza uchumi wa nchi hii tunahitaji wafanyabiashara walio wazalendo, wafanyabiashara mbalimbali. Uchumi wa nchi hii

kwa sasa uko karibu asilimia 80 nje ya Wazalendo, wazalendo wana *percent* 10 *control* ya uchumi wa nchi hii. Na kama uchumi wa nchi haujawa chini ya mikono ya wazalendo, hata kama tutafanya nini kwa miaka nenda rudi hatutakaa tuikomboe nchi hii. Pesa zote zitakuwa zinaingia na zinatoka nje na tusiwategemee sana wawekezaji ambao tunawapigia kelele na kuwasifia.

Wawekezaji wanaletwa hapa na nchi zao waje wakachume wapeleke kwa nchi zao. Hawaji hapa kwa ajili ya kutuchumia sisi. Mimi ni mfanyabiashara nawaelewa hawa wakija hapa wanakuja kuchuma kwa ajili ya nchi zao na sio kwa ajili ya wazalendo. Na kabla hatujaweza kutawala uchumi wa nchi hii hata tungekuwa na bajeti nzuri namna gani tungeandika vitabu mara mia tano kabla wazalendo hawajashika usukani wa kutawala uchumi, tutakuwa bado tunapiga *marktime* na tunajidanganya. (*Makofi*)

Tutawapataje wazalendo ambao watafanya kazi ya biashara? Kwa sasa hivi naweza kusema Tanzania yetu wafanyabiashara watakuwa ni hawa weupe; hawa wenzetu wahindi. Kama kuna waafrika ni wachache lakini ni wajanja na mimi nitaita wengi ni wezi tu, huwezi kuwa tajari ununue *Mercidez-benz,* ujenge nyumba ya ghorofa kwa biashara ya miaka mitatu, mfanyabiashara *five to ten percent profit,* basi huwezi kuniambia unaweza kwenda kukopa benki shilingi milioni 100 kwa kufanya biashara kwa miaka mitatu, hiyo *cash flow* yako utakuwa umepata wapi hizo pesa? Nani atakuamini? Tumekuwa na matatizo ya wauza unga katika nchi hii, tumekuwa na tatizo la wezi wanaoiba katika Serikali na hawa ndio wanaibuka, ndiyo wanakuwa wafanyabishara wakubwa tunaowaamini katika nchi hii. Hawa ni wezi, hawa hawa ndiyo wanachangia vyama vyetu, ndiyo wanatuleta katika Bunge hili na tunawaamini, hawa watu ni hatari! Tumeambiwa kuna wauza unga majina yanapelekwa kwa Rais hayajatoka! Nani amekwisha sikia hawa wezi ndiyo wafanyabiashara tuliona nao, tuanze kutafuta na kujenga wafanyabiashara katika nchi hii.

Tunaweza kujenga wafanyabiashara kwa kuwatumia wamachinga. Wamachinga ndiyo wafanyabiashara wazuri tulionao katika nchi hii. Wamachinga wengine ni wasomi, tusiwadharau ni watu wanaanzia chini na ndiyo watakaofanya kazi nzuri ya kujenga wakiwa wameanzia chini. lakini Serikali inawa-*frustrate,* na wao hatuwapi mwelekeo. Hatuonyeshi kuwapa *support* inayotakiwa. Unasema unampa mmachinga laki moja au shilingi elfu hamsini akaanze biashara, biashara ya kuuza kuku au biashara gani maandazi? Wamachinga unawapa pesa unawafukuza mjini, mjini tunataka miji yetu iwe misafi, tunawafukuza lakini nenda London utakuta *open market* ziko katika barabara mpaka katikati ya mji. (*Makofi*)

Kuna ubaya gani katika miji yetu siku moja moja kuzifunga barabara na kufanya biashara za *open market*, kama wenzetu wanavyofanya katika miji mikubwa. Sisi tunashindwa kufanya hivyo, Mheshimiwa Mramba umepita nchi nyingi duniani, umeona unashindwa kufanya nini barabara za Kariakoo kila wiki moja au mbili unaufunga ule mtaa. Wamachinga wanafanya biashara, wote wanafukuzwa wanaambiwa nendeni Manzese, nendeni porini. Sasa unawafukuza mjini ule mji akae nani? Au wakajifunze wapi kufanya biashara? Mimi hawa wamachinga nina imani nao ni watu wazuri. Jana alisema Mheshimiwa Mrema wamachinga walijikusanya kule Arusha wakiuza mtumba,

Rais alikwenda pale, alivyofurahiwa aliwapa hata hati ya kukaa katika eneo lile liwe lao la kudumu.

Lakini kwa kigezo tunataka miji iwe misafi, tunawafukuza mjini hatuwatendei haki hawa! Mama nitilie hata wale wanaofanya kazi ofisini sasa wameanza kukonda, hawapati chakula. Kutakuwa hakuna tena mama nitilie mjini, haki ya Mungu, wamekonda, hakuna mama nitilie mjini wamefukuzwa wote! Walikuwa wanatoa huduma nzuri, lakini utaratibu jamani ni namna ya kupanga utaratibu ili uweke mambo yako sawa na watu waweze kwenda. Na Wamachinga hawa tuwalinde waweze kuwa ndiyo wafanyabiashara, hawajaiba hawa, ni wasafi na tukiwajenga tutapata wafanyabiashara wasafi. Hawajauza bangi; hawajauza dawa za kulevya. Hawa watakuja kuwa kweli wafanyabiashara wazuri wa kujali nchi hii na ndiyo kweli watakuwa wazalendo wa nchi hii.

Mheshimiwa Mramba kule Moshi kwenye soko la Kibororoni la mitumba kama lile la Arusha, kwa kisingizio cha kusema tunataka usafi wamefunga soko lenye historia ya miaka 20 mpaka 30 na zaidi. Wakafukuzwa wote kama mbwa na kwenda nje. Tunawatendea haki kweli?

Hawa ni wafanyabiashara, ndiyo wamachinga wenyewe wanafukuzwa, baada ya kufukuzwa juzi nimekwenda Moshi nimekuta sehemu ile CCM wamejenga mabanda, wameshajenga zaidi ya ofisi 20 za kufanya maduka *this is shame*! Wameshajenga 20 sehemu ile ilikuwa vijana wa mitumba walikuwa wanauza. Wamechukua ile sehemu wamefanya yao, sasa wamejenga majumba wawaite waje wawatoze kodi wawaambie sasa lipeni. Kitu gani hiki? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokuja katika viwanda, kama mnajua historia ya viwanda, viwanda vikubwa vinaanzishwa na viwanda vidogo vidogo vya kina mama yaani vyumbani na uwani *(beckyard industry)*. Hapa Tanzania tumesahau hilo tunakimbilia viwanda vikubwa, hakuna viwanda vidogo vidogo vya kusaidia ambavyo ndiyo vina *feed industry* kubwa ambapo ndiko watu wangejifunzia, wanatoa *item* moja moja, ndiyo zinakwenda kwenye kiwanda kikubwa. Sisi tumeua viwanda vile tunakimbilia viwanda vikubwa, hii ni *mistake*!

Mheshimiwa Mramba, kule Moshi kuna matatizo ya viwanda vimefungwa. Kiwanda cha madawa ya kahawa na kule tunapanda kahawa; kiwanda cha magunia, wanapiga kelele wanauliza, "Mbunge hufungui viwanda?" Mbunge na viongozi wako. Sasa mimi natoa kauli hapa kama hamuwezi kuvifungua, wale waliuziwa kama hawawezi nipeni mimi nitavifungua. Nirudishieni vyote mimi nitavifufua vyote na watu wa Moshi watapata ajira. Nasema na kiburi hicho ninacho. Maana yake watu wanateseka, mtu ananunua kiwanda anafunga. Sasa tuseme nini, kiwanda unasema utasaidia watu halafu huwasaidi unakifunga, maana yake nini? Mimi nasema Waziri Mramba wakati utakapojibu unanipa hivyo viwanda au unawaambia wavifufue. Nataka jibu na watu wa Moshi wanasikia bwana na wewe ni mdau wa Moshi, kwa hiyo, unajua kule Moshi wanakusikiliza. (*Makofi*)

Sisi tunachosema tungeomba Serikali sasa ipitishe wawekezaji wanapokuja katika nchi hii lazima wawe wabia na Mtanzania mzawa. Hii desturi ya mzungu au nani anakuja hapa *hundred percent share* anaanza kampuni peke yake tuachane nayo! Lazima mzawa achukue sitini mzungu achukue arobaini. Tutawale mali zetu hapa, wanakuja wanatuibia hapa hapa na sisi tunaangalia! Kwa nini? Tungeomba kila mbia anayekuja katika nchi hii na tuifanye ni sheria, lazima mzawa apewe *share*. Na zile kampuni zilizoko hapa sasa tutunge sheria walazimishwe lazima waingize wazawa katika hizo kampuni zao. Ndiyo njia moja wapo ya kulinda maslahi ya nchi hii na ndiyo njia mojawapo itakayofanya nchi hii ikue.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalalamika juu ya maduka yanauza spea *sub-standard* hasa za magari, tunauliza zimeingiaje katika nchi hii unakwenda unaambiwa unataka *genuine* au unataka *non genuine.* Pesa nyingi zinapotea! Nani anaruhusu *non genuine* ziingie katika nchi hii? Mheshimiwa Waziri *non genuine* zinaharibu gari, tunapata hasara kubwa. Kwa nini tusikataze hizi *non genuine spare parts* tukakubali wenye viwanda vya magari yale tu waagize hizo spea au anayetaka kufanya biashara ile alete zile ambazo ni spea halisi. Maana yake tunapata hasara kubwa na sio sisi, ni mwenye magari mengi sana katika nchi hii ni Serikali. Serikali ndiyo inapata hasara kuliko watu wengine wote, kwa nini tusikubali kupiga marufuku? Uganda imepiga marufuku, hakuna *spare* ambazo ni *non genuine*. Kule Uganda huwezi kuona *spare* ambazo utaambiwa ni *non genuine.* Ukienda dukani utapata spea halisi. Kwa nini hapa Tanzania tunakubali kuleta spea feki? Kuondokana na matatizo kama haya, tupitishe sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. (*Makofi*)

**MHE. AHMED ALLY SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara. Moja katika kitu muhimu sana katika nchi hii kuimarisha na kukuza pato la nchi ni kuwa na viwanda. Hakuna nchi duniani ambayo imepiga hatua ya kasi nzuri na ya haraka bila kuwa na viwanda, tena viwanda ambavyo vinalenga katika kununua malighafi inayozalishwa na wakulima wa maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda ndiyo soko na viwanda ndiyo kitu muhimu ambacho ndiyo kinasababisha bei ama ya mazao wanayolima wakulima ya kibiashara kupanda na kuwa katika *stable market* katika nchi yetu. Mkoa wa Dar es Salaam, una viwanda vikubwa, nimemwomba Naibu Waziri kuniletea idadi hapa, nimehesabu nimepata karibu 186, sijui kama ni sahihi. Na ukitizama viwanda vyote vilivyo katika Mkoa wa Dar es Salaam au kwa namna moja katika Serikali ya Awamu ya Kwanza, viliwekwa tu bila kuzingatia umuhimu wa kiwanda kile kinapaswa kuwa wapi. Ndiyo maana uzalishaji au bei ya bidhaa zetu zinakuwa juu mno kuliko vitu tunavyo *import* kutoka nchi za nje. Ukiagiza khanga kutoka India unaikuta rahisi mno kuliko khanga inayotengenezwa hapa hapa. Malighafi kwa maana ya pamba inayotoka Shinyanga inatoka Tanzania humu humu, kiwanda kiko hapa hapa, lakini ukija kufanya tathmini ya *cost production,* sisi bei ya bidhaa inakuwa juu mno kuliko vile tunavyoagiza kutoka nchi za nje. Hii ni kwa sababu hatujajipanga vizuri ni wapi kiwanda kiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wakati ule miundombinu katika mikoa ilikuwa kweli haiwezi kuwavuta wawekezaji. Lakini leo hakuna sababu hiyo. Nitoe mfano mmoja tu. Katika Mkoa wa Shinyanga kulikuwa na kiwanda cha nyama ambacho kilijengwa mwaka 1974, kilishindwa kufanya kazi mpaka juzi kimepata mwekezaji kwa sababu ya miundombinu tu. Naipongeza Serikali walitupatia mwekezaji huyo lakini vilevile nigependa kujua kiwanda hiki kitaanza lini, sio kinanunuliwa tu halafu inakuwa hadithi ndefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichotaka kusema ni kwamba sasa hivi umefika wakati Serikali kufanya utafiti na kuyatambua maeneo ambayo wapi viwanda vinatakiwa viwe Shinyanga. Nitoe mfano, katika Mkoa Mkoa wa Shinyanga ninakotoka ambako ndiko nina uzoefu nao sana, tunazalisha asilimia 60 ya Pamba. Lakini viwanda viko Dar es Salam, kuna viwanda zaidi ya sita vinatengeneza nguo, sasa hivi viwanda vilishindwa kuwekeza Shinyanga kwa sababu Shinyanga hapakuwa na miundombinu kwa wakati ule, lakini sasa hivi maji mengi, barabara lami kutoka Dar es Salaam kimebakia kipande kidogo hapa tu cha Singida. Sasa hivi nina imani kuwa Wizara ya Miundombinu inafanya kazi yake nzuri. Naiomba Wizara kupitia *TIC* kuwa na mikakati na kuwa na data kwamba mwekezaji anapokuja anapewa ushauri vilevile, sio anaachwa tu hivi hivi. Mwekezaji akija anawekeza Dar es Salaam, ndiyo maana tunashindwa kuwa katika ushindani wa bidhaa hata katika Afrika ya Mashariki tu. Unakuta bidhaa za Tanzania ni za bei juu mno kuliko za Kenya kwa sababu malighafi hapa hapa, *labour* hapa hapa, kila kitu hapa hapa, ukija kusema *cost production is high*. Vipo viwanda kweli vinatakiwa viwe karibu na soko hatukatai ambavyo hata malighafi hatuna hapa, tunatuma hapa tunaazima *input* kutoka nje. Lakini kuna viwanda viwe karibu na malighafi. Shinyanga asilimia 60 hatuna kiwanda hata kimoja sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningemwomba Waziri kuwa na mikakati kabambe kufanya utafiti wenye uwezo wa kupokea wawekezaji na hasa wa ndani ya nchi na hata wa nje ya nchi wawaeleweshe kwamba kama unataka kuwekeza kwenye kiwanda cha nguo nenda Shinyanga. Kama unataka kuwekeza kiwanda cha Sigara nenda Shinyanga, kama unataka kuwekeza Kiwanda cha dengu, nenda Jimbo la Solwa. Jimbo hili lina dengu Tanzania hii, labda hamjui sisi tunaongoza. Kule India ndiyo wanunuzi wakuu hawaijui Dar es Salaam, wanaijua kata moja katika Jimbo la Solwa inaitwa Salawe ndiyo makao makuu ya ununuzi ya dengu. Wao ni moja kwa moja wanakuja Salawe, kuna mnunuzi mmoja alikuja Salawe ndiyo mji mkuu wa Tanzania. Kwanza alivyoikuta Salawe akashangaa sana akasema, "mabilioni ya pesa haya tunayonunua dengu, dengu yenyewe mji wake ndiyo huu?" Nikamwambia, "hakuna tatizo, sera ya Chama cha Mapinduzi iko imara tutaelekeza na tutawekeza vizuri." Juzi tu nilikuwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Ngeleja, ninafanya juu chini sana kuona kwamba umeme unafika ili iwe moja katika vivutio vya wawekezaji katika jimbo la Solwa na Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi tukapiga hatua bila kuwa na mfumo na kujipanga kabisa kwamba viwanda vikae maeneo gani, hatuwezi! Tutakuwa tunahangaika tu, sijui tuko kwenye *SADC, COMESA, East Africa, at the end* tunajikuta

bidhaa zetu haziuziki, bei juu. Haiwezekani! Mimi ninao uzoefu wa biashara. Naongeleaa haya kwa uzoefu mkubwa. Tarehe 13 Julai, 2007 tulikuwa na Bodi ya Pamba, tumekaa pale mikakati ni mizuri sana ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Ina mikakati mizuri sana, lengo lilikuwa ni kuongeza uzalishaji wa pamba kwenye maeneo ya wanaolima pamba. Nikasema, hivi sasa tu uzalishaji wa pamba ulioko katika Mkoa wa Shinyanga bei yake ni kati ya shilingi 350 mpaka shilingi 400, wanunuzi wanasuasua, hivi tukiongeza mara mbili ile *gap* ya kuongeza nani anainunua kama hakuna viwanda? Sasa ningeomba Serikali itazame kwamba kuongeza pato la Mtanzania hasa pato la wakulima kwa mazao ya biashara ni kuwa na viwanda, kuwa na soko la uhakika. Kutawezesha Watanzania kuingia kwenye mfumo mzima wa MKUKUTA kwa maana ya maisha bora kwa kila Mtanzania kuwekeza viwanda.

Mimi niko kwenye Kamati ya Uwekezaji na Uchumi. Tulitembelea kiwanda kimoja cha mafuta ya *Korie* kipo Dar es Salaam, nikamuuliza mwenye kiwanda, "ununua malighafi Tanzania asilimia ngapi ya uzalishaji wako?" Akasema, "kumi tu!" Nikaendelea kumuuliza, "viwanda hivi vitatu unaingiza hivyo hivyo asilimia 10?" Inaonekana viwanda vilivyoko Tanzania havisaidii wakulima, vinawasaidia wakulima walioko nje ya nchi. Sasa Wizara ilione hilo tena, na mimi natumia fursa hii kuwaambia kwamba sasa Shinyanga imekamilika tuna maji mengi, miundombinu inakamilika vizuri.

Tunaye Mkuu wa Mkoa safi, Mheshimiwa Balele, anafanya kazi vizuri. Mje Shinyanga, tunahitaji viwanda vya nguo, sigara, *juice*, dengu, tunahitaji viwanda vya kila aina. Shinyanga imezungukwa na nchi jirani Rwanda, Burundi, Kenya, Uganda, Zaire, vilevile imezungukwa karibu na mikoa sita. Kwa hiyo, soko la ndani tu peke yake linatosha mno kwa kumwezesha yule atakayewekeza Shinyanga pale ku-*operate* na kupata faida.

Kuna soko la nchi jirani, ni kupanu wigo wa jinsi gani tuuze bidhaa zetu nchi jirani na hiyo ndiyo moja katika mikakati itakayoisaidia Serikali kuongeza pato lake badala ya kujibanana leo tunaongeza bei ya mafuta kesho tutaongeza sijui *alcohol* na kadhalika. Kuongeza pato la Serikali ni kutengeneza makampuni mapya, viwanda vipya ndiyo kunajenga ajira kwa suala zima la kuwa na *power of purchasing* ili Serikali iweze kupata pato lake zaidi ya hapa tunavyopata sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona dakika kumi hizo zimepita, lakini ningependa kuongelea sasa *TBS,* uagizaji wa magari kutoka Dubai, Japan, *London* na kadhalika. Ukinunua gari nje ya nchi, sasa hivi wanakwambia lazima uikague. Mimi napingana kabisa na hili suala.

Tulipokuwa kwenye Kamati ya Uwekezaji na Biashara tuliwaagiza hawa watu wa *TBS* kwamba watuletee taarifa ya jinsi gani umuhimu wa kukagua haya magari kutoka Dubai, Japan au *London.* Wakasuasua, tukashitukia tu wameruka Dubai sijui wameenda, wameongea na watu kule, wakawaahidi mpaka jinsi nani na nani watawapa hizo *tender*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naongea kwa machungu sana. Sasa hivi Tanzania tunafanya juu chini ili *balance of payment of our country* iwe *favourable* lakini

utakuta tunatoa maamuzi mengi bila kujali kuna *self interest* tu pale, kama mtu mnamweleza kwamba suala la ukaguzi wa magari halina umuhimu wao nang'ang'ania, kuna nini hapo? Aliyepewe *tender* kwa wakati ule sijui sasa hivi amejenga nyumba ya dola milioni 6 kwa fedha wanayokamuliwa Watanzania.

Naongelea Dubai tu acha *Japan*. Hivi alizokusanya yeye ni ngapi? Unalipa dola 130 kwa gari, na kuna dola 130 zingine gharama ya kutoa kuipeleka, ukitaka kujua fedha ambazo Watanzania wanapoteza kwa kitu ambacho hakina *impact* na uchumi wetu chukua magari yanayotoka nje kuja Tanzania mara dola 130 kwa gharama za kule. Kwa sababu eti ya kuifanyia ukaguzi gari ili ije safi.

Mimi nimekwenda kununua gari nimeikagua jinsi ninavyojua, sasa hii gari inanifurahisha, wewe unanilazimisha nikaikague, kama kuna chochote kibovu si nitaitengeneza Tanzania tu! Sheria ya *TRA* inasema gari ikiwa chini ya umri wa miaka saba unalipa sawa sawa, ikizidi zaidi ya miaka kumi unapigwa ushuru chakavu, tayari mtu anapigwa ushuru chakavu, wewe unaikagua ya nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba suala hili la ukaguzi wa magari liondolewe kabisa, halina umuhimu wowote, linatengeneza *self interests.* Yule tena anayepata zaidi ni yule anayepewe *tender* siyo huko! Maana yake ukiwa kule wanaongea wanunuzi wa magari, wanalalamika, wengine wanasema hata *TBS* wana nini katika hili au saa nyingine kuna vigogo wanasema hapana, tutakwenda kuliwasilisha Bungeni na namwomba Mheshimiwa Waziri wa Viwanda alichukulie kwa muhimu wake kuliondoa kabisa. Hili ni tatizo kubwa kwa wanunuzi wa magari. Serikali inapoteza fedha za kigeni kwa kitu ambacho si muhimu kabisa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibiwe hilo na majibu yenyewe yawe kama ninavyoona kwa sababu ndiyo maoni ya wanunuzi wa magari wa Tanzania wanayotoa nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeiomba *TIC* na yenyewe iwe na data, zilizo sahihi na zilizo na mwelekeo wa kuwaelekeza wawekezaji kuwekeza sehemu gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona *time* imeisha, naomba kuunga hoja mkono kwa asilimia mia moja, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi mchana huu ili niweze kuungana na wenzangu kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Awali ya yote naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha vizuri bajeti yake, naomba pia niwapongeze watendaji wote wa Wizara hii kwa namna moja au nyingine kwa kusaidia kupunguza tatizo la umaskini tulionao Watanzania. Bila kuchelewesha muda kwa sababu tunaokoa muda hapa naomba niendele moja kwa moja katika mchango, nina mchango ufuatao: -

Kwanza, Serikali ya Awamu ya Nne ina jitihada za makusudi za kuhakikisha inatoa vipaumbele kwa mikoa ya pembezoni, mikoa ambayo iko nyuma kiuchumi. Lakini nasikitika kwenye bajeti hii sijaona mahali popote ambapo panalenga moja kwa moja

maalumu kwa ajili ya mikoa hiyo. Mikoa kama Mtwara, Lindi, Kigoma na Tabora inatajwa ni mikoa yenye matatizo sana *(marginalized regions)* lakini hapa sioni jitihada za makusudi zinazoonyeshwa kuamua kuikoa kwa makusudi kabisa mikoa hiyo. Sasa ningependa Waziri anipe maelezo ya kutosha ni hatua gani za makusudi zinazochukuliwa na Wizara hii ili kuisaidia mikoa hiyo ya pembezoni? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nitoe mfano rahisi tu, mimi nilifurahishwa sana na bajeti ya Wizara ya Elimu na Ufundi. Waziri alituambia kabisa kuwa kwenye bajeti iliyopita Mkoa wa Lindi ulitengewa kiasi fulani, lakini sasa tunawa-*fever* kwa sababu *marginalize* tumewaongezea, Mtwara hivi, Ruvuma hivi, Rukwa lakini hii hapa haipo, mimi ningependa nipate maelezo ya kutosha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna visingizio. Sasa mahali kama Mtwara kuna bandari nzuri, kuna uwanja wa ndege mzuri, barabara nzuri tunayotarajia katika muda mfupi ujao ikamilike, gesi ya Mnazi *Bay* ndio hiyo sasa, kwa nini tusiwe na mikakati moja kwa moja barabara ikiisha ile kesho kutwa hapa tuanze kufanya vitu vya kiuchumi? Nadhani ujumbe umefika kwa sababu tunaokoa muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa anaweka jiwe la msingi la mradi wa gesi ya asilia ya Mnazi *Bay* alitoa maelezo kwa wananchi kwamba ziko jitihada zinafanywa za kuhakikisha kunafunguliwa kiwanda cha mbolea na kiwanda cha vifaa vya plastiki. Mimi nakumbuka ulikuwa mwezi Novemba, 2006 muda huo nilidhani ulikuwa unatosha kwa Wizara kutoa tamko hapa nini sasa kinafanyika au inawaahidi Watanzania wale wa Mkoa wa Mtwara lakini katika bajeti hii imekuwa kimya. Mimi ningependa nipate maelezo ni jitihada gani zinachukuliwa kwenda sambamba na ahadi ya Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 82, Jedwali la saba mauzo ya nje ya mazao asilia ya biashara yaani *traditional export crops* imeelezwa kuwa mwaka 2006/2007 nchi yetu iliweza kuuza korosho tani 92,342. Mimi ninaamini kwamba tani hizi ni chache sana, zingewezwa kuuzwa zaidi na zaidi na tungeweza kuipatia pato nchi yetu pengine hata maradufu kama jitihada za makusudi zingeweza kufanywa kuhakikisha kwamba wakulima wale wa korosho wanasaidiwa.

Katika hali ya sasa ya biashara ya korosho kuwa legelege na ovyo ovyo malalamiko mengi ya wananchi katika hali ya sasa ya wazalendo walionunua viwanda vya korosho kwamba wanashindwa hata kusaidiwa haraka haraka kupata *credit guarantee scheme* ili iweze kuongeza thamani, korosho zetu zingeweza kuongezwa thamani *(value added).* Zingeweza kuleta ongezeko kubwa sana la uchumi wetu, tungeweza kuuza na kuleta pato kubwa sana la nchi yetu lakini kwa kweli hatujawa *serious,* tumewaacha tu vyovyote, mimi nashangaa sana, viwanda vile sasa tumewauzia wazalendo hivi kuna tatizo gani?

Mheshimiwa Naibu Spika,  naomba Wizara ya Viwanda, Masoko na Biashara isiahidiane na Wizara ya Fedha kumaliza hili tatizo, hivi wazalendo wale watakimbilia wapi? Tunataka tatizo gani? Tuwasaidie, tena wengine wana rasilimali ambazo zingekuwa vyanzo vya wao kuweza kukopa lakini tumekuwa tukiwazungusha,  nafikiri wakati umefika sasa kuwasaidia Watanzania hawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu waliotangulia kusema hasa nikimkariri Mheshimiwa Sinani, Mbunge wa Mtwara Mjini, alisema sana kuhusu suala la viwanda vidogo vidogo.  Mimi nina habari kwamba Wizara ya Viwanda na Biashara warasimu kidogo, yuko mtu hapa alitaka kuwekeza Mtwara kwa kiwanda cha *juice* za maembe na kule maembe yanaoza lakini urasimu wa Wizara yetu umefanya mpaka akakimbilia Msumbiji, sina *proof* za kutosha kuthibitisha hili lakini ninachotaka kusema kama hili lipo tubadilike jamani *bureaucratic procedures* za nini? Tunataka kujenga uchumi imara wa nchi yetu na hii hali mpya, kasi mpya na nguvu haiwezi kwenda kama uchumi wetu hatuuboreshi  ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala la wakala wa vipimo, wananchi wetu wamekuwa wakinyonywa sana, wamekuwa wakinyonywa vipimo visivyoeleweka.  Mara kangomba, mara lumbesa, mara bata *oil* na kadhalika. Hata ile mizani michache iliyopo kule vijijini imefanyiwa ujanja ujanja haina vipimo *standard* vinavyokubalika. Sasa nimefanya utafiti mdogo nikagundua wakala wa vipimo hawajapewa uwezo wa kutosha kuweza kuwafikia Watanzania wote vijijini tukikumbuka kwamba Watanzania wengi wanaishi vijijini.  Mimi nafikiri Wizara iwaangalie hawa wakala wa vipimo iwasaidie wafike vijijini kule, na ushahidi mwingine, hata jana nilisoma magazeti hapa, jana na juzi kulikuwa na habari kwamba hata hawa wauza mafuta hizi  *filling station* s zaidi ya asilimia 75 wamefanya ujanja.   Nadhani wakati umefika sasa tukachukua jitihada za makusudi kuhakikisha Watanzania wengi hawanyonywi kama hali ilivyo sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala la malighafi ya sementi,    *gypsum,* nashukuru baadhi ya waliotanguliwa waligusa hili lakini mimi nataka kuongeza, ukanda wa Mtwara na Lindi una *gypsum* ya kutosha sana na wala hatuna sababu ya kununua *gypsum* nje badala yake sisi ni kuuza  kutengeneza viwanda vya semeniti  pale ambapo *gypsum* ile ipo. Kijiji kama Mandawa pale Lindi kuna *gypsum,* kama basi miundombinu ya Mandawa ni pagumu , hivi  haiwezekani kuweka Lindi mjini pale au Mtwara? Tunarajia nini na tunataka nini? Rasimali tunayo lakini hakuna jitihada tunazozifanya za makusudi kuhakikisha kwamba rasilimali hizo tunazitumia ipasavyo. Mimi ningeomba Wizara ya Viwanda ifanye kila jitihada inayoweza kuhakikisha kwamba kama nilivyotangulia kusema awali *gypsum* hii ipo katika mikoa inayoitwa *marginalized* basi iwe *considered* tujenge pale kiwanda ili tupunguze umaskini wa wananchi pale.  Hatuna sababu ya wananchi wale kuendelea kuwa maskini maana kuwepo kwao pale na kiwanda kikiwepo  kina-*create employment*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la *EPZ,* mimi naona suala la *EPZ* yale maeneo ya uendelezaji wa mauzo ya bidhaa zetu  nje  ni kama kwamba kazi nyingi ni *paper work* zaidi kuliko vitendo. Kasi iliyopo siridhishwi nayo.  Kwa kweli  ningeomba Wizara sasa ichukue jukumu la makusudi kuongeza kasi  na miundombinu ya hizo *EPZ* ili  tuboreshe uchumi wetu, uchumi wetu ukue. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwa *serious*, tukiwa *committed* mimi nina hakika uchumi wetu utaongezeka na hivyo tutaboresha maisha ya Watanzania. Uliomba suala la muda na ukaomba watu wakuachie dakika mbili mbili na mimi nafikiri niwe muungwana ili wenzangu wapate angalau kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naweza kusema sasa naunga mkono hoja lakini ningeitaka Wizara itoe maelezo ya kutosha kweye zile hoja nilizotaka maelezo, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niongelee machache kuhusu bajeti hii muhimu sana katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ningependa kuchukua nafasi hii kuwapongeza wananchi wangu wa Musoma Vijijini kwa kazi nzuri wanayofanya ya ujenzi wa shule, ujenzi wa barabara kwa umoja wao mkubwa hususan upande wa Halmashauri ya Musoma Vijijini, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa narejea kwenye hoja hii muhimu ya Wizara ya Viwanda. Wiki iliyopita nilipozungumza nilizungumza kuhusu elimu, nilisema elimu tuliyonayo haitakuwa na maana kama malengo yake yatakuwa siyo kupeleka vijana wetu kwenye viwanda. Nilisema viwanda havitakuwepo mpaka hapo shule zetu zitakapobadilika kuweza kutoa mfumo wa sayansi ili wanafunzi wengi wafanye viwandani. Hiyo ndiyo kasoro kubwa. Hivi sasa hakuna ushirikiano unaojitokeza kwa dhati kati ya Wizara ya Viwanda na Wizara ya Elimu hususan pale wanapofanya mipango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa wanafunzi wanaomaliza shule huenda barabarani. Hawaendi viwandani kwa mantiki hiyo ile ndoto ya kuwa na ajira nyingi au tutatoa ajira kwa Watanzania nadhani haipo. Vijana wetu watazidi kubaki barabarani kwa kuwa viwanda havipo. Lakini kwa nini viwanda havipo ukiacha mambo ya wanafunzi wenyewe kwamba hatuna wanafunzi wanaofanya masomo ya kuweza kukidhi mahitaji ya viwanda na kwa nini tatizo hili ni kubwa?

Kwanza, ukiangalia Bunge hili tulivyo ndani utaona makochi tunayokalia yote tuna-*import* kutoka nje, ukiona *carpet* humu ndani inatoka nje, tukijiona sisi hata suti tunazovaa zinatoka nje, tai tunazovaa zinatoka nje. Tunaagiza nje hiyo ndiyo sababu shilingi yetu inazidi kuteremka chini siku hadi siku. Wenzetu India hawafanyi hivyo, India ukiona akina mama wa kihindi wao wanavaa sare za kutoka India, sare ndio zile nguo zao ndefu huvaa akina mama. Zinatengenezwa India kwa *rupee* yao. Maana yake wahindi wapo karibu bilioni 1.3 lakini nguo za wanawake ni za kwao, sisi Tanzania kila kitu *imported*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunapenda viwanda vya nje hatupendi viwanda vya Tanzania. Tunapoenda kantini kuanzia sufuria, mpaka kijiko kinatoka nje,

hata *biscuits* zinatoka nje, *sausage* zinatoka nje, jamani hata *sausage* hatuwezi kutengeneza hapa?

Viwanda hakuna! Inanikumbusha miaka 25 iliyopita ndugu yangu, rafiki yangu Mheshimiwa Basil Mramba akiwa Waziri wa Viwanda, nilianza kutengeneza maziwa ya watoto nikapigwa vita sana pale. Nilikuwa natengeneza *baby food* pale Vingunguti wakati huo huo rafiki yangu Abdu Faraji alikuwa akijaribu maziwa ya watoto kule Arusha.

Viwanda vyote vilipigwa vita, hakuna hata kimoja. Nililetewa wataalamu wengi kutoka nje kuja kuua kiwanda hicho cha kwangu. Walithubutu kuniletea hata mwalimu aliyenifundisha *Food and Drug Law* kuja kuki-*condemn* kiwanda hicho. Alipofika akaniambia Mkono unatengeneza maziwa ya watoto? Nikamjibu, ndiyo, akaniambia tengeneza.

Mheshimiwa Waziri Mramba alikuja pale na Marehemu Chiduo kuja kunitetea, miaka zaidi ya 25 iliyopita na maziwa hayo yalikuwa yananywewa na Watanzania. Nakumbuka siku moja mama mmoja akiwa Bungeni alisema maziwa haya ya Mkono watoto wakinywa wanatema na mimi nikaulizwa na mtaalamu kwa nini wanayatema? Nikasema wamezoea maziwa ya kizungu ndio maana haya wanayatema. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hiyo ndiyo hali halisi. Jana tulipitisha bajeti ya Wizara ya Maliasili, pale sehemu wanapandisha bei ya magogo, gogo moja la *hard wood* nadhani lina-*cost* zaidi ya dola 1,300 kwa *cubic* mita kwa kuwa *hard wood* ndiyo hutumika kutengeneza viti na meza nzuri.

Ukienda Mahakama Kuu ya Tanzania utapata ile *hard wood* yetu ndiyo imetengeneza meza zote. Sasa unawaambia wenye viwanda Tanzania wanunue *hard wood* kwa bei kubwa walizoweka Wizara ya Maliasili .

Ndio maana *hard wood* yetu hupelekwa nje kimagendo na badala yake wenye viwanda hulazimika ku-*import cheap labour* kutoka *Mozambique. hard* Sasa najiuliza AGOA tunayozungumza Watanzania wapeleke *manufactured goods* Marekani, itatokea kweli? Haiwezekani! lazima Viwanda vipate *incentive* ya kutumia malighafi ya Tanzania siyo ku-*import* malighafi kutoka nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia ofisi za Serikali wakoloni waliacha meza nzuri za mninga, meza zile zote zimetupwa. Tumeagiza meza za *formeca* halafu unasema shilingi yetu inaporomoka sana wewe unaagiza tani kwa tani kutoka nje na wewe hupeleki nje, itakuwaje shilingi yako iwe *strong*? Haiwezekani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Musoma Vijijini mimi sina kiwanda chochote. Kwa hiyo, namwomba Ndugu yangu Mheshimiwa Basil Mramba aje Musoma Vijijini ajionee mwenyewe *SIDO* tunayoizungumzia haipo pale. Miaka 45 ya Uhuru hakuna *SIDO* Musoma. Watoto wetu wanasoma shule za sekondari, wanakaa *boarding,* lakini

*SIDO* miaka 45 haiwezi kutengeneza hata jiko la kuweza kutumia rasilimali za kwetu hapa.

Hata jiko tu Watanzania hatuwezi kutengeneza, *biogas* hatuwezi kutumia. India ukieenda unakuta kila Mhindi ana ng'ombe na ng'ombe huyo kinyesi chake ndio *energy* yake anayoitumia.

Kwa hiyo, ng'ombe anampa maziwa anampa na kuni, Tanzania ng'ombe wanatupa maziwa. Tuna miaka 45 badala yake tunakata miti halafu linakuwa ni janga tunaloliona kama ukame na kadhalika. Mimi nashauri tuangalie tulikotoka hivi wazazi wetu walikuwa wanafanyaje kuhusu *energy* ya kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwetu kuna watu wanaitwa wahunzi, waingereza wanaita *smith.* Makabila mengine wanawadharau sana hawa wahunzi , walikuwa wanapuliza chuma, wanatengeneza majembe ya kwao, walikuwa hawa-*import* na walikuwa wanajilisha. Leo hawa wahunzi tumewatupa, wala hatuwasaidii na tunasema tuna Wizara ya Viwanda, tunazungumza juu ya Liganga, miradi mikubwa mikubwa mnahitaji wahisani kutoka India, China, Marekani.

Mimi nadhani tungeenda sehemu nyingine kuliko kujilinganisha na mataifa makubwa namna hiyo, yale ni *advanced* yanatumia sayansi na teknolojia sisi bado hata sayansi ya kupika chakula hatuna, utafiti tunaozungumza kwenye bajeti hii upo wapi?

Ningependa kuona *boarding school* zetu zote zinatumia malighafi ya kwetu hapa, zinatumi *cow dung* au zinatumia *biogas* badala ya ku-*import* na ku-*keep importing* hatutafika tunakokwenda. Tujiulize tatizo la Tanzania ni la nani? Ni la Watanzania au ni la wananchi wanaotuletea vitu.? Tanzania yetu ni sisi wenyewe. Mipango yetu kwa sasa ni mibaya. Tubadilike. Tuanzie Bungeni humu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Musoma Vijijini kuna mawe mazuri sana na ukiyakata unapata marumaru nzuri sana, kwa nini nchi nzima ina-*import* marumaru kutoka nje ambapo sisi tuna mawe mengi ya kufanya marumaru nzuri kuliko tunayo-*import*? Wizara iko wapi? Ningependa tufikirie kwanza nyumbani ndio nje, tutakuza uchumi wetu kwa kasi mpya na nguvu mpya kuliko sasa tunavyofanya.

Lakini pamoja na hayo ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri alizofanya, nimeona *plan* yake pengine ata-*reverse* hii *trend* tuwe na *industrial policy* ya kutunza tulichokianza na kukiendeleza kwa kutumia watu wetu wa Tanzania lakini hilo tu litatokea kama tutabadilisha tena mfumo wa shule, tusipofanya hivyo, tusipofundisha sayansi viwanda, ni ndoto haiwezekani! Ongea na Wizara ya Elimu tutafika tunakoenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache niliyosema naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge tukirudi saa 11 nafikiri tunaweza kutoa ruhusa kwa wachangiaji watatu: atakuwa Mheshimiwa Chrissant

Mzindakaya, Mheshimiwa Juma Kaboyonga na Mheshimiwa Richard Nyaulawa. Kwa hiyo, nategemea tutaenda vizuri.

Lakini pia Mheshimiwa Spika asubuhi alitangaza kwamba Mwenyekiti wa *APNAC,* Mheshimiwa Dr. Zainab Gama anaomba wanachama wake wa *APNAC* wakutane Jumapili saa tano kwenye Ukumbi wa Msekwa kwa ajili ya kuzindua taarifa ya *APNAC*. Kumbe si wanachama wa *APNAC* tu, ni Waheshimiwa Wabunge wote. Kwa hiyo, masahihisho ni kwamba ni Waheshimiwa Wabunge wote wanakaribishwa kushiriki katika shughuli hiyo siku ya Jumapili saa tano katika Ukumbi wa Msekwa. Baada ya kusema hayo naomba nisitishe shughuli za Bunge mpaka jioni saa 11 na ninawatakia mchana mwema.

*(Saa 6.56 mchana Bunge liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)*
*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, katika *Speaker's Gallery* kuna wageni wa Spika; Mheshimiwa Dr. Billal, ambaye alikuwa Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Awamu ya Tano. Halafu ni mmoja wa wanasayansi wetu wa mionzi wa mwanzoni kabisa, yupo na wasaidizi wake. Karibu sana, tunafurahi kukuona kwenye *gallery* yetu.

Lakini pia tuna wanafunzi wetu wapendwa sana wa Shule ya Msingi Chazungwa, Wilaya ya Mpwapwa, wanafunzi 36 na walimu wao. Tunawakaribisheni sana, mlikotoka ni mbali, tumefurahi mmepata nafasi ya kuja, karibuni sana. Wageni wengine tunawakaribisheni, hii ni *Public Gallery,* kila mtu anaweza kuja, karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, nilisema wakati tunafunga Kikao cha Bunge mchana kwamba tutakuwa na wachangiaji watatu; Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, tutamalizia na Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutumia nafasi hii kukushukuru sana, kwa kunipa nafasi hii niweze kutoa mchango wangu katika hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza kabisa, ningependa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Naibu Waziri na Wataalam wao wote, kwa maandalizi ya hotuba hii nzuri, ambayo Waziri ameiwasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kwetu tuna methali inayosema; "mwindaji usinyee kambi, kwa sababu unaweza ukarudi tena katika kambi hiyo." Kwa hiyo, ninafurahi kama Mheshimiwa Basil P. Mramba aliondoka vizuri katika Wizara hii na amerudi na wenzake wamempokea vizuri. Tunamtakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, ningependa kutoa mchango wangu kama ifuatavyo: Kwanza, kuhusu Sera ya Viwanda. Mimi ushauri wangu ni kuwa, sera ni nzuri, lakini nadhani mambo ambayo ningeishauri Serikali ifanye ni makubwa mawili.

Kwanza, itengenezwe Programu na Mikakati ya Kutekeleza Sera yenyewe na katika sera hiyo tuseme nani atakayeleta Viwanda Tanzania. Kwa sababu hapa katikati, umeingia ugonjwa kana kwamba, bila wawekezaji nchi haiwezi kwenda. Hiyo ni kasoro kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wenye wajibu wa kuiendeleza Tanzania ni Watanzania wenyewe na si wageni katika nchi hii. Nitatoa mfano unaoweza kueleweka, South Africa walikwishaweka sera na ndiyo nchi pekee inayoweza kuitawala Afrika kiuchumi. Miradi yote wanayopeleka katika nchi zote ikiwemo Tanzania ni kuja kuwekeza ili wapate faida na maendeleo ya nchi yao, ndiyo ukweli huo. Kule South Africa kwenyewe wafanyabiashara wa nchi ile mwisho kikomo cha kutoa fedha za kigeni ni kama dola 60,000. Lakini huku kwetu kwa sababu mlango uko wazi wa ku-*invest,* wanaweza kuchukua fedha wanazotaka.

Lakini vilevile tuona tofauti Watanzania wote Wazalendo, waliowekeza katika nchi hii, fedha zao za kigeni wanazozalisha zinarudi hapa nchini. Juzi nilikuwa Arusha, naomba kuwapongeza Watanzania wa Mkoa wa Kilimanjaro na Arusha, jinsi wanavyohangaika kwa maendeleo, hoteli nzuri zote za kitalii zilizojengwa katika Mkoa wa Kilimanjaro na Arusha ni za Wazalendo wa nchi hii. Nawapa pongezi sana. Hii ndiyo tunayoitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano mwingine mzuri, sisi majirani zetu Kenya, walibanwa na wakubwa kutokuwapa misaada, maana ndiyo ugonjwa wetu sote. Wale Wakenya wamejitahidi sana wenyewe kwa kutoza kodi na ku-*invest* wenyewe na sasa wanaongoza kwa kuwa na fedha za kigeni kuliko sisi Tanzania, ambao tunaendelea kupata misaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nasema hii ni shule tosha kwa mfano wa nchi jirani ya Kenya. Kwa mfano, hivi leo ninazungumza shilingi za Tanzania 17, ndiyo sawa na shilingi moja ya Kenya. Kwa hiyo, lazima na sisi tujitahidi, ukipima rasilimali iliyopo Tanzania na iliyopo Kenya, sisi tunawashinda. Mwenyezi Mungu, alipounda dunia na akasema binadamu ninawapeni vyote vilivyopo huko mkatawale, ukiorodhesha rasilimali zilizopo Tanzania, Mungu alitupendelea kwa kuumba hakuna tulichokosa. Tumepewa kila kitu, lakini sasa mbele yetu ni *challenge;* namna gani tunatumia hizo rasilimali zetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naomba Wizara itusaidie, nani ataleta viwanda? Mimi ninapendekeza moja kwa moja kwamba, kwa kuwa Serikali ina Shirika la kuhudumia Viwanda *(SIDO),* naomba Serikali ikubali kurudisha *SIDO* ya zamani, maana sasa hivi tunakoelekea, *SIDO* imekwishakuwa ni *Housekeeper* wa biashara ndogo ndogo. *SIDO* ilianzishwa kwa ajili ya kuanzisha viwanda vidogo vidogo, siyo kufanya biashara na *Industrial Estate* ambazo Mheshimiwa Waziri ni shahidi, tulijenga mimi na yeye; wakati mimi nikiwa Mwenyekiti na yeye alikuwa *Director General*, sasa nyingine zimeingiwa popo. Kule Sumbawanga tulijenga *Industrial Estate,* tuliweka *machinery*

zilishauzwa kwa watu binafsi na wamekwishaziondoa *Industrial Estate*. Sasa tunakoelekea ni tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo mimi na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, tulikwenda *Study Tour* India. Tulipokelewa na tulisaini Mkataba wa kwanza wa Ushirikiano kati ya India na Tanzania wa Viwanda Vidogo. India hivi sasa tunavyozungumza, ajira kwenye viwanda vidogo ni watu milioni 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, kuzungumzia viwanda vile vikubwa bila kuzungumzia viwanda vidogo ni kujidanganya. Lazima tukubali kwamba, maendeleo ya haraka yataletwa na viwanda vidogo na viwanda vya kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, India leo wana Wizara ya Viwanda Vidogo na vya Kati. Natoa mifano ya haki, tulikwenda Japan, Wajapani magari mnayoyaona wanatuletea hapa Toyota, hawafanyi kila kitu ndani ya kiwanda kikubwa, kuna *small industries*. Wapo wanaotengeneza *spoke,* wapo wanaotengeneza magurudumu na ndiyo wanaounganisha gari likamilike na kuletwa Tanzania, lakini vitu vingi vinatoka katika viwanda vidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nashauri sasa Serikali mwaka ujao iipe *SIDO* fedha ili ianze kujenga viwanda, ku-*promote* watu wadogo kueneza viwanda nchini, badala ya kuwa na Wamachinga, haiwezekani. Tanzania kasoro iliyopo, vitu vya kuagiza kutoka nje ndivyo vinatufanya tupate kodi ya ushuru. Kwa sababu ndani ya Tanzania, ukifanya utafiti wanaozalisha ni wachache sana, wanaochuuza ndiyo wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimewahi kufanya hesabu, kilo moja ya sukari tangu inapotoka kwenye Kiwanda cha Mtibwa au Kilombero mpaka ifike Sumbawanga, imekwishapita kwenye mikono saba, watu watapata bei nafuu hapo, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ukweli mwingine, *interest* ambazo zimewekwa na mabenki yetu, zinawekwa kwa ajili wafanyabiashara si kwa ajili ya wakulima na wenye viwanda. Nani atajenga kiwanda Tanzania, halafu akope mkopo alipe *interest* ya asilimia 18 mpaka asilimia 30? Hao wanaolipa *interest* hiyo ni wauza unga, mtu anayezalisha mahindi, hawezi kulipa *interest* hiyo. Hivi bei ya mahindi iko wapi ya kulipa *interest* hiyo? Kwa hiyo, lazima tukubaliane na ninaomba Serikali bila kuchelewa, itangaze rasmi na ianzishe *Tanzania Investment Bank,* iwe ni Benki ya kuleta maendeleo ya viwanda na kilimo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano, wawekezaji wote mnaowaona kuja hapa, wanakuja na *package* mbili; moja ni ya benki za kutoka kwao na nchi zao zimeziambia zile benki zitoze *interest* nafuu, ndiyo maana wanatengeneza migodi. Hayo yote mnayoyaona siyo fedha zao, zile ni fedha za benki za kwao na Serikali zao kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo na sisi tuanze kuzungumza na marafiki zetu, namna ya kuanzisha hizo benki. Kwa mfano, *CRDB* wamesaidiwa sana na Denmark,

waliingia pale Denmark, mimi nina uhakika kwa jina zuri, ambalo hata Rais wa Awamu ya Nne, amelijenga Duniani na heshima ya Tanzania, uwezo wa kufanya mambo hayo makubwa tunao mkubwa sana. Kwa hiyo, natoa ushauri huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba niseme aina gani ya viwanda tunataka vitangulie mbele, tuanze na viwanda vipi. Kwa mfano, nilikuja hapa na chupa za *juice*, nilikuja hapa na chupa za pilipili za kutoka Canada na sehemu nyingine, yaani ile pilipili ya kusindika inatoka Canada, inakuja hapa. Sasa huo ni utani mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Uarabuni ni jangwa, madukani nenda utakuta *juice* za matunda *proper,* wanaagiza matunda kutoka Tanzania na kutoka katika nchi nyingine, wanakwenda kusindika kule. Sisi viwanda vyetu ni vya kuchanganya dawa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa sababu ya uzoefu, leo atamke rasmi hapa; je, ni aina gani ya viwanda tutajenga? Tutaendelea kuwapa watu *juice* zetu za kuchanganya dawa za *chemicals*. Kwa nini tusiwape fedha watu waagize mitambo ya kuja kuchanganya *juice*, ku-*refine juice?*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Waziri ni shahidi, *FOIL* ndiyo kilikuwa Kiwanda Tanzu cha Kwanza. Kilikuwa kinauza bidhaa zake mpaka Kenya na kilikuwa kinatumia malighafi ya pamba ya Mwanza, kile kiwanda kimeuawa. Wanao-*refine* mafuta, wamekuja wamejenga viwanda na Serikali imekubali, wanakuja wanalidanganya Bunge hapa kwamba, wanaleta *crude oil,* waongo. Mimi nimefika Malaysia, mwaka juzi niliiomba Serikali iende ikaone, akaenda Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, Katibu Mkuu wa Rais, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, wote wamekwenda Malaysia wamekuta hakuna *crude oil*, hao wanatudanganya tu hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa zuieni viwanda hivyo, anayetaka kujenga kiwanda cha mafuta, mwambie aingie Mkataba na Mkoa na mimi namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, yupo imara sana na amekwishaiita Mikoa yote. Ninapendekeza Ofisi ya Waziri Mkuu yenyewe iongoze, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, wao wenyewe wakae watengeneze mpango na waiambie Mikoa iingie ifanye mikataba na wenye viwanda vya kutengeneza mafuta, tuachane na takataka za kutoka nje. Tutaendele kuwa manamba mpaka lini kwa nchi tajiri kama yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa ninazungumza kutokana na usikivu wa Serikali yetu, imewapiga kodi ile *ten percent* walikuwa wanabishana muiondoe. Leo *sunflower* imepanda bei na Wakenya wanakuja kununua *sunflower* hapa. Haya ndiyo mapinduzi. Kwa hiyo, napendekeza hiyo kwamba, mazao ya michikichi, *sunflower* na kadha wa kadha, yaanze kulimwa kwa mikataba. *Contract farming* iwe ni uamuzi na Sera na Mikoa itambuliwe, ipewe malengo na isimamiwe kutekeleza mambo hayo. Tuseme miaka mingapi ijayo tutajitegemea kwa vitu ambavyo tunaweza kama *juice*, mafuta ya kupikia na kadha wa kadha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka niseme Mheshimiwa Waziri ni shahidi, tulikwenda naye Arusha, tukamkuta mtu mmoja ana kiwanda kama futi 6 kwa 10, ameweka mashine moja, akasema Mr. Milicer, *I make six million by turnover here.* Kuchanganya *juice* kwenye chupa, anafanya biashara kuliko wanaolima. Sasa hii nayo si nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa iwe *package* pia, tutafsiri elimu tunayotaka kutumia. Kwa mfano, Watanzania wanaosoma katika vyuo vilivyopo, tena elimu ile tuliyorithi *collar job* wanaokwenda kusoma Ulaya hawazidi 100. Sasa wenzetu kwa mfano, Waingereza tulikuwa huko mwaka jana, mimi na wenzangu, Muingereza mmoja alituambia kwa Kiingereza: *"How slight now India and China*? Mimi nikamwuliza kwa nini, akasema Bwana hao watu wameamua kusomesha watu wao kweli. Tena wanaingia kwa nguvu sana katika masomo ya sayansi. Wachina wanasomesha kwa mwaka mmoja watu milioni nne. Wahindi wanasomesha watu milioni tatu, sisi tunapeleka nje watu 100. Sasa mimi nauliza swali ni sayansi na teknolojia gani sisi tunataka kwenda katika milenia hii, mbona mimi siioni tafsiri hasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano mmoja, nilipokuwa nimejenga kiwanda pale, ile mitambo niliyoweka ya *refrigeration* inatumia *ammonium gas na* hivi vitu mimi nimevisoma katika umri wa utu uzima. Sasa nimetafuta Mtanzania wa kuja kufanya *welding* ya *pulps* zile ili *ammonium gas* ikija kuwekwa isivuje, nimemkosa. Wazungu wakaja kuniambia kwamba, wao wanao Kenya, wakanipa kampuni niagize watu wa kufanya *welding* vile vyuma vya *ammonium gas* kutoka Kenya. Walipopatikana, wakaniambia Bwana Chrisant, lazima ulipe dola 5,000 ili tuje hapa kukufungia hiyo. Nikashindwa nikaagiza Zimbabwe, nikampata Mzimbabwe mmoja yupo Dar es Salaam. Kati ya wale wakimbizi ndiye aliyekuja kunisaidia kufunga, hakuna Mtanzania aliyeweza. Hivi kule kiwandani kwangu nimekwenda kumnyang'anya kijana mmoja mdogo tu ni *technician,* ndiye ninaye pale, nimekosa *ammonium engineer,* anayeweza kusaidia kuendesha mitambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi ninasema tutafsiri aina ya viwanda, tusomeshe watu wetu watakaokuja kutuendeleza kwa aina hiyo hiyo. Hatujatafsiri, ndiyo maana hatujui tuwasomeshe nini. Tutachagua Wachina pokeeni idadi kadhaa. Mimi ninaomba Mheshimiwa Waziri, ombeni sasa mbona watu wanatupenda. Tuanze kuomba fedha za kuwasomesha watu wengi kwenda nje na ule ni utundu tu, *deliberate* utundu. Hii ndiyo itatuchelewesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine hata hao wanaosoma *SUA* na sehemu nyingine, tujue kila mwaka wanapatikana wangapi ili *SIDO* na Mashirika mengine, pamoja na *NDC*, *I declare my interest,* maana mimi ni *Chairman* huko. Waanze kuhangaika namna ya kuanzisha viwanda kwa ajili hiyo. Tuna watu sasa hivi watakuja kutupiga ngumi, kwa sababu wamesoma hawana kazi, kumbe nafasi tunazo chungu nzima na rasilimali chungu nzima tunazo. Kwa hiyo, hilo nilipenda nilishauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu vilevile, napendekeza kwa Serikali tusaidiane, jambo hili ni baya kweli. Juzi mimi nilikwenda South Africa, ukifika hotelini na kwenye maduka kote, mtu hataki kuona dola yako anataka *rand.* Kwenye kibao cha hoteli

wameandika bei kwa *rand* kama una dola wata-*convent* watakupa. Lakini sisi hapa hata kwa uchumi wanataka waanze kuuza kwa dola. Mimi ninayo makaratasi hapa, wafanyabiashara wote wanataka dola, tutaua nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Awali ya yote, napenda nitoe shukrani zangu za dhati, kwa wananchi wa Jimbo la Tabora, kwa kuniwezesha kuwa hapa kama mwakilishi wao. Lakini vilevile nawapa pongezi nyingi sana, kwa kujenga shule za sekondari katika utaratibu wa kusaidiana wa Serikali, chini ya uongozi shupavu wa *DC*, Ndugu Chan'ga, pamoja na Madiwani wote na mimi mwenyewe nikishiriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo, sasa naomba vilevile nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wao wote, kwa matayarisho mazuri ya bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchangia kama ifuatavyo: Wizara hii ni moja ya mihimili mikubwa na tena muhimu katika uchumi wetu wa Tanzania. Kwa sababu viwanda vinaongeza ajira, viwanda vinaongeza thamani ya mazao yetu, viwanda vinaongeza na vinatoa taswira tofauti ya mazao yetu tunayoyauza nchi za nje na hilo ni la muhimu sana hasa kwa wakati huu, ambapo urari wetu wa malipo ya nje umeelemewa.

Kwa mujibu wa takwimu ambazo Wizara imetuambia, inaonesha kwamba, tunanunua bidhaa toka nje zenye thamani ya takriban bilioni 3.7 na tunauza bidhaa za takriban bilioni 1.7. Kwa maana ya kwamba, bidhaa tunazouza nje hazikidhi hata nusu ya mahitaji ya fedha za kigeni, ambazo tunahitaji kwa ajili ya kununua bidhaa kutoka nje. Hili ndilo tatizo ambalo linajitokeza katika *exchange rate* yetu kuwa mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tukitilia mkazo kwenye viwanda, bila shaka tutaweza kufanikiwa kubadilisha tatizo hili la kujikuta hatuna mazao mengi ya kuuza kama ilivyo sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yupo mchumi mmoja alijulikana kwa jina la W.W. Liontef. Mchumi huyu alitengeneza dhana ya kuangalia uchumi wan chi nzima katika *box* la miraba miraba. Hiyo miraba miraba, kila mraba mmoja ulikuwa una *represent activity* katika uchumi. Kwa hiyo, alichokuwa anafanya ni kwamba, alionesha jinsi ambavyo mraba mmoja unategemewa na mraba mwingine na mwingine unategemewa na mraba mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale ambao wanafahamu ninachoongea, kwa urahisi zaidi ni kwamba, hii ndiyo *theory* ya *input, output analysis,* ambayo Bwana Liontef alii-*develop* na kwa kweli tunahitaji na sisi ku-*adopt* na kuifanyia kazi. Kwa sababu, *input, output analysis* ndiyo inayoweza kukupa kile tunachokiita *backward and forward linkages* katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa uchumi wa Tanzania ni lazima tuuangalie katika *context* hiyo. *Base* yetu ni kilimo, lakini kilimo hiki baada ya kulima tunapeleka wapi mazao yetu? *What is the forward linkage* ya mazao ya kilimo chetu? Kwa kweli mazao ya kilimo chetu ndiyo msingi wa viwanda vyetu. Kwa hiyo, *the forward linkage* iwe ni viwanda. Nitatoa mfano, tunalima pamba, *forward linkage* iwe ni viwanda vya nguo. Hakuna sababu kabisa kwa Tanzania kuuza pamba ghafi wala hakuna *excuse*. Tukifanya hivyo ni makosa na makosa hayo ndiyo yanayotuletea kukosa ajira na kukosa thamani za ziada juu ya mazao tunayozalisha. Kwa hiyo, tukienda na hii *input output analysis,* tunaanza na *cotton*, iende kiwandani itengeneze nyuzi. Ikishatengeneza nyuzi, tutengeneze nguo au *grey cloth* ambayo baadaye tutaibadilisha itakuwa khanga au kitenge au fulana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukikosa kufanya hivyo, yale maboksi badala ya kuwa Tanzania, mengine yatakuwa nje ya Tanzania. Sasa tunalima pamba, tunapeleka nje wanatengeneza nguo wanaturudishia. Kwa mfano, tunacho kiwanda kimoja kinaitwa *Karibu Textile* hapa Tanzania, kinatengeneza khanga na vitenge, lakini ni suala la kujiuliza; wanatengeneza khanga na vitenge kutokana na *grey cloth* gani? Ukweli ni kwamba, wanatengeneza khanga na vitenge kwa kutumia *grey cloth,* yaani ile bafta ambayo imeagizwa kutoka nje. Huko nje wametumia *cotton* iliyotoka Tanzania, ikaenda nje ikatengeneza bafta ikarudishwa Tanzania, ikapitishwa kwenye mtambo wa kutia rangi na picha za khanga na vitenge, halafu sisi tunasema tunatengeneza khanga na vitenge!

Mheshimiwa Naibu Spika, Tabora Textile inatengeneza nyuzi hakuna sababu kwa nini iishie kwenye nyuzi. Naungana mkono na Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya aliyekaa sasa hivi *industrial strategy* ni nini? Hakuna sababu kiwanda kile kisiwe *un integrated textile mill* kinatengeneza nyuzi, kinatengeneza *grey cloth*, kinatengeneza vitenge, kinatengeneza khanga pale pa Tabora, kwa maana hiyo hata uchumi wetu utakua. Kwa hiyo, nilikuwa nataka kusisitiza hilo na twende tufanye hivyo ili uchumi wetu uweze kwenda vizuri na viwanda vyetu viweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna kiwanda kinachojulikana kwa jina la *General Tyre East Africa.* Miongoni mwetu, wenye umri kama mimi hivi na tunaokaribiana karibiana, tunafahamu kiwanda hiki kilipoanzishwa, kilianzishwa kwa ajili ya Soko la Afrika Mashariki na ndivyo ilivyokuwa hivyo. Matairi ya *General Tyre* yalikuwa ni matairi ya Afrika Mashariki. Sisi wenyewe tukazubaa, nchi moja jirani ikaanzisha kiwanda kingine kushindana na kiwanda ambacho kilianzishwa chini ya utaratibu wa *East African Treaty to Catter for East African Market,* baada ya kuendelea kuzubaa, tumezubaa mpaka kiwanda hiki sasa *almost* kime-*collapse*. Kime-*collapse* mbele ya macho yetu na ni mali ya Serikali kwa hisa za asilimia 74 na *International Continental* 26.

Mheshimiwa Naibu Spika, Soko la Afrika Mashariki, kwa nini hatuwezi kuhakikisha kwamba, kiwanda hiki kina-*re-capture the market,* kama ambavyo kilikuwa kimetakiwa kufanya na hasa wakati huu ambapo tunazungumzia juu ya Soko la Afrika Masharikikwa maana ya *common market*. Sisi tulikuwa na faida tayari, tulikuwa na *product* ya kuuza katika *common market,* tumezubaa mpaka sasa tumekosa tena!

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kuwa bado kiwanda kipo hai kinasuasua, hebu Serikali kwa sababu ndiyo mwanahisa mkubwa, iangalie uwezekano wa kukifufua kiwanda hicho ili kuendelea ku-*catter for East African Market,* kama ambavyo kilikuwa kimetarajiwa kiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Tabora, ambacho nimesema ni vizuri kikawa *full integrated mill,* kinahitaji kutengenezewa mazingira ya kufanya hivyo. Wapo pale wawekezaji ambao tukiwapa *incentives* ambazo zitaonesha kwamba kweli Serikali inajali na inawataka waweze kukifanya kiwe *integrated mill,* watafanya. *Declare that place Special Economic Zone,* waambie wawekezaji wa sasa wakifanye *full integrated mill. These are incentives* watafanya. Matokeo yake ni kwamba, *employment* itapanda, *exports* zetu zitapanda na *value added* ya mazao yetu itaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala sasa hivi hai. Suala hai linalohusiana na mazungumzo kati ya nchi zetu hizi zinazoendelea, pamoja na nchi zilizoendelea baada ya ule Mkataba wa *ACP* wa *Lome Convention* kuwa unakaribia mwisho. Sasa hivi nchi zetu zinazoendelea, zinahitajika kufanya mazungumzo na nchi za Ulaya, chini ya utaratibu wa *Economic Partnership Agreements (EPA)*. Hizi *Economic Partnership Agreements,* zinatakiwa zifanywe chini ya utaratibu wa makundi ya *Customs Union*. Sisi kama Tanzania, tunajua kwamba, tuko kwenye *East African Community,* lakini vilevile tupo kwenye *SADC*. Wabia wetu kwenye *East African Community;* Kenya na Uganda, wapo *COMESA*. Lakini chombo ambacho kingetuwezesha kuzungumza *negotiations* za *EPA* ni chombo ambacho kiko karibu na mbele yetu kabisa ni *East African Community*.

Mheshimiwa Naibu Spika, inashangaza kwamba, ndani ya *East African Community,* hatuelewani juu ya hili ilimradi Tanzania sasa tunazungumza *EPA* chini ya utaratibu wa *SADC*, sawa ni uhuru wetu tunaweza kufanya hivyo. Lakini mbaya zaidi wenzetu wa Kenya na Uganda, wanazungumza *EPA* chini ya *COMESA* na *yet* sote tupo kwenye *East African Community!* Je, *East African Community* tunamwachia nani sasa na ni chombo chetu wenyewe? *(Makofi)*

Kwa hiyo, nimeona nilizungumze hili kama Mbunge katika Bunge la Tanzania, kuionesha Serikali yetu kwamba, katika hili ipo haja ya kuwashinikiza wabia wenzetu kwenye *East African Community* kwamba, *East African Community* ni chombo chetu, tukitumie hiki kuzungumzia masuala ya *EPA*. Hata kama tuko katika Mashirika mengine, lakini hili ni letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuanzie hapa kwanza, tukiliacha hili likaenda kama ambavyo linavyokwenda sasa hivi, mimi kwa mtazamo wangu, ubao uliyo mbele yangu, kuna maandishi *very clear, black and white* kwamba, hata *future* ya *East African Community* ina matatizo. Ikiwa hatuwezi kukubaliana juu ya hili ambalo ni dhahiri shahiri kwamba, sote ni watu wa *East African Community,* kinachotakiwa ni kuzungumza tu habari ya *EPA;* kwa nini tusiitumie kama *a negotiation tool,* badala yake tumekwenda wengine *SADC,* wengine *COMESA?*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie fursa hii pia kusisitiza jambo ambalo mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara alilizungumzia, kuhusu ukaguzi wa magari yanayonunuliwa na Watanzania nje ya nchi. Ukaguzi wa magari yanayonunuliwa na Watanzania nje ya nchi ni hoja ambayo Kamati iliibaini kwamba ni tatizo. Mimi nasisitiza kwamba, hilo ni tatizo na naishauri Serikali itazame jambo hili kwa madhumuni ya kubadilisha utaratibu huu ili kero hii iondoke.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa bado nina dakika nadhani naweza kumwachia mwenzangu ili twende vizuri. Yale makubwa niliyotaka kuzungumza nimemaliza, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuongea, ahsante sana. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. RICHARD S. NYAULAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante. Kwa niaba ya Wananchi wa Mbeya Vijijini, nakushukuru sana kwa kupata nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii. Awali ya yote, natoa pongezi kubwa sana kwa Waziri na Naibu wake, pamoja na Katibu Mkuu na Wafanyakazi wa Wizara, kwa utayarishaji mzuri wa bajeti hii na kuweza kuiwasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wa Taifa hili unategemea sana kilimo. Lakini utegemezi wa kilimo utakuwa ni mzuri zaidi, kama utakuwa umekwenda sambamba na uhusiano mkubwa zaidi na ukaribu zaidi kati ya kilimo na viwanda. Wananchi wanaokaribia asilimia 80 wanategemea kilimo, mchango wa kilimo kwenye Pato la Taifa ni asilimia 45 na mchango kwa fedha za kigeni ni asilimia 16. Asilimia 16 kutoka kwenye mchango wa kilimo ni asilimia ndogo; hivi tunafanya nini ili kuongeza pato la fedha za kigeni kwa kupitia kilimo?

Sasa hivi asilimia 43.7 ya manunuzi kutoka nchi za nje, yanatokana na mauzo yetu yote ya nchi za nje. Kwa maana hiyo, ni dhahiri kama mwenzangu alivyosema kwamba, tunatumia fedha nyingi kuagiza vitu kuliko tunavyopata kutoka nchi za nje. Kwa hiyo, si ajabu kwamba *exchange rate* yetu inakuwa mbaya siku hadi siku na hatimaye inaathiri viwanda vyetu, inaathiri ajira zetu na kadhalika.

Kwa hiyo basi, itakuwa ni vizuri kwa sasa hivi, kama tukianza kuwa na mikakati madhubuti ya kuhakikisha kwamba, tunauza zaidi nchi za nje. Pamoja na matatizo mengine makubwa ambayo yako kwenye upande wa kilimo yakiwa ni pembejeo, mbolea, mbegu, zana za kilimo, lakini tatizo moja ambalo ni kubwa vilevile ni tatizo la soko na hasa soko kwa wakulima wadogo wadogo, ambao ndio wengi zaidi kuliko wakulima wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima hawawezi kuuza bila kujua soko linahitaji kitu gani. Kwa tatizo ambalo tunalipata ni taarifa za soko, tukitaka kuuza vitu vingi nchi za nje na kuweza kupata fedha za kigeni, basi inatulazimu tuwe na mikakati kadhaa. Kwa hivi sasa soko la nje lipo na kwa hivi sasa kama Tanzania, tuna viwanja vingi ambavyo tunaweza kuvitumia sawa sawa ili kuweza kusafirisha mazao yetu kwenda nchi za nje. Lakini vilevile tuna bandari yetu, tuna Uwanja wa Songwe, ambao unajengwa Mbeya, nina imani baada ya miaka miwili unaweza kutumika vizuri kwa kazi hiyo. Kuna

uwanja wa Kilimanjaro, kuna Uwanja wa Julius Nyerere na kuna Uwanja wa Mwanza, ambao unatengenezwa vizuri. Viwanja vyote hivi kama tukivitumia vizuri vinaweza kutumika sana na kwa unafuu zaidi kuhakikisha kwamba, mazao ambayo si ya kibiashara yanaweza kusafirishwa kwa kutumia viwanja hivyo.

Kwa hiyo, tunahitaji kuwa na mikakati ya kuchagua mazao machache, hatuwezi kuwa tunataka kuuza nchi za nje mazao yote duniani. Tunahitaji kuwa na mazao machache na kwa mtazamo wangu, nilikuwa nafikiria kwamba, tungeweza kuwa mazao ya mbogamboga, ndizi pamoja na maparachichi. Maparachichi, ndizi na mbogamboga, zinalimwa karibu sehemu kubwa sana ya Tanzania na zinalimwa na wakulima wadogo wadogo, ambao kama tungeweza kuwasaidia kwa kuwa na *contract farming,* hawa wakulima wadogo wadogo wangeweza kupata nafasi ya kuweza kuuza mazao haya nchi za nje na wakapata kipato kizuri zaidi. Kinachohitajika kwa upande wa Wizara ni kuwa na mikakati ya aina nne. Moja ni kuhakikisha kwamba, mazao tunayachagua machache ambayo tunaweza kuyafanyia kazi zaidi ili tuweze kufanya utafiti nchi za nje na kisha tuweze kuwa na taarifa hizo ambazo tunaweza kuwaletea wananchi.

Utafiti ambao unahitajika ni utafiti kuhusu ubora mambo ya *packaging* na masharti mbalimbali ya kuweza kuuza nchi za nje. *Board of External Trade,* inasemekana kwamba inastahili kufanya kazi hiyo, lakini sidhani kama inafanya kazi hiyo vizuri zaidi, kuweza kuwanufaisha wananchi wengi wa kutosha. Kwa hiyo, ningeomba *Board of External Trade* au Idara mojawapo katika Wizara, ifanye kazi katika kufanya utafiti wa masoko ya nje ili tuweze kuwa na mazao ambayo tunaweza kuwahusisha wakulima wadogo wadogo, waweze kuuza nchi za nje.

Pamoja na kwamba tunaweza kupata taarifa hizo, kuna udhaifu mkubwa sana kwa maana ya kwamba, hakuna kiungo kikubwa cha kuweza kuunganisha Wizara ya Biashara na Kilimo. Utafiti ambao unafanyika hauwafii wakulima kule chini ni kwa sababu hakuna kiungo ambacho kinaunganisha kati ya Wizara ya Biashara na Wizara ya Kilimo. Kwa hiyo, taarifa nyingi za masoko, hazifiki kwa wakulima ambao wangeweza kuzalisha mazao kufuatana na mahitaji ya soko. Kwa hiyo, ningeomba Wizara ijaribu kuangalia kuwa na mikakati ya kuweza kujenga uhusiano huo wa karibu zaidi kati ya Wizara ya Viwanda, pamoja na Wizara ya Kilimo ili hatimaye mkulima wa kawaida, aweze kunufaika kwa kuzalisha mazao ambayo yatakuwa yanahitajika katika masoko ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, soko lingine ambalo ni la muhimu ni soko la ndani. Soko la ndani ni dhahiri kwamba ni kubwa kwa mazao ya aina mbalimbali. Kuna sehemu kubwa ya Tanzania, ambayo inazalisha mazao mengi zaidi na inazalisha kwa wingi kwa mfano, Mkoa wa Mbeya, tunazalisha mahindi, mpunga, viazi, lakini bei za kule ni ndogo. Wakati huo huo kuna sehemu kubwa ya Tanzania ambapo labda mazao hayo yanahitajika huwa tunatumia fedha nyingi sana katika kuagiza chakula kutoka nchi za nje, wakati chakula hicho kinaweza kupatikana hapa hapa nchini. Mazao ambayo yanapatikana yanaoza katika sehemu hizi ambako yanapatikana kwa wingi. Kinachokuwa ni tatizo ni taarifa ya soko kuhakikisha kwamba, watu wa Dodoma, Singida, Dar es Salaam na Arusha, wanaweza kujua bei ya mazao kutoka sehemu ambako yanazalishwa kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hizo hazipatikani, kwa hiyo, biashara inakuwa duni sana na kwa kufanya hivyo, wakulima wetu kila mara wanalalamika kwamba, hawana soko la mazao yao. Lakini natumaini tatizo letu ni kwamba, kitengo kinachohusika na utafutaji wa bei za mazao ndani ya Wizara, hakifanyi kazi sawa sawa.

Sina uhakika kama Kitengo hiki kinatambua kwamba, wateja wao ni wakulima sio Serikali, kwa sababu mara nyingi taarifa zinaweza kukusanywa lakini zinakuwa zimepitwa na wakati na haziwezi kutumika na mfanyabiashara au na mkulima yeyote yule. Kwa hiyo, nataka kuwe na mabadiliko ndani ya kitengo cha masoko ili kiweze kwenda na hali halisi ya kisasa, kuweza kutoa taarifa zilizokuwa makini na ziweze kuwalenga wakulima. Kwa kufanya hivyo, wakulima watakuwa na uhakika wa kuweza kuwa na sehemu ya kuuzia masoko yao.

Lakini vilevile nataka kutoa ushauri kwamba, katika kila Wilaya, wananchi wanapenda sana kuwa na masoko ya kisasa kwa ajili ya kuweza kuuza mazao yao, kwa sababu tatizo kubwa mojawapo la wakulima ni soko la ndani vilevile. Kwa hiyo, kinachohitajika ni kwamba, Halmashauri zingeweza kupewa mikopo hususan labda mikopo kutoka *Local Government Pension Fund* ili kujenga masoko ya kisasa huko kwenye Wilaya. Kwa kufanya hivyo, wakulima wangeweza kuwa na masoko ambapo wangeweza kuuza mazao yao kwa urahisi zaidi na kisha kuweza kujenga ajira na kuwaelimisha wajasiriamali na kuwaendeleza wakulima vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi moja ambayo inahitajika kufanyika na Wizara hii ni kuendeleza viwanda, kwa kutumia malighafi za hapa hapa nchini, kuna watu wengi ambao wana fedha lakini hawajui mahali pa kuwekeza. Kazi ya Wizara ingekuwa ni kuwa chachu ya kusukuma uwekezaji kwa kutayarisha *profile* za viwanda ikiwa ni mchanganuo ambao unaonesha viwanda vya aina gani ambavyo vingeweza kujengwa katika mikoa mbalimbali. Kwa hiyo, wafanyabiashara ambao wana pesa, wakiweza kuwa na *profile* hizo, wataweza kuzitumia kama changamoto ya kuweza kujua kitu gani kinaweza kujengwa katika eneo gani ili waweze kuwekeza katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuna matatizo makubwa katika kuwatumia wabunifu wetu. Kuna watu wengi ambao wamewahi kufanya kazi za kugundua namna ya kutengeneza redio, kutengeneza bunduki, vyombo vya muziki, lakini watu hawa mara nyingi tumewaona kama ni wahalifu, badala ya kuweza kuwachukua na kuwasaidia kuweza kujenga viwanda. Kwa hiyo, tunapozungumzia kuhusu teknolojia, hao watu ni wabunifu na wanaweza kugundua vitu mbalimbali lakini bado hatuwezi kuwatumia vizuri. Nina imani kama tungeweza kuwatumia vizuri, badala ya kuwaona ni wahalifu, kazi ya uhalifu ingeweza kupungua zaidi kwa sababu wangeweza kuwa wanazalisha katika sehemu inayojulikana na ujuzi wao ungeweza kutumika katika kuzalisha mali mbalimbali ambazo zingeweza kutumika na wananchi mbalimbali katika nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningetaka kumalizia kuhusu suala la *dumping.* Tanzania sasa hivi inatumika kama nchi ya kutupa vitu vyote vilivyokuwa duni. Vifaa vya umeme vinavyoingizwa katika nchi hii ni hatari kabisa. Nina imani kabisa kwamba, majanga mengi yanayohusiana na kuungua kwa nyumba au majengo makubwa, yanatokana na vifaa vya umeme kuwa duni, ikiwa ni nyaya za umeme na vitu vinginevyo

mbalimbali ni duni sana. Vifaa vya kilimo ni duni, samani tunazonunua ni duni, lakini bado tunatumia fedha nyingi kwa ajili ya vifaa hivyo ambavyo tungeweza kuvitengeneza sisi wenyewe.

Kwa hiyo, ningeshauri kwamba, Wizara ihakikishe kwamba, inaimarisha Shirika la Viwango kwa kuwapa uwezo wa kukagua vitu mbalimbali, ambavyo vinaingizwa katika nchi hii na kuhakikisha kwamba, inaweza kuwachukulia hatua kali wale ambao wanaweza kuwa wanaingiza vitu ambavyo ni duni, vitu ambavyo wanatumia fedha nyingi za kigeni lakini bado vinakuwa vya manufaa makubwa kwa Watanzania.

Lakini vilevile wangeweza kuimarisha Shirika la Viwango kwa kuhakikisha kwamba, wanakuwa na vituo maalum katika mipaka mbalimbali ya Tanzania ili kuhakikisha kwamba, bidhaa mbalimbali zinapoingizwa, ambazo ni duni, basi zinaweza kuwa zimeshikwa huko huko na zisiweze kuingizwa tena nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja. Asante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MATHIAS M. CHIKAWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nampongeza Waziri na Wizara yake kwa kuleta Bajeti nzuri katika Bunge lako Tukufu. Nitamke moja kwa moja kuwa naunga mkono hoja hii.

Naomba nichangie moja tu katika Wilaya ya Nachingwea yapo mazao muhimu ambayo yanahitaji kuongezewa thamani. Korosho na mbegu za mafuta ni mazao yanayozalishwa kwa wingi Nachingwea. Wizara ifanye juhudi za makusudi kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo vya kubangua korosho na kukamua ufata na mbegu zingine za mafuta ili wakulima wapate bei nzuri na faida kubwa kuliko wanavyouza sasa. Lakini hata kabla ya viwanda hiyo kufika Nachingwea, Wizara ihakikishe kuwa mazao haya ya wakulima yanapatiwa masoko hivi yalivyo masoko ya uhakika. Korosho zinunuliwe kwa bei zinazofahamika ili kuondoa matatizo ambayo yalilikumba zao hili mwaka jana. Korosho za mwisho Nachingwea zimenunuliwa wiki moja iliyopita wakati msimu ujao umebakiza miezi miwili tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni uanzishaji na uimarishaji wa *SACCOS.* Wizara Inatakiwa iongeze mabwawa ushirika wa kutosha ili wananchi wahamasishwe kuanzisha *SACCOS* zitakazo waondolea umaskini. Wizara iongeze maafisa ushirika ili wafanye kazi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biasahari.

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na wafanyakazi wote wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii wakati huo huo ningependa kupata mawazo ya Wizara juu ya kutusaidia utaalamu kuanzia mtaa wa Viwanda katika Halmashauri ya Mji wa Njombe, hasa Njombe Mjini kwa kuanzia. Mheshimiwa Waziri, mji huu umepewa hadhi ya kuwa Mji Mkuu wa Halmashauri mpya ya Mji wa Njombe. Tungependa kwa mapema kuondokana na hali ya miji mingi ambayo kila mahali ndani ya mji kuna viwanda vidogo vidogo, gereji na kadhalika. Sisi tumekwishatenga eneo na uhakika wa umeme upo hivyo tunaomba tuungwe mkono kwa kupata utaalamu kuanzisha eneo hilo chini ya utaratibu wa *SIDO*. Maombi yameletwa *SIDO* Makao Makuu. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. CASTOR B. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri kwa kipindi cha mwaka 2006/2007 mchango wangu utahusu yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni biashara. Kuhusu fursa mbalimbali za kuuza nje tatizo kubwa la ukuaji uchumi wetu kwa kasi ndogo ni uwezo mdogo tulionao wa kuuza bidhaa nyingi nje ya nchi. Akipitisha Bajeti yake ya mwaka 2007/2008 Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji pia alilielezea hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitoa mchango wangu kwa kutilia mkazo mazao yasiyo asilia ambayo siyo dhahabu, almasi au mazao ya viwandani. Wakati mkazo unawekwa kwa kuwasihi wananchi wanachangamke kutumia fursa mbalimbali, wananchi hawajaelezwa wazi wazi juu ya fursa hizi. Kwa mfano, katika mchango wangu kwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji niliomba orodha ya fursa ya kuuza katika masoko kama *AGOA, Canadian Pact,* Korea ya Kusini na China tupewe sisi Wabunge kwa madhumuni ya kuwahamasisha wananchi wetu lakini sikuwahi kupata jibu. Sasa kwa vile Wizara yako imelirudia jambo hili, naomba katika majumuisho Waziri atueleze ni bidhaa gani zimeorodheshwa katika bidhaa 1835 chini ya soko la *AGOA, EBA* na kadhalika?

Je, Wizara itakuwa tayari kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kuunda bodi ya kushughulikia masoko ya mazao yasiyo asilia ambayo yanatokana na kilimo *(Agricultural Crops which are non traditional)* mfano, ufuta, kokoa, alizeti na kadhalika? Ni fursa gani nyingine ambazo kama wananchi wetu watahakikishiwa soko waweze kuchangamkia?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda vidogo vidogo, *SIDO* katika nchi yetu imefanya kazi nzuri sana katika kukuza shughuli za wajasiriamali wadogo wadogo. *SIDO* kwa kiwango kikubwa shughuli zake zimejikita zaidi katika ngazi ya mikoa jambo ambalo umuhimu wake hauwagusi wananchi wengi. Wananchi wetu walio wengi hufaidika kwa kuangalia shughuli za *SIDO* katika maonyesho yanayofanywa katika miji mbalimbali. Lakini *SIDO* ingekuwa kichocheo kikubwa cha kukua kwa uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napandekeza yafuatayo, Serikali kwa makusudi ingewekeza *SIDO* ili kuchochea ukuaji wa viwanda vidogo vidogo mpaka Wilayani au ngazi ya kata; maeneo yaliyokuwa *electrified* yapewe kipaumbele katika kuanzisha

viwanda vidogo vidogo. Tuchukue nchi kama Urusi walianza na *rural electrification* nchi nzima na kisha pakafuata *industrialization*; kama *SIDO* itaenda hadi kwenye kata na vijiji ajira nyingi kwa wananchi wetu ambao wanapenda kuhamia mijini.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naipongeza Wizara hii hasa kwa kusimamiwa vizuri na Mheshimiwa Waziri Basil Mramba, Naibu wake Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, na kuwasilisha hotuba yao ya Bajeti ya matumizi mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda katika nchi yoyote ni kitu kimojawapo chenye kujenga uchumi na kwa upande wa nchi yetu ya Tanzania inayo viwanda lakini bado jitihada za lazima zifanywe na Wizara isimamie kwa faidi ya Taifa letu kuongeza viwanda na majengo yanayoendana na wakati, wawekezaji bora, elimu nzuri, kuondoa wabadhirifu na mambo mengine ya kusafisha nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, masoko yawepo au yatafutwe kwa bidhaa zinazozalishwa na soko la ndani na la nje kwa kupata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara wakubwa na wadogo wote naomba wawezeshwe kwa mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leseni kwa wafanyabiashara zisiwe na pingamizi na vizingiti vingi na zisiwe kwa fedha nyingi. Pia mikataba yao itazamwe vizuri na masharti yake yazingatiwe kwa faida ya Serikali kwa huduma zote na bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bidhaa zote zinazoingia nchini zikaguliwe na ziingizwe kisheria na vipimo vyote viwepo na *TBS* ipewe nguvu na kuwezeshwa kifedha ili kuweza kufanya kazi zake, pia wafanyakazi kwenye viwanda wasisumbuliwe na wawekezaji au matajiri wa viwanda hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia ipitishwe hoja hii.

**MHE. DIANA MKUMBO CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Waziri, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii mahiri sana. Nawaombea Mwenyezi Mungu awe nao awatie nguvu, amani na mshikamano ili waweze kutekeleza kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi sasa nianze kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu soko la uhakika kwa mazao ya biashara mkoani Singida, ni matumaini yangu kuwa Serikali inatambua jitihada za wakulima wa mkoa wa Singida kwa kulima kwa wingi mazao ya alizeti, pamba, ufuta, dengu, vitunguu

na kadhalika. Tatizo kubwa ni soko la uhakika la kununua mazao haya. Hivyo basi naiomba Serikali kusaidia soko la uhakika kwa mazao haya. Endapo wakulima watapa soko tutawatia moyo kuzalisha zaidi mazao haya kwa lengo la kuinua hali yao kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kiwanda kikubwa cha kukamua alizeti Singida, ni ukweli usiofichika kuwa Singida inalima sana zao la alizeti. Pamoja na juhudi hizi alizeti kwani mashine zilizopo ni ndogo sana zinawatesa sana wakulima kwnai ukamuaji unakuwa wa polepole hivyo kukesha usiku na mchana wanapokuwa alizeti zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufufua Jineri ya Mjini Singida, napenda kuijulisha Serikali kuwa zao la pamba lilikuwa linalimwa kwa wingi sana mkoani Singida lakini zao hili limepungua sana kwa sababu kuu mbili nazo ni, kukosa soko la uhakika pamoja na kufungwa kwa jineri ambayo ilikuwa inachambua pamba na kurahisisha usafirishaji. Naiomba Serikali itafutie mwekezaji wa uhakika wa kununua na kuchambua pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo cha kisasa, napenda hujulisha Serikali kuwa kilimo ndio uti wa mgongo kwa Watanzania walio wengi hasa vijijini, kwa bahati mbaya sana wataalamu wa kutoa elimu ya kilimo cha kisasa pamoja na usambazaji wa mbegu bora ili kuzalisha mazao bora yenye kuvuta wawekezaji wachache tena wamepitwa na wakati (maafisa kilimo) wa kata na vijiji. Naomba isomeshe maafisa kilimo wengi ili kusaidia elimu kwa wakulima wetu.

Kuhusu soko la visonzo, wanawake wa mkoa wa Singida wako mstari wa mbele katika kusuka visonzo vyenye ubora wa juu. Tatizo ni pale wanapokosa soko la uhakika la kuuza visonzo hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Meneja wa *SIDO* wa mkoa wa Singida anavyojitahidi kuwasaidia wanawake hawa kwa kuwapa msaada wa mitaji na kuwatafutia soko la bidhaa mbalimbali za akinamama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kuchukua nafasi hii sasa baada ya mchango wangu ambao nategemea kupewa majibu kuunga mkono kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimekua Mbunge ambae popote ninapopata nafasi ninazungumzia suala la *EPA.* Tarehe 9 Februari, 2006, nilipokuwa nachangia hotuba ya Rais nilizungumzia suala hili na niliwataka muwe makini kufanya maamuzi kuhusu *negotiating group.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 14 Julai, 2006 niliulize swali Na. 210 kuhusu kwa nini hatutumii *EAC Configuration* kwa *EPA*, Wizara yako ikaleta siasa, haikujibu swali. Pia tarehe 7 Agosti, 2006 nikichangia hotuba ya Wizara yako niliwataka muwaombe Kenya na Uganda wajitoe *ESA Configuration* na tuunde *EAC Configuration,* Wizara yako ikajibu siasa tupu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yangu kama Waziri Kivuli wa mipango, Uchumi na Uwezeshaji ya mwaka 2006/2007 na mwaka 2007/2008 nilishauri kuwa twende *EAC – EPA* na tuwaombe *DRC* waje huku pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, *consistency* yangu ni kwa sababu mimi ni mtaalamu wa masuala haya. Majibu yote ya Serikali yamekua siasa tupu. Maslahi ya nchi yapo wapi? Mmeshindwa kazi? Mtupishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Council of Ministers of EAC* iliazimia kuwaomba *Heads of State* kuwa tusaini *EPA* kupitia *EAC,* Mheshimiwa Eliya Kategaya akatumwa kwa *Heads of State* wote. Akapata ridhaa, barua ikaandikwa *EC, Brussels* ili *EAC - EPA* ianze kufanyiwa taratibu kwa uficho, Waziri wa Biashara wa Kenya Mukhisa Kifayi akaandika barua *(copy* ninayo) kwa *EC* kupinga *EAC - EPA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Heads of State Summit* iliyofanyika Kampala ikashindwa kufanya maamuzi juu ya suala hili. Kwa nini tunawabembeleza Wakenya? Twaweza kuwa na *EPA* bila ya Kenya. Tanzania kwa nini hatuangalii maslahi yetu? Ninaitaka Serikali itoe tamko juu ya mwelekeo wa *EPA* katika *EAC*. Imeishauri Serikali ya Tanzania kuhusu *DRC* Kongo - Kinshasa ni *strategic country* kwa Tanzania yenyewe imeamua kusaini *EPA* peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nipo tayari kutumwa na Serikali kama *Tanzania Special envoy on EPA* ili baadae tuwe na *common market* kubwa *(Great Lakes Common Market - gloom).* Nipo tayari kufanya kazi na Serikali kuhusu suala hili kwa maslahi ya Taifa. Tusilale kila nchi inainyemelea Kongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo la mawasiliano kati ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na Balozi wetu Brussels. Wataalamu wa Wizara hawatoi maelekezo yoyote ya kikazi Brussels. Hawajibu barua na hivyo kumfanya Balozi ashindwe kazi. Kumezuka tabia Wizarani ya ku-*monopolise* maamuzi na hivyo kucheleweshа maamuzi ya kimsingi. Juzi juzi alitakiwa afisa wa Wizara kwenda Bagamoyo kwa ajili ya kueleza *state of play* ili kutengeneza mahitaji ya nchi kwa ajili ya *Regional Indicative Programme – SADC*. Maamuzi yalichelewa.

Naomba nipate maelezo ya kina kutoka kwako Mheshimiwa Waziri kuhusiana na udhaifu wa utendaji Wizarani. Vinginevyo nitaeleza kila kitu katika Kamati ya Matumizi. Napenda kuona Watanzania waliopo Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, kazi bila woga na kwa uhuru mpana. Pia nipate maelezo kuhusiana na mahusiano ya kikazo kati ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, Brussels na Wizara ya Fedha. Nawasubiri katika Kamati ya Matumizi.

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wafanyakazi wa kiwanda cha *General Tyre* – Arusha, namshukuru Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko na Waziri Mkuu kwa kuingilia kati na kutoa maamuzi ya kuhakikisha *General Tyre (GTEA)* haifilisiwi na maendeleo kuzalisha matairi. Nawapongeza kwa kukutana na viongozi wa *continental AG* ya *Hanover Germany* na kukubaliana njia muafaka ya kuiendeleza *General Tyre*. Msimamo huo wa Serikali na

walifurahishwa mno na msimamo huo. Tunamshukuru pia Waziri wa Fedha pamoja na na ujumbe wake kwa kuja kiwandani kutathimini hali halisi. Kitendo hiki kimeongeza imani ya wote kwamba msimamo wa Serikali itafanikiwa bila kuchelewa.

Pamoja na imani kubwa niliyonayo kwamba msimamo wa Serikali kama ilivyothibitishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu hawajabadilika na utatekelezwa maana moja bado kuna wasiwasi unaotanda. Naomba Waziri awatoe wafanyakazi wa *GTEA* na wananchi warudishe wasiwasi kwa kuwathibitishia haya na kuwaeleza ni lini utekelezaji utafanikiwa. Hii ni muhimu kwa sababu Serikali ni mwanahisa mkubwa asilimia 74 na *GTEA* 26% na ni kiwanda muhimu Arusha na kwa Taifa kwa ujumla na kama kuna matatizo yoyote basi yatatatuliwa kwa kukutana na *Collateral Manager* atakayesimamia kwa pamoja na uongozi uliopo matumizi ya mkopo wowote utathaminiwa na Serikali pamoja na kuthamini ule uliotolewa awali. Yote hayo yaende sambamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna umuhimu wa kuweka bayana nani anayesimamia *GTEA* Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko au *PSRC?* Uelewa wetu ni kwa sababu hii ni *joint venture* kati ya *GT* pekee, *GTEA* ilikuwa ile *specified* na kurudishwa Wizarani. Hapa ndio mahali pake.

Mwisho mashamba ya *rubber,* Serikali ihakikishe zinabaki kuzalisha *rubber* kwa ajili ya *GTEA* na *export*.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwa ufupi Wizara hii katika kipengele cha uwekezaji katika Mkoa wa Kigoma unayo madini mengi ambayo wananchi huyachimba kienyeji. Hali kadhalika Mkoa unayo chokaa nyingi katika Wilaya za Kasulu na Kibondo zimezungukuwa na pori kubwa la Moyowosi kiasi kwamba warina asali wanavuna asili nyingi kutoka katika pori hilo. Asali hiyo hutumika kama dawa na kupendwa sana ndani ya nchi na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kigoma unayo mazao makubwa yatokanayo na kilimo kama vile mahindi na mihogo yanayolisha Mkoa, Mikoa ya jirani pamoja na nchi jirani kama vile Burundi, *DRC,* Rwanda na Kenya.

Kutokana na mazao hayo ambayo yanapatikana kwa wingi ni muda muafaka sasa wa kutafuta wawekezaji kwenda kuwekeza katika Mkoa wa Kigoma na Wilaya zake ili huo utajiri uwe ni chachu ya maendeleo kwa nchi pamoja na wananchi wa Kigoma, ujenzi wa nyumba za watu binafsi na majengo ya Serikali kwa Mkoa mzima hutumia chokaa ambayo wananchi wanaichimba kwa kutumia mkono na kuuza kila 50 kwa shilingi 3000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ambalo ni kubwa ni Mikoa kutokuwa na maafisa biashara wenye uwezo na wakutosheleza mahitaji ya Mkoa hadi Wilaya. Naishauri Wizara ipewe uwezo wa kuajiri watumishi wa kutosheleza mahitaji ya Mikoa na Wilaya zote. Naweza nikasema kuwa nyuma kwa Mkoa wa Kigoma wenye utajiri tele, ni kutokana na Mkoa kutokuwa na kiwanda hata kimoja wakati Mkoa unao utajiri mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ambayo naomba maelezo yake, naunga mkono hoja.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuitumia fursa hii kwanza kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wapiga kura wangu wa jimbo la Kwimba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wazifanyazo katika Wizara hii. Aidha, pongezi zangu nazipeleka kwa awaye yote katika Wizara hii aliyeshiriki katika uandaaji wa hotuba hii. Ni hotuba nzuri na inaashiria mwanga na kuongeza mwanya wa kuliendeleza Taifa letu yaliyomo yakitekelezwa vilivyo. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi naomba niitumie fursa hii nitoe ushauri na maombi katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, viwanda vidogo na biashara ndogo. Napongeza sana hatua zilizochukuliwa katika eneo hili. Kuwafikia wananchi huko waliko na kuwapa elimu ni jambo la msingi. Ombi langu *SIDO* na mashirika mengine yaongeze nguvu katika eneo hilo. Aidha, Serikali iongeze fedha za mafunzo ili kuyawezesha mashirika haya kama *TIRDO, SIDO, CARMATEC* na mengine kama haya yapate uwezo mkubwa zaidi wa kuwafikia na kwa kiwango fulani kuwawezesha wananchi kuanzisha viwanda vidogo vidogo huko huko waliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti na maendeleo ya teknolojia, napongeza sana kazi nzuri zinazofanywa na *CARMATEC, TEMDO* na *TIRDO* kuhusiana na ubunifu na maendeleo ya tafiti zao mbalimbali, mazao yatokanayo na tafiti hizi ni mazuri sana. Hata hivyo hata kama mazao/matunda hayo ni mazuri na yenye manufaa kwa wananchi, wananchi wengi hawajafahamu kutokana na ukweli kuwa maonesho ya matunda ya kazi zao yanafanyikia au mjini au kwenye maonesho kama Sabasaba tu, maeneo yasiyochelewa au kufikiwa na wananchi wengi. Aidha, maonesho haya ni ya muda mfupi tu. Nashauri matokeo ya kazi za utafiti wa mashirika haya yawekwe kwenye vituo maalumu vya maonesho kwenye ngazi za chini zaidi kama Wilaya au Tarafa kunakoweza kufikiwa na wananchi wengi na wakaangalia kwa muda wa kutosha ili viwe vituo vya kudumu, pia vitakuwa na vituo vya mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikaino wa Kiwizara, viwanda vingi vinakwamishwa na huduma itolewayo na Wizara zingine hivyo Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko inakuwa haina uwezo mkubwa na kuvinusuru hata pale Wizara inapoyatambua matatizo ya viwanda hivi. Viwanda vinahitaji umeme (Nishati na Madini) na maji (Wizara ya maji). Upo mfano wa *Mwatex,* kiwanda kikubwa ambacho kwa aibu kubwa kilifungwa kutokana na ukosefu wa maji licha ya kuwa karibu na maziwa. Kukatika kwa maji kulisababishwa na kukatika katika kwa umeme kwenye mashine za kusukumia maji kwenda *Mwatex.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukosefu wa maji, kiwanda cha *Mwatex* kikawa kinajiendesha kwa hasara, hasara iliyokisababishia kushindwa kulipia bilI ya umeme (Nishati). Kushindwa huko kulisababisha umeme kukatwa, kiwanda mpaka kilifungwa na waajiriwa wengi kukosa ajira. Mfano wa pili uko Jimboni kwangu.

Nimeomba umeme kwa viwanda viwili vya pamba, Jineri ya Malujo na Sangu zipatiwe umeme kwa zaidi ya miaka 10 licha ya kuendelea kuomba Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini, hata dalili tu hazionekani. Wenye viwanda hatimaye wameanza kufikiria kuhamisha viwanda vyao kuvipeleka kuliko na uhakika wa umeme. Kwa maelezo yao kuendelea kuendesha viwanda hivyo kwa *generator* ni gharama kubwa mno. Hivyo kama *Mwatex* huenda navyo vikafungwa. Hivyo naulizia ni lini Wizara zinazoshirikiana katika maendeleo ya viwanda lini vitakuwa na chombo cha kushauriana ili waondokane na utamaduni wa kila Wizara kupanga mipango yake kama ni Wizara inayojitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, usalama wa wafanyakazi viwandani. Nimepata fursa ya kutembelea viwanda vingi hapa nchini. Ninavipongeza sana viwanda vinavyozingatia usalama wa wafanyakazi viwandani. Aidha, kupitia Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana napongeza *Osha* pamoja na ugumu wa mazingira ya kazi waliyonayo kwa kazi nzuri wazifanyazo kukagua na kuhimiza usalama wa wafanyakazi viwandani.

Naomba nitumie fursa hii kuiomba Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kuwahimiza wenye viwanda kila pale inapowezekana kazi za mikono zipunguzwe *(Manual works)* ili zile kazi ziwe *automatic* (zifanywe kwa mashine kwa kadri itakavyowekana. Nina amini inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubunifu asilia, mashirika kama *CARMATEC, TIRDO* na wengine wanatemea zaidi teknolojia ya nje. Naomba mashirika haya yaende vijijini si kwa nia ya kufundisha bali kwa nia ya kujifunza. Kujifunza huko kutayawezesha mashirika haya yaelewe zaidi matatizo ya wananchi, jinsi wanavyoyatatua na nyenzo asilia. Inawezekana na naunga mkono hoja.

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuelezea juu ya *SIDO*, wakati wa Serikali ya awamu ya kwanza kila Mkoa ulijengewa mtaa wa *SIDO (SIDO Industrial Complex).* Kwa bahati mbaya sana Mkoa wa Mtwara mtaa wa *SIDO* haukukamilisha ujenzi kwa hiyo, ukitembelea ni shughuli chache sana zinazofanyika. Kipindi fulani jengo la *SIDO* lilikuwa linakodishwa kulihifadhi korosho. Wakati Waziri atakapojibu hoja naomba kupata maelezo ya kuridhisha kwa nini mtaa wa *SIDO* Mtwara haukukamilika na nini mipango ya Serikali katika kuendeleza mtaa wa *SIDO* Mtwara?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda vya korosho, korosho inachangia asilimia nne ya Pato la Taifa. Tanzania inavyo viwanda vingi vya korosho ambavyo vina uwezo wa kubangua korosho zote bila hata kusafirisha ambazo hazijabanguliwa. Hata hivyo viwanda hivi havifanyi kazi kwa sababu wenye viwanda hawana fedha za kununua korosho toka kwa wakulima. Soko la korosho zilizobanguliwa ni kubwa. Je, kwa nini Serikali isiwadhamini wenye viwanda vya korosho kupata mikopo ili korosho zote zibanguliwe nchini, kuongeza thamani ya korosho *(value added)* na pia kuongeza ajira? Naomba kupata maelezo ni nini kinakwamisha wenye viwanda vya korosho kupata udhamini wa mikopo kama wapatavyo wanaosafirisha maua nchi za nje?

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya wanga, mkoa wa Mtwara na hasa Wilaya ya Newala unazalisha muhogo kwa wingi ambao unaweza kutumika kuzalisha wanga. Zamani *NDC* ilikuwa na mpango wa kujenga kiwanda cha wanga katika kijiji cha Chiwonga, Wilayani Newala lilipatikana lakini utekelezaji ukasimama. Je, Wizara inaelezea nini wakulima wa muhogo ambao wanahangaika na soko. Lakini pia muhogo unaweza kusindikwa na kuuza unga au kusafirisha makopa nchi za nje. Zamani mihogo yote ilikuwa inanunuliwa na *unions* zetu na kusafirishwa nje. Hivi ni kweli kuwa Serikali imeshindwa kupata soko la muhogo nchi za nje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu biashara za mpakani, watu waishio mipakani wanafanya biashara ya bidhaa mbalimbali kwa mfano katika Mikoa ya Rukwa na Mbeya zaidi ya nusu ya sukari inayoliwa inatoka Zambia na Malawi. Sukari inayozalishwa hapa nchini ikipelekwa Sumbawanga inakuwa na bei kubwa kuliko ile itokayo Zambia kwa sababu ya gharama za usafiri. Watu waletao sukari toka nje wanabugudhiwa na kukamatwa mara kwa mara. Serikali iwaruhusu waletao bidhaa kama sukari toka nje kujiandikisha kukata leseni ya kulipia kodi ili waingize bidhaa bila bugudha yoyote. Naomba kuwasilisha.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Wizara yake, pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwanza ni kuhusu viwanda, kwa kuwa Wilaya ya Mpwapwa na Mkoa wa Dodoma wanalima sana karanga, alizeti na ufuta; na kwa kuwa hakuna kiwanda cha kukamulia mbegu hizo za mafuta, je, Serikali itakubaliana nami kwamba iwapo kitajengwa kiwanda kikubwa cha kukamilisha mafuta hapa Dodoma kitasaidia sana kukamua mafuta ambayo yatatumika hapa nchini badala ya kuendelea kuagiza mafuta ya kula nje ya nchi na mengine kuwa na madhara kwa walaji/wananchi.

Je, Serikali itakubalina nami kwamba iwapo kitajengwa kiwanda hapa Dodoma wakulima watapata soko la kuuza mazao hayo na pia kuongeza ajira kwa wananchi wa Mkoa wa Dodoma na Watanzania kwa ujumla, je, Serikali ina mpango gani wa kufufua Kiwanda cha Mvinyo cha Dodoma *(DOWICO)* ili kusaidia wakulima wa zabibu wa Mkoa wa Dodoma kupata soko la kuuza zabibu na kuwaongezea kipato chao kuliko hali ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko kwa hotuba yake ya Bajeti nzuri na iliyofafanua vizuri masuala yanayohusiana na sekta anazosimamia, nampongeza sana. Bado kuna viwanda vingi vilivyobinafsishwa ambavyo kwa kipindi kirefu, havifanyi kazi. Viwanda hivi viko kwenye Manispaa za Moshi na Morogoro na kwenye Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, amewahi kutishia kwamba angechukua hatua za kuhakikisha kwamba viwanda hivyo vinafanyakazi, ikiwa ni pamoja na kurudisha Serikali ambavyo vingeendelea kufungwa. Ni viwanda vingapi vimerudishwa Serikalini kutimiza ahadi hii? Inaelekea Wizara inakosa ubavu wa kutekeleza ahadi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi ya kilimo kama yetu ujenzi wa viwanda vya kusindika mazao ya kilimo ni muhimu na ndivyo vinavyopaswa kutangulia aina nyingine za viwanda na kwa kweli kuwezesha kujengwa kwa aina nyingine za viwanda. Kwa sasa hakuelekei kuwapo mkakati maalumu na kujenga viwanda vya aina hiyo na hata vile vilivyojengwa na Serikali ya Awamu ya Kwanza havifanyi kazi hata baada ya kubinafsishwa. Serikali inapaswa kuliangalia suala hili na kuelekeza uwekezaji kwenye viwanda vya kusindika mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Kwanza ilikuwa na dhana ya kujenga viwanda mama na baadhi, kwa mfano, *Kilimanjaro Machine Tools* vilijengwa. Awamu ya Serikali zilizofuata hazikuendeleza dhana hii kutokana na kudodosa sana kwa hali ya uchumi. Kwa kuwa hali ya uchumi imeanza kuimarika ni muhimu kurejea dhana hii na kuona uwezekano wa kuiendeleza. Wizara inapaswa kulipa suala hili umuhimu mkubwa sana kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maoni yangu kwamba nchi yetu haifanyi jitihada za kutosha kukuza soko la ndani na kufaidika na masoko ya nchi za Afrika na Mashariki ya Kati na ya mbali, badala yake nchi yetu imegeuzwa dampo la bidhaa kutoka duniani kote. Inabidi Serikali iandae mkakati wa makusudi wa kuzalisha kwa lengo la kufaidika na masoko hayo na kuandaa wajasiriamali ambao watatekeleza mkakati huo. Inabidi tubadilike haraka sana kama kweli tunataka kuinua ubora wa maisha ya kila Mtanzania, kazi bado kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *SIDO* na *VETA* wanafanya kazi nzuri sana za kuwaandaa wajasiriamali katika nyanja mbalimbali. Taasisi hizi zipewe rasilimali za kuziwezesha kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inatubidi tukimbie sana maana wengine wanapaa. Kwa kasi ndogo tunayokwenda tutaachwa nyuma mbali sana. Wizara hii ina nafasi muhimu sana katika kuongoza maendeleo ya viwanda na biashara nchini. Naunga hoja mkono.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na kuhudhuria katika kikao cha leo. Napenda kukupongeza wewe Naibu Spika, Spika, Wenyeviti wa Bunge pamoja na viongozi wa Kambi ya Upinzani kwa kutuongoza vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya viwanda ikiimarishwa inaweza kuchangia kwa asilimia kubwa Pato la Taifa letu. Hii ni kutokana na rasilimali nyingi zilizopo nchini ambazo zinaweza kutumika kama malighafi za viwanda vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa asilimia kubwa ya wananchi wetu wanategemea kilimo, viwanda vitasaidia wakulima kupata masoko ya uhakika ya mazao yao. Mazao haya yakisindikwa kupitia viwanda yatasaidia kuongeza pato kwa wakulima na Taifa kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matunda mengi kama vile machungwa, mananasi, embe, nyanya, zabibu na kadhalika lakini yanaoza kwa kukosa soko kwa sababu hakuna viwanda vya kusindika matunda. Kwa hivyo wakati umefika sasa kwa Serikali kuimarisha viwanda kwa ajili ya kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwekeza katika viwanda kutasaidia kupatikana kwa ajira na kuongeza pato la wananchi na Taifa hasa ukizingatia kuwa malighafi nyingi zinapatikana hapa hapa nchini. Biashara iwe ya ndani au ya nje inasaidia kutoa ajira kwa wananchi na kukuza Pato la Taifa. Wafanyabiashara wadogo wadogo wakiimarishwa kwa kupatiwa elimu ya biashara, mikopo, pamoja na mazingira mazuri ya kufanyia kazi zao wataweza kujikomboa kutokana na unyonge na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, masoko vile vile ni muhimu sana kwa wazalishaji kuweza kuuza bidhaa zao bila usumbufu. Kwa hivyo, masoko hayo ni nyema yakaangaliwa kwa uzito wake. Ahsante.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa kiwanda cha saruji Itigi, naiomba Wizara (Serikali) iandae mkakati wa kuwashawishi wawekezaji ili wajenge kiwanda cha saruji eneo la Itigi, kwa kufanya hivyo kutasaidia sana watu wa Kanda ya Magharibi kununua saruji kwa bei nafuu kuliko hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa malighafi ya kutengeneza saruji ni wa uhakika kwa sababu kuna hazina *(deposits)* ya kutosha ya *gypsum* (jasi) katika Kata za Itigi, Sanjaranda na Ipande. Jasi hii ina ubora wa kiwango cha juu baada ya kuthibitishwa na maabara ya Chuo Kikuu cha Sokoine kwa kulinganishwa na jasi ya Makanya, Kilwa, Lindi na Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, jasi ya Itigi imekuwa ikisafirishwa na wafanyabiashara kwenda viwanda vya saruji nchini na nje ya nchi, kuna chokaa ya kutosha na pia *redsoil* ya kutosha tarafa nzima ya Itigi, kuna kiwanda cha chaki pale Itigi na chaki inauzwa hapa nchini na nje, kuna miundombinu mizuri ya Reli ya Kati, barabara ya kwenda Mbeya, Singida na Arusha, Singida-Shinyanga-Mwanza, Itigi-Tabora, Itigi-Dodoma-Dar es Salaam na pia kuna *warehouses,* maghala ya *TRC* ambayo kwa sasa hayafanyi kazi na miaka ya nyuma yalitumika kwa kuhifadhi chokaa kabla haijasafirishwa na pia kuna umeme wa kutosha wa gridi ya Taifa, Itigi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kuna kila sababu ya kuwa na kiwanda cha saruji hapa Itigi na kutasaidia sana kuwapatia ajira ya uhakika wananchi wa Kanda ya Kati, kuna nyumba nyingi za *TRC* ambazo hazitumiki (za *East African Road Services)* na hata kama Shirika la *TRC* litabinafsishwa, kwa utaratibu wa *private operations* hawatahitaji watu wengi na *complex* za *infrastructure* kama hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali inipatie majibu ya uhakika inafanya nini kuhusu ombi hili. Nami pia nahamasisha na nitakuwa tayari kusaidiana na Serikali.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wengine wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanazofanya, nawasihi waendelee na juhudi hizo kwa faida ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iramba Mashariki kuna vikundi vingi vya wajasiriamali wanaofanya kazi za ufundi, kuna akina mama wanaosuka vikapu na kuuza ndani ya nchi na nje ya nchi (tatizo kubwa walililonalo ni elimu, vitendea kazi na mikopo kwa ajili ya kupanua shughuli zao). Naomba *SIDO* Mkoa iendelee kutembelea vikundi hivi kutoa elimu kwao na pia kuwasaidia kupata mikopo kwa ajili ya kuendeleza kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliahidi kujenga soko la Kimataifa Iramba Mashariki kwenye mji mdogo wa Iguguno ambapo mazao ya aina mbalimbali kutoka ndani ya Wilaya ya Iramba, Wilaya za jirani na pia Mikoa mingi inayozunguka eneo hili. Ningependa kufahamu ahadi hiyo imefikia wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia bado naikumbusha Serikali kututafutia bei ya mazao ya alizeti, vitunguu, giligilani na kadhalika ambayo yanastawi vizuri sana eneo letu. Bado nakuomba sana utusaidie kuendeleza kazi nzuri inayofanywa na vijana wetu upande wa viwanda vidogo vidogo na pia kwa wakulima wetu ili tuendelee kuondoa umaskini kwa watu wetu. Naunga mkono ohja asilimia mia kwa mia.

**MHE. ADAM K. A. MALIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Basil Mramba na Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, kwa hotuba nzuri ya Bajeti ya Wizara hii, kwa mwaka huu 2007/2008.

Naomba kutumia nafasi hii kwa namna ya pekee, kumpongeza Katibu Mkuu wa Wizara hii Dr. Tax Bamwenda, kwa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushika nafasi hii ngumu, namfahamu na sina mashaka naye hata kidogo. Ni mfano mzuri sana wa uwezo wa mwanamke wa Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungumza sana katika majadiliano ya hoja zilizotangulia masuala ya uzalishaji wa umma *(mass production)* ya kilimo. Tumezungumzia suala la kuongeza uzalishaji wa kilimo lakini hatujazungumzia suala la nini cha kufanya baada ya ongezeko la uzalishaji, si kwa kuongeza uzalishaji tu na suala la masoko litajirekebisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mchango uliotangulia nimezungumzia suala la Serikali Kuu na Serikali za Halmashauri za Wilaya kusimamia kwa kutoa mwongozo wa masuala mbalimbali ya kuondoa umaskini. Moja katika masuala hayo ni kuongeza uzalishaji wa kilimo na hapo hapo Serikali kufanya mikakati ya kufungua masoko ili

jitihada ya mkulima mdogo iishie karibu na eneo la uzalishaji. Mkulima mdogo anapolazimika kusafirisha pamba yake kutoka Shinyanga mpaka Dar es Salaam ni kumuanika mkulima kwenye mazingira ambayo ataibiwa na kuingizwa mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima Serikali kwa pamoja ikubali kwamba kuna *coordinated effort* ya Wizara na Idara mbalimbali za Serikali ili mikakati inayopangwa kutokea uzalishaji mpaka viwandani na baadae masoko ya nje ni jitihada itakayoratibiwa na Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Masoko, lakini wadau wengine watahusishwa kwa ukamilifu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, wakulima wa korosho wa mkoa wa Pwani, hususan wale wa Wilaya yangu ya Mkuranga wanazalisha tani kama 10,000 kwa msimu hali ya kwamba uwezo wa kuzalisha kwa mwaka ni kuzalisha kwa mikakati iliyo bora hadi tani 35,000. Lakini hata hiki kiasi kidogo cha uzalishaji hakipati soko na hivyo kinaondoa motisha ya kuongeza uzalishaji. Nina imani kwamba Wizara hii inatakiwa itupatie mwongozo wa mwelekeo wa biashara ya nje na hivyo kutupa *indicative prices* (bei za mwelekeo) za mazao ya biashara zingestahili kulipwa kwa mkulima *at base level.* Naomba nipatiwe maelezo kuhusu utekelezaji wa majukumu hayo kwa mazao yote na ni kitengo gani na fedha gani zimetengwa kwa ajili ya kuboresha kazi za Idara hii.

Naomba maelezo ya mikakati ya biashara ya mazao ya kilimo mbadala *(non-traditinal export crops)* kama ufuta, alizeti, mihogo, vanila, hiriki, karafuu, pilipili mtama, tangawizi na viungo vinavyoota katika maeneo mbalimbali ya Tanzania. Mimi nimekuta viungo hivi vya karafuu na hiriki vinaota na kwa viwango vizuri sana maeneo ya Matombo - Morogoro, Turiani na hata Muheza, Tanga. Nani anafanya utafiti wa kujua mahitaji ya masoko ya nje ya bidhaa hizi na uwezo wa wakulima wetu wa kuzalisha kwa ajili ya masoko hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu na nipewe pia taarifa za biashara za mazao kama dengu, asali *(bee honey)* ambazo zinazalishwa kwa wingi katikati ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maelezo ya utekelezaji wa mikakati kwa malengo ya viwanda vidogo vidogo na hasa vile viwanda ambavyo vinahitaji pesa ndogo kusimama, vinahitaji malighafi asilia inayopatikana karibu na viwanda na ambavyo vinaajiri wafanyakazi wengi wasiohitaji taaluma *(non skilled labour).*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo mazuri ya Waziri, hakuna maelezo yenye utekelezaji kwa muda kamili *(specific time frame)* ya kufikiwa kwa utekelezaji wa mikakati hii kwa kushirikiana na *SIDO,* MKURABITA, Hazina, MUU na kadhalika.

Kuhusu mazingira ya biashara katika nchi za wenzetu na hasa nchi zilizoendelea, Wizara ya Biashara ndio Wizara inayotoa mwelekeo wa biashara ya nje na ndani na hivyo ni Idara nyeti kwa nchi hizi. Mimi nina mashaka ya idadi na kiwango cha taaluma katika Wizara hii kiasi cha kuweza kufanya kazi za kutathmini na kupanga mikakati ya biashara na mahitaji ya fedha na rasilimali zingine ili Tanzania iweze kuongeza mapato yake ya fedha za kigeni *(foreign exchange earnings).*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri anihakikishie kwamba ataimarisha uwezo wa kitaaluma *(capacity building)* ambao utaweza kutupa mwelekeo wa kuongeza mapato yetu kwa kufanya *best use* ya rasilimali zetu. Nina imani Waziri na wataalamu wake wanaelewa kazi kubwa inayowasubiri katika kuimarisha sekta ya biashara na viwanda katika zama hizi. Nawatakia kila la kheri na naunga mkono hoja.

**MHE. SALOME J. MBATIA:**Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa fursa hii niliyopata ili niweze kuchangia hoja hii muhimu iliyo mezani. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yao yote kwa kazi nzuri kwa mwaka 2006/2007 na mipango mizuri ya mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda ni sekta muhimu sana kwa maendeleo thabiti ya nchi yoyote, viwe vidogo au vikubwa. Viwanda vina *process* au kuongeza thamani mazao ya kilimo, viwanda vinatengeneza mashine na vipuri mbalimbali, viwanda vinatengeneza umeme, bidhaa na vifaa mbalimbali, hivyo sharti kuwa na viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ukweli kuwa sekta hii kwa kiasi kikubwa tumeahidiwa sekta binafsi, ni muhimu sana Serikali kusimamia na ku-*chart out* kama kutoa mwelekeo wa namna wanataka sekta hii iwe, lazima kutoa mwongozo fulani. Kwa mfano, juhudi tunayoweka sasa katika kuanza kuchimba makaa ya mawe, matumizi ya gesi, kuchimba chuma cha Liganga na kadhalika. Sina shaka hata kidogo kuwa Waziri Mheshimiwa Basil Mramba, anao uwezo wa kusimamia hili. Tuanze kupiga hatua sasa, *we should run fast while other are walking.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kilimanjaro umeathirika sana na ubinafsishaji. Viwanda karibu vyote vilinunuliwa na wamiliki binafsi na kufungwa!! Nashukuru hivi karibuni Mheshimiwa Basil Mramba ameonyesha kuanza kushughulikia tatizo hili. Tatizo hili ni kubwa kwa sababu limesitisha ajira kwa watu wengi na pia limedumaza mzunguko wa fedha na hivyo kuathiri uchumi wa mkoa huu. Baadhi ya viwanda ni kiwanda cha Magunia, viwanda vya Ngozi, *Kilimanjaro Machine Tools,* viwanda vya mbao, Hoteli ya Moshi na *Livingstone* na kadhalika na kadhalika. Nitamwomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni nini kinaendelea katika suala hili, hasa suala la kiwanda cha magunia, ambacho wafanyakazi wake vile vile hawakuachishwa kazi kwa haki na wanahangaika hadi leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Kilimanjaro Machine Tools* eneo lile lilitengwa kuwa *Special Economic Zone.* Je, suala hili limefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wizara hii inashughulikia pia biashara; na kwa kweli biashara nayo ni mtoto wa viwanda katika kukomaza uchumi, naiomba pamoja na juhudi zilizopo kupitia *SIDO, EOTF* na kadhalika, ianzishe elimu kwa njia mbalimbali ya ujasiriamali. Bahati mbaya Watanzania katika eneo hili hatuna mwamko mkubwa. Bila mwamko, ari, ujanja wa biashara, namna ya kuchukua *risk* katika biashara, hesabu ndogo ndogo, utamaduni wa kuweka akiba na kadhalika na kadhalika biashara

haitakua. Hivyo, nashauri Wizara hii isimamie zaidi katika eneo hili pia. Vinginevyo ninawatakia kheri na kazi njema Wizara iwe changamoto kubwa mbele yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupata maelezo kuhusu kiwanda cha magunia. Naunga hoja mkono.

**MHE. MUSTAFA H. MKULO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kilosa kuna Kituo cha *SIDO* kama kilometa nane kutoka Kilosa Mjini. Kama Mbunge wa Jimbo la Kilosa sina hakika kama kituo hiki kinatumika kwa ufanisi na katika maeneo gani. Nashauri wataalamu wa Wizara na wa *SIDO* washirikiane na mimi ili kukitembelea kituo hiki kwa wakati muafaka na kuona nini kifanyike ili kituo hiki kiwe na manufaa kwa wananchi wa Jimbo langu na Wilaya ya Kilosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza kwa Bajeti nzuri na naiunga mkono hoja hii.

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na utendaji wake mzuri wa kazi pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, naomba Wizara ijenge hoja, barabara za viwandani Temeke zihudumiwe na *TANROADS* Taifa kutokana na umuhimu wa mchango wa viwanda hivyo katika Pato la Taifa, Manispaa ya Temeke uwezo wake ni mdogo kimapato kuhudumia barabara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimwia Waziri kwa bidii zake binafsi dhidi ya kiwanda cha *Alfa Match Corporation Limited* cha kibiriti Temeke kupatiwa malighafi na Wizara ya Maliasili na Utalii, barua ya Mheshimiwa Waziri ya tarehe 07 Machi, 2007 kwenda kwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe hadi leo hawajapata malighafi, wafanyakazi 350 wamesimama kazi, naomba sana Mheshimiwa Waziri kwa huruma zako Mheshimuwa Waziri usaidie kiwanda hiki cha *Alfa Match Corporation Limited* wapatiwe malighafi kuokoa ajira za wananchi 350.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kusimamia na kuagiza mabanda yote yaliyozunguka uwanja wa Sabasaba kubomolewa, hii ni kero ya siku nyingi na uchafu kwa sura ya uwanja wa Sabasaba na kupongeza sana kwa hilo pamoja na Mkurugenzi wa uwanja wa Sabasaba bwana Khalfani, kusimamia maagizo vizuri na kwa ushupavu mkubwa na maboresho makubwa yaliyofanyika katika maonyesho ya mwaka 2006/2007, hongereni sana wafanyakazi wa uwanja wa maonesho ya Sabasaba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho Mheshimiwa Waziri naomba sana utenge muda wako utembelee wajasiriamali wa Keko wanaotengeneza samani mbalimbali pale

Keko pembeni ya barabara, nakukaribisha sana Mheshimiwa Waziri Temeke na ninakutakia afya njema. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ni Wizara muhimu sana kwa maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda, hakuna nchi inayoweza kuendelea bila viwanda. Juhudi za Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika zinategemea sana kuwepo kwa viwanda vitakavyosindika mazao ya wakulima ili kuyaongezea thamani. Wakati wa msimu wa mananasi, maembe, machungwa na kadhalika mazao haya huwa ni mengi mno sokoni kiasi kwamba yanapoteza thamani sana. Wakulima badala ya kunufaika kwa mazao hubaki katika hali ya unyonge lakini kwa mazao ya biashara kama pamba, mkonge, tumbaku na kadhalika yanauzwa nje ya nchi kama yalivyo bila ya kupitia viwandani ili kuviongezea thamani, pia wazalishaji wa mazao hayo wanapata bei ndogo. Kwa hivyo, Wizara hii haina budi sasa kuwa na mkakati maalumu wa kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ili mazao yetu yote yasindikwe ili tuuze nguo badala ya pamba, sigara badala ya tumbaku na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu biashara, sasa hivi tunaagiza zaidi kuliko tunavyosafirisha na mapato yetu ya fedha za kigeni yameshuka. Tuna fursa kubwa ya kuuza bidhaa zetu nje ya nchi kwa kutumia fursa ya Mashirika ya Kimataifa kama *AGOA*, *EPA* lakini hatujazitumia ipasavyo. Wizara haijawaeleza Watanzania walio wengi ni aina gani ya bidhaa zinauzika katika masoko. Wizara iandae vipindi vya *TV* na redio bidhaa gani inauzika wapi na utaratibu mzima utakaotumiwa toka kwa wakulima. Zaidi Wizara iwe makini kuangalia bidhaa zinazoingizwa nchini ziwe na ubora wa Kimataifa. Kuna tetesi kuwa bidhaa nyingi zinazoingizwa nchini sasa hazina ubora wowote hivyo kuhatarisha afya za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwaruhusu wageni kufanyabiashara ndogo ndogo kule Kariakoo, Dar es Salaam kunawanyima wenyeji nafasi za kufanya biashara hizo. Viwanda vilivyobinafsishwa baada ya kufa navyo havijafanya kazi iliyopangwa. Kwa nini Serikali haiwanyang'anyi wawekezaji hao? Tanzania ina malighafi nyingi kwa ajili ya viwanda vidogo vidogo, lililobaki ni kujipanga vizuri kuweka kipaumbele na kuwashawishi wawekezaji kwa kuweka miundombinu yote inayohusika. Ahsante.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Mheshimwa Basil Pesambili Mramba, Naibu Waziri Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Katibu Mkuu wa Wizara na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri ya matayarisho ya Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya viwanda, biashara na masoko ina umuhimu mkubwa kwa maslahi ya nchi na wananchi kwa ujumla. Viwanda mbali na kuzalisha bidhaa mbalimbali kwa matumizi ya binadamu, kadhalika viwanda vinasaidia ajira kwa vijana na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zote zilizoendelea duniani zile zenye viwanda ambazo zinazalisha bidhaa mbalimbali zikiwa kwa ajili ya matumizi ya ndani na nje.

Viwanda hivi vyaweza vikawa na umiliki wa Serikali au watu binafsi. Uchumi wa soko kwa nchi unategemea sana viwanda na nchi kupiga hatua za kimaendeleo haraka. Nchi yetu wakati inpata Uhuru iliwekeza nguvu kubwa sana ya kuanzisha viwanda vingi mali ya Serikali (mali iliyogusa wananchi wote) viwanda hivi vilifanya kazi nzuri na kukuza soko la ndani na kuleta maslahi kwa wananchi wote na pato la Serikali lilikuwa zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo wa mabadiliko ya kiuchumi yaliyotoka nchi za Magharibi na mabadiliko ya sera za CCM za miaka ya 1990 uliiomba Serikali katika umiliki wa viwanda na kukazikisha uwekezaji jambo ambalo lilikuwa zuri kabisa, kuiondoa nchi Serikali katika biashara na kuibakiza katika utawala pekee na hivyo kusimamia viwanda hivyo kisera na kuhakikisha kodi ya Serikali inapatikana, wazo hilo zuri sana lakini, kwa nini uwekezaji wa sekta hii ya viwanda unabagua maeneo ya kuwekeza?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ihakikishe viwanda vilivyopo sasa nchini vifanye kazi kwa ubora wa bidhaa zenye viwango vya kuridhisha, pia bidhaa za ndani zinazozalishwa na viwanda vyetu zipewe kipaumbele na Wizara ishirikiane na *SIDO* kusaidia uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo vya kusindika matunda na kukamua mafuta.

Pia Wizara idhibiti mfumo wa soko unaotokana na uzalishaji wa bidhaa wa viwanda vyetu, bidhaa ziwe na viwango vya ubora *(quality)* ya bidhaa zinazouzwa nchini na zile zinazouzwa nchi za nje na pia Wizara katika kipindi cha mwaka wa fedha 2007/2008 itoe kipaumbele kuhakikisha bidhaa za wakulima zinapata soko mfano zao la kitunguu linalolimwa sana mkoani Singida hususani Wilaya ya Iramba zao la alizeti, ufuta na karanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafunzo na uwezeshaji, uangalie vikundi vya ujasiriamali ambavyo mara nyingi hufanya kazi za ufaundi mbalimbali mfano ufundi seremala, ufundi chuma na cherehani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri akifanya majumuisho ningependa anieleze juu ya Msajili wa Makampuni (*BRELA*) kwa nini ofisi ya msajili huyu ipo mahali pamoja na isiwe na ofisi za Kanda na kadhalika. Naunga mkono hoja.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana kwa hotuba yako nzuri Mheshimiwa Basil Mramba, Waziri wa Viwanda na Biashara, Naibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja na watendaji wa Wizara nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu uko kwenye makaa ya mawe na chuma cha Liganga kilichopo mkoani mwangu Iringa. Mradi huu wa makaa ya mawe na chuma cha Liganga ni mradi mkubwa sana, nashauri kuwa zabuni ya kupata mwekezaji iwe ya Kimataifa *(International Tendering Procedure).*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itasaidia sana kwa Taifa letu kupata mwekezaji mwenye uwezo na wenye ujuzi wa kutosha. Kwani siyo siri Taifa letu linapoteza mapato mengi sana kwa kupata wawekezaji wababaishaji. Vile vile tuboreshe sana miundombinu

ya umeme, barabara, reli na kadhalika ili kuweza kusafirisha hayo makaa ya mawe na chuma kwenye bandari zetu, wenzetu wa *NDC* wana ujuzi wa kutosha ni vizuri tungefuata ushauri wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile umeme wa Gridi wa Taifa upo Makambako na sasa umeingia maeneo ya Kidugula na Wanging'ombe naomba Wizara inisaidie kupata kiwanda cha alizeti kikubwa kupitia Serikali *(SIDO)* au wawekezaji ili wananchi wa Njombe au Mkoa wa Iringa wapate uchumi na maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba kujengwe kiwanda cha nyama au ngozi katika Tarafa ya Wanging'ombe au Makambako kwani kuna ng'ombe wengi sana kutoka maeneo ya Mbeya na Ruvuma. Kuna minada ya ng'ombe pale Wanging'ombe na Saja lakini ng'ombe hawa wanasafirishwa hadi Pugu Dar es Salaam. Endapo kikijengwa kiwanda basi gharama za usafiri zitapungua na kupata ajira kwa maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SIDO* ifundishe ujasiriamali ili wananchi na vijana waweze kujiajiri na kuweza kuibua ajira kwa Watanzania wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo ushauri wangu juu ya kupata wawekezaji wa Kimataifa kwa kutumia *International Tendering Procedures*, basi zile changamoto kuu za sekta za viwanda, biashara na masoko zitaweza kutatuliwa kwa urahisi zaidi. Changamoto ambazo zinaweza kutatuliwa ni kama zifuatazo; uduni na ukosefu wa miundombinu, ukosefu wa ujuzi na utaalamu na uchanga wa sekta binafsi ya ndani, najua udhaifu na udogo wa soko la ndani lenyewe ambalo lazima lisaidiwe na masoko ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ninawapongeza sana kwa kazi nzuri inayofanya Wizara yako ya Viwanda, Biashara na Masoko chini ya Mheshimiwa Basil Mramba. Naunga mkono hoja.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zilizoendelea za Ulaya zimefikia hatua hiyo ya maendeleo kutokana na sekta ya viwanda na siyo kilimo. Sekta ya viwanda inapokua sekta ya kilimo utegemezi wake unapungua. Nchi za Asia Mashariki kwa mfano, Malaysia zimepiga hatua za kiuchumi kutokana na maendeleo au ukuaji wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri maendeleo ya kweli ya nchi yetu yatatokana na ukuaji wa sekta ya viwanda. Ni bidhaa za viwanda ndiyo vitapata bei nzuri huko nchi za nje. Ushauri wangu Wizara hii iwahamasishe na iwasaidie wananchi angalau waanzishe viwanda vidogo vidogo ili bidhaa zetu za kilimo ziweze kutengenezwa. Kwa mfano, ubanguaji wa korosho, utengenezaji wa *juice* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa letu linakabiliwa na tatizo kubwa la kutouza bidhaa za kilimo nchi za nje ikilinganishwa na nchi jirani. Wananchi hawajasaidiwa ipasavyo kupatiwa masoko na njia bora ya ufungashaji *(packing)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilitegemewa kuwa matumizi ya gesi ya asilia katika viwanda, biashara zingepungua lakini sio hivyo, ni lini gesi hiyo itasababisha bidhaa za viwandani zipungue. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri anieleze je, umeme wa maji gharama yake ni sawasawa na umeme unaotokana na gesi asilia. Ahsante.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, nami naungana na wenzangu kwa kuiunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu ni kuhusiana na ng'ombe walio wengi kwa Mkoa wetu wa Mara kama mnavyoelewa. Napenda kufahamu nini mpango wa Serikali kusaidia Mkoa wetu wa Mara tupate kiwanda cha nyama kwa Mkoa wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja hii.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Iringa una mazao mengi sana ambayo ni *perishable,* lakini hakuna viwanda, mazao hayo ni viazi - Njombe, ngano - Makete, matunda na mboga mboga *(cabbage)* – Kilolo, je, nini nafasi ya Wizara katika ku-*promote* uanzishwaji wa viwanda? Mkoa wa Iringa hauna viwanda vya usindikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, soko huria katika nchi inayoendelea kama Tanzania ni kumwonea mkulima. Serikali ni lazima iweke masoko na hasa pale ambapo mazao hayanunuliwi. *SGR* ni lazima inunue mahindi na mazao mengine ili wananchi waendelee kulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa kujua viwanda na mashirika kama *National Milling Corporation (NMC)* nini hatma yake? Maana hivi ni vitega uchumi vikubwa sana katika nchi yetu na vilikuwa na uwezo wa kuajiri wafanyakazi wengi sana takriban 3,000, vilikuwa vinanunua mahindi na kuuza mahindi na unga, je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza hizi *National Milling Corporation* hasa ile ya Mkoa wa Iringa?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo tajwa hapo juu na baada ya kupata ufafanuzi nitaunga mkono hoja hii. Ni muhimu pia Serikali ikaweka *incentives* katika kuanzisha viwanda nchini Tanzania ili kuvutia wawekezaji, *incentives* za mikopo na nyingine nyingi.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia na kujua mambo yanayonisumbua kwa muda mrefu nipate majibu. Kuna viwanda vilivyoanzishwa kwenye Mkoa wa Kagera. Suala la kukosa elimu na mtaji viliharibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na kiwanda cha Majani Maruku na wananchi wa sehemu ya Bukoba Mjini na Bukoba Vijijini hicho kiwanda kilikuwa kinaitwa *Bukoba Tea Estate.* Kwa sasa mwekezaji inaonekana nguvu zake ni ndogo sana,

wakulima wadogo wadogo walikata tamaa pamoja na kushuka kwa bei. Naomba nipate majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kahawa, kuteremka kwa zao la kahawa kumesababisha wakulima wakate tamaa na viwanda vilivyoko Bukoba Mjini ulipaji wao sio mzuri hasa *KCU* pamoja na kiwanda cha *Amra Bukop TANICA.* Viwanda vyote hivyo bei yao si nzuri, ni kwa nini Serikali isiingie kwenye soko huria kuliko wakulima kutegemea hao wanunuzi wadogo wadogo? Soko huria likapatikana kwa wakulima wote wa Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo chao kikubwa kilikuwa ni kahawa, sasa naomba nipatiwe majibu, hiki kilimo au wakulima wa zao hili mkoani Kagera wana matatizo gani, kwa kuwa mazao mengine kama pamba kidogo bei yake sio mbaya je, kahawa ina matatizo gain? Bei ya samaki iko juu sana. Naomba Mheshimiwa Waziri atembelee hivi viwanda vya Mkoa wa Bukoba na Mwanza, Bukoba Mjini kuna kiwanda kimoja. Pia kwa nini *SIDO* hapo Bukoba haiendelei? Unakuta *SIDO* sehemu nyingine zinaendelea vizuri, naomba Wizara inipe jibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tunaulizwa maswali mengi mambo yote niliyoyaweka kwenye mchango wangu na mengine mengi ya mchango wangu yapo kwenye Kamati yangu ya Uwekezaji na Biashara na haya ninaamini nitajibiwa vizuri sana na Mheshimiwa Waziri. Naomba kuwasilisha. Ahsante.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na naiunga mkono hoja hii. Naomba maelezo na ufafanuzi katika maeneo yafuatayo:-

Katika ibara ya 112, Mkoa wa Tanga una maeneo yapi na viwanda vingapi vya *EPZ?* Ibara ya 24 naipongeza Kampuni ya *Unnat Fruit Processing Limited* (Morogoro) kwa kuwakwamua wakulima wa mboga na matunda kwa kupitia Wizara. Tunaiomba Kampuni hiyo iwekeze Wilayani Lushoto ambako kuna matunda mengi. Kuhusu ibara ya 42 ni lini *SIDO* itajenga *cluster* ya viwanda vidogo Wilayani Lushoto?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Serikali ina mikakati ipi kupima dhahabu inayouzwa na masonora, watu wengi wanalalamika kuuziwa bangili, pete, mikufu kwa bei kubwa. Lakini unapotaka kuiuza tena unapewa pesa kidogo na hii inatokana na wenye maduka kujua dhahabu hiyo haina thamani. Nataka kupata maelezo Serikali inapata kiasi gani cha mapato kutokana na ukaguzi wa magari toka Dubai?

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia siku ya leo kuamka salama. Pia nakushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako uliobora .

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba nitoe shukrani kwa Mhehismiwa Waziri kwa hotuba yake iliyo bora.

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye mchango. Watanzania walio wengi wanaishi kwa kufanya biashara; wapo wa maduka na pia wanauza vitu vyao kwa njia ya kwenda huku na kule. Huyu ni mfanyabishara wa kawaida ila amekosa kitu ama eneo la kufanyia biashara ama mtaji. Mtu huyu sisi hatutaki aishi kwa nini? Kwa kweli mji kuwa safi ni vizuri, lakini Serikali ingewaruhusu wafanyabishara wadogo wadogo kufanya biashara humo mjini kwa kufunga baadhi ya mitaa kama vile Jumamosi na Jumapili ili kuwawezesha wauze bidhaa zao. Mpango huu uko hata London ambako kuna *Sunday Market.* Hii inamsaidia mfanyabiashara huyu kufanya biashara na mara nyingi huyu ndiye anayeuza kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda, nchi haiwezi kuendelea haraka bila kuwa na viwanda. Nchi yetu ina kila aina ya mazao na pia madini na vile vile ardhi kubwa. Kwa nini Serikali haijengi viwanda kwani kwa kufanya hivyo ni kukuza uchumi wetu. Mazao mengi kama vile nyanya, machungwa na kadhalika vinaharibika bure kwa ukosefu wa viwanda. Hivi sasa nchi jirani ya Kenya inakuza uchumi wake kutokana na matunda yanayozalishwa Tanga. Sisi hatuna uwezo kweli wa kumiliki kiwanda angalau cha *juice?* Naitakia Wizara itimize wajibu wake. Ahsante.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza sina budi kumshukuru Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kuchangia hii leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ni moja kati ya Wizara zinazotoa ajira nchini na zinazoinua Pato la Taifa na zinazoinua hali ya wananchi katika maisha ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vingi nchini vinategemea malighafi kutoka nchi za nje na kuacha rasilimali zetu kwa kuona hazina ubora. Lazima tujipe moyo wa kujiamini na kutumia rasilimali zetu, kwa mfano, *gypsum* inayotoka Japan haina ubora kama *gypsum* inayopatikana nchini mwetu. Je, Serikali haioni sasa tufanye ari ya kuzalisha zaidi kuliko kuagizia nje na kutia hasara Taifa badala ya kuleta faida kwa kutumia chetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara/Serikali ifanye jitihada za makusudi kwa wajasiriamali wadogo wadogo kwa kuvifufua viwanda vilivyokufa ili wajasiriamali hao waweze kuongeza ajira nchini. Pia Serikali kama haiwezi kuvisimamia viwanda hivi, basi wapewe wawekezaji ili wafufue. Lakini katika viwanda hivyo kuna tatizo la miundombinu ya umeme na maji. Kwa hiyo, kwanza la kufanya ni kuhakikisha hayo yanapatikana ili mwekezaji aje kufanya kazi ili wananchi wetu wafaidike.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itahakikisha viwanda vyetu vitaimarishwa ili masoko yetu yazidi kukua, biashara nayo izidi kukua ili wananchi wapate ajira na wao waishi kwa raha katika Taifa lao?

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na timu yao kwa Bajeti hii yenye mwelekeo wa kuleta mabadiliko nchini. Naunga mkono hoja. Mungu awape heri.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri wa Wizara hii Mheshimiwa Basil Mramba kwa juhudi kubwa ya kuhakikisha kuwa Tanzania inaondokana na uchumi legelege wenye utendaji duni wa kibiashara na usio na ujasiriamali na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Naibu Waziri, kaka yetu Mhehimiwa Hezekiah Chibulunje, kwa kuhakikisha wanaenda bega kwa bega na Waziri wake. Pia nampongeza Katibu Mkuu pamoja na timu ya wataalamu. Napongeza pia Maonyesho ya Saba Saba na mafanikio yake. Hii inaonyesha mahitaji ya wajasiriamali hao kuwa na sehemu kama hizo za kudumu ili kuweza kuonyesha bidhaa zao kila inapohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kuwa ipo haja ya kuwa na eneo la maonyesho ya Kimataifa nje kidogo ya Mji kama *Bagamoyo Road* ambalo litawezesha pia hata maonyesho ya bidhaa za kilimo. Pia eneo hilo linaweza kuwa na maghala ya kuhifadhi chakula kama *SGR* ambayo kila mwaka ihakikishe chakula cha awali kimekuwa *phased out* kwa bei ambayo naamini itakuwa ya chini kuliko ya mwaka huo lakini juu kidogo kuliko ya kununulia. *Of course* inahitaji *study* zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize Wizara kama ambavyo nilihoji jana Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ninamwamini Mheshimiwa Waziri kuwa ni mtu makini na ana uwezo mkubwa akiamua. Hivi hii *R & D Instituion, TIRDO* imekosa nini mpaka inadhalilishwa hivi kwa kunyimwa hati yake? Wizara inashindwaje kushughulikia suala dogo tu hili? Nashauri suala la hati ya *TIRDO* lipewe kipaumbele kwani hii inaleta hisia ya mkono wa mtu.

Suala la Jumuiya ya *EPA* likamilishwe mapema lakini pia uchambuzi wa kina wa kuzingatia hali ya usalama wa *block* lizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SIDO* ipewe ruzuku ya gharama za kufika vijijini ili kuwafikia walengwa wengi zaidi. Kuhusu Mchuchuma na Liganga vipi? Naunga mkono hoja.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko na pia nampongeza Naibu Waziri pamoja na watendaji wote kuanzia Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yoyote ili iweze kuendelea, lazima iwe na viwanda vingi na vinavyozalisha bidhaa nzuri na bora kwa masoko ya ndani na nje. Lazima tuweke malengo ya uzalishaji na pia tuwe na mikakati ya kutafuta masoko ya uhakika ya nje na kuyafuatilia kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, soko la Marekani ni kubwa na la uhakika. Marekani wanahitaji kahawa, chai, vikombe, *table mats* kwa maduka makubwa ya New York. Naomba Serikali kwa kupitia *BET* kusimamia soko hilo liimarike. Soko la New York linaitwa *Big Apple,* kila mtu anaweza kumega hapo. Njia rahisi na bora ya kuingia soko hilo kwa urahisi na uhakika ni kuwa na mwakilishi wa biashara kwenye Ubalozi wetu wa Umoja wa Mataifa. Mwakilishi huyo awe na taaluma ya biashara, asiwe *Diplomat.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu sasa imekuwa *dumping place.* Bidhaa hafifu ambazo hazina viwango zimezagaa kwenye maduka. Wafanyabiashara wanasema wazi wazi kwamba wanazo bidhaa hafifu na bora na bei ni tofauti. Bidhaa hafifu na za kiwango cha chini zinadidimiza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo bidhaa hafifu nyingi madukani kama vifaa vya umeme na ujenzi. Nyumba nyingi zinaungua hasa shule kwa kuwa nyaya zake ni za ubora wa chini na shule nyingi zimeungua kwa sababu hiyo. Madukani kuna nyundo hafifu, betri hafifu, kalamu hafifu, balbu hafifu, misumari hafifu, chuma hafifu na vingine vingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara ichukue hatua ya haraka kumaliza tatizo hili. Viwanda vingine kama *Tanzania Breweries Ltd. (TBL)* inakataza wafanyabiashara kuuza bia zake Kenya, hii ni tabia isiyo nzuri. Naiomba Wizara ikemee tabia hii. Pia *TBL* inayo tabia ya kutangaza zaidi *Castle beer* kuliko zile *brand* za Tanzania kama Safari na Kilimanjaro. Hili litupiwe macho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza *Serengeti Breweries* kwa kujitahidi kuuza bia zake Kenya kwa utaratibu unaofaa, pia naipongeza *SIDO.* NaishauriWizara iwaongezee fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nashauri Watanzania wasaidie, wawezeshwe kuanzisha viwanda na kuzalisha bidhaa bora kwa masoko ya nje na kutumia fursa ya masoko ya Marekani, China, Korea na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei za uzalishaji ni kikwazo kikubwa kuingia kwenye masoko kwa mpango wa *AGOA* na kadhalika.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii na taasisi zake kwa kazi nzuri wanazofanya na mwelekeo wa uboreshaji wa huduma za viwanda, biashara na masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa ushauri wa ziada katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu biashara ya matunda toka Muheza na Wilaya nyingine kwenda nje ya nchi (nchi jirani), bashara kati ya Tanzania na Kenya ya matunda hasa machungwa inafanywa kienyeji. Mwaka 2001/2002 nilieleza Bunge hili na Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu biashara hiyo licha ya Wizara wakati huo kuahidi kuja

kutafiti na kusimamia, hawakutekeleza. Wageni toka nchi jirani wanaingia hadi mashambani, wananunua machungwa kwa fedha za Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, wageni wanakodisha magari na kulipa gharama za usafiri kwa fedha za Tanzania kwa 80% na kuwapa fedha za Kenya 20% ili magari hayo yaweze kununua mafuta kutoka Nairobi na posho kidogo ya madereva, pia Tanzania haina *record* za mauzo hayo nchi jirani na haipati fedha yoyote ya kigeni licha ya kuuza nje ya nchi, wafanyabiashara wa nchi jirani wanabadilisha fedha zao huko kwao kwa kununua fedha za Tanzania katika maduka ya kubadilisha fedha na hivyo kuwawezesha kununua machungwa Muheza kwa fedha za Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania walipojaribu kufanya biashara hiyo kwa kupeleka machungwa Nairobi na kuyauza huko, walifanyiwa vitendo vya ukatili na hivyo kuingizwa katika hasara na kujiondoa katika biashara hiyo, wafanyabiashara hao wa nchi jirani wanafanya biashara hiyo hapa nchini bila ya kuwa na leseni za biashara wala hawalipi kodi ya mapato na *TRA* hawana habari!

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Muheza imeshindwa hata kupata ushuru halali wa machungwa yanayosafirishwa kutoka Muheza hata kushindwa kuwataka wageni hao kuwa na leseni za biashara! Pamoja na kushindwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, je, Wizara inasema nini juu ya kutokuwa na kumbukumbu halisi za mauzo ya nje kama Taifa na kuuza nje ya nchi machungwa kwa fedha za Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, hatuoni kwamba kwa mapungufu hayo inachangia kuongeza upungufu wa mauzo ya nje Kitaifa na upungufu wa mapato ya fedha za nje Kitaifa! *Balance of trade*, *balance of payment.*

Kwa kuwa mtindo wa biashara nilioainisha hapo juu unafanyika hivyo pia katika Wilaya nyingine hasa katika maeneo ya mipaka ya nchi jirani Kaskazini na Kusini mwa Tanzania ni vema Wizara ikabuni utaratibu mzuri wa kisheria ili kuliokoa Taifa katika mfumo huo hafifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuanzisha kiwanda cha usindikaji wa matunda Muheza, njia mbadala ya kuondokana na mfumo huo hafifu wa bishara ni kuanzisha kiwanda cha usindikaji wa matunda Muheza pamoja na kujengwa haraka kwa soko la Kimataifa la matunda na mbogamboga Segera.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii iwe ni changamoto kwa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko sasa kumsaidia Mheshimiwa Rais kukamilisha azma hiyo ya kuisaidia Muheza kupata wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani kwamba Wizara itasimamia mapendekezo haya na taarifa waliyoweka bayana mwaka huu na isiwe tena ukimya kama ilivyotokea mwaka 2001/2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima wa afya na kunijalia kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kuwasilisha vyema hotuba yao pamoja na ushirikiano alionao na watendaji waliofanikisha kutengeneza hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hotuba hii katika Halmashauri ya Biashara ya Nje *(BET)*. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Fuoni ambao walishiriki katika kutembelea Maonesho hayo kwa mwaka 2007 niipongeze Halmashauri hii *(BET)* kwa kufanikisha kwa kiwango kikubwa na kizuri ya Maonesho ya mwaka huu kwa kuonyesha bidhaa bora zilizopo nchini kwetu na hasa hasa bidhaa zilizotengenezwa na wajasiriamali wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la kuruhusiwa kwa wingi wajasiriamali ni la kupongezwa na linafaa kuendelezwa, kwa sababu ni suala la kuwatia moyo na kuwatangazia kazi wanazofanya na kuwatangazia soko ambalo watauza bidhaa zao na kuwaongezea kipato na kauli mbinu ya Chama cha Mapinduzi ya kupunguza umaskini (MKUKUTA).

Mheshimiwa Naibu Spika, nauliza Halmashauri hii sijui kama baada ya kuangalia bidhaa hizo kama kuna ushauri wowote waliotoa kwa wajasiriamali katika bidhaa zao kwa sababu bila ushauri wa kile walichozalisha itakuwa hatujawatendea haki na kufanya maonesho yetu yawe hayana maana badala ya kukusanya fedha za viingilio tu. Naiomba Halmashauri iwe na tabia ya kuwaelimisha ili ubora wa bidhaa upatikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Halmashauri kuangalia bei za kuingilia katika viwanja kwa sababu bado kuna malalamiko kuwa bei ni kubwa sana na wananchi wengi wanashindwa kuingia kuangalia maendeleo ya Watanzania ya biashara na utendaji wa kazi zetu kwa taasisi mbalimbali na huishia kuona na kusikia katika vyombo vya habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ikipungua wananchi wengi wataingia na mapato yataongezeka. Nadhani lengo la kushinda maonyesho na sio biashara lakini Mheshimiwa Waziri atanielekeza zaidi wakati wa majumuisho. Kwa hayo machache naunga mkono hoja.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika hapa Bungeni hali nikiwa mzima. Pia kukupongeza wewe kwa umahiri wako na kutuongoza pale tunapokosea na kutusifu pale tunapofanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu haya, sasa nitoe shukrani zangu kwa Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri iliojaa mategemeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba uniruhusu nitoe mchango wangu kwenye Wizara husika kwa kuanza nianzie matunda. Nchi yetu imejaaliwa na matunda mengi sana lakini mpaka sasa tumeshindwa ku-*export* nje. Baadhi ya wakulima wetu hapa nchini kwa Kanda ya Tanga wakulima ambao hulima nyanya na maembe wanauza bidhaa zao katika nchi jirani kama Kenya. Kenya wananunua bidhaa hizo hapa, lakini sisi tumeshindwa. Bidhaa hizi Kenya husafirisha nje na kutengeneza *juice* ambayo tunaletewa sisi hapa nchini. Sio hivyo tu wanatengeneza hata nyanya za makopo *(tomato Paste)* na kadhalika. Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha matunda yetu na mengineyo yanakuwa kwenye *good quality?*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kushangaza jinsi matunda yetu hapa nchini yanavyopotea kwa njia ya kuoza. Msimu hadi msimu Watanzania huvuna matunda mengi sana na mengi ya mazao hayo hutupwa. Kitendo hiki hakimpi tija mkulima wetu. Ni vyema Serikali impatie soko mkulima huyu ili imwezeshe na pia kuinua uchumi wa Taifa letu.

Kuhusu masoko, Watanzania walio wengi wanafanya kazi za aina kwa aina lakini kikwazo ni soko. Hivyo ni vyema Serikali itupe majibu ni lini Mtanzania atakuwa na uhakika wa soko la kuuzia bidhaa zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu biashara, kupatikana kwa uchumi wa nchi na wananchi wenyewe kunatokana na kuwepo kwa biashara. Hii inampelekea mwananchi wa kawaida kuishi katika maisha bora kwa kila Mtanzania. Tunahitaji viwanda nchini, katika viwanda vyetu sisi hivyo vilivyopo vimekosa kuzalisha kutokana na ukosefu mambo kama, maji, umeme, vipuri na upandaji wa mafuta. Kama haya yanakosekana ni lini biashara yetu itatuwezesha?

Mheshimiwa Naibu Spika, naitakia Wizara ifanikishe azma yake. Ahsante.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Naomba Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kuwezesha na kuongeza ajira kwa wakulima. Naomba kuangalia uwezekano wa kuanzisha Kiwanda cha Kusindika Mazao ya Matunda. Geita ina maembe ya kutosha, tikiti maji za kutosha na nanasi nyingi sana ambazo ni daraja la kwanza ulimwenguni.

Naomba atafutwe mwekezaji anayeweza kuzalisha *juice* badala ya kununua za kutoka nje kama Uganda, Kenya na Afrika Kusini. Tafadhali leteni kiwanda ili matunda ya Geita, Lushoto, Tabora na Ukerewe yawekwe katika pakiti hii itaingiza pesa nyingi za kigeni na itaongeza ajira kwa vijana. Watu wengi hawanywi pombe, wanakunywa *juice,* Wizara hii naiomba itusaidie kupata kiwanda cha kusindika mazao ya tikiti maji, nanasi na maembe. Hatuma pa kuyaweka, yanaoza na wananchi wanakata tamaa. Nanasi za Geita zinaongoza katika daraja la uzuri wa nanasi ulimwenguni.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri na wataaalamu wake waende Geita wakajionee na waishauri Wizara. Ahsante. Naunga mkono hoja.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, duniani kote nchi zilizoendelea zilifika hapo baada ya mapinduzi ya viwanda. Baada ya uhuru nchi yetu ilianzisha na kufungua viwanda vingi mbalimbali. Hapa katika miaka ya hivi karibuni Serikali na sekta binafsi imeteteреka katika kuanza na kufungua viwanda vipya na kuviendeleza vya zamani. Upo wapi mkakati wa muda mrefu, kati na mfupi ili kufufua viwanda vya viberiti, jembe, viatu, baiskeli, nguo na nyama?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini nchi yetu itaondokana na utegemezi wa kuletewa vitu vya viwandani kutoka nje? Wenzetu wa Kenya wapo na viwanda vingi ambavyo soko lao kubwa lipo kwetu. Tanzania ni nchi ya tatu kwa wingi mifugo hadi sasa tunayo viwanda vya nyama vitatu tu. Je, kuna mpango gani wa kuwa na viwanda vya nyama walau katika kila mkoa wenye mifugo wengi kuwa na kiwanda kimoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mazao mengi ambayo Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko yatakiwe kuvitafutia masoko nje ya nchi, mazao kama asali, vitunguu, mchele, ng’ombe na kadhalika. Ninawatakia kheri, baraka katika kazi.

**MHE. NURU AWADHI BAFADHIL:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza nitazungumzia kuhusu viwanda. Jiji la Tanga lilikuwa na viwanda kadhaa ambavyo viliweza kutoa ajira kwa wananchi na kuwapunguzia makali ya maisha. Viwanda hivi vilikuwa vikifanya kazi saa ishirini na nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi viwanda hivyo vingine havizalishi vizuri na vingine vimekufa kabisa. Viwanda vinavyozalisha kwa kiwango cha chini ni Kiwanda cha Sabuni (Foma), Kiwanda cha Sabuni (Mbuni, Gardenia na kadhalika), Kiwanda cha Nguo *(Afritex)* japokuwa vingine ni vya makampuni binafsi lakini vilisaidia kukuza ajira kwa wananchi wetu na kuwapunguzia makali ya maisha. Kuna viwanda ambavyo vimekufa kabisa kama Kiwanda cha Mbolea *(TFC),* Kiwanda cha Plastiki *(Amboni Plastic)* na Kiwanda cha Chuma *(Steel Rolling Mills).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kiwanda cha Chuma wawekezaji wote wanaomba kuwekeza inaonekana kwamba Serikali haina kinachopata kutokana na uwekezaji huo sana sana baadhi ya wafanyakazi kuiba baadhi ya vifaa mbalimbali wakiwemo na wale wezi wa mitaani ambao nao pia wanachangia kufanya vitendo viovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia pia kuhusu wafanyakazi na masoko ya biashara zao. Mfano kuna wafanyabiashara wanaotengeneza samani nzuri ambazo zinalingana na samani ambazo zinaagizwa kutoka nchi za nje. Tatizo wao wanatengeneza samani lakini soko la kuuza samani hizo hawana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iwe na utaratibu wa kuthamini bidhaa zinazotengenezwa hapa nchini ili kuinua ari ya wananchi wetu na kukuza thamani ya bidhaa zetu ambazo zinaweza kuliingizia Taifa uchumi na kupunguza makali ya maisha.

Kuna wajasiriamali wetu ambao wana viwanda vidogo vidogo vya kusindika chakula. Serikali haioni huu ni wakati muafaka kwa kukuza viwanda vyetu vidogo vidogo na kuachana na kununua vyakula vinavyosindikwa kutoka nje. Vyakula vyetu ni vizuri pia virutubisho ambavyo vinatengenezwa viwanda vya nchi za nje vyakula ambavyo vingine vimepitwa muda wa kuvutumia lakini bado vinauzwa na kuna wananchi wengine hawaoni umuhimu wa kuangalia tarehe ya mwisho wa kutumika kwa vyakula hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara/Serikali ifanye jitihada za makusudi za kutoa mafunzo kwa wajasiriamali wadogo wadogo ili waweze kujiendeleza na idadi ya wajasiriamali kuongezeka kitu ambacho kitasaidia kuongeza ajira.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwa maandishi kwa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa mwaka 2007/2008. Naipongeza Wizara hii chini ya Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalamu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia suala la wafanyabiashara ndogo ndogo. Nawaipongeza Wizara kwa kuongeza uhamasishaji na ujenzi wa viwanda vidogo vidogo ambavyo ndio njia pekee ya kuwasaidia wajasiriamali kuondokana na umaskini hivi sasa vyakula na matunda yaoze kwa kukosa soko, njia ya ukaushaji na usindikaji ndio njia pekee ya kuinua uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua masoko ya jiji la Dar es salaam yapo chini ya Halmashauri hizo lakini yapo chini ya Wizara hii. Kuna kero kubwa na adha kwa wananchi kutokana kuingizwa taka za majani na nyasi zinaharibu mazingira ya masoko kwa uchafu. Pia masoko haya baadhi ni mabovu mno na kuathiri hadhi ya Jiji mfano Buguruni, Mwananyamala na kadhalika pia miundombinu duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ifuatilie wawekezaji wa Kichina wamekuwa wakileta baadhi ya bidhaa hazina hadhi mfano viatu ni vibovu mno, ufanywe uchunguzi ili kudhibitisha haya na kuuza kwa bei ndogo sana na hivyo kuathiri wafanyabiashara wa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, madini ya Liganga na mkaa wa mawe wa Mchuchuma na mradi wa madini ya chuma Liganga na pia kuangalia madini mengine ambayo ina thamani zaidi, kama *vanadium* na *titanium* pia Serikali iangalie vijiji na Halmashauri yaliyozunguka maeneo hayo jinsi itakavyofaidika na mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ifuatilie wanachi ambao wanafanya kazi katika viwanda vyenye kemikali bila kupatiwa vifaa vya kujihifadhi wanapokuwa kazini, pia Wizara iwe na utaratibu wa kukagua mara kwa mara ili kuepusha madhara kwa wafanyakazi hao. Wafanyabiashara wasio waaminifu na mafisadi wanaochanganya mafuta ya magari na maji na upandishaji bei umedhibitiwe. Vipi hadi sasa takribani wiki sasa vyombo vya habari wamekuwa wakikuonyesha vituo kadhaa ambavyo vimekuwa na mafuta ya gari na maji je, ni hatua zipi zimechukuliwa hadi sasa? Huu ni ufisadi kwa magari ya wananchi.

**MHE. AME PANDU AME:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Waziri na Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko kwa hotuba yao nzuri na mimi nitoe mchango wangu kwa sekta ya viwanda, biashara na masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu Tanzania inayo rasilimali nyingi mno iwapo Serikali itajenga viwanda na kuzitengeneza rasilimali tulizonazo, vifaa vinavyohitajika kwa binadamu kama vile viatu, vinywaji, nguo kusindika nyama na kadhalika. Watanzania walio wengi wataondokewa na umaskini. Viwanda vidogo ndio chanzo cha viwanda vikubwa na ndio chanzo cha biashara kwa sababu bila viwanda biashara nyingi haziendi. Pia kuruhusu bidhaa ambazo nchi yetu ingeweza kuzitengeneza inashusha hadhi pia ya nchi yetu. Ili wananchi wa Tanzania waondokewe na umaskini ni kuwafanya waweze kufanya biashara ambazo zitakuwa na masoko ya kuuzia biashara zao hapa nchini na pia nje. Naunga mkono hoja.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali kabisa kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Hai, naomba niwapongeze nyote Wizarani nikianzia kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wengine wote kwa kazi nzuri mnazofanya kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ushauri kwenye maeneo machache yafuatayo; kwanza uratibu wa viwanda nchini. Ni muhimu kwa viwanda vyote hapa nchini vikawa chini ya hii Wizara kwa maana ya kuratibu na kuwa na takwimu sahihi, pili, uanachama wetu kwenye Jumuiya za Kibiashara, muhimu hapa ni maslahi ya Taifa letu na tusiingize siasa katika maamuzi haya, tatu, kuhusu vituo vya utafiti, pamoja na Bajeti finyu napendekeza vitafutwe vyanzo vingine vya kuweza kuapata fedha kwa maana ya kuziwezesha taasisi zilizochini ya Wizara hii kwani ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu na nne, *EPZA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri mamlaka hii iongezewe watumishi ili kumsaidia Mtendaji Mkuu wake Dr. Meru anayejitahidi sana pamoja na kuwa wachache sana lakini ameweza kutembelea na kukagua maeneo mengi kwa muda mfupi. Pia Serikali za Mikoa ziharakishe utambuzi wa maeneo yao ya uwekezaji. Pia nashauri kuwashirikisha wananchi na Serikali za Halmashauri katika maeneo yote ya *EPZ* kwa ajili ya kuondoa migogoro inayoweza kujitokeza. Bado pesa ni kidogo sana kwa *NDC,* kuhusu *TBS* wanafanya kazi nzuri sana, ila ile shughuli ya ukaguzi wa magari nje ya nchi isitishwe kwani haina tija kwa nchi na viwanda Mkoani Kilimanjaro. Kuna mkakati/mipango gani ya kuhakikisha vile viwanda vilivyobinafisishwa vinafanya kazi? *Kilimanjaro Machine Tools (KMT)* iliyopo Jimboni kwangu Hai nayo ni kimojawapo, lakini zaidi ni lile eneo jirani na kiwanda hiki ambalo tunalihitaji sana katika Halmashauri yetu mpya kwa sababa kuna wawekeza wengi wanahitaji maeneo pale wa ndani na nje. Naunga hoja mkono.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Basil Mramba, Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko kwa hotuba yake nzuri na yenye uchambuzi wa kina kuhusu malengo tuliyojiwekea kuona nchi yetu inaendelea

kwa haraka katika eneo la viwanda na biashara. Ni kwa msingi huo naomba nitamke bila kuchelewa kwamba naunga mkono hotuba hii. Naomba nikumbushe Wizara kwamba Siha sasa ni Wilaya na Makao yake Makuu yapo katika mji mdogo unaokuwa kwa haraka sana kibiashara wa Sanya Juu. Katika huu mji wapo vijana wengi ambao hawana ajira pamoja na wale wengine wote waliopo katika Wilaya hii mpya. Naomba kuchukua fursa hii kuiomba itusaidie katika uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo *(SIDO)* katika eneo hilo. Sisi viongozi wa wananchi tupo tayari kushirikiana na Wizara katika ngazi mbalimbali ili kulifanya zoezi la kuanzisha viwanda vidogo vidogo kwa kuunganisha nguvu za wananchi linafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba Serikali itueleze kwa kina hatua inayochukuliwa kwa wote ambao wananunua mazao bila ya kutumia mizani na vyombo vilivyokubalika. Tatizo hili lipo katika Wilaya yangu ya Siha na zinawaumiza sana wananchi hasa akinamama waishio Karansi, *West Kilimanjaro,* Sanya Juu ambao wanauza viazi, mahindi, maharage kwa mtindo unaoitwa lumbesa. Naomba Serikali itoe kuali kuhusu suala hili. Narudia tena kwa kuunga mkono hotuba hii.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Naomba *SIDO* ipewe uwezo wa kifedha kwa ajili ya mafunzo ya wajasariamali wengi zaidi ili waweze kupata uelewa wa kusindika mazao yao na mafunzo mengi. Hii itasaidia kuongeza ajira kwa wajasiriamali wengi na wataweza kuanzisha viwanda vyao vidogo iwapo wakisimamiwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazalendo wapewe upendeleo maalumu wa kudhaminiwa na Serikali *(Government guarantee)* kwa kuanzisha viwanda vikubwa na vya kati kwa lengo la kuongeza uchumi wa nchi na wa mtu mmoja mmoja. Kuhusu *VETA* na *SIDO* ndio uti wa mgongo kwa maendeleo ya vijana na wanawake katika kuwaondolea unyonge wajasiriamali wetu. Wizara izingatie kwa undani zaidi kwa kuongeza wataalamu wengi na hata kutoka China, India na kwingineko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nawapongeza sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa hatua nzuri na kazi kwa ujumla. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wakurugenzi na watendaji wote kwa kazi nzuri sana mnazozifanya na matokeo mazuri. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, *EPZ* na *SEZ* – Shinyanga, ningependa kuelewa kama Wizara imekwishatenga maeneo ya *EPZ* au *SEZ* katika Mkoa wa Shinyanga. Kama tayari naomba kuelewa maeneo hayo. Nashukuru.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, nami niweze kuchangia hoja hii ya Wizara yetu ya Viwanda, Biashara na Masoko, iliyowasilishwa leo hii asubuhi na Mheshimiwa Waziri, ambayo mimi naiunga mkono na ninaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote, tuiunge mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kutoa shukrani kwanza kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa imani aliyoendelea kuwa nayo juu yangu, kwa kuniteua mwezi Oktoba, 2006 kuwa, Naibu Waziri katika Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Masoko, nikitokea Wizara ya Kilimo, ambako nilikuwa natumikia awali.

Pili, naomba nimshukuru sana Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, kwa uongozi na maelekezo yake ya mara kwa mara kwangu, ambayo yananisaidia sana katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku. Naomba nimshukuru pia Waziri wangu ninayemsaidia, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, kwa kunishirikisha vizuri sana katika shughuli za kusimamia Wizara, ambayo mimi ni msaidizi wake, kusema kweli nafaidika sana kwa kufanya kazi naye pamoja. Vilevile naomba niwashukuru wafanyakazi wote wa Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Masoko, pamoja na Mashirika yote yaliyoko chini ya Wizara hii kwanza, kwa kunipokea vizuri kwenye Wizara na vilevile kwa ushirikiano mzuri, ambao wanaendelea kunipa, wananisaidia sana ninawashukuru mno.

Mheshimwa Naibu Spika, naomba nimalizie shukrani zangu kwa kuwashukuru sana wananchi wenzangu wa Jimbo letu la Chilonwa, ninaowawakilisha hapa Bungeni kwa imani yao kubwa sana kwangu na ushirikiano ambao wanaendelea kunipa katika utekelezaji wa majukumu ya kuendeleza jimbo letu la Chilonwa. Naomba kuendelea kuwaahidi ushirikiano wangu mkubwa na kuendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote na kwa uwezo wangu wetu.

Mwisho, niungane na wenzangu waliotangulia kusema, kwa kutoa salamu za rambirambi kwa misiba mbalimbali iliyotupata na hasa ile iliyotugusa moja kwa moja hapa Bungeni, kwa kuondokewa na wenzetu Mheshimiwa Juma Akukweti na Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, naomba Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. *Amin.*

**NAIBU SPIKA:** Usisahau kumshukuru mke wako.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Namshukuru sana mke wangu, Violet na kusema kweli nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani mke wangu huko Dar es Salaam akisikia, ataona jinsi ambavyo ulivyo mwema sana kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba nichangie hoja mbalimbali kwa kujibu hoja zilizojitokeza hapa katika kuchangia hoja hii. Kwanza, nianze kushukuru kwa ujumla kwamba, wachangiaji wote waliochangia hoja hii michango yao tunaithamini sana na tutaendelea kuitumia, lakini kwa vile muda ulioko hapa ni mfupi wa kuzijibu zote, napenda kama kawaida niahidi kwamba, tutaendelea kuziandaa vizuri na kuziandika kwa kina ili kila Mbunge aweze akapata majibu yake kwa kadri alivyokuwa amechangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, sasa nijielekeze moja kwa moja kwa baadhi ya hoja ambazo zimechangiwa na Waheshimiwa Wabunge hapa ndani kwa kusema na kwa kuandika, ambao Mheshimiwa mtoa hoja baadaye atasimama kuwatambua wote rasmi kama ilivyo kawaida yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lilijitokeza suala hapa la kwamba, gharama za uzalishaji na uendeshaji viwanda zipo juu, ikilinganishwa na nchi nyingine. Hili nataka niseme kwamba, sisi tumelipokea na tunakubaliana kabisa, lazima tulifanyie kazi. Kwa hiyo, tunaungana mkono na hoja zilizotolewa, tutaendelea kulifanyia kazi kwa kuwa na madhumuni ya uzalishaji viwanda hapa ndani ni kuona viwanda vyetu vinazalisha bidhaa kwa unafuu zaidi ili wananchi waendelee kunufaika, kwa hiyo tunakubali kwamba tutaendelea kulifuatilia. Lingine lilikuwa ni uendelezaji wa viwanda mama vipewe kipaumbele. Hilo nalo ni la msingi. Suala la kuendeleza viwanda mama ambavyo baadaye vinaweza vikazalisha viwanda vingine, tunaliafiki na hivi sasa mchakato unaendelea, Serikali kupitia na kushirikiana na *NDC*, kazi inafanyika, kwa hiyo, tunalipokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni katika uwekezaji wa viwanda vya Mchuchuma na Liganga. Uwepo uwazi, utaalamu na uwezo wa kifedha vilevile Wananchi wa Ludewa washirikishwe. Hili kama ambavyo tumeshajibu mara kwa mara, hapa Bungeni na tumeshazungumza vilevile na Kamati yetu ya Uwekezaji na Biashara, tunakubaliana nao kabisa kwamba, katika mradi mkubwa kama huu, kwa manufaa ya wananchi lazima kuwe na uwazi unaotosha na hata katika maelekezo ya Serikali ambayo sasa hivi yanafanyiwa kazi, maelekezo ni hayo hayo kwamba, kuwe na uwazi wa kutosha. Kwa hiyo, Kamati za Kitaalamu zitakazoundwa, pamoja na zile nyingine ambazo zitakuwa zinashughulikia suala hili, kutakuwa na uwazi wa kutosha. Tungependa tuahidi hivyo na tunaomba tu Waheshimiwa Wabunge wote wale watakaokuwa wana taarifa za ziada za kutusaidia katika jambo hili, tuendelee kushirikiana nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji katika *EPZ* ni kutoka nje, pawe na mkakati wa kuwashirikisha wawekezaji wa ndani na pawe na *time frame* ya utekelezaji. Hili nalo tunakubali, lakini tuseme tu kwamba katika upatikanaji wa hao wawekezaji, tunaweza tukajikita kule tukasema kwamba, tushirikishe wengi kutoka hapa ndani. Lakini kama ninavyofahamu kwamba, tuko katika mchakato wa kujenga hii *process* ya *EPZ,* wale watakaokuwa wamejitokeza kwanza kama watakuwa wametoka nje tutawapokea. Lakini tunataka tutoe mwito hapa, kuhimiza basi na wananchi wengine ambao watakuwa wako tayari wajitokeze na sisi hatutasita kuwashirikisha. Kwa kweli ni jambo zuri sana kwa wananchi wazalendo kushirikishwa katika shughuli hizi kama ikiwezekana hata kama ni wote, wakishirikishwa itakuwa ni jambo zuri. Lakini kama mnavyofahamu, katika jambo hili linahitaji mambo mengi sana, unahitaji ujuzi, unahitaji vitendea kazi, vyote hivyo kwa pamoja vinaweza vikawa ni vitu ambavyo vinaangaliwa katika uanzishaji wa jambo hili.

Labda pia nishauri juu ya suala la ubia, ya kwamba, wakipatikana wawekezaji wa kutoka nje na wakapatikana watu wengine wazalendo humu ndani kuingia nao ubia,

nadhani itakuwa ni sehemu mojawapo ya wananchi kushiriki katika suala hilo la uwekezaji. Liko suala la mtambo wa Uvinza uliouzwa. Hili naomba nimwachie Mheshimiwa Waziri, atakuja kulitolea maelezo kwa ufasaha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, kutoka Mikoa ya Kusini, lilikuwa ni Wizara ihamasishe wawekezaji kwenda kuwekeza Mtwara. Kwa vile sasa hivi tayari kuna miundombinu, kuna umeme na kuna gesi, tunakubaliana nalo. Lakini hata kabla ya kupata maelezo haya, tulikwishaanza kufanya uhamasishaji huu. Mimi mwenyewe nilishakwenda Mtwara, nadhani kama mara mbili hivi, nimetembelea vile viwanda vya chumvi, nimeshatembelea kile Kiwanda cha Kubangua Korosho. Kwa hiyo, katika hili tunakubaliana na Waheshimiwa Wabunge wote kutoka Mtwara kwamba, tunashirikiana nao na kazi hiyo tumekwishaianza na wao wenyewe tunaomba tuendelee kushirikiana nao.

Wizara itembelee Kiwanda cha Korosho Mtwara ili kuona hali halisi, nimeshajibu kwamba, nimeshakwenda Mtwara. Tulishatembelea vile viwanda vilivyoko pale ambavyo vimeshachukuliwa na baadhi ya wananchi waliovinunua, lakini pamoja na vile ambavyo wananchi wazalendo wanafanya kazi kule. Nimewahi kwenda huko kwa hiyo, hili tulishaanza kulitekeleza. Jambo lingine ambalo limeelezwa hapa kwamba tuwawezeshe wafanyabiashara wazalendo ikiwa ni pamoja na kujenga utamaduni wa kununua bidhaa zinazozalishwa ndani na kuwawezesha wajasiriamali wadogo wadogo, kuwezesha ubia kati ya wawekezaji wa ndani na wa nje. Hili nimekwishakueleza, ndiyo kazi tunayoifanya na msisitizo wetu mkubwa ni kujivunia chetu na hata katika hotuba ambayo imewasilishwa na Waziri leo asubuhi, msisitizo mkubwa ulikuwa ni huo kwamba, tujivunie chetu. Tunapotengeneza vitu vyetu, tukivinunua nadhani litakuwa ni jambo la maana zaidi kuliko kutegemea vitu vya nje na nadhani hapa Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanazungumzia kusisitiza yale ambayo tulikuwa tumeyaeleza katika hotuba yetu ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyojitokeza hapa ilikuwa ni Serikali iongeze jitihada za uongezaji wa thamani katika usindikaji wa mazao ya kilimo, misitu na bahari, *agro-processing.* Hili tunaendelea nalo katika Wizara yetu Mashirika yale ambayo yako chini ya Wizara yetu; *TEMDO, TIRDO* na *SIDO*, yanasaidiana na Serikali katika suala la uhamasishaji kwa kutoa mafunzo ya kusaidia usindikaji wa mazao hayo. Kwa hiyo, tunapenda tuahidi kwamba, tuendelee kushirikiana katika kutekeleza hili ni jambo zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala juu ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya *EPZ,* ambalo limeelezwa na baadhi ya Wabunge wa Mikoa, hasa Mikoa ya Ziwa. Hapa tumeeleza kwenye hotuba yetu kwamba, katika kuhamasisha uanzishaji wa *EPZ,* tumeanza kwa kuanzia katika ile mikoa ya pembezoni, tumeitaja mikoa ile kwenye hotuba asubuhi ikiwemo Mikoa ya Mara, Kigoma, Arusha, Kilimanjaro, Rukwa na Mbeya, hii yote tumeshawasiliana nao kupitia kwa Wakuu wa Mikoa na baadhi wamekwisha kutoa majibu na mahali pengine tumekwishakuona maeneo ambayo yameshatengwa. Juzi juzi hapa tuliwasiliana na wenzetu wa Mkoa wa Mara,

wametutengea eneo kubwa sana pale Wilaya ya Bunda, kwa hiyo, tumeanza katika utaratibu huo. Lakini katika maeneo mengine, katika mchakato wetu tutakwenda hatua kwa hatua, lakini kwa kuanzia tumeanza katika mikoa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo imetolewa hapa inazungumzia habari ya upo wapi mkakati wa muda mrefu na wa kati ili kufufua viwanda vya viberiti, majembe, viatu, baiskeli, nguo na nyama, hili Mheshimiwa Waziri, nadhani atalifafanua vizuri atakapokuja kuhitimisha hoja yake hapa. Iko hoja ambayo imejitokeza hapa pia ya Tanzania ni nchi ya tatu kwa wingi wa mifugo, ambayo wote tunakubali. Hadi sasa tunavyo viwanda vya nyama vitatu na kuna mpango gani wa kuwa na viwanda vya nyama walau katika kila Mkoa wenye mifugo mingi. Hili labda niseme tu kwamba, wenzetu wa Wizara ya Mifugo, juzi walipokuwa wanawasilisha hoja yao hapa, nadhani waliliongelea kwa uzuri sana na uko mkakati mzuri tu ambao unaandaliwa na sisi kama Wizara tunayosimamia Wizara ya Viwanda, tutashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Mifugo kwa vile Serikali ni moja, kuhakikisha kwamba, mapendekezo haya yanayotolewa na Wabunge na kadri tutakavyokuwa tunafanya utafiti ili jambo hili nalo liweze likatiliwa maanani, kama mnavyofahamu kwamba, mifugo ni rasilimali kubwa sana ya Taifa letu, kwa hiyo, tunaafikiana nalo.

Liko suala la Kiwanda cha *General Tyre,* ambacho hata mzungumzaji aliyezungumza muda si mrefu, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga amelizungumza hapa, hili naomba nimwachie Mheshimiwa Waziri aje alitolee maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine sasa yaliyojitokeza kwa njia mbalimbali labda nigusie moja ambalo Mheshimiwa Mgana I. Msindai, amekuwa akiligusia mara kwa mara kwa kuuliza maswali na hapa leo ametuandikia, juu ya Soko la Iguguno. Nitoe tu maelezo hapa kwamba, maombi ya kuwa na soko kubwa pale Iguguno ni ya siku nyingi kidogo na sisi kama Serikali tulishatoa ushauri ya kwamba ili kuanzisha soko pale Iguguno ambapo ni katikati ni vizuri basi wazo hilo kwanza, likaingizwa katika mipango ya Halmashauri ya Wilaya ili mipango hiyo itakapokuwa imekamilika, basi na sisi kama Serikali tunaweza tukatoa ushauri wetu.

Ninachoweza kusema leo ni kwamba, bado tunaendelea kutambua tatizo la hitaji la soko pale Iguguno, mimi mwenyewe nilishafika hapo tukazungumza na wananchi na kwa kweli nilichoeleza ni hiki hiki tu kwamba, Halmashauri yetu ya Wilaya ya Iramba iingize wazo hili katika mipango yake na baada ya hapo tushirikiane nao ili kuona kama uwezekano huo upo na mpango huo unaweza ukatekelezwa. Lakini kwa kuanzia, tungemwomba Mheshimiwa Mbunge ahakikishe kwamba, wazo hili linaanzia kule kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Iramba.

Mzungumzaji mwingine ambaye ameleta hoja yake kwa maandishi ni Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa kwa kuulizia juu ya viwanda vya usindikaji mafuta katika mikoa ya kati ambavyo vinaweza vikainua uchumi wa wananchi katika kanda hii. Hilo nalo tunakubaliana nalo kwamba, kupatikana kwa viwanda vya kusindika mbegu za mafuta, utakuwa ni ukombozi mkubwa sana katika

mikoa hii ya kati. Hapa tutakachoomba ni kumwomba Mheshimiwa George M. Lubeleje, tushirikiane naye kuhakikisha kwamba tunahimiza kupata wawekezaji.

Katika suala hili la wawekezaji si lazima awe mwekezaji kutoka nje, hata sisi wenyewe Wabunge, inawezekana kabisa tukajishirikisha kama sehemu ya uwekezaji. Viwanda kama hivi vya kusindika mafuta sasa hivi watu wengi wamekwishaanza kujitokeza kushiriki. Ninavyozungumza hapa Dodoma kuna kikundi kinachohimiza ulimaji wa mbegu za mafuta na kuhakikisha kwamba wanawapatia mbegu wakulima hao ili waweze kuwasaidia kupata hizo mbegu na baadae wanakiuzia kiwanda hicho mbegu za mafuta baada ya mavuno.

Lingine ambalo Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo kalizungumzia ni suala la kuwasaidia wakulima wa korosho, kupata masoko na kuwawezesha wawekezaji kupata mikopo na masoko. Kama ambavyo tumekwishajibu mara nyingi hapa, suala la kushughulikia soko la korosho sasa hivi ni ajenda ambayo tumeipa kipaumbele sana katika mipango ya Serikali. Kwa hiyo, kwa sasa hivi kama ambavyo tumeshakujibu kwamba, Serikali inatekeleza suala zima la uimarishaji wa vyama vya ushirika. Lakini vilevile upo ule mpango wa stakabadhi za mazao ghalani, ambao ni sehemu ya ufumbuzi wa tatizo hilo na vilevile kuhakikisha kwamba tuhimize uuzaji wa korosho zilizobanguliwa.

Hivi karibuni tumekuwa na mazungumzo na baadhi ya wanunuzi wa viwanda vilivyonunuliwa kule Mtwara na Mikoa hii ya Kusini, kuona uwezekano wa namna ya kuwasaidia ili kuhakikisha kwamba, viwanda vile vinafanya kazi ili korosho iweze kuuzwa ikiwa imebanguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, michango ni mingi na kuijibu kwa kipindi hiki kifupi haitawezekana, lakini nimalizie kwa kugusia suala la Mheshimiwa Mbunge, kauliza kuwa ni hatua gani zinachukuliwa kwa wale ambao wananunua mazao bila kutumia vipimo vinavyokubalika. Hili nalo tumeshalitolea maelezo mara nyingi kwamba, iko Sheria Namba 20 ya mwaka 1982, ambayo inapiga marufuku kusema vipimo vyote ambavyo siyo halali, vikiwemo hiyo lumbesa ambayo imetajwa hapa, ndonya, kangomba makopo, vyote hivyo vimeleezwa kwamba ni vipimo ambavyo si halali.

Kwa hiyo, kwa kupitia sheria hiyo, mtu yeyote atakayekuwa anatumia vipimo visivyo halali, anavunja sheria na naomba ushirikiano ambao utatufanya tusaidiane kwa wale wote watakaokuwa wanafanya hivyo, waweze kuchukuliwa hatua za kisheria. Lakini hatua nyingine ambayo imekwishachukuliwa na Serikali ni pamoja na shirika letu la vipimo limeshaanzisha elimu kwa umma, kuwataarifu wananchi juu ya madhara ya kutumia vipimo visivyo halali. Kwa hiyo, kimeanzishwa kipindi cha TV kila Alhamisi, kuanzia mwezi uliopita na mipango ipo mbioni kuanzisha kipindi kinachofanana na hiki katika vipindi vya redio ili kuwaelimisha wananchi, juu ya madhara ya kutumia vipimo visivyo rasmi kuhakikisha kwamba, wale wote ambao wanatumia vipimo visivyo rasmi, wanachukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, nimalizie mchango uliokuwa unajielekeza katika kuomba Taasisi zote za Utafiti chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, zipewe fedha za kutosha na kwa hiyo visiweze kufanya kazi zake kwa ukamilifu. Hapa niseme tu kwamba, tunagawana kidogo kilicho katika Hazina yetu na kama ninavyofahamu kwamba, tunavyo vipaumbele ambavyo tumejiwekea, tumekubaliana navyo, tunakwenda navyo hivyo, lakini kile kidogo kilichopatikana kwa sasa hivi tunahakika mashirika yetu yatakuwa makini sana, kutumia hicho kuhakikisha kwamba wanatekeleza wajibu wao na kadri uchumi utavyokuwa unaendelea kukomaa basi na mashirika yetu haya ambayo yanaombewa yapate fedha nyingi zaidi, yatakuwa yanafikiriwa kwa kadri uwezo utakavyokuwa unaimarika.

Mheshimiwa Spika naomba tu nimalizie kwamba, michango hii yote kama nilivyosema mwanzo, tunaithamini sana, tutaitumia na tutawaandikia Waheshimiwa Wabunge wote waliotuandikia michango yao tutawasambazia. Kwa hiyo, naomba kumalizia kwa kusema naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana kwa kunipa tena nafasi hii. Awali ya yote na mimi nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kunirudisha tena kwenye Wizara ambayo nilianzia kazi mwaka 1980. Wakati ule ilikuwa ni Wizara ya Viwanda, baadae ikawa Viwanda na Biashara, nikaendelea kuwepo baadae Awamu ya Pili nikarudishwa tena hapo na leo ni Awamu ya Nne na nafikiri ni ya mwisho, kwa sababu umri unakwenda, nashukuru sana.

Lakini niseme hizi Wizara hazifanani, Wizara ya mwaka 1980 ilikuwa zaidi inazungumzia bidhaa adimu na ugawaji wa bidhaa na usimamizi bora wa bidhaa. Wizara ya leo inazungumzia mambo mengine kabisa na biashara hasa leo ni biashara za kimataifa na kuna mambo mengi kama mlivyozungumza hapa ya *EPA, WTO, Doha round.* Ni mambo tofauti kabisa. Kwa hiyo, sio kurudi kufanya kazi kwa mazoea, kwa kweli ni mambo mapya sana. Niwashukuru pia wapiga kura wangu wa Rombo toka mwaka wa 1985 wamenibeba mpaka leo, ukiondoa kipindi kifupi cha likizo kati ya 1995 mpaka 2000, ambapo nilienda kusaidia watu wa Mbeya na kuwapa maarifa na sasa nimerejea tena huko na tunaendelea kukaa nao, nawashukuru sana. Vilevile niishukuru familia yangu, ambayo imenibeba toka mwaka wa 1980 na mimi kazi zangu zimekuwa ni za kuzunguka na mara nyingine huwa nafikiri sijui niko Hotelini au nipo nyumbani, maana tunazunguka sana na mara nyingi familia huwa haipendi mambo namna hii. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshangaa nimeona watu wengi wameichangamkia hotuba ya leo. Walioandika hasa ndiyo walikuwa wengi na niwataje kwa haraka haraka na watanisamehe kwa sababu ya muda, sitaweza kutaja Majimbo, nao ni Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Azan M. Zungu, Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu, Mheshimiwa Salome J. Mbatia Felix C. Mrema, Aloyce

B. Kimaro, Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Sevelina S. Mwijage, Mheshimiwa Castor R. Ligalama, Mheshimiwa Ania S. Chauremo na Mheshimiwa Herbert J. Mntangi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Capt. George H. Mkuchika, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Mohammed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Anne S. Makinda, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, Mheshimiwa Mathias M. Chikawe, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Khadija Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Adam K. A. Malima, Mheshimiwa Vedastus M. Manyinyi na Mheshimiwa Hezekiah N. Chibulunje.

Hawa wote nawashukuru sana, wengi wametoa mawazo mazuri, baadhi nitayajibu hapa kwa ujumla na mengine tutawajibu kwa maandishi mmoja mmoja na wengine tutazungumza nao ana kwa ana, mimi mwenyewe ama Naibu Waziri ili kuhakikisha kwamba, tutakuwa pamoja katika fikra na katika kuelimishana na kueleweshana juu ya masuala yanayohusu Wizara hii.

Wapo wale waliopata bahati ya kuchangia kwa mazungumzo ambao ni Mheshimiwa Anna M. Komu, ambaye alizungumza kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mohamed S. Sinani, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Ahmed A. Salum, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga na Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, aliyezungumza kwa niaba ya Kambi ya Upinzani ni Mheshimiwa Lucy F. Owenya.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Lucy F. Owenya, alizungumza kwa niaba ya Kambi ya Upinzani. Nashukuru kwa kuniweka sawa. Hawa wote nawashukuru na mengi ya mambo waliyosema nakubaliana nayo. Kati ya hayo yaliyoandikwa na hayo yaliyosemwa kwa muhtasari nitajaribu kuyajibu. Labda niseme nakubaliana mia kwa mia na mawazo ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara na vilevile nakubaliana na ushauri ule mzuri uliotolewa na Kambi ya Upinzani. Yale ambayo nadhani yalitokana na kutoelewa vizuri nitayafafanua. Chukua kwa mfano, hizi hoja juu ya viwanda vilivyo binafsishwa kwamba, havijaanzishwa havifanyi kazi. Kwenye hili naona viwanda vya Moshi labda ni kwa sababu na mimi nimetoka huko, walitaka kuniweka kwenye kitimoto. Naona wala si kitimoto sana, maana hata Mheshimiwa Salome J. Mbatia naye kalisemea jambo hili kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya Moshi vina matatizo makubwa matatu. Kwanza, kubwa kabisa viwanda hivyo havikuanzishwa kwa sababu ya ukosefu wa malighafi. Viwanda vyote vilivyotegemea mbao za *soft hood* kutoka misitu iliyopandwa, vimesimama kwa sababu havina malighafi. Viwanda vyote ni kimoja tu kinachotegemea ngozi kimesisimama kwa sababu watu wanaokusanya ngozi, wanapendelea zaidi kuuza nje kuliko kuuza kiwandani, kwa sababu kule nje wanapata bei zaidi. Jibu ambalo tunalo sasa Serikali kwa viwanda vyote vya namna hiyo nchini wala si Moshi ni kwamba, tumeanzisha ule Mfuko ambao ulitajwa na Waziri wa Fedha wa Kuendeleza Sekta ya Ngozi na utakuja hapa kabla ya mwisho wa Bunge hili. Mfuko ule utakuja hapa kisheria ili uanze kufanya kazi.

Tayari Mfuko ule una takriban shilingi bilioni 4.5. Mfuko ule utasaidia sana kwa sababu unatokana na ushuru ambao tumeuweka kwenye watu wanaouza ngozi ghafi nje ili ushuru ule utumike kuendeleza sekta yenyewe. Ulikuwa asilimia 20, lakini kabla Bunge hili halijaisha, Waziri wa Fedha atapandisha na ninyi mkiafiki twende mpaka asilimia 40, ili izidi kuwa vigumu kwa mtu kuuza ngozi ghafi nje na badala yake wauzie viwanda na hii inalingana na hoja nyingi zilizotoka hapa za Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga na wengine waliosema, msiuze malighafi nje na ndivyo tunavyochukua hatua hiyo kwenye ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha *Moshi Pesticides* ni kiwanda kingine kilichosimama. Hiki kinategemea shaba. Bei ya shaba imepanda sana duniani. Kwa hiyo, malighafi ile imekuwa aghali mno na kwa hiyo, uzalishaji ni mdogo si kwamba hawazalishi. Wao wako mbioni sasa kufanya utafiti kuona wazalishe kitu kipi kingine kwenye kiwanda hicho badala ya kuendelea kung'ang'ania hiyo *copper,* ambayo kwao imekuwa ni ghali na haina tija. Kwa hiyo, matatizo ni mawili, moja malighafi kwa mbao na ngozi. La pili, bei kuwa ghali mno, ambayo vilevile maana yake ni ukosefu wa malighafi na la tatu kuhusiana na viwanda viwili vya magunia ni kwamba, kuna mgogoro unaohusiana na hati ya kiwanda kile.

Kiwanda kile kabla hakijabinafsishwa, hati yake ilikuwa imechukuliwa na Benki. Benki hiyo hiyo ambayo Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, alikuwa Meneja Mkuu wake, *East African Development Bank*. Benki ile ilishika hati ile, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga ni shahidi na mpaka leo wameshika hati ile, kwa sababu kuna utata kama deni lile lilikuwa limeshalipwa au hapana. Serikali inasema ilishalipa, *PSRC* wanasema lilishalipwa, rekodi kule kwenye Benki wanasema hatuna uhakika. Imechukua muda mrefu lakini nimehakikishiwa kwamba, hivi punde watalimaliza na kama hati ile ikikamilika, mwekezaji atafunga mitambo ataanzisha kiwanda. Hili naahidi nitalisimamia.

Kiwanda ambacho hakijabinafishwa ni *Kilimanjaro Machine Tools*. Hiki ndiyo sasa tunatafuta wawekezaji, kwa sababu kilikuwa kwenye *EPZ*, sasa kuna utata kama kiwe kwenye *EPZ* au hapana, lakini tumeshaanza kupeleka matangazo kwa wawekezaji, mimi natumaini kwamba tutapata mwekezaji. Kuna aina nyingine ya viwanda vingi, viwanda vya korosho ambavyo navyo vina tatizo vimebinafsishwa tena kwa wazalendo, lakini vyote havijaanza kazi. Kimoja kimeanza kwa kiasi vingine vinasuasua. Wiki mbili

zilizopita, nilikutana na wenye viwanda hivyo, nilizungumza nao, nimeelewa tatizo lao kubwa ni fedha za kukarabati viwanda na kununulia malighafi, ambayo ni korosho ghafi kutoka kwa wakulima.

Kuna mchakato ambao unaendelea sasa hivi kati ya Wizara yangu, Wizara ya Kilimo na wenye viwanda na hatimaye tutafika Hazina na Benki Kuu ili tuone namna tunavyoweza kuwasaidia hawa wazawa, waliobinafsishiwa viwanda hivi ili kwanza viwanda viwe ndiyo soko la korosho na pili, viweze kuzalisha na kujiendesha kama inavyotakiwa. Hili nalo ninalo lakini si la siku nyingi sana, kwa sababu viwanda vyenyewe vilibinafsishwa muda mfupi uliopita. Niunganishe na hapo kuhusiana na *General Tyre*, ingawa haijabinafsshwa, lakini kuna tatizo kama lililosemwa hapa na niseme tu hapa kwamba, kwa muda wa miezi kadhaa sasa tumekuwa tukishughulikia *General Tyre*. Tatizo lake kubwa ni ukosefu wa fedha za kuendeshea kiwanda. Siku mbili zilizopita, Waziri wa Fedha mwenyewe alikuwa pale na tumaini letu ni kwamba, baada ya Waziri wa Fedha kushuhudia tutapata jawabu, Waziri Mkuu mwenyewe amehusika lakini tuna matumaini ya kupata jawabu na kwa hiyo, kiwanda chetu hiki hatutakiacha kife. Ninachoweza kusema, kitaendelea kuwa ni kiwanda bora cha Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo la *Tabora Textile (Tabotex)*, tayari imeshabinafshwa, kinafanya kazi kwa kusuasua, lakini wazo kwamba tukifanye kiwe *EPZ,* tutafikiria hasa kwa kuzingatia ushauri uliotoka kwa yule Profesa Jeffrey Sacks, ambaye alikitembelea hivi karibuni na kushauri kwamba si tu kwamba tutafute namna ya kukiendeleza kiwe kizuri lakini vilevile tuangalie uwezekano wa wakulima wa eneo lile, kulima pamba ili malighafi itoke Tabora, badala ya kutoka Mikoa mingine kama ilivyo hivi sasa. Hilo nalo tunalo na kuna mapendekezo mahususi yaliyofanywa na wataalam waliofanya uchunguzi kuhusiana na viwanda vya nguo na nadhani hilo nalo hatutaliachia tunalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, ombi lililotoka kwenye Kambi ya Upinzani juu ya kiwanda cha chumvi kwamba, kiwanda hiki kimesimama, si kweli. Kiwanda cha chumvi kilibinafsishwa mwaka wa 1998 cha Uvinza kilibinafsishwa mwaka 1998 kikiwa kinazalisha tani 8,000 kwa mwaka. Hivi leo kinaendeshwa vizuri sana na kinazalisha tani 35,000 kwa mwaka na toka kibinafsishwe, kimekwishalipa kodi Serikalini, kodi zote kwa ujumla shilingi bilioni 1.25. Kwa hiyo si kweli kwamba kiwanda kimesimama. Ni kweli kilikuwa kinaendeshwa wakati kikiwa cha Serikali kwa kutumia mitambo ya umeme na wakati mmoja kilikuwa kinaendeshwa kwa kutumia kuni.

Lakini sasa wenye kiwanda wamedhamilia kuachana na umeme, kuachana na kuni, sasa watatumia *solar* na mitambo iliyoko sasa ni ya *solar* na wataendelea kuzalisha kwa utaratibu wa *solar.* Hata hivyo, kwa wote hawa walioonesha maduku duku ya viwanda vilivyobinafsishwa, mwisho niseme tu kwamba, kikao cha *Fast Track* ambacho kinashughulikia matatizo haya ya viwanda vilivyobinafsishwa chini ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kilikutana hivi karibuni na kutoa agizo ambalo sasa linafanyiwa kazi na Wizara yangu na Wizara nyingine zote zinazohusika kwamba, tufanye uchambuzi kila Wizara iliyokuwa na viwanda mfano, Wizara ya Maliasili na

Utalii, Wizara ya Viwanda na Wizara ya Kilimo, ichunguzesasa vile viwanda baada ya kubinafsishwa viko wapi na vinaendeleaje na kama kuna matatizo yaletwe kwenye kikao hiki cha Mheshimiwa Waziri Mkuu ili tuweze kuamua hatua za kuchukua. Hii ni kwa viwanda vingine vyote, kwa hiyo, kama kuna viwanda ambavyo vinajulikana ambavyo labda vilibinafsishwa na havijaanza kazi au vina matatizo, tafadhali tuvielewe, vitafanyiwa kazi kwa mujibu wa agizo la Kamati hiyo ya *Fast Track* chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo narudia, ushauri wa Kamati hizo mbili tutauchukua, siwezi kusema kila jambo lililoko kule kwa sababu ni mengi lakini niamini kwamba tutayafanyia kazi, mapendekezo yote hayo kadri ya uwezo wetu. Ni kweli kwamba, ungetegemea viwanda vikitumia gesi bidhaa zake zingekuwa za bei nafuu zaidi. Sisi tumekuwa tukifuatilia baadhi ya viwanda vinavyozalisha kwa kutumia gesi. Mfano, Kiwanda cha Saruji cha *Wazo Hill* kutumia gesi bado saruji haijateremka bei na bidhaa nyingine zinazozalishwa namna hiyo. Jambo la kufanya katika sura kama hii ni kufanya *cost analysis* ya kila kiwanda, kujua kwa nini pamoja na kutumia gesi; bei hazibadiliki? Hii kazi nimekwishaelekeza tushughulikie na tunaanza na viwanda vya saruji, vile vyote vinavyotumia gesi na baadae tutahamia kiwanda kwa kiwanda kwa lengo la kutafuta jibu la kisayansi. Hilo tunalo na nashukuru kwamba hata ninyi mmeliona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuanzisha na kuendesha viwanda, ukisikiliza sana kwa makini utasikia wanaozungumza juu ya viwanda vidogo na viwanda vikubwa, Serikali ifanye hiki au kile. Ndugu zangu, Serikali hii ilishatoka kwenye kuanzisha viwanda viwe vikubwa au vidogo. Serikali imekuwa ikiweka mazingira mazuri ili wananchi wajianzishie viwanda viwe vikubwa ama vidogo. Lakini kweli pamoja na Serikali kuweka mazingira, unaweza kufagia nyumba ikawa nzuri, ukaweka hata marashi ikanukia lakini watu wasiingie humo ndani. Kwa hiyo si kweli kwamba, ukishaweka mazingira basi wawekezaji watashindania kuingia kwenye mazingira hayo, si kweli. *(Makofi)*

Kwa hiyo, jambo hili tumeanza kulifikilia pale Wizarani na ndiyo maana kwenye hotuba yangu ile nimesema, mwaka huu wa fedha, tutaanza kushughulikia kitu kinachoitwa *Integrated Industrial Development Strategy,* nimeitaja kwenye ukurasa wa 23 wa hotuba ile ambayo pamoja na mambo mengine, itarejea tena ile sera iliyokuwepo ya viwanda wakati ule mimi nikiwa Waziri wa Viwanda, Awamu ya Kwanza iliyokuwa inaitwa *Basic Industry Strategy*. Katika hiyo mojawapo ya mambo ni kutouza malighafi zako nje, hii inayopigiwa kilele hapa tusiuze malighafi nje ni kweli kabisa usiuze pamba ghafi, ngozi ghafi au hata magogo. Waziri wa Maliasili alikuwa anapigiwa kelele hapa ni kweli usiuze magogo. Kwa hiyo la kwanza kabisa ni kuwa na mkakati wa kutouza malighafi zetu ovyo nje. Ni lazima tupate kitu kinachoitwa *value addition*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *Basic Industry Strategy* katika utaratibu wa *Integrated Industrial Strategy* itakuwa mojawapo na hata viwanda vidogo vitakuwa sehemu ya mkakati huo. Tunaomba tufanye kazi hiyo mwaka huu wa fedha, halafu ikibidi tutakuja hapa kuwaeleza mambo ambayo tutakuwa tumeamua kuyafanya. Mojawapo litakuwa nafasi ya Serikali katika kusukuma viwanda; je, ni sawa Serikali

kusema mazingira yamekuwa bora, basi viwanda vije visipokuja itakuwaje? Ni lazima vilevile tuweke kitu kama kichocheo, ambacho kitaifanya Serikali yenyewe ijihusishe, haiwezi kuweka mikono nyuma ikasema njooni labda lazima ijihusishe. Ndiyo maana hivi sasa tunaendeleza uchunguzi wa chuma cha Liganga na Makaa ya mawe ya Mchuchuma, ndiyo maana unasikia tunazungumza habari za magadi soda Ziwa Natroni.

Tunazungumzia mambo mengine ya namna ile ni kwa sababu Serikali lazima iwe *catalyst* na mara nyingine ni lazima iwekeze na uzoefu tulioupata hapa Dodoma, tulipokwenda kuanzisha kiwanda kile cha nyama wakati ule, aliyekuwa Waziri wa Mifugo, ambaye sasa ni Waziri Mkuu wetu, kama mwendawazimu tu aliamka hapa akatafuta hela akapeleka Dodoma akaanzisha kiwanda. Mimi nilikuwa Waziri wa Fedha, akaniambia wewe unajua ulishanipa hela nikaanzisha kiwanda, kiko wapi akanipeleka pale, nilishangaa maana hata sikukumbuka kwamba nilishampa hela. Matokeo leo tuna kiwanda cha nyama. Tungelikuwa tumempa hela nyingi wakati ule akaanzisha viwanda kumi, leo vingekuwa kumi. Lakini baada ya Serikali kuanzisha hicho kiwanda, imewezekana kukitangaza na matokeo wamekuja wawekezaji kuungana na Serikali ili kuendesha hicho kiwanda. Kwa hiyo, fedha zile tulizouza hicho kiwanda, asilimia 51 ya hisa tutazitumia kuanzisha kiwanda kingine mahali pengine ili baade watu binafsi waungane nasi. Vivyo hivyo kwa mzunguko, ndiyo maana umeona Waziri wa Mifugo, ametangaza tenda ya kuanzisha viwanda kumi vya nyama na kuchinja mifugo, maana na hili suala limejitokeza hapa kwa maandishi

Kwa hiyo ni kweli Serikali ikiwa *catalyst*, watu binafsi wataunga mkono na kwenye hili la nyama, watu binafsi wanaotuunga mkono ni kina nani? Ni *NICO,* lile Shirika la Wazalendo, wamejiingiza huko kwa kuona kwamba, kumbe na baba yao Serikali ipo huko ndani. Bila baba yetu kuwa huko ndani, wangeweza kuwa na wasiwasi wasiingie. Kwa hiyo, ni kweli lazima Serikali ichukue *catalystic action,* hatua ya kuchochea ili waje wawekezaji na humo humo ndani katika kuangalia mchakato huu, wazo kwamba, Watanzania tuwafanye nini ili washiriki zaidi basi? Lazima litajitokeza. Je, *credit guarantee scheme* itatosha; je Mfuko Maalum wa Kuwakopesha na Benki Maalum kama *TIB* iliyokuwa inazungumzwa hapa au Benki nyingine za Biashara?

Mambo kama hayo ndiyo yatakuwa muruwa na muafaka wakati huo. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema ni kweli tutafanya hivyo, lakini lazima vilevile kutokee kitu cha kuwawezesha Watanzania kushiriki vizuri zaidi kwenye mkakati huo wa kusukuma viwanda na kuelekeza. Kama ni kuelekeza kijiografia, kama ni kuelekeza kimali ghafi na kadhalika na kadhalika. Kwa hiyo, wazo kwamba, *TIB* iwe benki ya namna hiyo, litazingatiwa na yale mawazo mengine ya namna ya kupata fedha yatazingatiwa. Sisi tunajua kuwa wenzetu wana mambo ya namna hiyo. Wenzetu nchi kama India ina hata Benki ya Umma ya Viwanda Vidogo, siyo vihela vidogo vidogo za vifuko vidogo vidogo, Benki hasa ya viwanda vidogo. Kwa hiyo, mambo kama hayo yatajitokeza katika huo mkakati tunaozungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nifafanue kidogo hili la *sponge iron*. Kuna watu wenye madukuduku ya kusema, lakini haya mambo mnataka kuanza kwa utaratibu wa viwanda vidogo. Mimi nikisema viwanda vidogo wanafikiri vile vya *SIDO*, hapana ni viwanda

vya vya mabilioni. Lakini kwa lugha ya chuma ni kiwanda kidogo. Sisi tumeona kwa sababu mchakato wa Makaa ya Mawe Mchuchuma unajulikana na umekamilika na mchakato wa chuma chenyewe haujakamilika ingawa tunajua, tunatafuta *vanadium* na madini mengi yaliyoko kule ndani. Lakini haujakamilika kwa maana ya kujua wingi na ubora, hatujajua. Kwa hiyo, ndiyo maana nikaomba fedha tuendelee kuchunguza hiki chuma cha Liganga, lakini badala ya kusubiri mpaka chuma kiwe tayari, ndiyo ukaunganishe na makaa ya mawe ya Mchuchuma uanzishe *steel plant,* kwa lugha inayojulikana duniani, hakuna sababu.

Unaweza ukaanzisha utaratibu mwingine ukapata chuma wakati unasubiri kile kikubwa kinachokuja na jambo hili si la Tanzania na wala si Mramba; liko China na pia liko India. India kuna zaidi ya viwanda 300 vya namna hiyo, China ndiyo kabisa, hata takwimu sina na wataalam wako nchi hizo. Nalisema hili kwa sababu nimeona mahali watu wakilalamika kwamba, sasa mmeanza tena kwenda kuleta watu Asia; utaalamu ukiwa Asia tutafanyaje? Utaalamu huo hauko kwa Wazungu, maana wanaudharau. Ukizungumza na watu kama Wajerumani wanaudharau, lakini utaalam huo uko China na ndiyo unaowafanya Wahindi leo wanakuwa *leaders in steel* duniani. Wahidhi ndiyo wanaoongoza leo kwa biashara ya chuma cha pua dunaini. Wameanza, wana chuma cha pua kwa maana ile kubwa ya *steel*, wana chuma cha pua kwa maana ya *steel rolling mills* na kwa maana nyingine nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunasema tukipata *sponge iron*, itakuwa malighafi kwenye *steel roling mills* zetu ambazo zitazalisha chuma kwa mfano, nondo na aina nyingine za chuma na kwa hiyo utaokoa fedha tunazotumia sasa kuagiza malighafi kwenye viwanda vyetu vya chuma. Utaokoa fedha za kigeni na mojawapo ya mambo tunayotaka kufanywa ni kuokoa fedha za kigeni. Kwa hiyo, mimi nafikiri mngenipigia makofi kwa kuwa mbunifu. Nimekuwambunifu, la sivyo, tungesubiri hapa miaka mingine kumi tukisubiri chuma cha Liganga kikamilike, ndio tuanze kutafuta wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa watu wanasema mnaanza kuleta Wahindi au mnaenda kuleta sijui watu gani. Hatujafika mahali pa kusema nani tutampa mchimbaji wa hayo makaa na chuma kwa ajili ya viwanda hivyo vidogo vya chuma. Tunatafuta wataalamu watushauri kwa mujibu wa watalaamu walioko India na China, hapo ndio tutaamua, sasa hivi hatujafika pale. Tuna kamati ambayo imeshaundwa, tuna mtaalamu ambaye tumekwisha ahidiwa kutoka India, atakapokuja ndio atatuelekeza itakuwaje. Lakini tunafanya hili jambo kisheria. Jambo hili litafanywa kisheria, kama ni kutafuta leseni ya kuchimba makaa ya mawe, kuna Sheria ya Madini, leseni ya kuchimba chuma chenyewe, kuna Sheria ya Madini, siyo Wizara yangu itakuja kutoa, kuna sheria na wanaotoa vibali hivyo wanajulikana. Baada ya hapo, mengine ndiyo tutashirikiana kama Serikali, Wizara mbalimbali ili kukamilisha mchakato wa kuanzisha viwanda au kiwanda cha *sponge iron* ili iwe malighafi kwenye *steel roling mills* ili kitoe chuma tuokoe fedha za kigeni tunazotumia sasa kuagiza malighafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wasi wasi kwamba, haya mazungumzo ya *Economic Partnership Agreements* yanatupeleka pabaya. Wapo watu, tumeona hata

magazeti yakisema hivyo. Jana nililieleza hili jambo kwa undani kwenye Kamati yangu na nafurahi kwamba, Kamati ya Uwekezaji na Biashara imelielewa. Nilieleze kwenu Waheshimiwa kwamba, kinachoendelea ni biashara kati ya nchi zetu hizi changa *(African Caribbean Pacific Countries - ACP Countries)* na Jumuiya ya Ulaya *(EU)*. Kama mnavyojua huko nyuma, tumekuwa tunafanya biashara nao kwa utaratibu wa *Lome Convention, Cotonou Agreement*. Sasa, safari hii wanasema hapana, tuingie kwenye utaratibu wa biashara unaoitwa *Economic Partnership Agreement*, yaani siyo kuuziana tu bidhaa, pamoja na kusaidiana misaada ya shughuli za maendeleo, lakini za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii dunia yote ya nchi ndogo hizo, nchi changa imegawanywa na sisi hapa Waafrika tumegawanywa kwenye makundi; kuna kundi linalojumuisha nchi zilizo wanachama wa *SADC*, lakini siyo zote, linaitwa *SADC – EPA*. Kuna kundi linalojumuisha nchi ambazo ni wanachama wa *COMESA*, linaitwa *ESA*, lakini siyo nchi zote wanachama wa *COMESA* wako huko ndani. Sisi Tanzania tuko kwenye kundi la *SADC*, siyo kwa sababu hasa tulitaka kwenda kwenye kundi la *SADC* ni kwa sababu ukweli tofauti na ilivyokuwa inazungumzwa hapa, hakuna kundi la nchi za Afrika Mashariki.

Wakati mambo hayo yakijadiliwa na kabla hatujaingia kwenye maelewano na Jumuiya ya Ulaya, nchi za Afrika Mashariki, zilikuwa zimeamua kwamba, tuwe na kundi letu na twende tukazungumze na Wazungu kama Afrika Mashariki. Lakini kwa bahati mbaya, baada ya kuamua hivyo, tukaja kubadilisha uamuzi, siyo rasmi, lakini wenzetu katika Afrika Mashariki wakaenda kwenye kundi la *COMESA,* nchi mbili. Sisi Tanzania tukaenda kwenye kundi la *SADC* kwa sababu tulibaki wenyewe na tukaona sisi kwetu ni *SADC*, anuani yetu sisi ni *SADC* siyo *COMESA*, kwa hiyo tukaenda *SADC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kumekuwepo michakato inayoendelea ya mazungumzo, sina muda hapa wa kuieleza kwa undani. Lakini ni kweli kwamba, jinsi mazungumzo yanavyoendelea ni lazima ikifika mwisho wa mwezi Desemba yaishe, sawa na yale mazungumzo mengine ya *Doha Round*, ikifika mwisho wa Desemba lazima yaishe. Sasa sisi hapa karibuni Afrika Mashariki, tumerudi tukasema hivi kweli wawili wakienda kule, sasa wamekuwa siyo wawili, watakuwa wanne; ukiweka Burundi na Rwanda. Wanne wakienda kule na sisi peke yetu tukaenda kule, huku nyumbani tutamwacha nani? Ni sawa na mtu mwenye tafrija, badala ya kuifanyia nyumbani kwake, anaenda kuifanyia kwa jirani na kwake tayari ana nyumba nzuri na imepambwa kila kitu safi. Sasa tukaanza kujiuliza hivi huku nyumbani tunamwacha nani na kutakuwaje huku nyumbani, yaani kitu kinachoitwa *deepening of integration in East Africa* itakuwaje? Sisi tulikuwa tunazungumza kwenda kwenye *Costums*, kwenye *East African Common Market* na *Federation*, ndio ajenda yetu. Sasa *Federation* itakuwaje kama sisi tunafanya biashara pengine? Hii *Federation* hasa nia yake ilikuwa tufanye biashara kwa pamoja na tayari tuna *Protocol* ya Biashara kwa pamoja, sasa iweje!

Ndio jambo lililozungumzwa na Wakuu wa nchi mwezi uliopita kule Kampala. Ndio sisi Mawaziri wa Biashara tumetakiwa turudi Arusha tulijadili sasa iweje. Kuna Mkutano ambao utafanyika wakati wowote kuanzia Jumatatu, ambao tunakwenda kujibu

hilo swali walilotupa Wakuu wa Nchi; sasa iweje. Baada ya hapo tutarudi kwa Wakuu wa nchi tuwaambie iwe hivi, wakiafiki tutakwenda kama watakavyokuwa wameafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna hoja ya kusema sasa iweje Afrika ya Mashariki, wote watano, maana yake kama siyo wote watano, basi angalau *majority* la sivyo, huku nyumbani kutaingia panya. Panya wataingia hapa ingawa sisi tulikuwa wastaarabu, tulikuwa tayari *the most advanced*, maana sisi tulikuwa na *almost the common market*, tulikuwa na msingi wote.

Hawa waliokwenda *COMESA*, hakuna msingi wa *common market*, hawa waliokwenda *SADC*, hakuna msingi wa *common market*. Sisi *East Africa* tulikuwa na *common market*. Tuliacha vipi kulala kwenye kitanda cha vono, tukaenda lalia mkeka hapo chini; tuliachaachaje haya mambo sasa tuondoke kwenye mkeka, turudi kwenye kitanda? Itakuwaje sasa na kule tumeshaanza kusema mkeka mzuri na wengine huku wanasema vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka mniamini kwamba, jambo hili nalifahamu, nalishughulikia sana na nalishughulikia kwa msingi wa *National interest*, maslahi ya Tanzania yako wapi. Baraza la Mawaziri, litaarifiwa mwelekeo. Kwa hiyo, tunafanya kazi pamoja na tunapokea maoni ya watu wengi, mtu yeyote mwenye mawazo alete, siyo *closed shop*. Lakini, kwa kweli jambo hili, fikirieni tu hata Rais mwenyewe alikwenda Brussels, alizungumza na wale wakubwa kule, Rais wa Jumuiya ya UIaya na yule Kamishna wa Biashara kujaribu kulielewa na Rais wetu analielewa sana sana na mimi nalielewa karibu kama yeye, kwa hiyo, ndivyo hivyo tunavyolipeleka. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la masoko, ninamheshimu sana Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa, wasi wasi wake ulikuwa wa kweli kwamba, taarifa hizi za masoko ziweje. Mimi ningependa niseme, eneo hili la masoko ndio hivi limeingia kwenye Wizara hii, lilikuwa kwenye Wizara nyingine, lakini tunalifanyia kazi vizuri. Moja ambalo tumelidaka mara moja ni lile la maghala, nimelieleza kwenye hotuba. Lakini hili la taarifa za masoko pia ni muhimu sana na nakubaliana naye kwamba, taarifa hizi lazima zilenge wananchi, siyo zangu Mramba, mimi siyo mkulima na si za Katibu Mkuu ni za wananchi. Kama swali lililoulizwa hapa na Mbunge wa Ngara wiki hii; maharage yatauzwa wapi? Mimi nilitakiwa niwe nimeshapeleka habari Ngara, kwa sababu najua wanalima maharage, kuwaambia soko la maharage liko Mwanza, liko Kampala, liko Nairobi na usitafute nje kwa sababu huliwezi. Ungekuta nimeshawaambia hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki hii nimeona matatizo ya ndizi kuanzia Mto wa Mbu, Arusha mpaka Rombo Tarakea, kuna tatizo la biashara ya ndizi. Watu wananiuliza wewe Mramba namna gani, wanashindwa kuuza hata ndizi! Nakwambieni kazi hii tunayo ya kuuza ndizi, vitunguu na hata dengu, ilizungumzwa hapa leo kuhusu dengu. Yote yale tunatafuta masoko na tutaweka utaratibu ili wakulima wajue saa zote kwa simu za mkononi, kwa njia zozote zile za mawasiliano ya kileo kwamba iweje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la *dumping* bidhaa feki wala siyo la Tanzania tu, sisi tunapiga piga kelele kwa sababu ndio kazi yetu. Lakini wiki hii wale mliokuwa

mnaangalia, mnajua China ni tatizo kubwa vilevile. China na Dunia, Wachina wanatengeneza magari yanafanana na Benz wanauza, kumbe siyo Benz. Wachina wanatengeneza vitu vikubwa zaidi, lakini sisi ni bidhaa ndogo ndogo hata chupi zinakuwa feki, hata nini. Lakini kuna wenzetu wanatengeneza vitu vikubwa, kwa hiyo ni kweli na ninafanya nini sasa? Kwanza, nimesema kwenye hotuba, tunaweka utaratibu wa kuanza kudhibiti bidhaa kule kabla haijaingia hapa, maana zinaingia kwenye njia za panya na njia nyingine za ovyo ovyo, kule. Utaratibu huo unaanza kupitia *TBS* na kadhalika. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwenye Bunge hili tutawaomba kwenye *Miscellaneous Amendment* itakapokuja, mtaona kuna *Amendment* tunayofanya kwenye sheria inayohusiana na mambo haya ya ukiritimba wa biashara na kadhalika, ambayo itatuwezesha sisi kukamata bidhaa, kuzikagua na kuchukua hatua kali. Kama mkipitisha hiyo wakati wa *Miscellaneous Amendment*, nina hakika nitakuwa nimeshapata silaha na mahali pazuri pa kuanzia kwa sababu sasa hivi hata sheria yenyewe siyo nzuri sana. Ninapiga kelele lakini sheria yenyewe siyo nzuri sana. Kwa hiyo, tutaanza kushughulikia *dumping* na mambo mengine ambayo ni feki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili nisipigiwe kengele maana mimi ni mzoefu, itakuwa ni aibu, niseme tu kwa kifupi, Wizara hii naifahamu ni mara ya tatu naingia huko. Viwanda navifahamu, viwanda vidogo ndio kabisa nimezaliwa huko na nawashukuru sana wanaviwanda vidogo ndio wamenifanya mpaka nikafika hapa nilipo. Nimezaliwa huko, biashara naifahamu, hata mimi mwenyewe kwa hulka tu ni mfanyabishara, kwa hiyo, naomba mnipe muda haya yote yaliyotoka hapa leo. Hakuna hata moja nililosema hivi ni kitu gani hiki? Hapana. Lakini ni mengi, lazima uanzie mahali.

Baba yangu alinifundisha, kule kwetu tunachoma ndizi; ukichoma ndizi uwe mwangalifu, ukichoma zote kwa mpigo, zote zitaungua. Lazima uanze ya kwanza, halafu ya pili, halafu ya tatu ili ziwe nzuri. Kwa hiyo, ndiyo naanza *one at a time*, lakini tutafika. Nataka kuwahakikishieni nafahamu, lakini tutafika. Naomba mnipe bajeti hii, wala siyo bajeti kubwa sana hii, lakini kitu ni kitu, usidharau. Nipeni nianze, halafu nije na mipango mbele ya safari niwaambieni sasa nimekuwa mkubwa zaidi, nipeni bajeti zaidi. Nataka kuwahakikishieni tutafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba tena kutoa hoja kwamba, Waheshimiwa Wabunge wapitishe ili niweze kufanya kazi kubwa iliyo mbele yetu. Nakushuru na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Asante. Katika mchango wake, nadhani tuweke *record* za *Hansard* sawa sawa. Mheshimiwa Abdallah S. Sumry alisoma hotuba kwa niaba ya Kamati. Halafu kuna mchangiaji mwingine anaitwa Mheshimiwa Ame Pandu Ame, wewe umemtaja kama Ame Ame. Kwa hiyo, sahihi ni Mheshimiwa Ame Pandu Ame na

mwingine umemtaja Ameir Ameir, lakini jina lake sahihi ni Mheshimiwa Ameir Ali Ameir. Kwa hiyo, nadhani tumeweka sawa sawa *record*. Waheshimiwa Wabunge, sasa ili tufikie kwenye uamuzi kamili, inabidi tuingie kwenye hatua nyingine.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 44 - Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko**

Kif. 1001 – *Administration and General*……………….Sh.3,467,477,800

**MHE. MOHAMED HABIBU JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya mwanzo. Katika mchango wangu, nilihoji mambo haya ya viwanda. Lakini ni vyema kwanza nianze kwamba, mnamo tarehe 18, niliiandikia barua Wizara ya Biashara na Viwanda, kunipa idadi ya viwanda vyote Tanzania vyenye *Boilers* zinazotumia kuni au mafuta mazito kwa lengo la kutaka kulinganisha na matumizi ya gesi na *volume* ya kuni zinazotumika au *cubic metre* ngapi, ambalo hilo sijalipata. Lakini bahati nzuri nikapata takwimu ya viwanda vinavyotumia gesi asilia na bahati nzuri nitatumia nakala ya takwimu ambazo zimo kwenye *document* hii, ambayo imekwenda kwa Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda, Bishara na Masoko, pamoja na Wizara ya Nishati na Madini. Nikapata taarifa kwamba, viwanda ambavyo vinatumia gesi asilia ni 17 mpaka sasa hivi na viko vingine vingi.

Kuanzia Julai, 2004 mpaka Mei, 2007, viwanda hivi 17 vimeweza kununua gesi ambayo ina thamani ya Dola za Kimarekani 66,410,803. Sasa ukichukua Hotuba ya Msemaji Mkuu Kambi ya Upinzani, alisema kwamba, kuna *saving* ya Dola za Kimarekani 744,289,401, kwa maana kwamba, viwanda hivi vingetumia mafuta mazito kwenye zile *boilers*, vingetumia Dola za Kimarekani 810,700,205. Kwa hiyo, *saving* waliyofanya ya Dola za Kimarekani 744 ni kubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa nataka Mheshimiwa Waziri atufafanulie Sera ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kuhusu matumizi haya ya gesi au hivi viwanda ambavyo vimepata upungufu, yaani ile *running cost* imepungua kwa kutumia gesi asilia na wamefanya *saving* hii ambayo kama utagawa kwa hivyo viwanda 17 ni kiasi cha shilingi bilioni 55.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hii *EWURA*, uzoefu uliopo mpaka sasa hivi *EWURA* wao wana-*regulate* bei za umeme, maji, ambayo ni *Energy*, *Water and Utility Regulatory Authority*, lakini vipi hii bei za bidhaa za viwanda na hivi viwanda, siyo viwanda vya Saruji tu, vipo viwanda vya nguo ndiyo vingi, viwanda vya mafuta ya kula ndiyo vingi. Sasa ikiwa wao wanafanya *saving* kama hii, *EWURA* hii inafanya nini? Ninataka Mheshimiwa Waziri, atufafanulie kwa sababu mwaka jana suala hili lilijichomoza na kwa wakati ule lilikuwa *formulated* namna gani, lakini kaka yangu Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. R. Msabaha, alijibu kwamba, atalifanyia kazi na atatujibu haraka iwezekanavyo bada ya kikao kile. Lakini mpaka leo hatujapata hilo jibu,

kwa nini viwanda hivi sisi hatupati punguzo, wananchi wakafaidika na matumizi ya hii gesi asilia inayozalishwa Tanzania? Nataka ufafanuzi.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anayosema Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa kwamba, viwanda hivi vimeokoa fedha na ni kweli anavyosema katika *logic* tu ya kawaida, ungetegemea kwamba, kwa sababu hawa wamepata unafuu, basi na mlaji angepata nafuu. Ndiyo maana nikasema wakati nikijibu kwamba, kwa sababu kuna utata huo ni lazima tuingie mle ndani zaidi kwenye kila kiwanda, kujua *cost structure* ya kiwanda ni kitu gani hasa. Kwa sababu unaweza ukaokoa kwenye gesi, lakini gharama nyingine zikaongezeka mara tano/kumi, kwa hiyo, *overall cost* ya kile kiwanda isioneshe nafuu yoyote kwa maana ya bei ya bidhaa ile na bei kwa mkulima.

Kwa hiyo, hatuwezi kusema bila kufanya hesabu na ndio maana nikasema mimi nataka kuanza na saruji kwa sababu kubwa mbili; kwanza, saruji kama saruji duniani kote ni bidhaa tata, kwa sababu ni watu wachache duniani wenye viwanda vya saruji na hata viwanda vyetu vya saruji hapa, wawekezaji wapo vilevile Kenya, nchi zinazotuzunguka na hapa hapa. Je, ni *monopoly* au ni *collusion?* Je, ni ukiritimba wa kimataifa na kitaifa; ni kitu gani?

Kwa, hiyo, ndio maana nataka kuanza na saruji na nimekwishamwagiza Katibu Mkuu wangu, atutafutie *independent consultants* waingie kule ndani, watuambie kulikoni kwenye saruji. *Next* mafuta ya kupikia kulikoni? Tukishafika pale, tukishapata sasa mahesabu, tutawaita tutawaambia kwa nini nyie hampunguzi bei hapa kama ni ya kupunguza. Tukiona siyo ya kupunguza, basi tutakuwa tumeelewa sababu zenyewe na wakati ule naweza nikakujibu kwa ufasaha. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED HABIBU JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali katika ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri, lakini nataka anifafanulie zaidi. Hawa *EWURA* wao kazi yao nini hasa ikiwa hivi sasa ndio itaundwa hiyo *team* ya ku-*investigate* hizo *cost analysis*, hawa wanafanya nini muda wote huo? Hivi wao kazi yao ni kupandisha tu, hawawezi kuona vitu kama hivi?

**MWENYEKITI:** Lakini *EWURA* si suala la *Energy* kule? Mimi ningependa sana usipokee suala la huyu anayeuliza, maana *EWURA* sasa tunaingia kwenye Fungu lingine ambalo tulishalipitisha. Mambo ya *EWURA* tulishamaliza juzi. Sasa upokee hii kwamba atafanya *investigation;* kwa nini bei zibakie vilevile wakati matumizi ya gesi yameshusha gharama za uendeshaji? Nadhani hiyo ndiyo *concern* kubwa hapa. *(Makofi)*

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwenye *Vote* hiyo hivyo, sitaki kusema ninasikitika, kwa sababu Mheshimiwa Waziri amesahau, katika mchango niliochangia leo sijajibiwa hata moja. Mawili ambayo nayaongelea hapa; la kwanza nilisema kwamba, Serikali kwa kutegemea tu mkoa mmoja kuwa na viwanda vyote si sahihi kwa uchumi wa nchi na kwa sababu sasa hivi nchi yetu

tayari ina miundombinu ambayo hakuna sababu yoyote ya kusema kwa nini viwanda visiende mikoani kwenye malighafi, kwenye maeneo husika na nikatoa mfano mzuri tu kwa Mkoa wangu wa Shinyanga kwamba, kuna Pamba nyingi, kule hatuna hata kiwanda kimoja cha nguo. Kigoma kwa mfano, sijui kama kuna kiwanda cha mafuta. Kupanua wigo wa viwanda Mikoani ni muhimu sana kwa uchumi, niliongelea vizuri hilo na nikasema Mheshimiwa Waziri, anieleze katika majibu yake, lakini sijajibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, anieleze ana mpango gani wa kuona kwamba, wawekezaji anawa-*convince* kwenda mikoani kwa maana ya kuleta miundombinu mizuri na kuwaeleza kwamba, mtakapokwenda kule, Wizara itawasidia hivi na hivi ili kupanua wigo wa makampuni mapya na viwanda vipya, wakulima waweze kufaidika na viwanda hivyo, kwa maana ya kuongeza pato la mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, niliongelea ukaguzi wa magari nje ya nchi. Nikasema kwamba, hili suala la ukaguzi wa magari nje ya nchi si sahihi kabisa, wala si kweli kwamba gari linapokaguliwa likiwa Dubai, Japan au London, ndio umelifanya liwe na ubora zaidi kuliko pale liliponunuliwa. Hii ni *routine* tu na njia imewekwa baina ya *TBS* na wale wanaopewa tenda, kutengeneza fedha na zaidi fedha wanaopata ni wale wanaopewa tenda kuliko *TBS* wenyewe wanavyong'ang'ania hili suala. Nikatoa mfano kabisa kwamba, tenda aliyopewa mtu mmoja wa Dubai, amejenga nyumba ya dola milioni sita. Ndugu zangu, hebu tuionee huruma Tanzania na Watanzania wanaoagiza magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri hili alielewe sana. Hili linawaumiza sana Watanzania wanaoleta magari kutoka nje, linawaumiza sana na linaiumiza sana Tanzania. Fedha hizi mabilioni yanatoka nje kwa kitu ambacho hakina umuhimu, sioni umuhimu kabisa, ingeweza kusadia mambo mengine ya Watanzania kwa maana ya kufanya vitu vingine zaidi ya kulipia hizi gharama za ukaguzi wa magari nje ya nchi yanayoingia hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi ulio sahihi kabisa, analichukuliaje hili kwamba litaendelea. Lakini mimi kwa maoni yangu, naomba alisimamishe kabisa na lisiwepo kabisa kwa sababu halina umuhimu wala halifai katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, una biashara ya namna hiyo?

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya ukaguzi wa magari nje ya nchi?

**MWENYEKITI:** Ya kuingiza magari?

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilifanya kwa muda mrefu sasa hivi nimeacha, lakini nina uzoefu mkubwa sana tena sana.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, kawaida yetu ungetumia kifungu 49(vii), kusema nazungumza haya nilikuwa na *interest in it*.

**WABUNGE FULANI:** Aliacha.

**MWENYEKITI:** Aliacha?

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeacha hiyo biashara.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mhehimiwa Mwenyekiti, asante. Ni kweli naomba msamaha kwamba sikuweza kumjibu kwa sababu tu ya muda. Lakini nakubaliana naye kabisa kwamba, kuna umuhimu wa kusambaza viwanda nchini. Sasa hili tena kwa taarifa yake, Solwa kule nadhani yeye afadhali hata kuliko mimi, mimi Waziri wa Viwanda, miaka yote hii sina kiwanda hata cha *SIDO* kule Rombo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri naomba uwe *brief.*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nataka kukubaliana naye kwamba, kuna haja ya kusambaza na sababu mojawapo ya kum-*convince* mtu aje Solwa ni miundombinu, iwe sahihi na najua anachosema. Pili, mali ghafi iliyo pale kwa mfano, pamba ya kwao, hakuna sababu kwa nini mtu anunue pamba Solwa akaitengenezee kule Shinyanga Mjini au Mwanza au wapi, yaani kwenye *Ginnery*, badala ya kuanzisha *ginnery* huko huko Solwa, kwa sababu pamba iko pale pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana nikasema kwenye *Basic Industry Strategy* na Mkakati huu niliousema huu wa viwanda, haya ndio mambo tutakayoweka kwenye sera itakayotokana na *review* hiyo ambayo tunataka kuileta. Tulikuwa na utaratibu wa Kikanda wa kusambaza viwanda huko nyuma, lakini utaratibu huo haupo. Lakini tujue ili tufanye hivyo, lazima tufanye mambo mawili; moja, kumbembeleza mwekezaji, lakini la pili, Serikali yenyewe kuchochea.

Nilikuwa nazungumzia suala la kuchochea, mimi nikiwa na fedha za kuanzisha kiwanda cha nyama Solwa au kiwanda cha nguo au kitu chochote kilichoko pale, nikawa nimeweka asilimia fulani ndiyo mtu mwingine ataniunga mkono, pamoja na Wanasolwa wenyewe. Kwa sababu kama ilivyosemekana hapa na mimi nakubaliana nao kwamba, mtu wa nje hawezi kuja kukuwekea kiwanda Solwa, Wanasolwa wenye tukianzia na Mbunge na wengine, tunaweza tukawahamasisha tukaanzisha shughuli za viwanda kule kule walipo. Kwa hiyo, nakubaliana naye na nitazingatia ushauri huo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naomba uwe *brief* Mheshimiwa Mbunge.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la magari nitalifanyia uchunguzi, jambo hili silielewi sawa sawa. Ninachoelewa mimi ni kwamba, mwaka huu kwenye bajeti hata bajeti iliyopita, tumekuwa tukiweka ushuru maalum kwa ngazi ya Afrika Mashariki, kwa magari yote makuu kuu yanayoingia nchini, tumeweka ushuru mgumu. Lakini vilevile nimesema kwenye hotuba hii kwamba, nataka kuweka utaratibu wa kukagua mali zote kule zinakotokea si Dubai, maana Dubai pale hawatengenezi magari, kama ni kukakagua nitakagua kule Japan, kama ni Toyota au mengine yanakotokea. Kwa hiyo, huu utaratibu mpya ninaotaka kuuleta utawauwa hawa wanaofanya mambo kama haya anayolalamikia Mheshimiwa Mbunge. Lakini pamoja na hayo, wakati nafanya mambo haya, nitalichunguza jambo hili na kwa kweli nitaangalia kama ni *relevant*, kama si *relevant* tutalifuta kama ni *relevant* tutaangalia tutakuwa namna gani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, nadhani hata Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga alisema na Kamati ilipita huko kuisaidia Serikali kueleza hayo mliyokuwa mnayaeleza kusudi waweze kufikia uamuzi mzuri zaidi. *(Makofi)*

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Ni *vote* hiyo hiyo na vifungu hivyo hivyo. Mimi ni mmojawapo niliyechangia asubuhi mapema kabisa kwa maandishi, lakini kwa bahati mbaya sikusikia jina langu. Hata hivyo nimethibitishiwa kwamba karatasi imefika.

**MWENYEKITI:** Endelea na hoja muda unakwenda.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka minane iliyopita (mwaka 1999), Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini, walituma mtu Itigi kwenda kuona ubora wa *gypsum,* pamoja na biashara inayoendelea hapo. Huyu mtu alikuwa anaitwa Ndugu Lipindu. Alikwenda hapo akajionea mwenyewe *gypsum* hiyo, aliona mabehewa mengi yanayosomba *gypsum* kwenda nchi jirani kupitia Kigoma kwenda Ruanda, Burundi na Uganda. Kwa hiyo, akajionea pia kuwepo kwa chokaa na akajionea pia kuwepo na *read soil,* basi akaondoka. Lakini sasa ni miaka minane toka wakati huo na wakati huo aliacha suala la umeme.

**MWENYEKITI:** Punguza hadithi sema shida yako.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Sawa, lakini ninachotaka kujua ni ufafanuzi kwamba; je, huyu mtu alikuja na ripoti gani na Wizara hii ina Mipango gani ya baadaye ya kuweza ku-*exploit* hiyo *gypsum* na hasa kuwahamasisha wawekezaji kuweka kiwanda cha saruji?

**MWENYEKITI:** Sasa ndiyo umesema. Yeye anatafuta kiwanda cha saruji, kuna Bwana Lipindu wala humkumbuki. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba radhi kwa Mheshimiwa John P. Lwanji ni kweli alikuwa ameleta kwa maandishi lakini *paper* ilisahauliwa, nadhani ilipotea kidogo kwenye makaratasi.

Kwa hiyo, nataka kukiri kwamba ni kweli alileta kwa maandishi na nataka rekodi ile iwe sawa kwenye *Hansard.* Naomba radhi.

La pili, nijibu tu kwamba, malighali kubwa katika utengenezaji wa saruji ni chokaa siyo *gypsum*. Lakini pia nikiri kwamba, gypsum ya Manyoni ni nzuri sana.

Tatu, ni kwamba, hata kama *gypsum* ingekuwa nzuri, ingekuwa nyingi na ingekuwa ndio malighafi, kuu kuna suala la umeme. Viwanda vya Saruji vinatumia umeme mwingi sana au *gas* nyingi sana na kadhalika. Kwa hiyo, nimekwishaagiza watalaam wangu wa *NDC* waende Manyoni wakafuatilie kwa sababu aliuliza swali hapa, baada ya kumjibu nilivyojibu nimeagiza Shirika la *NDC* liende Manyoni, likafanye uchunguzi, liniletee taarifa kama Kiwanda cha Saruji hata kidogo, maana hata saruji pia inawezekana kwenye viwanda vidogo, hata kidogo kama kinawezekana ama hapana. Taarifa hiyo ikitoka, nitamweleza Mheshimiwa Mbunge hali itakuwa namna gani. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi nina mawili; la kwanza, namshukuru sana Waziri kwa ufafanuzi wa dhana ya kujitoa na sina hakika ni Watanzania wangapi wanaoelewa Serikali inaposema imejitoa, inasema nini. Tungeomba kuwepo ufafanuzi uliofanyiwa uchunguzi wa kutuonesha maana ya Serikali kujitoa ni nini, hasa pale nyumba imesafishwa ikatiwa marashi kumtega mwekezaji ambaye hakuja. Sasa Serikali ina wajibu gani katika mazingira kama hayo, kwa mfano, tunahitaji kiwanda cha mbolea tuna *gas* katika maeneo makubwa matatu sasa. Hebu Waziri anieleze hiyo nyumba tukisafisha ni mwekezaji gani tunamtegemea kuja kutujengea kiwanda cha kutengeneza mbolea? Namba sana hilo.

La pili, nalo ni fupi, tulikuwa na dhana ya viwanda mama, ndivyo vilivyosababisha tukajenga viwanda kama *Kilimanjaro Machine Tools* na vingine vya aina hiyo. Hii dhana nayo imeishia wapi; *strategy* gani ambayo Wizara inayo sasa ya kuendeleza hii sekta ya viwanda? Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Asante maswali mazuri.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumjibu Mheshimiwa Mbunge wa Ubungo, kama ifuatavyo:-

Kuna aina nyingi za mbolea lakini kwa zile mbolea ambazo nahisi yeye anazifahamu sana, kwa sababu alikuwa Waziri wa Kilimo, hizi tunazotumia hapa, fikra zilizoko sasa ni kutumia *gas* kwa sababu ni mbolea ambazo zinaweza zikatengenezwa kutokana na *gas* tuliyonayo na hasa tunalenga *gas* ya Mtwara. Kama Wabunge wa Mtwara watakumbuka, Mheshimiwa Rais alikwenda Mtwara mwezi Novemba, 2006 kuzungumza na wale wenye *gas,* uwezekano wa kuanzisha kitu kinachoitwa *Petrol Chemical Complex,* maana yake hiyo ni mbolea na bidhaa za *plastic* na bidhaa nyingine za kemikali. Hivyo ni viwanda mama. Vilevile tunao wawekezaji wawili ambao wameshakuja kufuatilia suala hilo, wanataka kuanzisha viwanda vya mbolea kwa kutumia *gas*.

Ni mapema mno kuweza kusema zaidi kwa sababu bado hatujafika mahali, lakini wako watu ambao wameonesha nia na *gas* tunayo pale Mtwara ni lazima tuelewane na mwenye *gas,* kwa sababu kuna wanaosema *gas* ile kuliko kuitumia kwenye *petrol chemicals* au mbolea, itumike kwa mambo mengine hata ungeuza uka-*export* lakini sisi tunasema kwa nini ku-*export* halafu tuka-*import* mbolea? Kwa hiyo, tunalo hilo na ningetaka kumhakikishia, aamini kwamba tunalishughulikia kikamilifu kwa msingi huo.

Hili la *strategy* ndiyo hili niliseme, *integrated industrial development strategy* ndiyo hiyo nitakayoifanyia kazi mara nikipa fedha leo. Hiyo ndiyo naweza nikaileta hapa kwenye hotuba ijayo kwa ufasaha zaidi na ndani yake kutakuwepo ile *basic industries strategy* na yale mambo mengine yote yanayoendana na hali za kileo za maendeleo ya viwanda kwa nchi maskini kama hii ya kwetu. *That is a strategy*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, tuisubiri hiyo tuendelee.

**MHE. SALIM ABDALLAH KHALFAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nitaomba maelezo ya ufafanuzi katika haya nitakayoyasema. Baada ya viwanda vyetu vingi kufa na kuvibinafsisha, wale waliopewa kuvifufua walikuwa na malengo tofauti na makubaliano. Lakini tulipohoji, tuligundua kwamba, Serikali ilikuwa haina meno ya kuwanyang'anya viwanda hivyo. Mfano wa viwanda vya korosho, alioutoa Mheshimiwa Waziri ni mfano hai.

Kwa kuwa vilevile kule Kariokoo Dar es Salaam, kuna wageni wengi wanaofanya biashara ndogo ndogo, ambao pole pole wanaanza kuchukua nafasi za wazawa, sidhani kama kwa sasa hivi tunahitaji wafanyabiashara wa nje, kwa biashara kama hizo kwa utaratibu ulio hivi sasa. Lakini kwa kuwa vilevile katika madini tumeona kwamba, wageni wanafaidika zaidi kuliko wazawa kwenye biashara kama hii na kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge, sasa hivi uchumi wetu unaanza kutawaliwa na wageni.

Je, hii ndiyo Sera ya Serikali ya Awamu Nne kwamba, *trend* sasa hivi inakuwa wageni wanakuwa juu na wazawa wanakuwa chini? Kama siyo, basi kuna hatua gani za haraka za kuyakomesha haya? Asante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumjibu kwa kifupi kwamba, kwa sekta yangu ya viwanda na biashara nimesema kwenye hotuba hii kwamba, katika kutafakari hiyo sera inayokuja ya *integrated industrial development strategy,* suala la nafasi ya Watanzania kwenye *strategy* hiyo litajadiliwa na litawekewa msimamo. Kwa hiyo, naomba tena asubiri sera hiyo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – *Finance and Accounts* …………………..……Sh. 192,355,200
Kif. 1003 – *Policy and Planning* ………………………Sh. 2,227,068,300

Kif. 1004 – *Information, Educat. Communication unit*……Sh. 194,172,700
Kif. 1005 – *Internal Audit Unit* ………………………………Sh. 49,161,600
Kif. 1006 – *Legal Service unit* ………………..............……Sh.24,589,800
Kif. *2001 – Industry* …………………………………..……Sh. 2,925,770,500
Kif. 2002 – *Small and Medium Enterprises Division* …Sh. 2,945,366,200
Kif. 3001 – *International Trade* …………………………Sh. 1,771,661,400
Kif. 4002 – *Commodity Market Development* …………Sh. 3,436,932,500

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 44 - Wizara ya Viwanda, Bishara na Masoko**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... ... ... .... .... ..... Sh. 70,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 - *Policy and Planning* ……………….........…Sh. 1, 884,000,000

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. *Vote 44, subvote 1003,* kifungu 1217 - *TBS*. Suala la viwango, kuna matatizo ambayo niliyazungumza katika mchango wangu na bahati nzuri wakati Kamati tulipotembelea *TBS,* niliwahi kuzungumza na wahusika kuhusu udanganyifu wa viwanda ambao unafanyika. Kuna zile bidhaa ambazo zinatoka nje lakini tuchukulie kuna hizi bidhaa za ndani. Kwa muda huu, tuchukue mfano wa hizi bidhaa za ndani. Utakapochukua bati na wewe ni mtu wa kawaida, labda huelewi mambo ya ufundi hata kidogo, ukiacha wale *contractors* unaambiwa bati hii *gauge* 28 na imepigwa mhuri wa *gauge* 28, lakini kumbe bati hili ni *gauge* 30. Utakapopata bati lingine kama lile kwa wale wanaotimiza, utaona kuna tofauti kubwa.

Hivyo hivyo na nondo, unaweza ukaambiwa nondo hii ni mm 12 lakini ukichukua nondo ya mm 12 ya Tanzania, ukaenda ukachukua nondo ya mm 8 ya Kenya, utashangaa kuona zinakaribiana. Ni *contractors* wenye utalaam tu ndiyo wanaofahamu, watu wetu wanaibiwa. Sasa basi hili suala sijui kama *TBS main power* yao ndogo kufuatilia au namna gani na kwa mfano hiyo *production* ya mabati ile mihuri wakienda pale watu wa *TBS,* wanaweza wakaoneshwa kitu *correct* lakini wakishaondoka, zinachukuliwa zile zinaletwa Dar es Salaam kwenye ghala, inachukuliwa mihuri inagongwa. Suala hili ni vyema Waziri alitolee ufafanuzi, *policy* iko vipi na namna gani tutafanya ili hawa *TBS* watimize wajibu wao na je, *main power* yao ndogo au namna gain, lakini hili suala tutafika vipi tunadanganywa viwango pamoja na bidhaa zinazotoka nje hasa vifaa vya umeme. Asante, tunaomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Kwamba, havifanani na *standard* zinazotakiwa, *TBS* inafanya nini?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu sielewi hilo duka ni lipi na ilivyokuwa niseme tu kwa kifupi kwamba, *standard* iliyowekwa na *TBS* ni ile ile haibadiliki. Kama nilivyosema kwenye hotuba hapa, *standard* zile zimewekwa ndani ya kiwanda chenyewe lazima kitoe ile ile na *TBS* huwa wanakagua kwa kushtukiza, kuona kama zile *standards* zinafuatwa au hapana. Lakini ni kweli vilevile kwamba, kwenye soko letu kuna mabati, siyo mabati yote yanayouzwa kwenye soko letu ni ya *ALAF,* kuna watengenezaji wengi na wengine hawana *standard* na mengine ni *imported.*

Kwa hiyo, muuzaji anaweza akakuambia hili la *ALAF,* hili samba, ndiyo maana unaona hapa karibuni kumekuwepo mkazo wa kila mtu kusema bati lake likoje kwenye matangazo hata kwenye redio ni kwa sababu kuna aina nyingi za mabati kwenye soko na kila mtu anajaribu kung'ang'ania kwamba ni *ALAF,* kumbe siyo. Kwa hiyo, naweza nikasema hivyo tu kwamba, *standard* ni ile ile lakini wauzaji wanajidai ni *ALAF* wapo wengi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nadhani yeye ametumia mabati kama mfano, lakini kuna vitu vingi vinavyofanana na hivyo, *TBS* wanafanyaje? *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Sawa sawa kwamba, *TBS* wana hizo *standards* ambazo wameshazitoa na huwa wanazikagua. Kwa hiyo, kama ningepata *specific example,* nitafurahi sana kufuatilia kujua kama *TBS* nao wanafanya magendo ama wanafanya mambo ya namna gani.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 - *Small and Medium enterprises Division* ....Sh. 2,982,900,000
Kif. 4002 - *Commodity Market Development* … … .. Sh. 2,458,476,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa mwaka wa fedha 2007/2008, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa liidhinishe makadirio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Makadirio ya Viwanda, Biashara na Masoko yamepitishwa na Bunge hili. Tunaomba tuwapongeze Wizara na yale mliyoahidi yaweze kutekelezwa hasa hiyo *strategic* ya viwanda ndiyo tunachokitafuta.

Baada ya hapo, sina jambo lingine isipokuwa kukumbusha kwamba, kesho Jumamosi tarehe 28 Julai, 2007 saa tatu asubuhi kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa, kutakuwa na semina ya masuala mbalimbali, juu ya watu wenye ulemavu. Wanawakaribisha Wabunge wote. Kama tulivyosema hapa, wanataka kutuelimisha sisi wenzao kwamba walemavu wako namna gani. Kwa hiyo, mtahudhuria hiki ni kitu ambacho kinatakiwa ni *humanitarian like a form of a seminar.* Kwa hiyo, ni vizuri tukajua kwa sababu hawa ni jamii yetu wenyewe, ama sivyo inakuwa ni unyanyapaa pia. Kwa hiyo, mnakaribishwa kule. *(Makofi)*

Halafu tarehe 29 Jumapili saa tano asubuhi katika Ukumbi huo huo wa Msekwa, watu wa *APNAC Tanzania*, wanawakaribisha wote kwenye uzinduzi wa ripoti yao. Siyo wanachama wa *APNAC* tu, wote saa tano asubuhi walisema wanachama tu lakini wote.

Halafu Mwenyekiti wetu wa *Bunge Sports Club,* Mheshimiwa Joel N. Bendera, anatutangazia sisi wote kuhusu kesho kutakuwa na mchezo wa mpira wa miguu kati ya timu ya Waheshimiwa Wabunge na timu ya maveterani wa Ukonga Dar es Salaam. Mchezo huo utafanyika katika Uwanja wa Jamhuri Dodoma kuanzia saa 10.00 jioni hivyo mnaombwa kuhudhuria wote bila kukosa la sivyo, mtashindwa halafu itakuwa aibu kwa hiyo, muhudhurie wote bila kukosa. *(Makofi)*

Baada ya hapo, nadhani hatuna shughuli nyingine, kama tulivyowatangazia Waheshimiwa Wabunge, akina mama wa CCM wapo wengi walikuwa na shughuli yao ya Uchaguzi Mkuu na nadhani mambo yanaendelea huko. Lakini napenda niwashukuru sana kwa kazi tuliyofanya wiki nzima, mimi binafsi kama ningeelezwa kwamba *marks* zinazidi kupanda juu kwenye Kamati ya Matumizi, sasa mnaanza kufanya vizuri zaidi kuliko tulivyoanza. Kwa hiyo, ni mategemeo yangu kwamba, siku zilizobaki napo tutafanya vizuri sana.

Waheshimiwa Wabunge, nawatakia *weekend* njema na naahirisha kikao cha Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.27 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu,*
*Tarehe 30 Julai, 2007 Saa Tatu Asubuhi)*